

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Nane – Tarehe 14 Mei, 2014

(Mkutano Ulianza Saa tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na :-

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K.A. MALIMA):

Taarifa ya Mwaka ya Tathimini ya Soko la Bima kwa Mwaka unaoishia tarehe 31 Desemba, 2012 *(The Annual Insurance Market Performance Report for the Year Ended 31st December, 2012)*.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 51

Ujenzi wa Vituo vya Afya

MHE. OMARI R. NUNDU aliuliza:-

Jimbo la Tanga Mjini lenye Kata 24 lina Vituo vya Afya vinne (4) tu ambavyo kati ya hivyo ni kituo kimoja tu kipo katika Kata za Vijijini ambako kuna Kata kumi (10) zenye vijiji ishirini na tatu 23.

(a) Je, Serikali imepanga kujenga Vituo vya Afya vingapi kama hivyo katika jimbo la Tanga Mjini?

(b) Je Serikali haioni umuhimu wa kuharakisha ujenzi wa vituo hivyo pamoja na kuvipatia yenzo muhimu?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari R. Nundu lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Miradi ya ujenzi wa Vituo vya Afya huibuliwa na wananchi wenyewe kupitia mpango wa fursa na Vikwazo katika Maendeleo (O&OD) na kutekelezwa kwa ubia kati ya Wananchi na Hamashauri.

Halmashauri huchngia gharama kidogo za utekelezaji wa miradi hiyo kwa kuwezesha upatikanaji wa vifaa pamoja na usimamizi. Halmashauri ya Jiji la Tanga ina Vituo vya Afya 10 ambapo kati ya hivyo vitano (5) ni vya Serikali na vitano (5) ni vya watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Afya kila Kata, Halmashauri imetumia shilingi 51,513,500/= kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Maere na shilingi 54,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Mabokweni. Fedha hizi zinatokanana bakaa ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo katika mwaka wa fedha 2011/2012. Ujenzi upo katika hatua ya msingi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri katika Bajeti ya mwaka 2014/2015 imetenga shilingi 40,000,000/= kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Afya Maere na Shilingi 40,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Mabokweni.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza Sera ya Afya ya mwaka 2007 ya kuwa na Kituo ha Afya kwa kila Kata kwa awamu kwa kuzingatia upatikanaji wa rasilimali feha kila mwaka.

MHE. OMARI R. NUNDU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwanza ninamshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, na hili swali liliulizwa Julai, 2012, na tunaona toka wakati huo kazi nyingi zimefanyika na ninawapongeza sana kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini kwanza amesema kuna vituo 10. Vituo vitano (5) ni vya watu binafsi. Ieleweke kuwa Vituo vya Watu Binafsi siyo vya kutoa huduma ya Afya. Hivi ni vya biashara, kwa hiyo tuongele, hivi vinavyotoa huduma kwa wananchi, na viko vine tu (4). Makorora, Mikanjuni, Ngamiani na Pongwe.

Lakini juhudi zimefanyika, kuna Kituo cha Duga ambacho kiko katika matayarisho na kimefadhiliwa *TULEDO* na Maweni pia *Cement* wamejaribu kufadhi. Ninaomba wafanya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

biashara wengine na wenye viwanda Tanga wafuate mfano huu, ili tupate Vituo vya Afya vya kutosha.

SPIKA: Mheshimiwa unachotakiwa kufanya ni kuuliza swali na siyo hotuba.

MHE. OMARI R. NUNDU: Mheshimiwa Spika, sasa swali langu tumeambiwa kuna Kituo cha Mabukweni na Maere, ambavyo vimetumia fedha kiasi fulani zilizotengwa na zinazotumika. Ninachotaka kujua ni kuwa mpaka kumalizika vituo hivi vitatumia pesa kiasi gani? Mpaka leo vimetumia kiasi gani na vitamalizika lini?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Nundu, kama hivi ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya (a) ni ya ufafaanuzi. Kwamba katika ujenzi wa Vituo hivyo kimoja ni cha binafsi. Ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya kuhimiza utekelezaji wa Sera ya Afya ya 2007, kwamba kila Kata iweze kuwa na Kito cha Afya na kila kijiji, kiweze kuwa na Zanahanati. Kwa hiyo wenzetu ambao wamewaidiana na Halmashauri ya Tanga katika kujenga kituo kile cha Duga ni chini ya Sheria Namba 8 ya 2010 katika suala zima la PPP.

Sehemu ya (a) ya kwamba ni fedha kiasi gani na ni lini kazi hii itakamilika. Hii inategemea upatikanaji wa fedha. Kulingana na hali halisi ya Bajeti ya nchi yetu.

Lakini pia kiasi hiki cha pesa ambacho kimepatikana katika mwaka ujao wa fedha shilingi milioni 40,000,000/= ni sehemu tu ya utekelezaji kwa sababu tutafanya Mchanganuo ili kusaidiana na Halmashauri na kuona nini wanachoweza na kile ambacho hakiwezikani basi Wizara ya Afya na wao tuweze kusaidiana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niwapongeze wenzetu wa Tanga. Kwa sababu sehemu ya utekelezaji wa Vituo katika ngazi za chini, hadi sasa tunavoyo Vituo katika nchi nzima vipatavyo 8,600, ukilinganisha na wakati tunapata uhuru, tulikuwa na Vituo vya Huduma ya Afya vipatavyo 1,256. Haya ni mafanikio makubwa sana katika utekelezaji wa Sera hii. (Makofi)

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Kwa vile Serikali ilitia maanani sana na kutia juhudi kwa wananchi kwamba wajitolee kujenga Vituo vya Afya kwa kila Kata. Lakini vingi mpaka sasa bado havijaanza kufanya kazi kama Vituo vya Afya, kama vile ilivyo Kata ya Mawindi. Kwangu kule Mbarali na Kata ya Mapogoro, kule Mbuyu.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani sasa, kuona kwamba jitihada za wananchi hizi hazipotei hivi hivi tu, kwa hiyo inawawezesha kuona hivyo vituo vinafanya kazi. Ni lini sasa Serikali itapeleka fedha ili kukamilisha vituo hivyo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri ninaomba ujibu kwa kifupi. Kwa yale uliyoulizwa tu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Modestus Kilufi, kama hivi ifuatavyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, suala zima la upatikaji wa fedha kwa ajili ya kumaliza vituo hivi ni suala ambalo kulingana na upatikanaji wa fedha katika Bajeti ya Serikali ambayo tutaifanyia kazi kusaidiana na Halmashauri na pia, tunahimza Watanzania wote suala hili la ujenzi wa vituo si kwa Serikali tu. Muundo wa Sera ni kwamba lazima tushirikiane na Asasi, mbalimbali watu binafsi, katika suala zima la sheria ambayo na utaratibu ulianzishwa katika nchi wa Sheria Namba 8 kama nilivyosemwa ya mwaka 2010 chini ya PPP.

Na. 52

Ujenzi wa Mabwawa ya Kunyweshea Mifugo, Majosho na Dawa za Mifugo.

MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR aliuliza:-

Wafugaji wengi wa jimbo la Nyang'hwale wamekuwa wakihangaika wakati wa kiangazi kutafuta maji kwa ajili ya mifugo yao:-

(a) Je Serikali iko tayari kuwachimbua mabwawa ya kunyweshea mifugo wafugaji wa Nyang'hwale?

(b) Mifugo pia imekuwa ikidhoofika kutokana na kukosa majosho na dawa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wafugaji hao ili mifugo yao isiendele kufa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninamba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, lenye sehemu (a) na (b), kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'wale ina jumla ya Malambo 25, ambapo kati ya Malambo hayo ni Malambo sita (6) ndiyo yanayotumika kwa hivi sasa. Malambo hayo yapo katika Vijiji vya Shabaka, Nyaluluguna, Idetemya, Rushimba, Nyabulanda, Izunya na bwawa moja katika kijiji cha Nyamigogwa. Aidha, malambo haya yanayofanya kazi yana mapungufu ambayo yanahitaji kurekebisha ili yaweze kufanya kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi milioni 64, zikiwemo milioni 30 kwa ajili ya ukarabati wa Lambo katika kijiji cha Shabaka na Milioni 34, kwa ajili ya uchimbaji wa Lambo jipya katika kijiji cha Bulangale Kata ya Bukwimba. Fedha kwa ajili ya uchimbaji wa Lambo jipya Bulangale ipo tayari na Mkandarasi wa mradi kwa ajili ya uchimbaji amepatikana. Utekelezaji utafanyika baada ya msimu wa mvua kwisha. Aidha, fedha kwa ajili ya ukarabati wa Lambo katika Kijiji cha Shabaka milioni 30, zimepatikana na utekelezaji utafanuliwa baada ya taratibu za kumpata Mkandarasi kukamilika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 kiasi cha shilingi 28,951,000/= kimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa Lambo katika kijiji cha Lushimba.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'wale ina jumla ya Majosho 10. Ambapo kati ya hayo . Majosho sita (6) ndiyo yanayofanya kazi na mengine yanahitaji ukarabati mkubwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2013/2014 hakuna dawa zilizopelekwa kwa maana ya ruzuku ya Serikali. Katika mwaka wa fedha 2014/2015. Kiasi cha shilingi milioni 15,350,000/= kimetengwa kutoka vyanzo vya mapato vya ndani vya Halmashauri, kwa ajili ya ununuzi wa dawa kwenye majosho hayo. Ahsante sana.

MHE. HUSSEIN NASSORO AMAR: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Ninapenda kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini ninapenda nimwulize maswali mawili kama hivi ifuatavyo:-

Amekiri kabisa kwamba Wilaya ya Nyang'wale inayo Malambo 25 na ni Malambo tisa tu yanayofanyakazi. Malambo 19 hayafanyi kazi. Amekiri pia kwamba kuna milioni 30,000,000/= ambazo zimetengwa kwa ajili ya Ukarabati wa Lambo ya Nyamgogwa.

Jibu hilo nilipewa hata mwaka 20013, kwamba lambo hilo lilitengewa shilingi milioni 30,000,000/= kwa mwaka uliopita. Hata mwaka huu, limerudiwa jibu hilo hilo.

Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi zake za kulifufua Bwawa hili la Nyamgogwa, na haya Mabwawa 19, yaliyobakia katika Wilaya hii ya Nyang'wale?

Naibu Waziri amekiri kwamba Jimbo la Nyang'wale, ama Wilaya ina Majosho 10. Lakini kati ya Majosho kumi (10) ni sita yanayofanya kazi. Majosho manne (4) hayafanyi kazi.

Je, anaweza kunitamkia hapa na kuwatamkia wafugaji wa Jimbo la Nywang'wale, majosho hayo sita yanayofanya kazi yako kwenye Kata gani? Hii ni kwa sababu hakuna Majosho yanayofanya kazi kutokana na haya majibu. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, kama hivi ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ameuliza Lambo la Nyamgogwa kwamba ni kitu kinacho jirudia sana. Naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba jana mimi mwenyewe. Nimeongea na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'wale, anaitwa Ndugu Fotunata Mallya, na amenihakikishia kwamba ujenzi wa Bwawa la Nyamgogwa, utaanza mara moja kwa sababu pesa zimepatikana.

Kilichositisha kazi hiyo isiendele sasa, ni kwa sababu ya hali ya mvua, ambayo inaendelea Jimboni au Wilayani Nyang'wale. Mheshimiwa yeye anatoka kule na anajua kama kweli mvua inanyesha. Lakini hizi ndizo habari ambazo Mkurugenzi nimezungumza naye jana usiku, amenieleza kwamba, mara bada ya msimu wa mvua kuishi, kazi hiyo itaanza mara moja.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, anauliza Majosho yako kwenye Kata gani. Ninachoweza kumwambia, ni kwamba. Majosho haya sita (6) yanayofanya kazi na Mheshimiwa atajua yako kwenye Kata gani. Lakini taarifa nilizo nazo ni kwamba yako katika vijiji vya Karumwa, Kayenze, Katongo, Chigulwe, Yijundu na Idetemya. Sasa kama Mheshimiwa Mbunge anajua haya hayafanyi kazi.

Lakini Mkurugenzi ametuambia bila shaka, Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye angepaswa kujibu hili angelikuwepo hapa, angelizungumza kwa sauti kubwa tuliyoizoea na kusema. Ninamwagiza Mkurugenzi kama Mabwawa haya ama Majosho haya hayafanyi kazi na amedanganya basi ahakikishe kwamba yanafanya kazi mara moja.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, mimi ninataka sasa nitumie nafasi hii, nimwagize Mkurugenzi kwa sababu nimezugumza naye jana na amenihakikishia kwamba yanafanya kazi, basi yawe yanafanya kazi kweli. Kama ameleta taarifa ambazo siyo za kweli basi tutahangaika naye. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Umejaribu kuiga sauti, lakini haikutosha. *(Kicheko/Makofi)*

MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa mgogoro wa Wafugaji na wakulima unatokana na wafugaji kuhamahama kwa ajili ya tatizo la maji. Ni lini Serikali itachukua tatizo hilo kufanya kwamba ni Mradi mkubwa katika maeneo ya Wafugaji, kwa kuweka Malambo, ili kusitisha uhamaji huo na mgogoro utapungua? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Michael Laizer, anasema kwamba tatizo la wakulima na wafugaji limekuwa linajitokeza na sababu kubwa ni kwamba wafugaji hasa wanakuwa hawana Malambo. Tuna mpango gani wa kufanya sasa shughuli hii ya kuchimba Mabwawa katika maeneo ya Wafugaji iwe ya kudumu?

Mheshimiwa Spika, ninavyofahamu, ni mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba tunaweka Malambo kwa ajili ya Wafugaji, mahali pale ambapo wafugaji wanaishi. Rai ambayo tunaitoa wakati wote ni kwamba Wafugaji wasiwe wanahama hama, wakae mahali pamoja ili iwe rahisi kwamba Serikali inapopeleka hata Mpango wa Malambo pale, ijue kwamba Wafugaji hao wataaendelea kuyatumia Malambo hayo, kuliko unajenga Lambo lakini unajua kwamba baada ya mwaka mmoja Wafugaji hao watakuwa wamehama maeneo hayo.

Kwa hiyo, ninaomba nisisitize na niziambie Halmashauri zote ambazo ziko kwenye maeneo ya Wafugaji, zihakikishe kwamba zinaendelea kutenga fedha na tumekuwa tukifanya hivyo.

Tunatenga fedha kwa ajili ya kujenga Malambo na niziagize Halmashauri nchini kote, zile ambazo ziko kwenye maeneo ya Wafugaji, ziendeleo kutenga fedha kwa ajili ya kujenga Malambo kwa ajili ya Wafugaji. Lakini pia na shughuli nyingine zinazohusu jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 53

Mpango wa Kukarabati Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kilwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. SELEMANI S. BUNGARA aliuliza:-

Kwa miaka mingi sasa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kilwa ambacho ni tegemeo pekee kwa vijana wanaoshindwa kuendelea na masomo ya Sekondari kimesahaulika katika kufanyiwa ukarabati pamoja na kukipatia walimu wa kutosha:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukikarabati chuo hicho katika Bajeti ya 2013/2014?
- (b) Je, ni lini Serikali itapeleka walimu chuoni hapo ili kuondoa tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, lenye sehemu (a) na (b), kama ifutavyo:-

(a) Wizara yangu imekuwa ikikarabati Vyuo kwa awamu na kwa viwango tofauti kuanzia mwaka 2003. Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kilwa Masoko kilifanyiwa ukarabati mwaka 2006 ambapo katika ukarabati huo jumla ya Sh.33,349,340/= zilitumika kubadili paa la jengo la utawala na nyumba ya Mkuu wa Chuo. Pia madarasa na mabweni yalifanyiwa ukarabati mdogo.

Kwa mwaka 2013/2014 Chuo hiki kimetengewa Sh.177,695,980/= kwa ajili ya ukarabati wa jengo lautawala na bweni.

Aidha chuo hiki kipo kwenye awamu ya pili ya vyuo vitakavyotoa mafunzo ya ufundi stadi yanayosimamiwa na Mamlaka ya Ufundi Stadi VETA hivyo kukifanya chuo hiki kuongeza idadi ya vijana watakapata mafunzo ya ufundi stadi. *(Makofi)*

(b) Mheshimia Spika, Wizara inatambua kuwa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kilwa Masoko, kina upungufu wa watumishi. Wizara inaendelea kuomba vibali vya ajira Serikalini kwa ajili ya kuajiri kada mbalibali za watumishi vyuoni.

Ni mategemeo yetu kuwa mara tutakapopata watumishi tutawapeleka katika maeneo yenye upungufu mkubwa wa watumishi ikiwa ni pamoja na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kilwa Masoko. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Bungara swali languine la nyongeza!

MHE. SELEMAN S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, sina swali la nyongeza, majibu ya Waziri ni mazuri sana, lakini nasisitiza tu kwamba watumishi hao watakapopatikana kwanza iwe Kilwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi/Kichelo)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Haya majibu mazuri, lakini anasisitiza tu. Mheshimiwa nani kule nyuma? Kwanza nianze na Mheshimiwa Susan Lyimo, halafu utafuatia.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sana vyuo hivi vya Maendeleo ya Wananchi vimekuwa vikisuasua na hata nikiangalia Bajeti ya mwaka huu ya Maendeleo wametengewa Tsh. Bilioni 1 kwa ajili ya ukarabati wa vyuo vyote. Watu wengi wamekuwa wakisisitiza kwamba, kuna umuhimu mkubwa wa vyuo hivi kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili vijana wetu waweze kupata Elimu ya Ufundi.

Je, wana mkakati gani sasa wa kuhakikisha kwamba, vyuo hivi vinaunganishwa na vile vya Elimu ya Ufundi ili watoto wetu wakitoka pale wawe na elimu ya kutosha?

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, utachanganya na lile la Mheshimiwa Bungara.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naomba kushukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Bungara kwamba, majibu yamekidhi.

Naomba sasa nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lyimo kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, vyuo hivi vimekuwa ni tegemea kubwa sana kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na havisuisui. Vyuo hivi vimekuwa vikisaidia sana watoto wetu katika maeneo mbalimbali, lakini pamoja na kusaidia Wizara ya Maendeleo ya Jamii imekuwa ikifanya kazi pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, tunavyo vyuo 25 ambavyo vimeishaingia katika programu ya kutoa mafunzo ya VETA kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na vyuo vingine vilivyobaki vitaendelea kushirikiana ili kutoa mafunzo ya VETA kwa awamu ya Pili na ya Tatu.

Kwa sasa vyuo 25 tumeishaingia navyo mkataba vinatoa mafunzo ya VETA. Kwa hiyo, ni namna gani Wizara inashirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, jambo hilo limeishazingatiwa kwa asilimia 100.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mikidadi, swali la nyongeza.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kilwa kipo katika Mkoa wa Lindi. Pia katika mkoa huo huo wa Lindi, kuna chuo cha Maendeleo ya Wananchi kinaitwa Chilala, Lindi Vijijini Rutama.

Je, chuo hiki nacho kitaanza kukarabatiwa lini?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mikidadi kwa kufuatilia sana masuala ya elimu hususan ya chuo hiki cha Chilala.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Naomba kusema kwamba, chuo cha Chilala kimeishaanza kufanyiwa ukarabati katika awamu ya kwanza na sasa kinatoa pia programu ya VETA kwa maana kwamba, vyuo ambavyo viko kwenye Wilaya ambako hakuna vyuo vya VETA, vyuo hivi vya Maendeleo ya Wananchi vimekuwa vikitoa programu ya VETA. Kwa hiyo, Chilala ni miongoni mwa vyuo ambavyo tayari viko kwenye programu ya ukarabati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa VETA tumetenga Tsh. Bilioni 1.8 na siyo Bilioni 1, ni shilingi Bilioni 1.8 kwa hiyo mara mtakapotupitishia tutaendelea na ukarabati wa vyuo hivi ikiwa ni pamoja na chuo cha Chilala.

SPIKA: Haya, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu, kwa niaba yake Mheshimiwa Rage.
Na. 54

Mpango wa Kufufua Ginnery ya Manonga

MHE. ISMAIL A. RAGE (K.n.y. MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU) aliuliza:-

Kati ya miaka ya 1960 hadi 1980, *Ginnery* ya Manonga iliyopo katika eneo la Chama cha Nkola ilikuwa muhimu sana kwa wakulima wa Pamba wa maeneo ya Ngw'ambiti katika mikoa ya Shinyanga na Tabora. *Ginnery* hii ilibinafisiswa kwa wawekezaji binafsi ambao walifilisika na kuacha majengo na miundombinu yake inaoza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuifufua *Ginnery* hii ili kumwinua mkulima wa Pamba?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha kuchambua Pamba cha Manonga kwa muda mrefu kimesitisha shughuli za uchambuzi wa Pamba na hivyo baadhi ya mitambo ya kiwanda hicho kuchakaa na kuhitaji matengenezo makubwa au uwekezaji mpya ili kiweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakishauri Chama cha Ushirika Igembesabo kufanya mazungumzo na Kampuni ya *Rajan Metal Industries* ambayo ndiyo mmiliki halali wa kiwanda cha Manonga ili kiweze kurejeshwa tena kwa chama hicho au kuangalia uwezekano wa kuingia mkataba wa kukifufua kiwanda hicho kwa Maendeleo ya Wakulima wa Pamba wa wilaya za Igunga na Nzega.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhamasisha wawekezaji binafsi kuwekeza katika viwanda vya kuchambua pamba ili kuongeza thamani ya pamba na hivyo kuongeza ajira na bei ya pamba kwa wakulima.

Aidha, kwa sasa kuna viwanda vitatu vya kuchambua pamba mkoani Tabora ambavyo ni *Igunga Ginnery*, *Tabora Ginnery* na *Roko Investment Ginnery* ambavyo kimsingi vinatosha kuchambua pamba inayozalishwa katika Mkoa wa Tabora.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali ni kuendelea kuwapatia wakulima mbinu bora za kilimo ili waweze kuzalisha kwa tija na hivyo kuongeza uzalishaji utakaokidhi mahitaji ya viwanda vilivyopo.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Rage swali la nyongeza.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ambayo kwa kweli hayakuniridhisha hata kidogo na leo nimeamini kwanini wananchi wa mikoa inayolima pamba wanagombana na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *Rajan Metal Industries* baada ya kutaifisha imeshindwa kukifufua kile kiwanda na waliotoa idhini ya kutaifisha ni Serikali. Sasa wananchi watapata Mamlaka hayo wapi? Ushirika wa Igembesabo wana uwezo wa kifedha, wanachoomba, kwa kuwa huyu mwekezaji ameshindwa na wala hayuko huko kwenye kiwanda. Je, Serikali inaweza ikaingilia wakakabidhiwa wananchi wenyewe?

Mheshimiwa Waziri umepewa taarifa ambayo siyo sahihi, *Tabora Ginnery* haifanyi kazi. Kwa hiyo, iko haja ya kuhakikisha kiwanda hiki kinafunguliwa na kijiografia kiko katikati ya Tabora na Shinyanga.

Kwa hiyo, wanaofaidika zaidi ni wananchi wa mikoa yote miwili na siyo mkoa wa Tabora peke yake.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Ismail Rage, kama ifiatavyo.

Mheshimiwa Spika, hili suala la *Ginnery* ya Manonga linaeleweka na kwamba, Igembesabo wenyewe waliishakuja pale Wizarani, (Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika) na kwa sababu kile kiwanda kiliishabinafsishwa na ubinafsishaji ule ulifanywa katika utaratibu wa kisheria, utaratibu wa kawaida, tulichofanya sisi ni kwamba tuliwasiliana na mwekezaji yule Rajan na tukamwambia nia ya Igembesabo kumiliki tena kile kiwanda ili kuwa na uzalishaji pale.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa namna ilivyokuwa makubaliano yaliyokuwepo pale, ni kwamba tuliwashauri pande zote mbili husika kwa maana ya mwekezaji na *ginnery* inayotaka, kukaa na kuzungumza nao, wafanye mawasiliano na sisi Serikali tungeratibu mawasiliano yale, ili uzalishaji pale uendelee.

Sasa nimepata mtihani kidogo kwa sababu sikujua kama Igembesabo walikuja wakawasiliana nao au hawakuwasiliana nao, lakini kama hawakuwasiliana basi Serikali iliishatoa fursa ya kuzikutanisha pande zote hizi mbili ili jambo hili lipate muafaka.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika majibu ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba uzalishaji na uwepo wa *ginnery* Tabora ulikuwa unaendana pia na uzalishaji wa pamba pale.

Kwa hiyo, mambo hayo yote Serikali ilizingatia lakini bado tulifungua njia kwa pande zote mbili na Rajani alituhakikishia kwamba, angewasiliana nao na Igembesabo pia tukawaambia kwamba, wangekutana na wawasiliane na kama ingehitajika kupatikana mtu wa katikati kuwawezesha kuzungumza Serikali ingefanya hivyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Eenh! Ahsante sana, naona kiwanda ndiyo hicho. Sasa tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Joshua Samweli Nassari atauliza swali hilo, kwa niaba yake nani atamwulizia? Mheshimiwa James Mbatia.

Na. 55

Bei ya Miche ya Kahawa

MHE. JAMES F. MBATIA K.n.y. (MHE. JOSHUA S. NASSARI) aliuliza:-

Kumetokea mkanganyiko wa bei ya miche ya Kahawa ambapo Halmashauri ya Meru imesema bei imepanda kutoka shilingi 100 hadi 250 na Kituo cha Utafiti cha Umbwe kikasema bei imepanda kutoka shilingi 250 hadi shilingi 500.

(a) Je, bei halisi ya miche wa Kahawa ni kiasi gani kufuatia mkanganyiko huo toka taasisi hizo za Serikali?

(b) Je, ni kweli kwamba Serikali imetoa ruzuku kwa Wakulima wa Kahawa katika miche hiyo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, Mbunge wa Arumeru Mashariki, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Miche ya Kahawa inayozalishwa na Kituo cha Utafiti wa Kahawa *Tanzania Coffee Research Institute (TaCRI)* kwa bustani mama za kuendeleza uzalishaji wa miche ya Kahawa inapata ruzuku ya asilimia 100 na hivyo hailipwi. Hata hivyo, miche ya kahawa inayopelekwa shambani kwa wakulima kwa ajili ya kuzalisha kahawa ina ruzuku ya asilimia 70 na inauzwa kwa Tsh. 300/=.

Mheshimiwa Spika, bei ya Tsh. 300 kwa miche ya Kahawa ilitokana na azimio la wadau wa kahawa lililopitishwa kwenye mkutano wa nne wa wadau wa kahawa uliofanyika mjini Morogoro Mei, 2013 ambapo wadau waliridhia kuwa bei ya miche iwe ni shilingi 300. Aidha, gharama ya kuzalisha mche mmoja wa kahawa kwa sasa ni shilingi 1,000/=.

(b) Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2007, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku kwa kituo cha Utafiti *TaCRI* ili kusaidia uzalishaji wa miche bora ya kahawa na kituo cha *TaCRI* kimekuwa kikitumia ruzuku hiyo ili kuzalisha na kusambaza miche bora ya kahawa hapa nchini na kuendelea kuwezesha wilaya na wakulima kuzalisha miche bora ya kahawa wenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 Serikali ilitoa kiasi cha shilingi milioni 200 kama ruzuku ya kuzalisha na kusambaza miche, mwaka 2012/2013 Serikali ilitoa ruzuku ya shilingi milioni 100 ili kuzalisha miche ya aina bora ya kahawa na katika mwaka wa 2013/2014 Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 400 kama ruzuku ya kuzalisha na kusambaza miche bora ya kahawa kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa wito kwa halmashauri zote nchini zinazolima kahawa ikiwemo Halmashauri wilaya ya Meru kuchangia angalau asilimia 20 ya mapato yatokanayo na kahawa ili kusaidia uendelezaji wa zao la kahawa kwenye halmashauri zao.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mbatia swali la nyongeza.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa zao la kahawa ni zao mojawapo ambalo linaiingizia nchi yetu fedha za kigeni na kwenye usambazaji wa miche hii Halmashauri ya Meru kituo kiko pale Tengeru, mche mmoja wakulina wanauziwa shilingi 500 badala ya shilingi 300.

Je, Serikali inaweza ikatoa kauli hapa kwa Halmashauri ya Meru na halmashauri nyingine zote nchini ili miche hii iwe shilingi 300 badala ya shilingi 500 ambayo ni bei ya ulanguzi?

Pili, kwa kuwa zao hili sasa hivi hawatoi baki, nyongeza na hali ya wakulima inasuasua, ili kuwapa motisha na uwezo wa kuliendeleza zao hili, fedha za kigeni tunazozipata kwa nini Serikali isione uwezekano mkubwa zaidi wa kutoa motisha zaidi kwa wakulima kote nchini ili zao hili liendeleo kuongeza fedha za kigeni?

Pia ni zao la ngapi kwa kuingiza fedha za kigeni hapa nchini?

SPIKA: Umeuliza maswali mangapi? Maana naona yamo mengi tu! Naomba Mheshimiwa Waziri ujibu mawili tu unayopenda.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa James Mbatia, Mbunge wa Kuteuliwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimeishasema hapa kwamba katika mkutano wa nne wa wadau wa kahawa uliofanyika Morogoro Mei, 2013 wadau waliazimia kwamba, bei ya mche mmoja iwe shilingi 300.

Mheshimiwa Spika, ilivyokuwa tangu mwanzo na tumesema hapa gharama za kuzalisha mche mmoja wa kahawa kwa maana ya gharama ukiacha ile mifuko inayotumika, udongo na utalam ilikuwa inafika shilingi 1000. Lakini tukaona kwamba ni gharama kubwa sana. Kwa hiyo, katika kikao cha wadau mwaka 2012 Morogoro bei ile ikapunguzwa kwa asilimia 50, ikawa shilingi 500.

Lakini bado tukaona ni gharama zaidi kwa mwananchi huyu na mwaka 2013 kwa maana ya kikao cha wadau kilichofanyika mwaka jana Mjini Morogoro tena, tukapunguza tena kutoka shilingi 500 kwenda shilingi 300 na hivyo ndivyo tunavyofanya mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, kama kuna Halmashauri na kwa maana ya vituo vya *TaCRI* nchini vinauzi kahawa hii kwa shilingi 500, hayo ni makosa na ninaomba nitumie nafasi hii kuagiza kwamba miche hiyo inayozalishwa na vituo vya *TaCRI* nchini kote iuzwe kwa hilingi 300 tu.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba tu niseme kwamba, wako wazalishaji binafsi ambao hatuwezi kuwaingilia ambao wanazalisha wenyewe na anauza na hao wanauza kati ya shilingi 500, 600 mpaka 800. Sasa kama kuna mkulima ambaye atapenda kwenda huko hiyo hatuwezi kuzuia. Ingawa naomba niseme kwamba mimi natoka Mbozi na pale nimekwenda kituo cha *TaCRI*, nimetembea pale miche iko mingi na wakulima wengi hawawezi hata kuinunua yote kwa shilingi 300.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kwa hiyo, wakulima wasifungwe, kama wako wakulima wa Mbinga au wapi, wako huru kwenda hata Mbozi kule kuchukua miche ya kahawa kwa bei ya shilingi 300 ili waweze kuzalisha.

Mheshimiwa Spika, sasa swali la pili Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba, hakuna mabaki au nyongeza na kwa maana hiyo ni kama vile mkulima huyu hana motisha.

Mheshimiwa Spika, hii yenyewe ya kupunguza miche ya kahawa kutoka shilingi 1000 kwa bei ya uzalishaji kwenda shilingi 300 ni motisha tosha kabisa kwa maana ya kumfanya huyu mkulima aweze kuzalisha.

Lakini pia sasa hivi tuna teknolojia ya kisasa kabisa ya kukoboa ile kahawa ambayo tunauzia wananchi zile *Central Pipers Units (CPU)*, tunawauzia kwa bei kimsingi ambayo tayari ina punguzo kubwa, ambayo kama mwananchi mwenyewe angeweza kununua basi angenunua kwa bei kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, yote hii ni motisha na mimi naomba nitoe rai kwa wakulima pia waweze kuendelea kutumia hizi CPUs kama sehemu ya kuboresha kahawa ambayo wakienda sokoni itakuwa na bei kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Mngodo swali la nyongeza.

MHE. REBECA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, tangia nchi yetu ipate uhuru bei ya zao la kahawa imekuwa ikipangwa na walaji (Watu wa Ulaya) kitu ambacho kimetufanya sisi Watanzania tuwe chini ya kongwa la Uhuru Mamboleo.

Ni lini sasa sisi tutaweza kujikomboa na kusimama wenyewe na kuweza kupanga bei katika hilo soko la dunia?

SPIKA: Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rebeca Mngodo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kuwaaminisha watanzania kwamba bei ya kahawa inapangwa na wazungu na watu wengine kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba ni vizuri Wabunge tuwe na taarifa kamili juu hili, kinacho-*determine* bei ya mazao yote ni soko la dunia, ndicho kinacho-*determine* bei ya mazao. Naomba niwaeleze kwamba, tunayo Bodi ya kahawa na kwa kweli tunazo Bodi mbali mbali kwenye mazao haya makuu na Bodi hizi ndizo husimamia kuona kwamba, mkulima huyu hapunjwi.

Mheshimiwa Spika, naomba niwaeleze Waheshimiwa Wabunge kwamba, jana usiku nilikuwa nazungumza na Mkurugenzi Mkuu wa TCB Ndugu Kumburu, kwamba wananchi wamekuwa wanalalamikia bei ya zao la kahawa, mnachukua hatua gani ili kuhakikisha mwananchi anaelewa namna ambavyo bei za kahawa na mazao mengine zinapangwa?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Ndugu Kumburu, Mkurugenzi wa TCB amenihakikishia kwamba, msimu unapoanza moja huwa wanaangalia soko la kahawa la dunia. Ndilo hilo wanatangaza na mambo haya yako kwenye mtandao, hakuna mtu ambaye anaweza akasema kwamba leo anakuja anawapangia Watanzania kwamba kahawa watauza kiasi gani. Hata hivyo, kimsingi niseme kinacho-*determine* bei ya kahawani bei katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niseme kwamba kahawa yetu imekuwa inalalamikiwa sana kwamba mazingira ya utayarishaji wa kahawa siyo mazuri, kwa hiyo ikienda kwenye soko wale waonjaji wakiona *taste* yake siyo nzuri, bei ya kahawa itakwenda chini. Kwa sasa hivi kahawa ina *grade* kama 16.

Kwa hiyo, tunapenda tuwahusie wakulima wafanye usafi zaidi kwenye kahawa yao ili tupunguze zile *grade* walau zifike Tisa au Kumi. Kwa maana hiyo kahawa yetu itakuwa na bei nzuri zaidi kwenye soko la dunia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Swali linalofuata Namba 56, nadhani kulikuwa na kujikanganya, maana yake linasema Wizara ya Kazi na Ajira. Lakini mnajua walemavu wako Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Kwa hiyo, kutokana na kuchanganyana huko jibu halijapatikana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mkanga, tutaleta jibu baadaye kwa leo hakuna jibu. Tunaenda Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, atauliza swali hilo.

Na. 57

Viwanda Vya Maji Zanzibar

MHE. YAHYA KASSIM ISSA aliuliza:-

Huko Zanzibar kuna viwanda vya maji safi na salama na vinazalisha maji mazuri kuliko haya yanayozalishwa kwenye viwanda vya Tanzania Bara na maji haya yanayozalishwa kwenye viwanda vya Tanzania Bara yanauzwa Zanzibar lakini maji yanayozalishwa na viwanda vya Tanzania Zanzibar hayauzwi Tanzania Bara.

- (a) Je, kuna siri gani katika utaratibu huu wa biashara ya maji?
- (b) Je, Serikali inatoa kauli gani, kwa nini maji ya Tanzania Zanzibar hayauzwi Tanzania Bara?
- (c) Je, Serikali haioni kuwa baadhi ya viwanda Tanzania Bara vinatoa maji yasiyo na ladha na Serikali inachukua hatua gani?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali haina siri yoyote kuhusu biashara ya maji Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Aidha, Viwanda vya maji vya kunywa vilivyosajiliwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, vinatakiwa kuzalisha maji safi na salama kutokana na Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009 mbayo inazuia mtu au kiwanda chochote kuzalisha na kuuza bidhaa zisizo na ubora unaotakiwa.

(b) Mheshimiwa Spika, pande zote mbili, yaani Tanzania Bara na Zanzibar zina haki ya kufanya biashara ya maji safi bila kubughudhiwa na mamlaka yoyote inayosimamia biashara nchini. Hadi sasa kuna viwanda takribani 32 vinavyozalisha na kuuza maji Tanzania Bara na kati ya hivyo viwanda vitatu (Uhai, Kilimanjaro na *Cool Blue*) vinauzi maji yake Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kati ya viwanda Sita vinavyozalisha maji ya kunywa Zanzibar, kiwanda cha *Zainab Bottlers Company Limited*, kinatarajiwa kutoa ushindani mkubwa Tanzania Bara kwani baada ya miezi miwili kuanzia sasa kiwanda hiki kitaanza kuuza maji yake Tanzania Bara baada ya kujimarisha. Aidha, kiwanda cha *Zan Bottlers Ltd.* Kimeishanunua mashine za kutengeneza chupa tupu ili kupunguza gharama za uzalishaji na baadaye kuanza kuzalisha kwa ajili ya kuuza Tanzania Bara.

(c) Ladha ya maji inatokana na mchanganyiko wa madini yaliyoko ndani ya maji ambayo ama yanatokana na uhalisia wa maji yenyewe au kuongezwa wakati wa uzalishaji kiwandani. Aidha, viwango vya maji vinazingatia pamoja na mambo mengine, mchanganyiko unaotakiwa wa kemikali zilizomo kwenye maji. Hivyo, ladha ya maji si kigezo pekee kinachoweza kuonesha kuwa maji hayo yana ubora na ni salama kwa matumizi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maji ya kunywa yanayozalishwa Tanzania Zanzibar yanakidhi viwango vya ubora, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wenye viwanda vya maji Tanzania Zanzibar hawana kizuizi chochote kuuza bidhaa Tanzania Bara kwani Tanzania ni moja na kila mwenye biashara yake anaweza kuuza popote ili mradi bidhaa yenyewe ni bora na inakubalika katika soko husika.

Mheshimiwa Spika, Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Yahaya Issa, swali la nyongeza.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, kuna kijana wakati wa sherehe huku Tanzania Bara alichukua maji na akazuiliwa bandarini na kwa kuwa mimi binafsi baada ya kupata maelezo haya nilichukua maji kutoka Zanzibar nikaja nayo Tanzania Bara na nilipata vikwazo pale lakini baada ya mahojiano makubwa nikaachiliwa.

Je, huoni kwamba hii ni kasoro kubwa na kuona kwamba kitendo cha maji kuzuiliwa maji ni cha kweli?

Swali la pili, ikiwa alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, ndivyo ilivyo.

Je, Waziri anatoa kauli gani kwa Serikali kutokana na sehemu zote husika?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Umeyaelewa hayo maswali? Mimi sijaelewa.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara...

SPIKA: Ngoja kwanza! Mheshimiwa Yahya ulichukua chupa ngapi?

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Spika, chupa 40. (Makofi)

SPIKA: Ulikuwa unafanya biashara? (Makofi/Kicheko)

Haya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NABIASHARA: Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama kuna aliyezuiliwa kuingia na maji Tanzania Bara pamoja na kwamba sifahamu sababu hasa zilizotumika, lakini kama ni kwa masuala tu ya kuyaingiza nchini kwa ajili ya matumizi nafikiri kulikuwa na kasoro, haikupaswa kuwa hivyo. Kwa hali hiyo basi, nitamke tu kuwa bidhaa yoyote ile ambayo imethibitishwa kuwa inafaa kwa matumizi ya wanadamu inaruhusiwa kuingia upande wowote ule wa Tanzania kama ni kutoka Tanzania Bara kwenda visiwani au kutoka Visiwani kuja Bara, ili mradi sheria za nchi hazivunjwi.

Mheshimiwa Spika, nataka tu niongezee kwamba tuna maji yanayotumika kwenye masoko, yametoka Ulaya, kuna *Eviane Water* na maji ya aina nyingi tu ambayo yanaingizwa nchini ilimradi yakiishathibitishwa kuwa yana usalama unaotakiwa na viwango vinavyotakiwa kwa sababu soko ni huria dunia nzima hayazuiliwi, sembuse iwe Zanzibar?

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, ni kwanini Waziri asitoe kibali kwa Wazanzibari kuuza mchele na nyama Tanzania Bara kwa kuwa Tanzania Bara wanauza mchele na nyama kwa wingi Zanzibar na kusababisha wafugaji na wakulima wa Zanzibar kukosa soko na kufanya hali zao za kiuchumi kuwa duni? (Kicheko/Makofi)

SPIKA: Maji na mchele wapi! Maji na mchele wapi? Haya ili mradi mchele unapikwa kwa maji, labda namna hiyo, hebu jibu. (Makofi/Kicheko)

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NABIASHARA: Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa maji naamini hata kwa mchele na bidhaa nyingine yoyote kama imethibitishwa ubora na haina matatizo sidhani kama kuna kikwazo. Nyama usafirishaji wake unasimamiwa na taratibu za kisheria ambazo zinaangalia usalama, mchele halikadhalika. Kama Zanzibar wana nyama ya kutuletea Bara basi wanakaribishwa na kama wana mchele vilevile tunapenda kuuona. (Makofi)

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usalama Kazini (*Industrial Safety Ordinance*) inamtaka mwajiri kumpatia mfanyakazi wake vifaa kwa ajili ya kulinda afya yake. Kwa nini hawa watu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wenye viwanda vya maji hawawezi kuwapatia wale watu wanaokota chupa kwa ajili ya kuzifanyia *recycling* maana wanaokota kwenye majalala bila *gloves* wala *musks* kwa ajili ya kuzuia harufu na kadhalika. Kwanini Serikali haijachukua hatua kuwalinda watu wa aina hii?

SPIKA: Pamoja na kwamba swali linahusika na maji, lakini hili ni lingine kabisa. Maana hapa ni kuondoa uchafu mitaani. Haya kwa sababu suala lenyewe ni muhimu kwa sababu hata kutupa chupa hovyoye kwenyewe ni kosa. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, nafurahi kuwa nimepokea swali kutoka kwa Mheshimiwa Aliko Kibona. Naomba nijaribu kulijibu kama ifuatavyo:-

Kuna utaratibu ambao unapaswa kuzingatiwa na wenye viwanda wakati wa uzalishaji na huo unatumika pale tu pale ambapo zile bidhaa ziko kiwandani. Hawa wanaoenda kuokota chupa barabarani wanasimamiwa na Manispaa na wale wanaosimamia usafi kwa ujumla. Kwa hiyo, sitegemei mtu wa kiwanda aanze kwenda barabarani kuwavalisha watu *gloves* au *gears* za kujikinga. Lakini nafikiri ni jukumu la Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa watu wanaofanya vitu kama hivyo kwenye mitaa yao wanasaidiwa au kuelekeza ipasavyo.

SPIKA: Naomba tuendelee na swali linafuata, Wizara ya Maliasili. Mheshimiwa Mariam Msabaha, atauliza swali hilo.

Na. 58

Kubomolewa kwa Majengo ya Kale Bagamoyo

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA aliuliza:-

Bagamoyo ni Mji Mkongwe na ni moja ya kati ya vivutio vya watalii hapa nchini, lakini kumekuwepo na tatizo la kubomolewa kwa majengo ya kale na kujengwa kwa majengo mapya ya kisasa:-

- (a) Je, Serikali haioni kubomolewa kwa majengo ya kale kunaweza kuathiri sekta ya utalii?
- (b) Je, ni lini Serikali itakarabati hayo majengo ya kale kama dhamira ni kukuza na kuendeleza sekta ya Utalii nchini?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Wizara inakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge kuwa kubomoka kwa majengo ya kale kunakotokana na uchakavu na kuzeeka kunaweza kuathiri sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeona na kutambua changamoto za kuendelea kuchaa kwa majengo ya kihistoria na kuanza kuchukua hatua. Wizara ilikutana na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya tarehe 8 Februari, 2014 ili kuona namna ya kukabilina na changamoto hii. Kutokana na mkutano huo, pamoja na mambo mengi ilikubaliwa kuwa Wizara kwa kushirikiana na watalaam wa Halmashauri wabaini umiliki na hali ya uhifadhi wa majengo yote

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

ya kihistoria ndani ya mji mkongwe. Kazi ambazo Wizara imepanga kuzitekeleza katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 zikamilishwe.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha Wizara imeanza na ukarabati wa makaburi ya Mwanamakuka na itaendelea na ukarabati wa gofu la Mgonera ambao unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2014. Aidha, tunaendelea kuwashawishi wadau wanaomiliki majengo ya kale kuyahifadhi na kuyakarabati kwa kwa kuzingatia sheria na kanuni na miongozo. Wizara kwa kushirikiana na watalaam wa Halmashauri imeanza kubaini kubaini umiliki na hali ya uhifadhi wa majengo ya kihistoria ndani ya mji mkongwe, kazi inayotarajiwa kukamilika katika mwaka huu wa fedha. Ukamilishaji wa kazi hiyo utajenga msingi wa kuandaa mkakati wa muda mrefu wa kuhifadhi, kuendeleza na kukarabati majengo yaliyomo katika mji wa kihistoria wa Bagamoyo.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Spika, asante. Kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri yenye mshiko. Kwa kuwa ambao wananunua majengo ya mji mkongwe Bagamoyo ni wafanyabiashara na hawa wamekuwa hawafuati sheria ya kujenga majengo kama yale waliyobomoa.

Je, Serikali ina mikakati gani kuwadhhibiti na kuchukua hatua za kisheria endapo watakiuka kujenga majengo haya kwa ramani wanazozitaka wenyewe? Swali la pili; hamuoni sasa kuna umuhimu wa kutoa elimu kwa wakazi wa Bagamoyo waliozungukwa na hifadhi hizi za majengo ya kale ili kujua namna ya kutunza majengo haya?

SPIKA: Ahsante sana kwa kuuliza maswali *direct!* Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Msabaha kwamba yeyote anayemiliki majengo ambayo yako kwenye hifadhi hizi hawaruhusiwi kufanya hivi mpaka wapate kibali kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mambo ya Kale pale Wizarani. Kwa hiyo hata mtu yeyote kama anaendelea bila ruhusa ya kibali chetu atakuwa anakiuka sheria, kwa hiyo hatua za kisheria zinatakiwa zichukuliwe dhidi yake. Kuhusu suala la kutoa elimu, ni kweli Wizara tumejiandaa na tumekusudia kutoa elimu na tumejipanga vizuri katika eneo hilo. Kwa kuanzia tu, safari hii Wizara ilitenga jumla ya shilingi 154,000,000/= kwa ajili ya kushughulikia majengo yaliyopo katika eneo hili la Bagamoyo. Nataka nimhakikishie tu kwamba Wizara tumejipanga na tutaendelea kutoa elimu katika hilo.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona.

Waziri anasema wanabomoa majengo na kukarabati makaburi, *that's very funny!* Kwa sababu hii tabia ya kubomoa majengo ya kale imekuwa inaendelea sana siyo tu Bagamoyo, siyo tu Mji Mkongwe, hata Dar es salaam. Siku moja napita maeneo ya Samora nikakuta yale majengo ya Mjerumani yaliyojengwa mwaka 1902, 1907, yanabomolewa. Nikiwa kama Waziri Kivuli wa Utamaduni nilisikitika sana kwamba hii nchi inakwenda wapi. Mheshimiwa Waziri ni lini mtakoma sasa kubomoa majengo hayo ili kuhifadhi utamaduni na historia ya nchi yetu Tanganyika? *(Makofi)*

SPIKA: Nchi Tanganyika ilikuwa ya mkoloni! Mheshimiwa Naibu Waziri majibu! *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTAMADUNI: Kwanza naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Naomba atambue kwamba siyo majengo yanamilikiwa na Serikali, kuna baaadhi tunamiliki kama Serikali na kuna baadhi yanamilikiwa na watu binafsi. Kwa hiyo maamuzi ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

matumizi yale sisi kama Serikali hatunayo *direct*. Lakini nimemwambia na kumthibitishia kwamba kutokana na Sera ya Malikale ya mwaka 2008 na Sheria Na.333 ya Mambo ya Kale, sisi kama Serikali tumetoa *directives* na mwongozo kwamba mtu yeyote haruhusiwi kuliendeleza au kulibomoa jengo lake nje ya utaratibu, na sisi kama Serikali hatubomoi majengo wala hatujengi makaburi, tunakarabati makaburi ambayo yako kwenye *history*.

SPIKA: Ahsante, tunaendelea. Inatakiwa watu wasimame wakati wanapoanza. Mheshimiwa Jasson Rweikiza atauliza swali hilo.

Na. 59

Uhitaji wa Chuo cha Ufundi Bukoba Vijijini

MHE. JASSON S. RWEIKIZA aliluliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga chuo cha Ufundi katika Wilaya ya Bukoba Vijijini ili vijana wapate Ufundi Stadi mbali mbali kwa faida yao na taifa kwa ujumla?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 – 2010, Serikali inaendelea na azma yake ya kujenga vyuo vya ufundi stadi nchini kwa awamu.

Aidha Serikali itajenga chuo cha ufundi stadi katika Wilaya ya Bukoba Vijijini baada ya kukamilisha ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi katika Wilaya ambazo ujenzi wake upo katika awamu mbili zilizotangulia.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Bukoba Vijijini ni moja kati ya Wilaya ambazo Serikali imejipanga kuzifanyia uchambuzi wa stadi zinazohitajika katika mkakati wa uanzishaji wa chuo cha ufundi stadi.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi haja ya sasa ya wananchi wa Bukoba Vijijini kupatiwa mafunzo ya ufundi stadi, Serikali inawashauri wana-Bukoba Vijijini kutumia Chuo cha Ufundi Stadi cha Kagera VTC kilichopo Bukoba Mjini, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Lubondo kilichopo Bihalamulo na Gera kilichopo Misenyi na vyuo vingine vinavyotoa mafunzo ya Ufundi Stadi ambavyo vimesajiliwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ili wananchi waweze kupata stadi mbalimbali. *(Makofi)*

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu aliyotoa, ingawaje suala hili limezungumziwa mara kwa mara hapa Bungeni na tumeliongea mara nyingi na wananchi wa Bukoba wanaona kama vile Serikali inawadanganya kwa sababu katika ilani ya CCM ni lengo la Serikali kujenga chuo cha ufundi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

katika kila Wilaya, na hakuna jitihada zozote ambazo zimeonekana kule Bukoba za chuo hiki kujengwa. Je, wananchi waone kama wanadanganywa na Serikali?

Swali la pili, pale Bukoba tuna Chuo cha Ufundi (CHACHAWATA) cha walemavu kule Kakarubale. Sasa hakifanyi kazi ingawaje kina majengo ya kutosha, kina vifaa vya kutosha na miundombinu mingine. Hakifanyi kazi kwa sababu hakina fedha.

Je, Serikali haioni kwamba ingekuwa busara kusaidia wananchi wa Bukoba chuo hiki kipewe fedha na kianze kutoa huduma ya mafunzo kwa vijana walemavu na wasiokuwa walemavu? Waziri yuko tayari kwenda na mimi kule tukiangalie halafu tukipatie fedha chuo hiki?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nicukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Rweikiza kwa sababu kwa kweli juhudi zake ni za wazi katika kuhamasisha mafunzo haya ya elimu ya Ufundi Stadi nchini. Ninampongeza sana na ninamwomba aendelee na juhudi hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza la nyongeza Mheshimiwa Rweikiza amekuwa akituhumu Serikali kwamba Serikali imewadanganya wananchi. Mheshimiwa Spika, lakini naomba niwape taarifa Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali imetekeleza azma yake hiyo. Kama nilivyosema imepanga mkakati wa ujenzi wa vyuo hivi katika awamu kulingana na vipaumbele na tafiti ambazo zimekwishakufanywa katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tayari Serikali imeishakamilisha ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi Wilaya ya Makete, tayari imeishaanza kufanya stadi kwa ajili ya kujenga Chuo cha Elimu ya Ufundi Stadi katika Wilaya ya Rudewa, Wilaya ya Namtumbo, Wilaya ya Kilindi, Wilaya ya Chunya, Wilaya ya Ukerewe. Kwa hiyo si sahihi kwamba Serikali inawadangaya Watanzania. Serikali iko makini na inatekeleza ahadi yake.

Mheshimiwa Spika, lakini katika hili la pili, Mheshimiwa Mbunge ameniomba na kuitaka Serikali ione uwezekano wa kushirikiana na chuo cha walemavu alichokitaja ambacho kiko hapo Bukoba Vijijini. Naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwanza niko tayari kuongozana naye na tutakwenda pamoja kukagua chuo hicho ili kuweza kuishauri Serikali namna gani tunaweza kufanya yeye pamoja na sisi tutakubaliana.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahamasishe wananchi wa Bukoba Vijijini Chuo hicho kwa kuanzia ili kurahisisha kazi hii wakimiliki wao wenyewe na kwa kuwa VETA ina utaratibu wa kufanya shughuli kwa pamoja na *private sector*, tuna uwezo wa kuwaunganisha lakini chuo kikianza katika umiliki wa mikono ya wana Bukoba Vijijini.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kuwahimiza sana Watanzania kuwapeleka watoto wao kujunga na vyuo hivyo kwa sababu nafasi tulizonazo katika vyuo vya ufundi stadi nchini ni takribani 41,472 lakini watoto wetu wanaosoma katika vyuo hivyo ni takribani 24,000 tu, ni kama 59% tu ndiyo wanaojiunga na vyuo hivyo na nafasi nyingi katika vyuo vilivyojengwa hazifanyiwi kazi. Kwa hiyo, tuhamasishane ili nafasi zilizopo pia ziweze kutumika vizuri.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Mabumba.

Kuwapatia Watanzania Mafunzo ya Elimu ya Ufundi

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA aliuliza:-

Ili Tanzania iweze kunufaika na fursa zilizopo za kiuchumi na kijamii, inahitaji kuwaandaa Watanzania kwa kuwapatia Elimu ya Ufundi (*Vacational Skills*) ili wawe na uwezo wa kuvumbua vitendea kazi ambavyo vitasaidia utendaji kazi kuwa mwepesi na wenye tija kwa Taifa.

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kufanikisha azma hiyo?
- (b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwatumia ipasavyo wataalam waliopo sasa?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sylvester Masele Mabumba, Mbunge wa Dole, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza uvumbuzi wa vitendea kazi na kuleta tija katika uzalishaji mali na kuongeza pato la Taifa, Serikali imekuwa ikivitumia Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi vya Serikali na visivyo vya Serikali kuwapatia wananchi ujuzi katika fani mbalimbali. Aidha, Serikali ina mkakati wa kuwa na vyuo vya Elimu ya Ufundi Stadi katika kila Wilaya ili kuongeza fursa za kuandaa Watanzania wengi kupata ujuzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mafunzo ya Stadi, VETA, inatekeleza programu ya kutoa mafunzo kwa wataalam sehemu za kazi ijulikanayo kwa Kiingereza *skills enhancement program*. Programu hii inaendeleza ujuzi wa wataalam wetu mahali pa kazi ili kuwawezesha kuwa mahiri katika utafiti na uvumbuzi. Aidha, Serikali imeweka mazingira wezeshi ambayo yanawawezesha wataalam wetu kubuni na kuvumbua vitendea kazi ambavyo vinasaidia utendaji wa kazi kuwa mwepesi na wenye tija kwa Taifa. Kwa mfano, wataalam wa Chuo cha Ufundi Arusha wametengeneza mashine za kuhamishika za kupukuchukua mahindi na kupanga mahindi hayo kimadaraja zijulikanazo kama *mobile maize and sheller and sorting*. Vilevile kupitia Chuo cha Teknolojia Tanzania Dar es Salaam kimewatumia wataalam wake kutengeneza taa za kuongozea magari barabarani katika Jiji la Dar es Salaam.

SPIKA: Swali la nyongeza Mheshimiwa Mabumba!

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA: Naipongeza Serikali kwa majibu yake lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza moja. Kwa kuwa tunao wavumbuzi wengi lakini ambao kwa bahati mbaya hawana mitaji, Serikali ina mpango gani sasa wa kuwakusanya na kuwapatia mitaji ili waweze kuendeleza kazi hizi njema ambazo hatimaye zitasaidia kurahisisha maisha ya Watanzania?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa katika siku za karibuni kumetokea utengenezaji wa silaha haramu kama mabomu na magabore ambayo kwa bahati mbaya yametumika kuathiri maisha ya Watanzania. Je, Serikali ina mpango gani kuwakusanya hawa wanaofanya uvumbuzi wa mabomu haramu wakapewa ujuzi na kutengeneza silaha ambazo hatimaye Tanzania inaweza kuwa ni nchi inayoongoza kwa kuuza silaha nje ya nchi yetu? Ahsante.

SPIKA: Haya Mheshimiwa Naibu Waziri, magobore.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa sasa Tanzania imeendelea kuwa na wavumbuzi wengi ambao wamekuwa wakivumbua zana nyingi mbalimbali ambazo zinaweza kuleta tija na kurahisisha kazi katika nchi yetu ya Tanzania.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme Serikali yetu kwa kuona umuhimu wa uvumbuzi katika nchi yetu ya Tanzania, mwaka 1986 ilitunga Sheria ya Bunge ya kuanzisha Tume ya Sayansi na Teknolojia na Tume hiyo ya Sayansi na Teknolojia kazi yake kubwa ni kufanya *promotion* hiyo ya teknolojia mbalimbali ambazo zimekuwa zikibuniwa na Watanzania ili kuweza kuleta tija katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, naomba kwanza niwashauri Watanzania wale wote ambao wameweza kugundua zana mbalimbali zenye kuleta tija, wawasiliane na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania hiyo ambayo ilianzishwa 1986 kwa Sheria za Bunge ili watambulike lakini wakishatambulika, Tume hiyo sasa ina kazi pia ya kuendeleza uvumbuzi huo kwa kuwapa mitaji na kuboresha uvumbuzi wao uweze kufanya kazi zinazohitajika katika nchi yetu ya Tanzania ipasavyo kwa wakati unaohitajika na kwa tija tunayohitaji. Kwa hiyo, hayo yanafanyika kabisa kupitia mipango hiyo na taasisi mbalimbali ambazo tunazo katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, Mheshimiwa Mbunge amesema kumekuwepo na ugunduzi wa kutengeneza silaha ambazo zinatumiwa isivyo halali wakati mwingine. Suala hili ni suala la kiulizi na usalama katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, siyo suala la kulishabikia tu harakaharaka watu hawa wawezeshwe ili waweze kutengeneza bila kuweka utaratibu unaotakiwa. Kwa maana hiyo, wagunduzi hawa kama wapo, ninaomba vyombo vinavyohusika kuanzia Kamati zetu za Ulinzi na Usalama maeneo mbalimbali ziwatambue ili kuhakikisha kwamba ugunduzi huo unaendana na sheria za nchi yetu na ili uwe ni ugunduzi wa kuleta tija na siyo kuvuruga amani na usalama katika nchi yetu ya Tanzania.

SPIKA: Ninaona muda umeisha na maswali yenyewe yameisha, tuendeleo kwenye hatua nyingine.

Niwatambue wageni ambao tunao humu ndani, tuna wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Nyalandu ambao ni Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Wakurugenzi Wasaidizi kutoka Wizarani wakiongozwa Katibu Mkuu, Bi. Maimuna Tarishi.

Wageni wengine ishirini na tatu ni Makatibu Kata kutoka Jimbo la Singida Kaskazini. Naomba hawa wageni wa Mheshimiwa Nyalandu, Makatibu Kata wasimame kama wapo. Nafikiri nafasi haijapatikana.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke kutoka Kasulu, wako pale wawili. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wa Mheshimiwa Charles Mwijage, anaitwa Christopher Kilaja asimame. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Vita Kawawa ambaye ni Makwaia wa Kuhenga, si tunamfahamu huyu? Ahsante, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Cyril Chami ambao ni wanafunzi tisini kutoka Imani *English Medium pre and primary school* na Walimu wao. Naomba hawa wasimame, mmependeza sana, karibuni na mfanye kazi ya kusoma vizuri. Wanaongozwa na Sister Hugolina Kimario, nadhani mnamuona, karibu sana Sister. *(Makofi)*

Tuna wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo, tunao wanafunzi mia moja kutoka Lukundo Sekondari ya Dodoma. Naomba wasimame walipo, ahsanteni sana, karibuni sana na msome kwa bidii. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo ya kazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba na nusu watakuwa na kikao chao Hazina Ndogo, namba 136.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Anna Abdallah, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana watakutana katika ukumbi namba 227.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Luhaga Mpina, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba kutakuwa na kikao cha Kamati pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Kikao hicho kitafanyika katika Ukumbi wa Hazina Ndogo Dodoma, namba 125.

Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Rajab Mohammed Mbarouk, anaomba niwatangazie Wabunge wa Kambi ya Upinzani Bungeni kuwa leo tarehe 14 kutakuwa na kikao kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa saa nane mchana. Kwa hiyo, Pius Msekwa kuna sekta mbalimbali, naomba mtumie lugha za Kibunge humu maana zingine huwa hatuelewi maana ukisema Mratibu ndiyo nani sasa? Kwa hiyo, nadhani kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Rajab anatangaza hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Katibu!

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015 Waziri wa Maliasili na Utalii

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ninapenda kumuita Mheshimiwa Rose Kirigini atafuatiwa na Mheshimiwa Mbatia na pia atafuatiwa na Mheshimiwa Lulida, hawa ndio wanaanza.

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kwanza kuweza kuchangia kwenye Wizara hii muhimu. Kwanza kabisa nianze kwa kuwapongeza Waziri na Watendaji wake wote kwa kazi ngumu na nzuri wanayoifanya kwenye Wizara hii. Mengi yamesemwa lakini mimi ninaomba niwape moyo kwamba pale unapofanya kazi nzuri basi utegeme madongo ni lazima yatakuwepo, naomba msife moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijielekeze kwenye tatizo la mipaka kati ya vijiji na Hifadhi za Taifa. Lipo tatizo kubwa sana kati ya mipaka na Hifadhi zetu za Taifa. Kwa mfano katika Wilaya yangu ya Meatu tunalo tatizo kubwa sana kati ya Kijiji cha Makao na Kijiji cha Kakesyo. Kwa maana hiyo kati ya Wilaya ya Meatu, Wilaya ya Ngorongoro au Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Ningemuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa aweze kuligusia hili kwamba kwa muda mrefu tumejaribu kutatua tatizo hili kama Wilaya na Wilaya lakini limeshindikana. Eneo letu la Wilaya limeingia kwenye Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa takribani kilomita za mraba 135. Siyo kwamba tunahitaji kama Wilaya eneo hili tuweze kulibeba kichwani au tulirudishe kwenye kijiji cha Makao, tunatambua kabisa umuhimu wa Mamlaka hii ya Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro, tunahitaji sasa yale mapato yanayotokana na Mamlaka ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro basi kwa zile kilomita 135 za Wilaya ya Meatu ambazo zinaingia katika mamlaka hii basi na sisi kama Wilaya tuweze kufaidika na mapato ya zile kilomita 135. Cha kusikitisha zaidi katika eneo lile la mgogoro kwenye zile kilomita 135, tayari wenzetu wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro wameanzisha *ranch* ya ng'ombe. Sasa ningetaka Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu atueleze *ranch* hiyo imeanzaanza vipi wakati kuna matatizo ya kimpaka kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizingumzie Hifadhi za Wanyamapori nikirejea kwenye Hifadhi iliyoko katika Wilaya yangu, Hifadhi ya Wanyamapori ya Makao yenye takribani kilomita za mraba 779. Kwa kutambua kabisa Wilaya ya Meatu ina takribani wafugaji 90%, tumeomba kule Wizarani poro lile au Hifadhi ile ya Jamii iweze kufanyiwa matumizi bora ya ardhi na tayari wenzetu wa *Frankfurt Zoological Society* wametusaia kufanya zoezi hili na tumetenga karibia kilomita 192 za mraba kwa ajili ya wafugaji wetu kuzitumia kwa ajili ya. Ninaomba mpango huu utakapokuwa umefika pale Wizarani basi wenzetu wa Wizara waweze kuupitia na kama kuna masahihisho waweze kutrudishia Wilayani tuweze kuwapatia eneo hilo ili wafugaji wetu waweze kulitumia kwa shughuli nzima za malisho. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye Taasisi ya Utafiti ya Wanyamapori yaani TAWIRI. Napongeza kazi nzuri sana inayofanyika kwenye taasisi hii lakini niwaombe sana watu wa Wizara wajaribu kuzingatia ripoti zote zinazodainishwa na taasisi hii. Kule ambapo wanyama wanaonekana wamepungua kwa mfano kwenye poro la akiba la Maswa au kule WMA ya Makao na kwingine kokote kule basi waweze kuelewa kwamba maeneo yale yanahitaji *rehabilitation* na waangalie pale wanapokuwa wanagawa maeneo yale kwa ajili ya vibali vya uwindaji. Tunapoendelea kuwinda katika mapori yale mwisho wa siku tutakuta mapori yale yanabakia na miti na majani tu na wanyama watakuwa wametoweka. Ninaomba Wizara iweze kuzingatia kwa umuhimu wake ripoti hizi ambazo zinafanywa na wataalam wetu wa TAWIRI. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa kwa sababu muda ni mdogo, nishukuru sana Wizara kwa kutuletea fedha kwenye Hifadhi yetu ya Jamii ya WMA Makao takribani USD milioni 22 kama ada ya pango lakini niombe sasa kwa upande wa Maswa *Game Reserve* bado tuna malimbikizo makubwa sana kule Wizarani na Wizara haijaweza kutuletea mpaka leo hii. Ie 25% ambayo inatakiwa kurudi kwenye Halmashauri yangu mpaka leo hii haijaweza kurudi. Ninamuomba Waziri atakapokuwa anajibu aweze kuniambia hii 25% ya *Maswa Game Reserve* itarudi lini kwa ajili ya kuwanufaisha vijiji vinavyohusika na poro hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nirudie kusema ninampongeza sana Mawaziri na ninawapongeza sana wataalam wote kwa kazi nzuri wanayoifanya na ninaomba kuwasilisha. Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mbatia.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi nitoe mchango kidogo katika Wizara hii. *GDP* inayotokana na utalii katika Taifa letu ni zaidi 17.2% ambayo ni karibu trilioni kumi ukilinganisha kwamba *GDP* yetu kwa sasa iko kwenye trilioni hamsini na tano. Naomba Mheshimiwa Waziri aweze kutueleza kwamba sekta ya utalii nchini ni ya ngapi kwa kutoa ajira kwa Watanzania na kama iko kwenye nafasi ya juu sekta hii inapewa vivutio kwa wawekezaji wa ndani kwa kiasi gani, wale wanaowekeza kwenye sekta hii ili sekta hii iweze kupanuka na kuweza kuongeza pato la Taifa zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012, watalii nchini walikuwa milioni moja sabini na saba elfu na hamsini na nane. Mwaka 2013 walikuwa milioni moja, tisini na tano elfu, mia nane na themanini na nne ambalo ni ongezeko la watalii elfu kumi na nane, mia nane na ishirini na sita

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

ambao ni takribani 1.7% ya ongezeko. Je, miaka mitano mpaka kumi ijayo, Wizara imeweka mpango mkakati gani wa kuhakikisha watalii hawa wanaongezeka zaidi ili kuongeza pato la Taifa?

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa sababu hata Kamati imelizungumzia hili, kuna taarifa zipo na zimezagaa kwenye vyombo vya habari kwamba Wizara au Serikali inataka kufungua mpaka wa Bologonja ambapo Masai Mara upande wa Kenya una kilometa za mraba 1510, upande wa Tanzania Serengeti una kilometa za mraba 14,763 ambapo ni takribani asilimia 90 ya eneo lote la hifadhi. Ukifungua mpaka huu wa Bologonja ambao Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere aliufunga mwaka 1977, ni kuleta maafa katika sekta ya utalii hapa nchini Tanzania. Naomba kama wazo hilo lipo, lisiwepo na ni wazo la kufedhehesha utalii katika sekta ya Tanzania. Hii itathiri hata viwanja vyetu vya ndege vya Kilimanjaro katika kuingiza watalii. Kwa hivyo, wazo hili Mheshimiwa Waziri kwa vile limesambaa sana linasemwa sana, tunataka kupitia Bunge hili Serikali itoe tamko kuzuia wazo hili ovu la kuuwa sekta ya utalii hapa nchini na kufungua mpaka wetu na Bologonja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sekta ya utalii hapa Tanzania ni ya pili kwa vivutio vya utalii duniani ukiacha Brazil. Takwimu za mwaka 2012 inaonesha kwamba sekta hii ya utalii kutokana kuwa ya pili kwa vivutio vya utalii duniani, ilikuwa inatuongezea mapato. Ukiweka kwenye mizania ya nchi 133 kwenye sekta ya utalii, Tanzania tulikuwa tunashika nafasi ya 110 kati ya nchi 133 wakati sisi ni wa pili duniani kwa vivutio vya utalii ukiachia Brazil. Je, kwa kuwa sekta hii inapanuka leo hii tunashika nafasi ya ngapi duniani kati ya nchi 133 katika kuongeza pato la taifa na kufanya Tanzania pawe mahali pazuri na salama zaidi pa kuishi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimemsikia Mheshimiwa Waziri kwenye vyombo vya habari akisema kwamba kwenye wanyamapori, Askari Wanyamapori walikuwa hawana Kanuni za Maadili (Code of Ethics) na sasa ndio wanaweka Kanuni za Maadili. Hivi kweli jambo la namna hii unaweza ukawaambia Watanzania kwamba mpaka leo hii Askari Wanyamapori hawana Code of Ethic na ndio mauaji yametokea, Watanzania wamepoteza uhai wao! Kuna mambo mengine kwa kweli yanatia aibu kwa Serikali, yanatia aibu kwa taifa kama mpaka leo hii Code of Ethics kwa Askari wetu, namna ya kulinda viumbe hawa, kulinda watu walio karibu na mazingira haya, mahusiano nao na ndio maana inatokea matatizo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa Kasulu kwenye ile Hifadhi ya Kagerankanda, Makere Kusini ambapo wakati inaanzishwa mwaka 1955 wakazi wa Kasulu walikuwa takribani laki moja na nusu hivi, leo hii wakazi wa Kasulu wanafikia takribani milioni moja. Je, ni mahusiano gani yanajengeka sasa, wakulima hawa ambao wameshalima, wamekaa kwenye maeneo karibu na Hifadhi zaidi ya miaka 30 iliyopita leo hii wanafukuzwa, wananyanyasika, Serikali inasema nini? Kwa nini tusijenge mazingira ambayo ni rafiki ili Watanzania waone nchi yao na hasa kule Kasulu panakuwa ni mahali salama zaidi pa kuishi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mbunge wa Kasulu Mjini anaulizia hilo, Mbunge wa Kasulu Vijijini anaulizia hilo. Sasa Mheshimiwa Waziri tunaomba tuwe *focused, let us think big, let us think globally but act locally* katika sekta hii ya utalii na hii itaiwezesha Tanzania pawe mahali mazuri pa kuishi. Tunaweza tukatumia sekta ya utalii tu Tanzania tukazungumzia lugha nyingine badala ya kusema, sekta ya utalii ni kubwa na pato lake lipo juu kuliko hata sekta ya madini na nishati.

Sasa kama tumepewa vivutio hivi na Mwenyezi Mungu basi tuvitumie vizuri ili viweze kutuwezesha Tanzania tukakuza pato letu na haya malalamiko madogo madogo yakaondoka.

Mheshimiwa Spika, sasa hili ni suala la kuwejiwekea mpango mkakati mzuri wa Wizara, suala la ubunifu wa Wizara na suala la kuhakikisha wawekezaji wa ndani tunawapa *incentives*, hoteli za kisasa katika mbuga zetu, hoteli za kisasa linganisha na majirani zetu, hali ya majirani

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

zetu ulinzi na usalama upo hoi bin taaban unajua Mheshimiwa Waziri. Hasa kwetu kwa kuwa pako salama basi tutumie fursa hii Tanzania tuweze tukaogelea kwenye utalii na kweli pato letu likawa kwenye hali ambayo ni nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho nisigongewe kengele ya pili, naunga mkono hotuba ya Kamati isipokuwa pale waliposema wanaipongeza Serikali kwenye Operesheni Tokomeza. Miezi sita tu iliyopita tulilaani mambo ya Operesheni Tokomeza na maisha ya Watanzania yalivyoangamizwa. Leo hii tunaipongezaje tena Serikali hiyo ambayo ilisababisha Mawaziri zaidi ya wanne wakajizulu kwenye hali hii! Tuwe tunakuwa *consistent* na Bunge hili liwe na mwelekeo sahihi ili tutumie Ibara ya 63 ya Katiba katika kusimamia na kuishauri Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (Makofi)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Lulida atafuatiwa na Mheshimiwa Meghji.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na mimi kunijalia kupata nafasi ya kuchangia Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, nataka ni-*declare interest* kuwa na mimi ni mdau wa Wizara hii kwa vile ni Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge cha kusimamia uhifadhi wa wanyamapori wakiwemo tembo na faru. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Nyalandu, Naibu Waziri na Katibu Mkuu. Nimefanya naye kazi tukiwa katika bodi moja miaka ya nyuma, namtambua kuwa huyu bwana ana uwezo mkubwa katika masuala ya utalii. Huyu bwana nikiwa pale nilikuwa namuita *digital* kwa sababu alikuwa anajiweza na kujitambua na aliiwezesha TANAPA kuruka na kupata mapato makubwa kwa kutengeneza *strategic plan* ya TANAPA. Kwa hilo ni lazima nimpongeza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mkurugenzi Mkuu wa Ngorongoro, Mkurugenzi Mkuu wa TANAPA na Mtendaji Mkuu wa Idara ya Misitu (Mama Tuli). Kwa nini nawapongeza? Ni kwa sababu wamejatahidi sana kuhakikisha mfuko wao wa Misitu unafanya kazi na naipongeza TANAPA na Ngorongoro kwa muda wa miaka yote wameweza kuongeza pato kubwa na kuisaidia Serikali kupata mapato makubwa, kila mmoja wao kupeleka zaidi ya shilingi bilioni kumi. Haya Mashirika inabidi yapongezwe na yasaidiwe. Kwa nini yasaidiwe?

Mheshimiwa Spika, leo hii TANAPA imeletewa msaada wa faru. Faru wale ili tuwatunze wana gharama kubwa kuliko kumtumza mtoto wa binadamu. TRA wanatoza ushuru wa wale faru na vifaa vyao itasaidia nini kwa nchi hii? Ili faru wale waweze kuendelea na kutunzika Askari Wanyamapori wanahitaji mishahara, vifaa vya magari, vifaa mbalimbali kama simu za mikononi na vitu mbalimbali lakini leo TRA inatoza kodi vitu kama hivi, huu ni uonevu.

Mheshimiwa Spika, ukichukulia barabara zinazojengwa ndani ya Hifadhi zetu inabidi zitozwe kodi kwa nini? Tunajila na kujikaanga kwa mafuta yetu wenyewe. Kuna mianya mingi ya mapato TRA imeiachia, ishughulikie maeneo hayo ili ipate pato la kuweza kuongezea tija sio kuangamiza TANAPA, Ngorongoro. Mashirika haya yanahitaji misaaada mikubwa kwa ajili ya wafanyakazi, kwa ajili ya uhifadhi wa wanyamapori na tunaona sasa hivi fujo ilivyokuwepo kubwa, tembo wanapungua, faru wanauawa na sasa hivi mpaka simba.

Mheshimiwa Spika katika taarifa tuliyokuwa nayo sasa hivi, tuna chita arobaini Serengeti, simba wanazidi kutoweka, ni kwa nini? Wenzetu sura pana au watu wa manjano

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wanawamaliza hawa wanyama. Maana yake nikitaja majina mtasema Riziki mbaguzi hapana, sura pana na watu wa manjano wameamua kuwamaliza wanyamapori. Leo katika utamaduni wao wanavaa ngozi za chita, wanavaa ngozi za chui ama za simba, jamani sura pana kwa kweli tuwaangalie na tuwasimamie wasije wakamaliza uchumi wetu. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie Pori la Akiba la Selous. Kwa kweli hili pori kila siku nalizungumzia na Waziri nilimwambia wewe ni *digital*, naomba katika miaka miwili hii usimamie Pori la Akiba la Selous ili Tanzania tuweze kupata mapato. Ni pori kubwa na lina uwezo wa kusimamiwa kwa vile kule nako kuna ushoroba na *corridor* ya tembo ambao wanatoka Niassa Mozambique. Jina la Selous lisipotee libakie palepale ili lizidi kuwa na vivutio vikubwa na tupate ajira kubwa katika Mapori yetu ya Selous.

Mheshimiwa Spika, kwa nini naizungumzia *Selous*? *Selous* ni pori kubwa na wanavijiji wanaozungukia Pori la Akiba la Selous hawajashirikishwa. *Engagement* ya *community* katika Mapori yetu itasaidia kutokomeza ujangili. Tutoe *training* kubwa kwa wanavijiji na wapate misaada ya maji, umeme, mawasiliano ya simu na kadhalika. Kwa mfano, sasa hivi lazima niwapongeze Wizara ya Nishati na Madini wanapeleka umeme vijijini katika Mikoa yetu ya Lindi, nina imani kuwa Mapori yetu ya *Selous* yatafanya kazi. Leo tunaona Waziri wa Mawasiliano anapeleka vijijini mawasiliano ya simu, kwa kweli taarifa zitakuwa zinapatikana ambazo zitasaidia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanzisha taasisi yetu humu ndani ya Bunge ya uhifadhi ya wanyamapori lakini inasema hivi, *only elephants and rhino should wear ivory and trophy*. Sasa tunasimamia na tuna wadau ambao ni *maliasili family* ndani ya Bunge lako na Mwenyezi Mungu akikujalia leo umekuwa mgeni rasmi kuizindua hii taasisi yetu. Nia na madhumuni tuwe wadau wa kusukuma maendeleo na sio wadau wakupondaponda kila siku. Penye mazingira mazuri tupongeze, pale penye kutetereke tujaribu kusahihishana isiwe kila siku ni kuponda, kuponda, kuponda! Huu ni mzigo mzito, mzigo mzito usimwachie mwenzio peke yake na wewe unawajibika kusaidia katika ule mzigo mzito. Tukijiangalia sisi wenyewe tulipokaa hapa sasa hivi kila mmoja ana upungufu, tuwe na tabia ya kusameheana ili tuweze kuleta marekebicho na tuweze kuenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mapendekezo kwamba ili Pori la Akiba la Selous ili liweze ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante. Nilisema anafuatia Mheshimiwa Meghji halafu atafuatiwa na Mheshimiwa John Cheyo.

MHE. ZAKIA H. MEGHJI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Naamua kuchangia mambo mawili kama muda utaniruhusu. Suala la mpaka au lango la Bologonja au *Bologonja gate* na la pili ujangili wa wanyamapori na mapendekezo yangu.

Mheshimiwa Spika, naanza na mpaka wa Bologonja. Kuna mazungumzo au kuanza kwa mazungumzo kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii na wenzetu wa Kenya juu ya kufungua mpaka

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wa Bologonja ambao uko Maasai Mara kati ya Kenya na Tanzania. Mpaka huu umefungwa karibu miaka 40 hivi sasa tokea wakati wa Mwalimu Nyerere alipokuwa Rais wa nchi hii. Mpaka huu unatenganisha Kenya na Tanzania kupitia mbuga ya Maasai Mara inayounganishwa na Mbuga ya Serengeti. Watalii wengi wanaokuja Tanzania, wanavutiwa hasa na kutembelea Mbuga ya Serengeti kuona wanyama mbalimbali lakini pia kuona maajabu ya nyumbu wanaohama kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa mamilioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka huu umebaki umefungwa kwa sababu kubwa za kiuchumi. Maasai Mara inatokea Tanzania mpaka Kenya. Hivi sasa watalii wanaotaka kutembelea Serengeti inabidi wapitie Tanzania na wanaporudi pia wapitie Tanzania. Kwa hivyo, unakuja kwa kupitia Tanzania na unarudi kwa kupitia Tanzania. Kwa hiyo, mapato yanayotokana na utalii kwa maana ya hoteli, *lodging*, hizi *tented camps*, usafiri, uuzaji wa vinyago na kadhalika yanabaki Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sera ya Tanzania ni utalii endelevu yaani utalii unaojali mazingira. Tunasema *low volume, high yield*, watalii wachache, mapato makubwa na bila ya kuharibu mazingira. Sera ya Kenya ni tofauti, wao ni utalii usiojali mazingira yaani *mass tourism*, ni sera mbili tofauti kati ya Kenya na Tanzania. Kwa hiyo, tujue tu kwamba tukifungua mpaka wa Bologonja kutakuwa hakuna haja ya watalii wanaotaka kwenda Serengeti kuja Tanzania. Wataingilia upande wa Kenya na kutoka upande huohuo wa Kenya.

Mheshimiwa Spika, upande wa Kenya hata ukisimama upande huu wa Tanzania unaweza kuona kule, wamejenga hoteli nyingi sana, *tented camps* nyingi sana, *tented camps* hoteli karibu 50 na bado wanaendelea kujenga hizi *tented camps* pamoja na hoteli. Pia tunajua kwamba nauli ya kutoka Europe ambapo ndio watalii wengi wanatokea kwenda Kenya ni ndogo ukifananisha na nauli kutoka Europe kuja Tanzania. Kwa sababu za kiuchumi pia, wana ndege zao Kenya Airways na kadhalika, kwa hivyo, wanalipa fedha kidogo kwa nauli kutoka Europe kuja Kenya ukifananisha na kutoka Europe kuja Tanzania. Sasa tujulize, kwa nini watalii waje huku kama pamoja na nauli ndogo watatembelea Mbuga ya Serengeti kupitia Maasai Mara upande wa Kenya? Waje kufanya nini? Kama wanataka kutembelea Serengeti watalipa fedha kidogo, wataingia Serengeti na kuona wanyama mbalimbali hakuna haja kwa wao kuja Tanzania kwa maana hiyo. *(Makofi)*

Sera hii ya kutofungua mpaka huu kama nilivyosema ni ya miaka mingi. Mimi nilipokuwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa muda wa miaka tisa, Waziri anayeshughulikia Afrika Mashariki pamoja na Mawaziri mbalimbali alijaribu sana kunishawishi tukubali tufungue mpaka huu ya Bologonja. Huyu Waziri nimtaje ndani ya Bunge alikuwa ni Mheshimiwa Biwott, nafikiri watu wengine wanamuelewa. Alikuwa Waziri, alikuwa na uwezo mkubwa sana, alikuwa na ndege na kadhalika, kwa hiyo, alijaribu kushawishi sana ili mpaka huu ufunguliwe lakini upande wa Tanzania tulikataa. Napenda kusema kwamba tuliungwa mkono kwanza na Waziri aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ambaye hivi sasa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia tuliungwa mkono na Rais wa wakati ule ambaye ni Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kabisa ningemuomba Mheshimiwa Waziri jambo hili aliache kama vile Kamati ilivyosema. Hivi sasa upande wetu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Dakika saba zimeisha.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MBUNGE FULANI: Muongeze.

SPIKA: Huo utaratibu haupo. Namwita Mheshimiwa John Cheyo.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza mahali ambapo watu wanafanya vizuri ni vizuri kuwasifu, mimi naona Idara hii ya Wanyamapori na Utalii kwa kufikia mpaka asilimia 17 GDP, ni kazi nzuri, wanahitaji kuungwa mkono na waendeleo.

Mheshimiwa Spika, pia ni lazima tuseme tunaishi na watu. Nchi yetu siyo ya wanyamapori peke yake. Sifa ya Tanzania ni pamoja watu 44 milioni ambao wanahitaji ardhi, wanahitaji haya mapori yaweze kuwafaidisha, wengine wana kazi zingine kwa mfano kilimo na ufugaji. Hivyo jambo hili la utalii pamoja na wanyamapori ni lazima liangaliwe katika *larger context* siyo tu kwa upande mmoja.

Mheshimiwa Spika, hapa ndiyo nataka kuanzia kwanza kabisa kwa kusikitika na hili labda ni la kwako kwamba miezi sita iliyopita tulikaa hapa tukalaumu sana yaliyotokea kwa Operesheni Tokomeza na Kamati yako ilitufikisha mahali mpaka tukawaachisha Mawaziri kazi zao na wengine wakajiuzulu. Miezi sita baadaye tunapongeza Operesheni Tokomeza na kuiomba Serikali iendeleo tena. Watu wanatuonaje sisi kama Bunge? Ningeshauri labda wewe kama ndio mwenye nyumba na kwa ajili ya kuweza kuhakikisha kwamba heshima ya Bunge hili inabaki labda ungeliangalia hili kwamba ni mazingira gani ambayo yameiwezesha Kamati yako kuweza kugeuza mawazo kutoka kulaumu Operesheni Tukomeza na leo wanaishukuru Serikali kwa kuwa na Operesheni Tokomeza.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba watu wengi walipata taabu sana, wengine walionewa bila hata sababu, bado tunasubiri tupate ushauri wa Tume na hatujapata hiyo Tume lakini tumeambiwa kwamba tunaipongeza Serikali kwa Operesheni Tokomeza. Namshauri Waziri siyo jambo zuri kukaa unajitapa kwamba una silaha, ukawa unagombana na watu bure, hata helkopta ambazo unazinunua unajua wewe ni risasi moja tu ikipiga kwenye mkia wa helkopta hata helkopta yako hiyo haiwezi kuwa na uhai. Mimi naona tutafute njia za kuweza kuishi vizuri zaidi na wananchi tulionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa nataka kuzungumzia juu ya wanyamapori, zaidi mapori tengefu na wafugaji. Mimi naona *model* ya Ngorongoro ya wanyamapori, watu na ng'ombe kuishi pamoja inawezekana. Imewezekana Ngorongoro kwa miaka mingi sioni ni kwa nini isiwezekane katika mapori ambayo yapo karibu na wananchi ambayo ni tengefu kwa mfano mapori ambayo yapo Longalombogo, Ng'walali na sasa amesema Makao na sehemu zingine. Mimi naona hili jambo badala ya kukataa tu labda ungeliangalia kwa sababu kinachogombewa hapa ni malisho, ni majani. Mimi nina uhakika tunaweza tukawaambia wafugaji wawasaidie sana wanyamapori kwa kuhakikisha kwamba mtu anayechunga kwenye hayo mapori haui wanyama, hakati miti. Hao wafugaji wanaweza kuwa walinzi kuliko hivi sasa kuonekana kama maadui. Naomba muangalie sana hiyo *model* ya Ngorongoro pia iweze kufanya kazi katika Wilaya ya Meatu, Wilaya ya Itilima, Wilaya ya Bariadi ili tuweze kuishi kwa usalama siyo sasa hivi ambapo inaonekana ni kama kuna vita kati ya Serikali na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, sisi upande wa *Western Corridor* au upande wa Magharibi hatusemewi sana lakini wewe unafahamu kuwa mapori kama sehemu ya lhandajega, sehemu yote ya Serengeti ambayo inapakana na Bariadi na sehemu zingine ni sehemu ambazo kabisa hazijaweza kuwekewa umuhimu juu ya watalii. Kwa sababu sasa kiwanja cha Mwanza kinajengwa, hoteli Mwanza zimeanza kuwa nyingi na hoteli zingine

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

zimeanza kufunguliwa Musoma. Pengine jambo hili lingepewa umuhimu ili mafao ya utalii yasiishie tu Arusha, mafao ya utalii yaweze pia kusaidia katika sehemu nyingine. Nafikiri hili jambo linawezekana kabisa na hiyo ndiyo njia ya kuweza kukuza utalii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Sika, jambo la mwisho nafikiri bado kuna nafasi kubwa sana ya kuweza kueneza utalii katika sehemu mbalimbali. Umezungumza kwa rasharasha, kuna haja kabisa ya kurudi kule nyuma ambapo kila Ubalazi ulikuwa na Afisa wa Utalii, kulikuwa na mtu ambaye anahakikisha kwamba watu wanakuja Tanzania kwa urahisi zaidi. Mimi naona hilo jambo sasa limesahauliwa na ni vizuri tukarudi huko ili tukiwekeza katika kuleta watalii, utalii utakua.

Mheshimiwa Spika, angalia tu Wakenya walivyowekeza katika kuhakikisha kwamba utalii kwenda Kenya unakuwepo lakini tunajua kwamba hakuna chochote Kenya, wengi wanataka kupitia Kenya lakini zaidi wanataka kuja Serengeti. Kwa nini sisi tusiwadake wale watu waje moja kwa moja, waje Kilimanjaro moja kwa moja na sasa hivi KLM inaleta watalii wengi sana moja kwa moja Kilimanjaro. Tunataka na wengine waige huo mfano ili tuweze kuhakikisha kwamba tuna wageni wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nitamuita Mheshimiwa Dkt. Haji Hussein Mponda atafuatiwa na Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi.

MHE. DKT. HAJI H. MPONDA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi ninchangie hotuba ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono lakini naomba nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa msaada na jitihada kubwa walizofanya kutatua tatizo la kuvuka kuelekea Wilaya ya Ulanga. Wamepeleka boti nne na Wanajeshi 20, namshukuru sana Jenerali Mwamnyange na Brigedia Ndomba, kwa jitihada zao za kasi ambazo zimeweza kuleta ufumbuzi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kutegemea na muda nitaongea kitu kimoja tu, nitaongea kuhusu *buffer zone*. Naomba Mheshimiwa Waziri unisikilize kwa makini kuhusu *buffer zone* kwa sababu siyo mara ya kwanza kuzungumzia suala la *buffer zone*.

Mheshimiwa Spika, wakati tunarejea Sheria ya Wanyamapori 2009, Bunge liliielekeza Serikali mambo mawili. Jambo la kwanza waangalie umuhimu wa kuweza kuendeleza au *maintain* mapori tengefu 42 yaliyopo hizi sasa. Jambo la pili kurekebisha mipaka ya mapori tengefu hayo dhidi ya mipaka ya vijiji. Naomba niseme kweli kwamba nasikitika katika mambo mawili haya Serikali mpaka leo hawajafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012, Serikali katika Bonde la Kilombero walichokifanya badala ya kurejea mipaka, waka-create kitu kinaitwa *buffer zone* ndani ya Pori Tengefu la Mto Kilombero. Katika *buffer zone* hiyo kuna vijiji 15 miongoni mwa vijiji 91 katika Wilaya ya Ulanga, maana yake asilimia 17 iko ndani ya *buffer zone*. Kule kuna watu elfu arobaini, kuna hekta za mpunga elfu tisini, ni tegemeo kubwa kwa wakazi wa Ulanga wao wenyewe binafsi kama kaya lakini pia ni tegemeo kubwa la Halmashauri. Halmashauri mwaka jana tumepata bilioni mbili lakini asilimia 80 imetokana na hilo eneo la *buffer zone*.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, tumewaeleza muda mrefu Serikali kuwa eneo hili la *buffer zone* ni tegemeo kubwa la wakazi wa Ulanga. Sasa kuna mambo mawili tu ya kufanya pale. Jambo la kwanza Mheshimiwa Waziri amepewa mamlaka ndani ya Sheria ya Wanyamapori ile ya 2009 kwamba yeye anaruhusu matumizi ya eneo lile la *buffer zone* lakini mpaka leo licha ya maombi, licha ya adha na taabu ambazo tunasimuliwa mara kwa mara amekaa kimya.

Mheshimiwa Sika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu mwezi wa 11 mwaka jana tulimuona akatusikiliza, akaridhia na kuona umuhimu wa kurejesha eneo la *buffer zone* kwenye Serikali ya Vijiji. Tarehe 17 Aprili mwaka huu ameandika dokezo kwa Wizara nne, Wizara ya Ardhi, TAMISEMI, Maliasili na Wizara ya Mazingira wakae wajadili namna gani watawezesha kurudisha eneo lile kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha wa mwaka huu maana yake mwezi wa sita.

Mheshimiwa Spika, nasikitika mpaka leo pamoja na amri na maelekezo waliyopewa na boshi wao, bado wakubwa hawa hawajakaa chini namna gani ya kurudisha ardhi ile au eneo lile la *buffer zone* ambalo nimeeleza ni tegemeo kubwa la wananchi wa Wilaya ya Ulanga. Tena naomba niwakumbushe eneo hilo kuna miradi mikubwa miwili ya Serikali. Mradi wa SAGCOT wanategemea eneo la *buffer zone*, kuna mradi wa FAMOGATA, Fanya Mkoa wa Morogoro kuwa Ghala la Taifa, lakini bado naona hamjafanya kwa vitendo kurudisha eneo lile.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuishauri Wizara kwamba kama wenzangu walivyodokeza, mmefanya vizuri sana katika kuongeza pato la Serikali lakini nawashauri tena kwamba bado kuna mianya mingi katika mazao ya misitu, tunaomba mbane mianya hiyo tunaweza tukafikia hatua nzuri sana ya kuongeza pato la Taifa na vilevile kuweza kuwasaidia Watanzania ambao wengi wao tunaishi maisha magumu.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atakapofanya hitimisho lake, wana Ulanga wanataka kusikia sentensi moja tu leo, ni lini utafanya mambo mawili, kwa kutumia mamlaka uliyopewa utawaruhusu watumie maeneo yale ya *buffer zone* wakati huo hizo Wizara nne mnafanya utaratibu wa kurudisha rasmi maeneo yale kwenye Serikali za Vijiji.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (Makofi)

SPIKA: Sasa namwita Mheshimiwa modestus Kilufi atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Kwa niaba ya wananchi wa Mbarali naomba niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani ya dhati kabisa kwa Serikali pamoja na Wizara kwa ujumla kwa kuona umuhimu wa kutatua mgogoro uliokuwepo baina ya wananchi wa Mbarali na mpaka wa hifadhi ukizingatia kwamba hifadhi ya Ruaha imesogea Mbarali eneo ambalo ni jipya lakini nashukuru sana kwa hatua tuliyofikia kwamba sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wa Wizara husika wamekubali kuja Mbarali kushirikisha Viongozi wa Mbarali na Wizara mbalimbali zinazohusika kuja kumaliza kabisa huo mgogoro. Nadhani Mheshimiwa Waziri utalieleza hili unapojibu ili wananchi wa Mbarali waweze kujua kwamba Serikali inawajali.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni ngumu sana, ushahidi upo kila Waziri anayekwenda pale hawadumu sana katika Wizara hii na inawezekana tukaona wote hawafai. Tatizo lingine ambalo ninaliona ni utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Wizara hii imekuwa ikipewa fedha kwa mfano bajeti ya mwaka 2013/2014 Wizara ilipewa Sh.75,681,745,000 lakini zilizopokelewa mpaka kufikia Machi ni Sh.29,000,000,000 tu. Katika hali hii inakuwa ni vigumu sana kutekeleza majukumu ya Wizara nyeti kama hii ambayo siku zote inapambana na majangili na watu wasioitakia mema nchi yetu kuhusu wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho watuhumiwa 391 walikamatwa na walikamatwa wakiwa na nyara kwa maana ya meno ya tembo 866 lakini pia wakiwa na meno ya kiboko 20, wakiwa na kilo za nyama 9,458, hii ni hujuma ya hali ya juu sana. Kama hili jambo halitaangaliwa vizuri na fedha hizi zikawa hazipeleki kule kwa maana ya kuimarisha mikakati hawa wanyama wetu wanaweza wakaendelea kutoweka. Ni jukumu la sisi sote kuona kwamba hawa wanyama wanatunzwa kwa faida yetu sisi na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo yote haya, hakuna uwezekano wa kulinda wanyama hawa kama hatutafanya ulinzi shirikishi. Tumefanikiwa sana Tanzania kuwa na amani lakini amani hii inakuja kutokana na mshikamano wa Watanzania wa pamoja wa kuchukia mabaya yanayofanywa na watu wasiotutakia mema. Katika kulinda hawa wanyama kama wananchi wanaozunguka hifadhi hizi tutaendelea kuona ni maadui hata tuongeze ulinzi kiasi gani hatutafaulu kulinda wanyama hawa, haiwezekani! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini si Wizara hii tu kwa maana ya Wanyamapori, ni maeneo mengi tumeshindwa kwa kutokuwa na ushirikiano wa kutosha na wananchi. Hatuwashirikishi vya kutosha, tunazungumzia sana suala la utawala bora na hili litumetuathiri sana katika Taifa hili, tunalizungumza kwenye makaratasi lakini tukija kwenye utekelezaji utawala bora na haki za binadamu tunasahau. Operesheni Tokomeza kilichofanyika katika nchi hii katika operesheni ile ni cha kulaani na kulaaniwa siku zote. Wamekamatwa watu wasio na hatia, wameteswa, wamenyanyaswa, yote hii ni kuonesha jinsi gani hatusimamii utawala bora na haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, nikitolea mfano Mbarali kuna watu wamekaa nyumbani ana bunduki yake amelipia, hahusiki na lolote anakuja anakamatwa. Mimi mpaka nikasema hivi kama mnahisia kuna watu wanawinda wanyama, wana miliki silaha hata kama ni kisheria lakini mna mashaka, kwa nini msiwaorodheshe, mkawashirikisha viongozi wa Wilaya wakaitwa kwa pamoja wakahojiwa?

Badala yake anafuatwa mmoja mmoja usiku, washukuru Mungu watu wale hawakuwa na ukorofi wangeweza kuwapiga risasi usiku wanapowachukua kwenye majumba yao. Hii yote ni kutokana na kutokuwa na msimamo wa kusimamia vizuri utawala bora na haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, hii imejitokeza katika maeneo mengi siyo katika Wizara hii tu, tumeona jinsi gani wafugaji ambapo wakati fulani wamenyanyasika kwa kutosimamia misingi ya utawala bora na haki za binadamu, tumeshuhudia wakulima wanavyopata shida nchi hii kwa sababu ya kutokusimamia utawala bora na haki za binadamu. Leo hii wafugaji nchi hii imekuwa kama siyo ya kwao, wanahangaika huku na huko, lakini sheria za utawala bora na haki za binadamu tunazo kwenye makaratasi inatusaidia nini? Leo hii wakulima wanavuna mazao yao wanarudisha nyumbani, Kiongozi aliyepewa dhamana kusimamia, anasimamia walipe ushuru, wakulima ametoka shambani! Amehangaika peke yake, anaambiwa alipe ushuru analipia nini ulimsaidia mtaji? Sheria iko wapi ya kumtoza ushuru mkulima anayetoka shambani kama siyo kukiuka utawala bora na haki za binadamu ni nini? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yangu mimi mwenyewe, Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba Serikali isimamie utawala bora na haki za binadamu,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

haiingii akilini kuona Watanzania wananyanyasika kwa watu waliopewa dhamana na Taifa hili. Haiwezekani kabisa! Mimi ninasema itafika mahali hawa Watanzania watachukua hatua, hapatatosha hapa nchini, wataonewa itafika mahali hawataweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mbarali nashuhudia mwenyewe na nimemwambia Waziri ikiwezekana alisema hili, wakulima wanatoka shambani wamehangaika, mageti yamewekwa mtu anatakiwa alipe ushuru, hivi wale waki-react wakawapiga wale wakawaumiza hii sheria ya kuwataka wakulima walipe ushuru imetoka wapi? Kwa kweli sijafurahishwa na jambo hili. Ikithibitika kwa ushahidi wa kutosha, Serikali ichukue hatua kwa wale wote waliohusika, si jambo la kucheka hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili tuimarisha utawala bora kwenye Wizara hii, naomba ziimarishwe WMA kwa maana ya ushirikishwaji wa wananchi wanaozunguka hifadhi zote kuhifadhi wanyama wanaotoka kwenye hifadhi za Taifa. Tukifanya hivi tukaimarisha, tukaweka na walinzi wanaotoka kwenye vijiji hivi vya kwetu, nina hakika majangili hawa wanapoingia kwenye hifadhi zetu wanapita kwenye maeneo haya na kwa sababu sisi tumeweka uadui na wananchi wetu inakuwa ni vigumu kutusaidia. Tuweke motisha kwa wananchi wote watakaotoa habari za kukamatwa majangili. Tuwekeze huko, tukifanya hivyo tutafanikiwa na tutadhibiti na ulinzi wa wanyama hawa unatakiwa uwe wa pamoja siyo mtu mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri hamtaweza kulinda wanyama hawa peke yenu hamuwezi. Ni lazima jamii zinazozungunga hifadhi zetu zishirikishwe na miradi ya maendeleo inayotolewa kwa zile jamii ionekane kwa uwazi. Tukifanya hivyo, nina hakika kabisa tutalinda wanyama wetu na ustawi wa wananchi wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wilayani Mbarali tulishaanza kutengeneza WMA. WMA hizi zinawapa nafasi wananchi kumiliki wanyama wanaotoka kwenye hifadhi kuwalinda na kuwatunza.

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Kengele ya kwanza?

SPIKA: Ya pili.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Aah! Mheshimiwa Spika, naunga mkono, naomba ushirikiano, utawala bora na haki za binadamu utunzwe. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hamad Rashid atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza niwapongeze Waziri, Naibu Waziri na timu yao kwa kazi nzuri wanayoifanya lakini pili niombe ushauri alioutoa Mheshimiwa Meghji muuzingatie sana, ni jambo la busara sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, ningemwomba Mheshimiwa Waziri katika kitabu chake tulitegemea atatueleza mapato yanayotokana na misitu lakini bahati mbaya sikuona takwimu. Ni vizuri akatueleza mapato yaliyotokana na misitu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, nne, atueleze vilevile juu ya uhifadhi wa hizi nyara zinazokamatwa. Kwa mujibu wa CAG inaonekana bado hakuna *proper records* za nyara zinazokamatwa. Tungeomba hilo nalo ulifuatilie.

Mheshimiwa Spika, tano, soko la utalii duniani linategemewa by 2020 kufikia *1.5 billion* na wanategemea kupata *revenue about two trillion, daily* wanasema *worldwide* tutapata *five billion*. Sasa ni vizuri tukaangalia katika hilo tunapataje. Sasa ukitazama kitabu cha Waziri ukurasa wa 50 kuna hawa *Package Tours* na *Non Package Tours*, hawa *Package Tours* kwa taarifa mbalimbali zilizopo wanasema zinachukua karibu asilimia 80 ya mapato ya utalii yanakwenda kwao hasa kwenye *air lines* na kadhalika. Kwa mfano Thailand peke yake *air line* inachukua asilimia 80 ya mapato. Sasa lile suala lililokuja kwa Wajumbe wengi hapa, kwamba ni vizuri tukawa na *air line* yetu, hapa ndiyo *area* inayotuwezesha kupata mapato mengi. Kwa mfano tunaisifu sana Thailand kuna watalii wengi lakini asilimia 80 inakwenda kwenye *air line* peke yake na *tours*.

Mheshimiwa Spika, halafu kuna suala zima la *export leakage* na *import leakages* hili nalo ni vizuri ukaliangalia vinginevyo *revenue* nyingi tutazikosa hasa watu wanapofanya *investments* zile *returns* za *investments* mara nyingi zinakula *revenue* zenu. Nafikiri nalo hilo ni jambo la kuliangalia na Waziri labda ungelitolea maelezo.

Mheshimiwa Spika, *area* nyingine ni ya *export leakages* nayo vilevile inahitaji kuangaliwa kwamba watu wanaoleta vifaa vyao, vyakula, vinywaji na kadhalika. *Those are areas* ambazo *revenue* nyingi zinaondoka na kwa *estimate* inasadikiwa kwamba *about 56%* ya *revenue* hiyo inaondoka. Kwa hiyo, inawezekana mnapata *one million* lakini kama *package* yenu itakuwa nzuri na hasa ku-*concentrate* katika hii *none package tour* mnaweza mkapata *revenue* kubwa zaidi kuliko hii tunayopata sasa hivi. Sasa hili soko la *1.5 billion* wanaotegemewa kuweco by 2020 tutazame sisi tunaweza kuwavuna kiasi gani kama tutakuwa na *package* nzuri. Moja tukiwa na hoteli nzuri ambazo zinatoa *good services*, barabara zinazokwenda kwenye utalii, kuwa na *air line* yetu, hayo ni mambo ambayo yanaweza ku-*encourage* kupata utalii.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa zaidi ni mambo mawili. La kwanza, amani na utulivu. Ukiangalia takwimu za Kenya sasa hivi ime-*drop by 1.23 percent* ya utalii wao kutokana na hali ya usalama ya Wakenya. Sasa hivyo ni vitu vya kuviangalia sana kwamba lazima tu-*maintain peace and stability in the country* ili kuwa-*encourage* hawa watalii waweze kuingia nchini.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni huduma tunazozitoa. Sasa hivi ukitaka *visa* uende kwenye Balozi zetu, kuna Balozi zingine zinaweka *stickers*, nyingine wanaweka stempu tu, pesa zinaliwa na kadhalika. Kuna utaratibu wenzetu wengine wameu-*design* wanaita *electronic visa* na hata wataalam walikuja hapa wakakaa na Kamati ya Bajeti wakawashauri, wakakaa na Wizara ya Mambo ya Ndani wakawashauri, tukashauri waje kwenu vilevile mshauriane, wanasema unaweza ku-*tape* watalii wengi kwa sababu unawaondoshea dhiki ya kupata *visa*. Sasa hili nalo ni jambo ambalo mngelifanyia kazi haraka sana. *Electronic visa*, hiyo *technology* ipo, inatumika na Balozi nyingi sasa hivi wanazitumia na inasaidia ku-*generate revenue* kwa haraka sana lakini vilevile unatumza mapato kwamba sasa hivi hata *Embassies* zetu hazitunzi vizuri mapato *billions and billions of money* zinakwenda lakini kwa utaratibu huu tutatunza fedha, watalii watakuwa hawaangaiki kupata *visa* kwa sababu wanatumia *electronic system* na hiyo itatusaidia kupata *revenue* kubwa. Ningeomba mambo hayo vilevile muyaangalie.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la mapato. Nimefurahi sana kuona mapato yanayotokana na nta na asali lakini ukitazama takwimu za Waziri alizozitoa hapa mapato ya mwaka 2004 yamekuwa makubwa sana kuliko leo wakati kuna *encouragement* kubwa kwamba watu wafuge zaidi na kadhalika. Watu wanafuga nyuki kwa wingi lakini mapato

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

mbona yanateremka? Ukichukua 2003 tulifika mpaka *one million dollar* leo tuko *four hundred and six*. Sasa huoni ile *development* ya kwamba kazi kubwa ya utalii inafanyika lakini mapato yanayopatikana ni kidogo sana. Sasa nafikiri kuna jambo hapa linatakiwa lifanyiwe kazi. Ama yanavuja pahala au hayakusanywi vizuri na haya ni maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la utangazaji. Wenzangu wengi wamelizungumzia kwamba kama utalii hautangazwi basi hatuwezi kupata *revenue*. Tumekuta katika nchi nyingine mbalimbali wanatumia asilimia kubwa sana ya fedha zao wanazozipata katika kuitangaza nchi, bado *speed* yetu ya kutangaza haijakuwa nzuri. Vilevile utunzaji wa mapato siyo mzuri. Hili Waziri lazima mlisimamie, suala la utunzaji wa mapato siyo mzuri hata kidogo, kuna haja ya kuliangalia. Hata ile 10% inayotakiwa mashirika haya yalipe Serikalini inakwama kwa sababu hakuna utunzaji mzuri wa mapato. Nalo nafikiri ni eneo lingine linalohitaji kuangaliwa sana kwa sababu utalii peke yake unaweza kutuingizia *revenue* ya kutosha na tukaweza kuendesha Serikali yetu bila ya kutegemea mapato kutoka kwa watu wengine.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa sana kulisemea ni suala hili la uhifadhi wa mazingira. Hili linaendana pamoja na *ecotourism*. Bado hatujalifanyia kazi vizuri na nafikiri bado hamjaunganisha nguvu zenu baina ya Wizara inayoshughulikia na mambo ya mazingira na Wizara ya Maliasili na Utalii, hili ni eneo ambalo mngeliangalia sana. Kwa mfano, kuna mambo ya utalii wa samaki wale wa mapambo, inaingiza *revenue* kubwa sana na watu ni wachache sana wanaokwenda lakini wanaingiza mapato makubwa sana lakini hauendelezwi, umeachwa tu, wala huna taarifa unazozipata kwamba sekta hii inaingiza mapato kiasi gani. Nakumbuka tulipokaa na wataalam wako walisema kama sekta hii peke yake ikiendelezwa inaweza ikatupa *revenue* za kutosha. Sasa kuna maeneo mengi ya utalii bado mengine hayajasimamiwa vizuri, mimi nafikiri mngeweza kuyasimamia na mapato yakaongezeka katika nchi. Kubwa zaidi nasema suala la usimamizi ni la muhimu sana. Ushawishi wa wenzetu nchi jirani kutumia fursa zetu ni mkubwa sana, tunahitaji kuwa makini. Mwalimu toka miaka hiyo aliona alikuwa *focused* alijua kwamba hili tukilifungua litatumiza sisi Watanzania na akalinda rasilimali hizo, tuendeleo na *spirit* ya kulinda rasilimali zetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, sijui kama yupo. Kama hayupo namwita Mheshimiwa Kigola, atafuatiwa na Mheshimiwa Bura.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naanza kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pamoja na kuwapongeza, kuna changamoto nyingi ambazo tunazona na sisi kama Wabunge ni lazima tuziseme ili waweze kuangalia jinsi ya kuzitatua.

Mheshimiwa Spika, kuna masuala mengine ya kujiuliza kwamba binadamu na hifadhi kipi kinaanza? Kwa akili ya kawaida tu anaanza binadamu na ndiye anatumiza misitu. Sasa tunaona kuna maeneo mengi sana ambayo ilichukuliwa na Serikali miaka ya nyuma wakati idadi ya watu ni chache na kila siku hilo tunaliongea na bahati nzuri sana hata Mawaziri waliopita hilo tatizo waliliona. Kwa mfano, Waziri Maige alipokuja Wilaya ya Mufindi alitembelea vijiji ambavyo vina hifadhi ya maliasili na ilionekana kwamba idadi ya watu inakuwa na hawana maeneo ya kulima wala maeneo ya kujenga shule. Katika mapendekezo yale, vile vijiji viliambiwa kwamba wanaenda kufanyia kazi halafu yale maeneo wataachiwa, hilo la kwanza.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, la pili amekuja Maige naye, alitembelea vijiji vile na bahati nzuri sana hata Mheshimiwa kaka yangu Mgimwa hili suala analijua. Wizara ilikiri kabisa kwamba kwa sababu watu wameongezeka kwa hiyo watatoa kauli wananchi wale waweze kuachiwa yale maeneo. Kwa mfano, kuna kijiji cha Ihomasa, Maduma, Kilolo, Kitasengwa, Uyela, hospitali ya Usokami ambako ni Jimbo la mwenzangu, kuna Kibengu ambako kuna eneo kubwa sana wanashindwa hata kujenga shule. Sasa Mheshimiwa Waziri ninakuomba wakati unakuja kutoa majumuisho kwa sababu suala hili ni la muda mrefu na Kamati ilishaundwa na wakaliona hilo, basi leo muweze kuwatamkia wazi wananchi wale waweze kujenga shule, waweze kupata sehemu ya chakula. Wilaya ya Mufindi sasa hivi kila kona wamepanda misitu. Wananchi wanashindwa pa kulima. Sasa yale maeneo niliyoyataja naomba Wizara hii iweze kuchukua hatua za haraka ili tukifika mwezi Novemba au Desemba waweze kuweka maandalizi ya maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine linahusiana na uvunaji wa misitu katika Wilaya ya Mufindi. Kwanza, naipongeza Wizara kwa utaratibu wa mwaka jana. Utaratibu wa mwaka ulikuwa nzuri sana kwamba Wizara iliweza kuangalia hata vijiji. Vijiji vingi sana vilipewa vibali. Wizara iliweza kuangalia Kata, Kata nyingi sana zilipewa vibali na watu walipewa vibali. Kwa utaratibu wa mwaka jana nakubaliana na Wizara. Hata hivyo, kulikuwa kuna jambo moja ambalo lilijitokeza siku za nyuma na sisi Wabunge hapa tukaongea, ilitokea kwamba waanze kukaguliwa mashine na watu walipeleka mashine pale wakapata gharama, hilo tukaongea mwaka jana halikufanyika hivyo na sisi tunashukuru kwa hatua zile zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna tatizo moja ambalo linakuja kujitokeza kwa wavunaji kwamba mwaka huu wananchi wengi sana wameomba vibali pale lakini kila mwananchi mmoja kwa fomu moja amejaza kwa shilingi elfu hamsini. Sasa unaweza ukaona katika familia labda wameomba watu hata watano, maana yake anatakiwa alipe karibu laki moja ili aweze kubahatisha labda atapata. Sasa sijaelewa Wizara ilivyochukua hili, sijui kama mliwashirikisha vizuri wananchi wale kwa sababu isije ikatokea kwamba mtu anatoa elfu hamsini akiwa na imani kubwa kwamba anaweza kupewa kibali. Sasa asipopewa kibali hiyo inakuwaje, kwa sababu tunasema kwamba kabla hatujafanya kitendo chochote inatakiwa kwanza kuwashirikisha wadau kwamba mwaka huu tunaweza tukatumia utaratibu huu. Sasa kama hatuwashirikishi wadau, tunachukua maamuzi haraka ikitokea baadaye wananchi wale wanaanza kulalamika, inaleta shida sana na tukizingatia kwamba msitu ule wa Mufindi watunzaji wakuu ni wana Mufindi wenyewe. Sasa isitokee wanalipia elfu hamsini matokeo yake wasipate kitu chochote, hii italeta shida sana kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine tunaona kwamba kuna watu wameanza kuwa kama wakala fulani. Sijui niseme ni wakala bubu. Mtu anapewa kibali, akipewa kibali anaanza kusema yeye ndiye amefanya mpango, mwananchi achangie milioni tano na hizi message ni nyingi sana nimepewa hata jana kwamba kuna wananchi wameanza kuchangia milioni tano kwa kila mmoja. Sasa mimi najiuliza hizo milioni tano za nini? Naomba Mheshimiwa Waziri hili aliangalie kwa makini sana isionekane kama ule Msitu wa Sao Hill wa watu fulani fulani wanachangisha hela. Mtu ana haki ya kupewa kibali na wale watu wanaosema kwamba labda wanatumwa na mtu fulani hebu wafuatiliwe wasije wakatuharibia sifa, wasituharibie sifa na hii itatuharibia sana sisi viongozi. Bahati nzuri kuna watu wamesema wamempigia hapa Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani analijua, sasa namwomba anapokuja kuhitimisha hapa aweze kulitamka hilo na kulikemea haraka sana. Hatuwezi kulivumilia kama kuna mtindo wa namna hiyo, maana yake wavunaji wa kawaida wale hawawezi kupata vibali kama kuna watu wanachangiachangia hela za ajabu ajabu hapa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni la mnada. Suala la mnada hili kwa *practical* ya haraka haraka kama kuna watu tayari wanaanza kuchombeza hela maana yake wale

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wavunaji wadogo hawawezi kupata hata siku moja, hawawezi kuingia kwenye ushindani wa minada. Mimi naomba masuala ya mnada tuachane nayo, tuendelee na utaratibu wa kawaida wa kuwapa wananchi.

Mheshimiwa Spika, halafu napenda niombe tena kwa mwaka huu tufanye kama mwaka jana, vijiji vyote vipewe, Kata zote zipewe na kuna vikundi vingi sana, bahati nzuri Wizara imehamasisha wananchi kwamba wawe na vikundi, vikundi vingi sana vimeomba. Mwaka jana mmetoa vibali kwa vikundi vichache sana. Sasa naomba mwaka huu vikundi vilivyoomba viweze kupewa. Bahati nzuri sana hata shule za msingi sasa hivi wameomba. Nadhani tukitoe hata kwa shule za msingi ili waweze kufanyia kazi kwenye shule zao, tutakuwa tumefanya jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kimoja ambacho nataka niongee maana hili ni tatizo la kitaifa. Kuna shule zingine, kuna siku moja nilikuwa naangalia kwenye TV nadhani ni Mkoa wa Tabora au Mkoa gani sijui, kuna wanafunzi wanakaa chini kwa sababu hawana madawati. Katika *East Africa* nchi inayotoa mbao na ambayo ina msitu mkubwa ni Tanzania. Sasa itakuwaje watoto wetu wanakaa chini wakati sisi tuna misitu mikubwa. Ukienda Tanga kuna msitu, ukienda Bukoba kule kuna msitu, ukienda Mufindi kuna msitu, sasa kwa nini watoto waanze kukaa chini? Hii inatuletea aibu kwa sisi Watanzania. Sasa nataka niombe Wizara hii iweze kuangalia kuhakikisha kwamba watoto wetu wote wanaweza kupewa madawati kutokana na msitu wetu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine mwaka jana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Nashukuru, muda umeisha.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Nilisema Mheshimiwa Felister Bura, atafuatiwa na Mheshimiwa John Lwanji.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi ya leo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri pamoja na watumishi wote wa Wizara hiyo pamoja na Katibu Mkuu, Dada yangu Maimuna Tarishi kwa kazi nzuri anayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii huchangia asilimia 17 ya pato la Taifa pamoja na changamoto mbalimbali zinazoikabili Wizara hii na hasa changamoto ya ujangili kwa wanyamapori. Waziri amesema wazi katika ukurasa wa nane wa hotuba yake kwamba matokeo ya sensa ikolojia ya Selous na Mikumi kwa mwaka 2006 tembo walikuwa 70,406 lakini ilipofika mwaka 2013 tembo 57,322 walikwishauawa. Katika ikolojia ya Ruaha mwaka 2006 kulikuwa na tembo 35,461 lakini baada ya miaka saba tembo 15,371 walikwishauawa.

Mheshimiwa Spika, hii ni hali mbaya na ya kutisha sana pamoja na kwamba watumishi wa Wizara hii na hasa Askari wa Wanyamapori wanafanya kazi katika hali ngumu, wanapambana na majangili ambao wanatumia silaha kali mno. Wakati huo TRA hawakuona umuhimu wa kuruhusu silaha mapema na silaha zikakaa mwaka mzima bila kuruhusiwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

bandarini, Serikali kwa Serikali na watumishi ni wachache sana hasa Maaskari wa Wanyamapori. Ninaamini kwamba Waziri utalishughulikia hili kwa haraka ili Maaskari waajiriwe wengi kiasi cha kutosha na kazi iwe nyepesi, silaha zipatikane, magari yapatikane kwa muda. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niungane na Kamati ya Maliasili na Mazingira kusema kwamba Operesheni Tokomeza ilifanya kazi nzuri. Sijui kwa nini bado wale watumishi ambao walihusika na kazi hii ambao walikuwa ma-cordinator tu, maana waliofanya kazi hii pamoja na Askari wa Wanyamapori walikuwepo Polisi, walikuwepo Wanajeshi lakini wale Wakurugenzi ambao walikuwa ni ma-cordinator bado tunaona kwamba hawakufanya vizuri. Kama hawakufanya vizuri warudishwe walikotoka au watafutuiwe kazi nyingine. Kama leo tunapongeza kazi iliyofanyika na Kamati ileile kwamba Operesheni Tokomeza ilifanya kazi nzuri wale Wakurugenzi tuwatafutie mahali tusiwadhalilishe.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Rais kwamba Tume ile aliyoiunda ikafanye kazi haraka na Operesheni Tokomeza iendelee kwa sababu hata ujambazi wa kuteka magari na kuvamia mabengi umepungua kwa sasa. Wakati malumbano yanaendelea nani awe Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori na nani asiwe Mkurugenzi, majangili wanaendelea kuvuna wanyama kule. Mheshimiwa Waziri naomba uchukue maamuzi ya haraka ili Mkurugenzi wa Wanyamapori apatikane. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimehuzunishwa na mambo ambayo yanaendelea katika Wizara hii. Kama tunavyojua Wizara ina Kanuni na Kanuni ndiyo zinazoongoza Wizara. Kanuni moja inasema kwamba inapofika Desemba uwindaji usimame ili wanyama wasibughudhiwe na wazae, ndiyo kipindi cha wanyama kushika mimba. Cha ajabu Kanuni imekiukwa na sasa agizo limetoka kwamba uwindaji utaendelea mpaka Machi. Je, aliyeruhusu au ni nani huyo anayemshauri Waziri kukiuka Kanuni ambazo tumejiwekea sisi wenyewe? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninakuomba, Waziri utakapokuja kujibu hili ulijibu na utuambie huyo anayekushauri vibaya, maana Waziri tunakuamini, tunakupenda, tunajua unaweza kazi yako vizuri. Lakini, anayekushauri vibaya kwamba uwindaji uendelee kipindi ambacho wanyama wanapata mimba na anakufanya ukiuke Kanuni, huyo ndiye tunataka ku-deal naye.

Mheshimiwa Spika, lakini pia fedha hizi za ada zinazolipwa na makampuni mbalimbali yanayomiliki vitalu ndiyo fedha zinazopelekwa katika maeneo ya mapori yetu, mapori ya akiba. Lakini, Kanuni inasema walipe mpaka mwezi wa 3, lakini sasa muda umesogezwa mpaka mwezi wa 6. Mheshimiwa Spika, ninaomba kumjua huyo anayemshauri vibaya Waziri.

Mheshimiwa Spika, tulitunga Kanuni kwamba, 85% ya umiliki wa vitalu iende kwa wazawa, lakini tumeona wazawa wasivyoweza kuendesha vitalu hivi. Namuomba Mheshimiwa Waziri alete Sheria hapa tuibadilishe, ili ikiwezekana wageni wamiliki 40% wazawa wabaki na 60%.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Waziri aniambie, kwa nini hataki kuunda Bodi ya Ngorongoro? Tatizo ni nini? Miaka nenda rudi Ngorongoro haina Bodi, TANAPA haina Bodi kwa sasa, TAFIRI haina Bodi kwa sasa. Je, mnayataki mema mashirika haya? Mashirika haya ndiyo yanayokusanya maduhuli makubwa katika Wizara hii, lakini hayana Bodi. Ngorongoro ni zaidi ya miaka minne, ukiwa Naibu Waziri na leo wewe ni Waziri, Ngorongoro haina Bodi, unawapa hali ngumu hawa Wakurugenzi ambao wako katika Bodi hizi. Mheshimiwa Spika, ninakusihi na kukuomba, Waziri atakapokuja kujibu atuambie ni lini mashirika haya yatakapopata Bodi zao?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, wale ambao wanamiliki vitalu na ni wazawa, na wameshindwa kuendesha vitalu hivi; ninakusihi Mheshimiwa Waziri vitalu hivi virudishwe, vitangazwe upya, pamoja na yale ambayo yamekosa ubora kwa sababu ya mifugo na shughuli za binadamu kuendelea katika maeneo yale. Haya ndiyo yamezungumzwa, hasa mambo ya mipaka kwamba mipaka sasa ionekane vizuri na vitalu hivi ambavyo havina ubora, basi viwe na ubora, ili vitangazwe upya na vipate wamiliki na Serikali iweze kupata mapato kutokana na vitalu hivi.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri kwamba wameamua sasa kuanzisha Mamlaka ya Wanyamapori. Hii itasaidia sana katika kukusanya maduhuli na kutatua matatizo mengi ambayo yanaonekana katika Idara hii. Na-*declare interest* kwamba mimi ni mdau mkubwa sana katika Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa hiyo, kuna haja na kama ulivyosema kwamba, mpaka mwezi Julai Mkurugenzi wa Mamlaka atakuwa amekwishapatikana kwa ajili ya kuanza kazi na kwa ajili ya mamlaka kuanza kazi. Tunategemea Kanuni pia zitatungwa mapema...

(Hapa Sauti ilikatika ghafla)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Asante. Sasa nitamuita Mheshimiwa Lwanji, atafuatiwa na Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie juu ya hoja ya Wizara hii.

Awali ya yote ninaunga mkono hoja hii na nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya, ameongoza *operation* maalum juzijuzi hapa katika Wilaya ya Manyoni na wakafanikiwa kukamata shehena kubwa ya meno ndovu katika harakati za kukabiliana na tatizo la ujangili. Tunawatakiya basi kila la heri waweze kutokomeza tatizo hili kubwa la nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niwapongeze kusikia kilio chetu cha muda mrefu, mimi ni mmojawapo niliyepigania sana tuwe na Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania – TAWA. Na kama mnavyojua sisi tuko pembezoni au tuko sambamba na mbuga au mapori ya akiba ya Rungwa, Muhesi, Kizigo na Mbuga za Chaya. Mapato mengi yanapatikana ambayo yanaingia katika Idara ya Wanyamapori, lakini kwa muda mrefu tulikuwa na mpaka sasa hatupati fedha za kutosha, hazirudi, sehemu kubwa zinatumiwa kwa shughuli za utawala katika Idara hiyo na kuacha vijiji vikiwa havina msaada wowote mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuundwa kwa Mamlaka hii nadhani inaweza kuwa tiba mojawapo ya kuweza kuvisaidia vijiji, si kupata 25%, ikiwezekana hata 75%; fedha chache zibaki katika Mamlaka hiyo, lakini fedha nyingi ziweze kuelekezwa kuweza kunusuru au kuweza kuvipa maendeleo vijiji vilivyo kandokando ya hizi Hifadhi au Mamlaka ya Mapori haya.

Mheshimiwa Spika, mimi ninalaumu uamuzi..., sioni wivu, lakini nashangaa jana wakati Mheshimiwa Waziri anatamka kuundwa kwa Mamlaka hii wamesema Makao yake Makuu yatakuwa Mjini Morogoro. Ni kweli, lakini inawezekana kuna sababu, labda kwa sababu ya *Selous*, lakini na sisi tuna mapori makubwa na hiyo *advantage* na sisi tunayo; na *advantage* nyingine tuliyonayo ni kwamba, sisi tuko katikati na ndiyo maana Manyoni ni Makao ya Kanda ya KDU yakawekwa pale.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Na mimi nilifikiri Mamlaka hii ingefananafanana na hali yenyewe ya Kazi, ni *wildlife*, sasa kwenda kuweka mijini huko, miji ya raha, ee miji ambayo kila kitu Mamlaka imepelekwa pale, rasilimali nyingi zinapelekwa, nadhani tungesambaza.

Mheshimiwa Spika, ningeomba kupata vigezo vilivyotumika, bila shaka kama ni wadau basi wadau wetu walipigwa mweleka kwa sababu ambazo hazijulikani. Mimi nilifikiri Makao hayo ya Mamlaka yangekuwa katikati ya nchi na hasa Manyoni, ili waweze kuwa *mobile* vizuri kuweza kufikia maeneo mengine katika *operation* zao kwa mfano mapori ya akiba 28 na mapori tengefu 42 haya yaweze kufikiwa kwa urahisi zaidi. Kwa hiyo, nadhani Wizara ijaribu kuangalia. (Ma)

Mheshimiwa Spika, kitu cha pili, mimi bado sijaridhika na jinsi Mfuko huu wa *Tanzania Wildlife Protection Fund* unavyofanya kazi au unavyogawiwa. Mfuko huu wa Hifadhi ya Wanyamapori kwa muda mrefu hatujaelewa jinsi unavyo-*disburse funds* zake katika Vijiji husika au katika maeneo husika. Kwa sababu, nilidhani kwamba, ingekwenda kusaidia katika maeneo ambayo yanahusika, haya mapori yaliyotengwa pamoja na misitu, lakini tatizo lake ni kwamba, yanakwenda kuweza kusaidia maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, mimi ninakumbuka mwaka 2007, takribani miaka 7 sasa imepita, tulipata fedha shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la Rungwa, lakini bwawa hili mpaka leo halijajengwa kwa kisingizio kwamba, fedha hizo hazikutosha. Na kwamba, wanajaribu kuona kama wanaweza kuongeza fedha zingine. Sasa hii ilikuwa *statement* ya miaka 7 iliyopita, na bwawa lile liliharibiwa mpaka leo halijaweza kujengwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningependa kupata maelezo wakati wa majumuisho ni kwa nini na hasa fedha hizi ziko wapi sasa? Zimeenda wapi hizi milioni 250? Na shahidi ni Mheshimiwa Lekule Laizer hapa, alikuwa *Board Member*, ndiyo tulipata, lakini tokea wakati ule hatujaona msaada wowote kutoka katika mfuko huu. Fedha hizi zinapekwa mijini ambako hazihusiani kabisa na shughuli zenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ningeomba suala la migogoro ya mipaka, na hasa hili la *buffer zone*, liangaliwe. Tuliomba Kijiji cha Lulanga, Wilaya ya Manyoni, Tarafa ya Itigi, ambacho kiko karibu kabisa na mpaka wa Mbuga ya Muhesi, waweze kusogeza. Hili liliwezekana kwa Kijiji cha Doroto, kwa nini isiwezekane kwa Kijiji cha Luhanga? Kwa nini isiwezekane? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, na hii *buffer zone* hii au hizi mita 500 kutoka ukanda na makazi ni mita chache sana. Mimi ningeliomba na ninapendekeza kwa Wizara kwamba, zingelikuwa mita 5,000, kilometa 5 kutoka hapa. Mpaka wa Doroto walifanya hivyo na wananchi wanaishi kwa amani na hakuna *friction* yoyote. Ninaomba nipate majibu juu ya hiki Kijiji na Vijiji vingine ambavyo tuliviombea. Maandishi yako pale Wizarani.

Mheshimiwa Spika, *fine* zinazotozwa kwa wananchi wanapoingiza mifugo yao katika maeneo haya kwa kweli wanawafilisi wananchi. Shilingi milioni 2, 5 mpaka 10 mtu mifugo yake iko pale atoe, ni kumfilisi. Ninaomba Serikali ije na mkakati wa kuweza ku-*review rates* hizi, atozwe ng'ombe mmoja, wawili na kwa kawaida huwa wanafuata maji. Basi watoe fedha, watenge fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa nje ya hifadhi hizi, ili watu waweze kupata maji kwa urahisi na kuacha kuingia katika maeneo hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lingine ni hizi fidia zinazotolewa kwa uharibifu wa mazao na wanadamu kuuwawa na wanyamapori, bado hazitoshi. Shilingi laki 2, shilingi laki 5, mtu katafunwa na samba, shilingi laki 5 analipwa, familia yake inaachwa, maana wanyama hawa ni mifugo ya Serikali. (Makofi)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. Na ninaomba Wizara ilifanyie kazi suala hilo. Asante sana. (Makofi)

SPIKA: Asante. Sasa namuita Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Massele, hayupo! Mheshimiwa Msigwa endelea.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Binafsi nianze kwanza kuipongeza Wizara ya Mazingira, Wizara ya Maji na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kwa sababu, tunapozungumzia Wizara hii, tunazungumzia masuala ya mazingira. Na tunapozungumzia Wizara hii ni kutunza mazingira kabla ya kuanza biashara.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza hawa kwa sababu, katika Manispaa yangu ya Iringa, kuna watu walikuwa wanataka kujenga stendi kwenye maeneo ya vyanzo vya mto mkubwa, Mto Ruaha, ambao ulikuwa ni uchafuzi wa mazingira ambao baadaye ungetuletea shida katika Manispaa yetu ya Iringa. Na nichukue fursa hii kusema kwamba, sasa tutapata maji safi kwa sababu, watu wa UN walitoa fedha ambazo tulijenga chanzo cha maji cha bilioni 74, sasa stendi ya bilioni 4 tusingependa ituchafulie mazingira. Kwa hiyo, naipongeza hata Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa kusimamia suala hili. Sasa nawahakikishia wakazi wa Manispaa ya Iringa kwamba, tutaendelea kupata maji salama kwenye mji wetu ambao ni 99% ya maji ambayo tunayapata katika mji wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nirudi tena kwenye Wizara hii. Mzungumzaji mmoja aliyepita amezungumzia masuala ya Bodi; katika mashirika haya yaliyoko katika Wizara hii, mashirika karibu yote yamekuwa hayana Bodi. Ngorongoro kumekuwa hakuna Bodi na Mheshimiwa Waziri mwaka jana nilikuuliza swali mwenyewe hapa, ulisema kwamba, bodi ingekuwa imeundwa ndani ya wiki mbili, lakini sasa hivi ni zaidi ya miaka miwili, Bodi ya Ngorongoro haipo. TANAPA hakuna Bodi na maeneo mengine hakuna Bodi na maeneo haya yote Bodi zinapokuwa hazipo ndipo kunakuwa na mianya mingi ya wizi wa fedha, kunakuwa na uingiliaji mkubwa wa watendaji wataalamu ambao wako katika maeneo haya. Kwa hiyo, ninaomba Waziri baadaye katika majumuisho yake anieleze ni kwa nini hakuna Bodi katika Mashirika hayo ya Umma? Na ni lini sasa Bodi hizo zitawekwa kwenye Mashirika hayo, ili Taratibu na Sheria zifuatwe katika utendaji, kusudi tuokoe pesa nyingi katika Mashirika hayo?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba, jana nilitoa ushahidi, lakini Kampuni hii ya *Green Miles* ina ukiukwaji mkubwa. Ningeomba nisisitize tena kwa upya kwa sababu, kampuni hii katika kuwinda, tumekuwa tukizungumza sana masuala ya ujangili. Sasa hawa ni aina ya majangili ambao wanafanya ujangili kwa *license*, wako *licensed*. Kwa sababu, wanapokuja kutoka nje wengine wanakuja kwa hadhi za kiuongozi, wanakuja na misafara na *protocol*. Hawa wanapokwenda kuwinda wanakuwa na walinzi, wengine ni wana wa Wafalme kutoka huko nje. Wanapokwenda kuwinda wanakuwa wana walinzi, wanawinda bila *PH (Professional Hunters)*. Ukiangalia wanawapiga ndege ambao hawaruhusiwi kupigwa, wanawapiga wanyama ambao hawaruhusiwi, wanawachezea hata pundamilia. Kwa mfano ametoka kuzaliwa, wanaanza kumkamata kinyume kabisa na Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, hawa ni watu ambao wako *protected*, kama watu ambao wana *license* wamekiuka sheria namna hii, je, wale ma-poachers ambao wanajificha usiku tutawezaje kuwadhibiti? Kwa sababu hawa wanaheshimiwa, wana misururu mikubwa ya magari, wanawinda na *private numbers* za magari, kinyume kabisa na Sheria ya Mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kanuni zilizokiukwa katika kampuni hii, haikupaswa iendelee kuwa kampuni inayofanya shughuli za uwindaji katika nchi yetu. Ningekuomba

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Waziri, kama kweli tuko *serious* na ku-*protect* wanyama wetu, ninaomba kampuni hii ichukuliwe hatua mara moja. Ninajua taarifa unazo ofisini kwako, ninaomba ichukuliwe hatua za mara moja kwa sababu ni ukiukwaji wa hali ya juu, wamevunja sheria nyingi na kanuni nyingi katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi kubwa ambayo sisi kama Mawaziri Vivuli tunafanya, Mheshimiwa Waziri, una timu kubwa ya Wakurugenzi popote unapotaka kupata taarifa unapiga simu kirahisi tu, lakini sisi Mawaziri Vivuli tunafanya kazi kwa shida, hatuna *information, information ni limited*. Ningeomba hii michango ya shida tunayoileta muifanyie kazi kwa sababu, tunaipata kwa shida sana. Muifanyie kazi na muitumie, ili kuisaidia Serikali kuokoa wanyama wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingiine; Mheshimiwa Waziri, pamoja na kwamba, *Operation Tokomeza* ilileta madhara sana katika nchi hii, lakini wale wote waliofanya kazi ya *Operation Tokomeza*, vijana wengi, wana malalamiko makubwa, hawajalipwa pesa zao mpaka leo. Zilichangwa fedha karibu bilioni 3 zilizotumika kwenye hiyo *Operation tokomeza*, lakini hamjawalipa pesa zao. Wanalalamika, walilala na njaa, wengine walifanya kazi kubwa. Pamoja na kwamba, ilikosewa, lakini pesa zao hawajalipwa mpaka leo. Nikuombe Waziri, hebu fanyeni utaratibu muwalipe pesa zao hawa vijana, siku nyingine mtawahitaji wafanye kazi, mtawahitaji washughulike kwenye *operation* nyingine. Ninaomba mufanye kila linalowezekana kwa ajili ya kuwalipa fedha zao.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine Mheshimiwa Waziri, ni hili la kuongeza muda wa uwindaji, ambao mzungumzaji na yeye amezungumza kwamba ina-*disturb* sana wanyama wanapokuwa wakati wa uzazi. Swali langu nataka nikuulize, huu muda mnaotaka kuuongeza je, mnaongeza na *quota* au *quota* inabaki ileile? Kwa sababu, muda unapokuwa mrefu *of course* wawindaji watafurahi, watapenda kwa sababu wao wanapata zaidi. Ningeomba nipate ufafanuzi, *quota* inabaki ileile au mnaongeza muda tu? Lakini kwa ushauri wangu muda uliokuwepo unatoshia, kwa sababu tunataka wanyama wasiwe wanakuwa *disturbed*.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, Mheshimiwa Waziri, muda mrefu tumezungumza sana kuhusu utangazaji wa Mbuga ya Ruaha, Mbuga kubwa, haijatangazwa vyakutosha kama mbuga za Kaskazini. Tunaomba mbuga hii itangazwe kwa sababu, inapokuwa imetangazwa, upande wa Kusini mapato yataongezeka. Mji wangu wa Iringa Mjini (Manispaa) tunakosa mapato mengi kwa sababu watalii wanapanda ndege moja kwa moja kutoka Dar es salaam kwenda Ruaha; wangetua Iringa Mjini pale, wangelala kwenye hoteli. Wakilala kwenye hoteli, hata akinamama wanaouza mbogamboga, *taxi*, watapata fedha, fedha itapatikana pale. Na barabara kutoka Iringa Mjini imekuwa mbovu, ninakuomba Wizara yako ishirikiane na Wizara ya ujenzi, mhakikishe barabara inajengwa mapema. Na hiyo barabara inapita hata kwenye Jimbo la Mheshimiwa Lukuvi na yeye atafaidi, wataokota mbogamboga kule njiani na yeye mapato yataongezeka katika Jimbo la Isimani. Nikuombe Waziri, tumepiga kelele sana Mbuga ya Ruaha, iongezeke, muifanyie mkakati mkubwa, ili pato hili liende na upande wa Kusini.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine, sielewi ni utaratibu gani ambao mnapata katika hii Sera ya Ulinzi Shirikishi. Maeneo mengine yote ya mbuga ukilinganisha, nilitaka nipate ni kiasi gani kwa mfano watu wanaozunguka Ruaha katika Ulinzi Shirikishi, mmewashirikisha vipi katika kuwahusisha na wanafaidi vipi. Kwa mfano na TANAPA, ni kiasi gani TANAPA imetoa michango katika Ulinzi Shirikishi wa wakazi wa Mbuga ya Ruaha, ukilinganisha na maeneo mengine?

Mheshimiwa Spika, mzungumzaji anayetoka katika Jimbo la Mbarali amezungumza sana, tusipowashirikisha wananchi ulinzi wa wanyama utakuwa ni tatizo sana. Ningeomba hili suala mulifanyie kazi, tuone hawa watu wanafaidi vipi, wale waliozunguka Mbuga ya Ruaha ambayo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

ni kubwa nchini, wamepata kiwango gani cha fedha ukilinganisha na mbuga zingine kulinda ile mbuga ili nao waweze kuwalinda hao wanyama?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa, shirikiana na Wizara ya Ujenzi barabara ijengwe ili wakati wa Kusini, pamoja na kwamba na Iringa, lakini na Katavi nayo muiangalie nao wafaidike na mbuga hizi za wanyama ambazo kimsingi zimekuwa kubwa na zina vivutio vikubwa. Ukiangalia wenzetu wa Kaskazini walitangazwa muda mrefu, tunaomba kama mlivyotangaza katika Wizara kwamba utalii umehamia *Nothern Circuit*, sasa hivi tunawaomba huo mkazo muutilie maanani utangazwe kwa hali ya juu sana kusudi watu wa Kusini nao wapate kufaidika na huu urithi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho; wamezungumzia kuhusu masuala ya misitu. Maeneo yenye madini watu wenye madini wanagawio rasmi maalum kwa ajili ya madini. Sasa watu wa Iringa tunazalisha mbao. Ni mpango gani maalum ambao nao wanapata rasmi kwa sababu ya mbao hizo wanazopata, kwa sababu hata hivi vibali wanang'ang'aniwa, wana-*compete* na watu wengine, wao peke yao hawana mgao rasmi kama wa madini. Kama watu wa madini wanapata mgao rasmi na sisi tunazalisha mbao ambazo tunazisafirisha nchi za nje, wale watu wa Mufindi na maeneo mengine ya Iringa wao wanatengewa kitu gani rasmi kwa ajili ya uzalishaji wa mbao kwa sababu Mungu alitupendelea hali ya hewa mbao zipo kwa wingi ambazo hatuna sababu hata watoto wetu wakae kwenye mawe yenye ncha kali.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi, asante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Kumbe siku nyingine unaweza kuongea vizuri mno! Ahsante sana. Sasa nilikuwa nimemuita huyu anaitwa Agustino Manyanda Masele, naona sijamuona. Anafuatia Mheshimiwa Abdulsalaam Amer, yupo? Hayupo! Sasa anayefuatia Mheshimiwa Mabumba, hayupo. Mheshimiwa Mntangi atafuatiwa na Mheshimiwa Zaynabu Vullu.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia japokuwa kwa muda mfupi kidogo. Kwanza katika Historia Wizara hii ni moja kati ya Wizara ambazo kwa kweli ni muhimu sana katika kukuza pato la Taifa. Kwanza, katika sekta ya utalii tunategemea fedha nyingi zitapatikana kutokana na watalii wanaokuja, lakini vile vile katika kulinda na kuhifadhi wanyamapori. Kwa hiyo ni vizuri kwa kweli hii Wizara ikafanya kazi zake vizuri kwa madhumuni hayo hayo ya kuhakikisha pato la Taifa linaongezeka. Kwa hiyo kikubwa leo nataka niseme naipongeza Wizara kwanza kwa kuanzisha hiyo Mamlaka ya Wanyamapori. Siku zote tumekuwa na wanyama, lakini hatukuwa na sheria nzuri za kuwalinda wanyama hao na kuwawekea misingi mizuri ya kusaidia hata wale wanaokaa katika maeneo yanayozunguka misitu kutambua hilo na kuheshimu wanyama wale. Sasa tunaunda hiyo mamlaka, lakini na sheria pia ya wanyamapori lazima tuhakikishe inafanyiwa kazi, hilo moja kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ambalo ni muhimu, nimezungumzia sekta ya utalii ni vizuri tukajitahidi sana kutoa elimu kwa hawa hasa sekta binafsi zinazohudumia watalii, na ninaposema sekta binafsi maana yake ni nini? Tuna sekta binafsi ya usafiri ambayo inahudumia watalii, lakini vile vile tuna sekta ya malazi kwa ajili ya watalii. Hawa wote wanawahudumia watalii, tujitahidi kuhakikisha wanapata elimu waweze kuwa-*handle* vizuri watalii wetu ili wanapokaa hapa nchini wajisikie vizuri na hata wanapoondoka wasifie huduma ambazo zinatolewa na sekta hizi binafsi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa nije katika eneo langu la Muheza. Katika eneo langu la Muheza naomba niikumbushe Wizara sasa, kuna madai ya fidia ya wananchi katika hifadhi ya Delema. Wananchi hawa walikubali kuhama ili kupisha eneo la

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

msitu wa Delema. Wako wananchi 1,028 walilipwa fidia na mimi ninakiri zaidi ya shilingi bilioni 3.5 zililipwa kama sehemu ya fidia. Lakini wananchi hao walijiona kama wamepunjwa katika fidia hizo. Naomba nithibitisha kwamba nimekamilisha kutafuta vielelezo vyote na nimevipeleka katika Wizara mvifanyie kazi, mchambue halafu tupate majibu ya uhakika kwa maandishi kama wananchi wale wana haki ya kuendelea kupata fidia kwa mpunjo huo ambao wanadai au hawastahili, ili tuondoe mgogoro. Tunachotaka ni kuendelea kuwasaidia wananchi hawa kwa kuwapatia maeneo ya mashamba ambayo tumekwishaandaa.

Naomba leo pia nimshukuru hata Mkuu wa Wilaya amefanya jitihada hizo, mashamba hayo yamepatikana, tutakwenda kuwahifadhi wananchi hawa 1,028 katika mashamba mapya, lakini tunatamka suala lao la fidia lifanyiwe kazi na tupate majibu ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo Wizara imeandaa utaratibu wa kufanya ziara ya mafunzo katika hifadhi ya misitu. Sisi Wilaya ya Muheza tuna maeneo makubwa, tuna msitu mkubwa wa miti ya Lunguza pamoja na Hifadhi kubwa ya Msitu wa Amani. Ninaomba wakati wa utekelezaji wa mpango huo Wilaya ya Muheza iwepo katika orodha. Tumeona kwamba mmesema mtapitia vijiji, lakini orodha ya vijiji ambavyo mtapitia kufanya kazi hiyo havijatajwa. Basi ninaomba katika Wilaya ya Muheza tuisahauliwe.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni hili ambalo mmelisema kwamba mtasaidia katika ujenzi wa barabara katika maeneo ya hifadhi, naomba nirudie tena, Muheza tuna shamba kubwa sana la miti ambalo linaingizia Taifa hili fedha nyingi, shamba la Lunguza. Ninaomba katika mpango wenu wa barabara ambao mmetaja kilomita ambazo mnakusudia kuzifanyia kazi miongoni mwa kilomita hizo basi muweke na barabara ya kutoka katika msitu ule wa Lunguza kuelekea katika kijiji cha Kambai, hao ndiyo wahifadhi wakubwa wa msitu ule wa Lunguza. Tunaomba katika sekta ya barabara tuwakumbuke ndugu zangu hawa, barabara hiyo ya kutoka Lunguza kwenda Kambai kwa ajili ya wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, lipo jambo lingine muhimu sana la hifadhi ya misitu pamoja na wanyamapori. Ni vyema tunajitahidi kwenye wanyamapori, tuendeleo pia kuhifadhi na maeneo mengine. Kwa mfano, Wilaya ya Muheza katika msitu huo wa hifadhi ya amani wapo vipepeo ambao kwa asili hawapatikani mahali pengine popote duniani, wako katika hifadhi hiyo tu ya Amani. Kitu gani ambacho kinatokea sasa? Kwa sababu vipepeo hawapatikani pale na utaratibu wa kuwahifadhi siyo mzuri, kinachofanyika sasa hivi ni kwamba watu wanafuata vipepeo wale, wanaweka wavu maalum kwa ajili ya kutagia mayai na wanachukua mayai yale wanayasafirisha kwenda nje ya nchi. Maana yake usipotambua ni kwamba wanasafirisha vipepeo kwa sababu wamechukua mayai wameyapeleka nchi za nje mayai yale yanakwenda kufanya nini? Watazalisha vipepeo kule, sasa badala ya vipepeo kuwa wanapatikana Tanzania peke yake sasa vipepeo hawa watakuwa wanapatikana katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, madhara yake ni nini? Madhara yake ni kwamba mvuto wa utalii kuja kwetu pia utapungua. Ninaomba hili mlíchukue, niliwahi kulizungumzia miaka iliyopita, lakini sijaona hatua zozote ambazo zimechukuliwa rasmi, basi mlifanyie kazi ili watu wasihamishe vipepeo. Jukumu letu ni kuhifadhi wanyamapori, lakini muhifadhi na vipepeo na wanyama wengine ambao pia wapo katika misitu yetu hawapatikani katika maeneo mengine nchini. Kwa hiyo tujitahidi na eneo hilo tulifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba Wizara inafanya kazi nzuri, lakini ina matatizo makubwa, makubwa sana. Sasa kuanzishwa kwa sheria hii na kuanzishwa kwa mamlaka hii iwe ni changamoto kubwa ya kuwezesha sasa utendaji kubadilika. TANAPA ninawafahamu na TANAPA wanafanya kazi nzuri sana na katika maeneo ambayo TANAPA wapo wanakumbuka kutoa huduma kwa jamii inayozunguka katika maeneo ya misitu. Nawapongeza sana TANAPA

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

na ninaendelea kuwaomba waendeleo kusaidia jamii katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja na asante sana. (Makofi)

SPIKA: Asante. Nilimwita Mheshimiwa Zaynabu Vullu, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdulsalaam Amer.

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi hii. Lakini awali ya yote kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetuwezesha sisi na mimi mwenyewe kuwa humu ndani na leo hii kupata fursa ya kuweza kuchangia katika bajeti hii ya Maliasili.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza Wizara kwa kuanzia na Waziri, Naibu wake na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote. Kwa hakika wamefanya kazi nzuri na tunategemea watafanya mengi ambayo ni mazuri ili kuweza kuhakikisha pato la nchi linaongezeka na kuhakikisha rasilimali zetu zinalindwa na kuutangaza utalii nchini na nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wengi wamezungumza mambo mbalimbali, lakini mimi nigusie suala la kuutangaza utalii ndani ya nchi yetu. Tuchukue nafasi hii, Wizara iweke utaratibu utakaowezesha vizazi vyetu kwa maana ya watoto wetu wa shule za msingi, sekondari hata kwenye vyuo wapate nafasi ya kwenda kutembelea mbuga zetu na kuona wanyama na rasilimali tulizonazo, hii itawapa fursa ya kujua Tanzania kuna nini. Najua watahitaji fedha, lakini Wizara ikitenga fungu maalum, ikiweka utaratibu maalum kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Wizara ya vyuo vikuu, nina hakika utaratibu huu utasaidia. Tuna mbuga nyingi ambazo ziko jirani na shule zetu na vyuo vikuu vilivyopo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningepomba Wizara ilianganalie hili kwa sababu tunapozungumzia kuutangaza utalii ni mara chache na wachache sana wanaopata nafasi ya kuangalia vipindi vya kwenye TV au kusikiliza redioni au kusoma majarida ambayo Wizara inatoa.

Mheshimiwa Spika, linguine, rasilimali ya mali za kale tulizonazo: Mafia kuna majumba ya kale, lakini zaidi yako Bagamoyo, yako Kilwa. Kisiwa cha Kilwa kinaliwa na bahari na pale kuna majengo mengi sana ya kihistoria katika nchi yetu. Niiombe Serikali ianganalie utaratibu wa kuzidi kuyatangaza na ukarabati na kuangalia kile Kisiwa kinanusurika vipi katika kuliwa na bahari. Kwa hiyo hilo nalo litasaidia kuongeza utalii wetu. Bagamoyo wametengeneza vizuri nawashukuru sana, watalii wengi wanakwenda, majengo ya kale yako pale na yanaboreshwa. Kwa kweli hilo limekwenda vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuanganalie makumbusho ya Taifa: makumbusho ya Taifa yana vitu vingi vya kale na vitu hivyo vina maana kubwa na historia kubwa kwa nchi yetu, tumeona utaratibu unaofanywa watoto wa shule wanapelekwa, lakini idadi ya watu wazima imepungua. Niombe, nizidi kuomba Wizara na mamlaka zinazohusika wazidi kutangaza kwa kuendelea kutumia vipindi vya televisheni, kutangaza kwenye redio na kuweka utaratibu wa jinsi gani watu wanaweza wakaenda wakaona rasilimali au vitu ambavyo vimekuwa vya kihistoria kwa nchi yetu. Hilo nalo ni jambo muhimu, ni jambo ambalo litaleta tija na ni jambo ambalo litatusaidia sisi Watanzania kujua ni vipi tunaweza kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la utalii wa watu wanaokuja wa *deep sea*. *Deep sea* wanaita ni kuzamia chini. Nataka wananchi wangu wasikie sitaki kuchanganya lugha. *Deep sea* ni kuzamia chini kwa kuzama *deep diving*. Ni vizuri Mafia ikaendelezwa kwa jambo hilo na kuna aina ya samaki ambao hawapo, kuna miradi mingi ya kuzuia uvuvi wa ovyo. Lakini naomba Serikali izidi kutangaza kwa sababu watalii wachache sana wanaoweza kwenda huko.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, tuna suala la misitu, idadi ya miti mingi inakatwa. Lakini tuombe kitengo husika kiongeze bidii kupanda miti mingi ili iweze kuvunwa. Lakini pia tuangalie mbaao zinazokamatwa, uwekwe utaratibu zipelekwe kwenye Halmashauri zinazohusika, watengeneze madawati watoto wasiendeleo kukaa chini. Kama hiyo haiwezekani, basi kuwe na utaratibu wa kule kunakovunwa miti basi tuambiwe tu labda leo Halmashauri fulani ina nafasi ya kwenda kukata magogo au miti ambayo itatengeneza madawati ili watoto wetu waweze kupata madawati ya kuweza kukaa na kusoma kwa raha sana. Baada ya kusema hayo nitoe nafasi kwa wengine nao wachangie, lakini niendeleo kuiomba Serikali, Wizara iongeze bidii ili kuweza kutangaza utalii nchini, asante sana. *(Makofi)*

MHE. ABDUSALAAM S. AMER: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii kuchangia Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Wizara kwa kusikia kilio changu cha kuomba kuainisha mpaka kati ya wanavijiji waliozunguka Hifadhi ya Mikumi. Nashukuru zoezi limefanyika na kwa sasa hivi limesimama kwa ajili ya mvua. Vijiji vilivyofaidika katika zoezi hilo ni Kijiji cha Mikumi, Lumango, Ruhembe, Kitete pamoja na Kielezo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ilikuwa adha kubwa kwa wananchi husika. Niliwahi kulalamika kuhusu tabu wanayoipata wananchi walio jirani na hifadhi hiyo, lakini kuanisha mipaka hii imekuwa ni kama neema kwa wananchi wanaohusika katika Hifadhi ya Mikumi. Ningeomba Wizara iangalie upande wa pili wa Kusini wa Hifadhi ya Mikumi kuna vijiji vya Lumango, Muhenda, Ulaya, Ilakala, Kiduhi pamoja na Kilangali. Sehemu hii pia ni adha kubwa kwa wananchi wanapata tabu na walinzi wa hifadhi hiyo. Kwa kweli tatizo kubwa linalotokea kwa sababu hakuna kuainisha mipaka kati ya wananchi na Hifadhi hii ya Mikumi. Ningeomba Serikali ifumbe macho iongeze fedha kwa ajili ya kuanisha mipaka. Hata Wabunge wenzangu walilalamika kuhusu mipaka kati ya wananchi waliozunguka hifadhi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kushukuru sana uongozi wa Wilaya ya Kilosa chini ya DC Mr. Tarimo na Mkuu wa Hifadhi ya Mikumi Mr. Dattomax Maselanyika kwa kutoa ushirikiano mzuri sana katika kuainisha zoezi hili la kuanisha mipaka.

Mheshimiwa Spika, suala lililobakia ni kutoa elimu kwa wanakijiji husika kwa sababu kwanza ilikuwa hawana uhakika wapi mipaka yao inaishia, wanaweza kukamatwa *either* kwa makusudi au kwa bahati mbaya, lakini adha wanayoipata Wizara inajua hali halisi wanayopata wananchi wetu kwa hiyo ningeomba zoezi hili lifanyike baada ya hifadhi ya Mikumi wangeenda kwa hifadhi zingine ili kutoa kero hiyo ambao wananchi wanalalamika *either* ni uonevu wa kweli au ni uonevu wa kawaida kwa wananchi wanaohusika sehemu ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu Wilaya yetu ni suala la misitu. Kwa kweli Wilaya ya Kilosa imevamiwa na wavamizi kutoka mikoa mbalimbali, miti inakatwa, mikaa ndiyo usiseme nahisi kupita hata Mkoa wa pwani. Malori na malori yanatoka katika Wilaya yetu, malori ya Fuso kila siku takriban lori kumi ya mikaa kuelekea Dar es Salaam. Sasa Halmashauri yetu uwezo huo haina, lakini ningeomba Wizara iangalie suala hili kuisaidia Halmashauri angalau fedha kidogo kuwawezesha kufanya *patrol* katika sehemu husika. La sivyo, Wizara kama haitafanya juhudi, baada ya miaka mitano/kumi Wilaya ya Kilosa itakuwa jangwa kama mikoa ya Kaskazini. Mheshimiwa Spika, pia nichukue fursa hii kuishukuru sana Hifadhi ya Mikumi kwa ushirikiano walioonyesha kwa wananchi na misaada wanayotoa kwa ujenzi wa visima, zahanati, madarasa ya shule, madawati pamoja na visima vya maji. Ningeomba sana meneja ndugu yangu aongeze *speed* na ushirikiano kuwasaidia wananchi wa sehemu husika ili kutoa dhana ya kwamba wao wanapata fedha lakini wananchi walio jirani hawawafikirii.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, suala lingine kuhusu *Hotel* ya *Mikumi Lodge*, naamini viongozi wengi walioko hapa na waliopita wa upande wa Kusini wa upande wa Iringa na Mbeya, enzi zao lazima wapitie *Mikumi Lodge*. Ni lodge iliyokuwa nzuri sana ya kitalii, lakini kwa sasa imekuwa gofu. Sijui Serikali inasema nini kuhusu suala hili! Wawekezaji wamejitokeza kuwekeza katika Hoteli hiyo. Sasa naomba Wizara leo itoe kauli kuhusu hiyo hoteli, kwa kweli hii Hoteli ilikuwa nzuri sana na kivutio sana kwa watalii wanaopita katika Hifadhi ya Mikumi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi naishia hapa naunga mkono hoja ya Wizara hii ya Utalii. Asante sana. *(Makofi)*

MHE. KHAJI KHATIB KAI: Mheshimiwa Spika, ahsante nakushukuru nami kunipa nafasi kuweza kuchangia katika hotuba ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, siku ya tarehe 31 Januari, 2014 Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilifanya ziara katika Hifadhi ya Taifa ya Nkomazi, ili kujionea maendeleo ya mradi wa faru weusi. Mambo yaliyojitokeza wakati Kamati ikipokea Taarifa ya mradi huo, yanasikitisha na ni aibu.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la aibu kubwa sana kwa nchi yetu anapotokea mfadhili au mhisani katika hifadhi hii anajitolea kwa nia njema kabisa kurejesha faru ambao wametokewa katika hifadhi ile pamoja na kujitolea kusaidia magari na hata silaha za kulinda katika hifadhi hii. Kwa bahati mbaya sana mtu ambaye amejitolea kwa nia njema, lakini ambaye amesaidiwa hayuko tayari kupokea msaada huo kwa nia njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu ni aibu na siwezi kusema kwamba ni uonevu kama mchangiaji wa mwanzo alivyosema. Ni aibu kwa sababu mfadhili amesaidia Hifadhi ya Taifa, hii ni Hifadhi ya Taifa siyo hifadhi ya TANAPA, kwa hiyo huwezi kusema kwamba ni uonevu, ni aibu kwa Taifa ambalo kila siku limekuwa likisema kwamba lina viongozi ambao wanaweledi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru kwa vifaa ambavyo vimeletwa kwa msaada kwa Hifadhi ya Taifa ya Nkomazi siyo ni aibu tu, ni udhalilishaji hata wa Taifa zima la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu uteuzi wa Naibu Kaimu Mkurugenzi wa Wanyamapori mtu anayeitwa Sarakikya: Juu ya hili nataka niwe mkweli, mimi nikiwa ni miongoni mwa wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ambayo ilienda kufanya tathmini na uchunguzi wa jinsi Operesheni Tokomeza ilivyowaathiri wananchi. Baada ya kuanza kufanya kazi hiyo tulianza kukutana na viongozi wa taasisi ambazo zilisimamia Operesheni Tokomeza. Baada ya kuanza kazi yetu, tulianza kukutana na Waziri na watendaji wake wa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kama kuna mtu ambaye alisababisha aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii kukosa taarifa, basi ni mtu anayeitwa Sarakikya. Mimi nitamuomba Mheshimiwa Waziri atutajie vielelezo ambavyo alivitumia katika kumteua Sarakikya kukaimu nafasi ya Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amekuwa akisema kwamba, kumwajibisha aliyekuwa Mkurugenzi wa Wanyamapori alifuata maelekezo ya Bunge ambayo yalitolewa na Kamati ambayo ilienda kufanya uchunguzi. Mimi nasema hili siyo kweli. Nasema siyo kweli kwa sababu kama Kamati iliota maelekezo ya wote ambao walihusika waweze kuwajibishwa, basi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kuna watu ambao walitajwa kwa majina na kuna watu ambao hata namba zao za simu zilirodheshwa katika ripoti ya Kamati, lakini hadi leo hawajawajibishwa. Kwa hiyo, kitendo hiki mimi sitaunga mkono hoja ya Wizara ya Maliasili mpaka Mheshimiwa Waziri atakapotuambia ametumia vigezo gani vya kumteua Sarakikya, kuweza kukaimu nafasi ya Mkurugenzi wa Wanyamapori. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo mimi sitaki nipoteze muda wako sana, siungi mkono hoja mpaka nitakapopata maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwa nini alimteua Sarakikya ambapo Sarakikya huyu alitajwa katika taarifa ya Kamati ambayo alitakiwa na yeye pia awajibishwe. Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, ahsante. (Makofi)

SPIKA: Haya! Hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani walisema wafuate taratibu za utawala bora, nadhani hilo mzingatie. Nilisema Mheshimiwa Sylvester Mabumba atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Philemon Owenya.

MHE. SYLVESTER MASELE MABUMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Awali ya yote nitoe pongezi kwa uongozi wa Wizara ukiongozwa na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu kwa kazi nzuri ambayo tokea ameingia wamekuwa wakifanya katika sekta hii muhimu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba matukio ya ujangili ambayo yalikuwa yamekuwa yakiripotiwa kila siku kwa kiasi fulani yameanza kupungua, hivyo naomba Wizara ikaze buti, iendelee kupambana na kulinda rasilimali hizi muhimu za wanyamapori na hata misitu yetu ambayo pia ni rasilimali muhimu kwa uchumi wa nchi yetu. Mheshimiwa Spika, nilitaka nimuulize Mheshimiwa Waziri jambo moja la msingi, kwamba Tanzania imejaliwa kuwa na rasilimali nyingi ambalo ni jambo la kweli, lakini bila kutangaza katika vyombo vikubwa vya magharibi si rahisi sana rasilimali hizi kujulikana na hivyo kuvutia watalii wengi kutoka sehemu mbalimbali dunia kutembelea nchi yetu. Je, Serikali ina mpango gani kutumia redio za Magharibi, TV za Magharibi na Magazeti makubwa ya Magharibi ambayo ndiyo yanayozalisha watalii wengi wenye fedha za kutosha kuweza kufahamu rasilimali zetu na hivyo kuwavutia watembelee katika nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, lakini la pili kama tutakumbuka vizuri Mheshimiwa Rais alizindua mabango ambayo yamefungwa katika viwanja vya ndege vya kimataifa hapa Tanzania ikiwemo uwanja wa Julius Nyerere Dar es Salaam, Mwanza, KIA, lakini pia mpango wa kufunga bango kama lile kule Zanzibar ulitakiwa ufanyike na mabango haya yaanze kutumika sasa ili watalii wanapowasili kupitia viwanja hivi waweze kuona rasilimali zetu za wanyamapori na hivyo kuwavuta kuendelea kuitembelea nchi yetu. Kwa bahati mbaya mpaka sasa hivi ninapozungumza toka Rais azindue mabango haya hayajaanza kutumika, ni lini sasa Serikali itaweza kutumika mabango haya ili yaweze kufanya kazi ambayo imekusudiwa?

Mheshimiwa Spika, la tatu; katika kukabili ujangili Serikali lazima iwe na mpango mkakati wa kuwezesha wananchi wanaoishi jirani au katika maeneo ambayo hifadhi na mapori ya akiba yapo kuwawezesha kiuchumi. Kwa sasa sijaona kama kuna mkakati mahususi ambao umelenga kusaidia mbali na kama takrima inayofanywa na wahifadhi katika maeneo hayo.

Naomba Serikali ituambie ina mkakati gani na kama inao mkakati huu ni fedha kiasi gani ambazo zimeshatumika mpaka sasa hivi kusaidia wananchi katika maeneo hayo na hivyo wananchi kushawishika sasa kutumika kama walinzi kushirikiana na Serikali yetu kutambua na kusaidia kutoa taarifa sahihi kuhusu mienendo ya majangili ambao katika siku za karibuni wamevinjari sana katika mbuga zetu na mapori ya akiba. Napenda pia Wizara iniambie ni ajira kiasi gani ambazo zimetengenezwa kutokana na sekta hii muhimu ya utalii ni hivyo kutekeleza mkakati wa Serikali wa kupunguza umaskini kwa Watanzania kupitia rasilimali hii muhimu ya utalii

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

na rasilimali zake kwa kipindi angalau cha miaka mitano iliyopita ili sasa sekta hii ya utalii ambayo kwa kweli ukiangalia nchi jirani ya Kenya, vilevile nchi ya Misri zimefaidika sana, na hata visiwa vya Shelisheli na Mauritius vimefaidika sana sekta ya utalii. Lakini katika nchi yetu inaonekana wengi hawajaona hasa mchango mkubwa wa sekta hii muhimu ambao kwa kweli kama ungetumika vizuri ungeweza kuchangia kukuza uchumi wetu na hivyo kusaidia kufikia Malengo ya Dira ya 2025 lakini pia Malengo ya Millenia na pia kuweza kutekeleza Mpango Mkakati wa Matokeo Makubwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kumaliza napenda pia kuiomba Wizara ituambie ina mpango gani katika mapori ya akiba ambayo hayajaendelezwa yaweze kutangazwa sasa hasa mapori ya akiba na hifadhi zilizoko ukanda wa Kusini wa nchi yetu ambao tukilinganisha na hifadhi na mapori ya akiba yaliyoko Kaskazini watalii ni wengi sana, kwamba wananchi wa maeneo ya Kusini ya nchi yetu sekta hii muhimu bado haijawanufaisha sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (Makofi)

MHE. LUCY P. OWENYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru awali ya yote naomba ku-*declare interest* kwamba mimi ni mdau katika sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro, Kilimanjaro ni kati ya hifadhi ambazo zinaingizia pato la Taifa fedha nyingi. Mwaka 2012 iliingiza zaidi ya shilingi bilioni 20. Lakini Halmashauri zinazozunguka Mlima Kilimanjaro hazifaidiki na mapato haya. Tumeongea mara nyingi lakini KINAPA huwa wanajenga tu darasa au kujenga choo, hii haifadishi wananchi wa pale. Tunaomba Halmashauri zile iwe kama kwenye Halmashauri zinazoizunguka migodi wanatengewa dola laki mbili. Pia Kilimanjaro na sisi watenge fedha kwa ajili ya Halmashauri zinazotuzunguka, Halmashauri ndiyo wapange wafanye nini na zile fedha wanaweza wakaamua wakapanda miti kwa ajili ya hifadhi ya mlima na wataona kuna motisha kuhakikisha kwamba na wao wanafaidika na fedha zile. Kuna shida za maji katika Halmashauri zinazotuzuka kule Moshi vijijini, vijiji vya Kikarara, Mahoma, Uru hamna maji. Kwa hiyo Halmashauri zinaweza kuamua kuchimba maji na kuwapatia wananchi wale maji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyopita, Wizara iliamua itafungua ile barabara ya *Old Moshi* na itakuwa ni kwa ajili ya watalii maalum. Lakini ile barabara kutoa Kibororoni kupitia Kikarara mpaka Kidia mpaka sasa hivi hakuna kitu kilichofanyika.

Ningependa Mheshimiwa Waziri atueleze mpaka sasa hivi wamefikia wapi ili barabara ile ianze kutumika kwa sababu sasa hivi inakuwa ni tabu sana kuwapandisha watalii kule na kama tunavyoelewa barabara ya *Old Moshi* ni nzuri sana hata kwa *day trip* ni muda mfupi, ni chini ya dakika kumi unafika kwenye misitu, kuna vipepeo, kuna ndege, kwa hiyo, ni sehemu nzuri ambayo watalii wanaweza kuja kwa muda mfupi.

Pia Mheshimiwa Waziri alituambia kwamba katika zile *camping routes* za Machame – Lemosho, wangejenga *tents* kwa ajili ya kulia. Lakini mpaka sasa hivi *tents* zile hazijajengwa na mazingira yanazidi kuharibika kule Kilimanjaro.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ningependa atueleze mpaka sasa hivi wamefikia wapi ili kupunguza ma-*porter* wengi sana kwenda kule mlimani na mazingira yanaharika, kwa hiyo wakijenga yale ma-*tent* itatusaidia sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni Bodi ya Utalii (Tanzania Tourist Board): Mpaka sasa hivi fedha walizopata ni milioni 800 na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ametueleza kwamba wataenda kutoa matangazo CNN. Kutoa tangazo CNN ni zaidi ya shilingi bilioni moja.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

TTB mmewapa shilingi bilioni 4.5, lakini wenzetu tukumbuke sehemu kama Kenya wametenga dola milioni 30 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 49 kwa ajili ya kutangaza utalii. *South Africa* wametenga dola milioni 70 sawa na bilioni 114 kwa ajili ya kutangaza utalii wao.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa mtawaonea wakurugenzi, mtawafukuza wangapi? Bila kuwapa fedha hawawezi kufanya kazi. Mmesema mtaweka maafisa wa utalii kwenye kila ubalozi, watafanya kazi namna gani bila kupelekewa fedha. Mnajua balozi zetu zimechoka.

Kuna wakati nilienda London, hata chai wanashindwa kukupa. Sasa mnampeleka Afisa Utalii pale ataenda kufanya nini? Kwa hiyo, naomba kabisa waangalie umuhimu wa kutangaza, bila fedha huwezi kutangaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ngorogoro, kama Mheshimiwa Bura alivyozungumza kuna haja ya kuunda bodi, kwa sababu ile barabara ya Ngorongoro mpaka sasa hivi haijafunguliwa, inabidi watalii wazungushwe kwenye barabara ndefu kuzunguka mpaka kule Sopa, inapoteza muda, foleni inakuwa ni kubwa.

Lakini kungekuwa kuna bodi labda hii barabara ungekuta imefunguliwa na matatizo mengi kuhusu malipo benki ni moja ni Exim, waongeze CRDB kwa sababu CRDB katika Mlima Kilimanjaro imeonekana inafanya vizuri. Kwa hiyo, mimi sioni sababu kwa nini wasiongeze benki zaidi ili kuweza kurahisisha watalii waweze kupata urahisi wa kwenda kwenye mbuga zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda naomba nizungumzie kidogo kuhusu wale twiga waliotoroshwa pamoja na wanyama wengine. Kuna huyu ndugu Kamran Ahmed, yeye ndiye aliyetoroshwa wale twiga. Kwa mujibu wa vyombo vya habari, kesi ilikuwa inaendelea lakini inasemekana ametoroka na Kamati iliyozungumzia suala hili ilipelekea mpaka Mheshimiwa Maige akajijuzulu.

Mheshimiwa Spika, lakini mpaka sasa hivi Serikali haijatuelezea *status* ya ile kesi imefikia wapi, je, mna mikakati gani ya kuhakikisha mnamkamata. Kengele ya ngapi?

MBUNGE FULANI: Kwanza!

MHE. LUCY P. OWENYA: Mnamkamata huyu mtuhumiwa ili aweze kurudishwa Tanzania na iwe fundisho kwa wengine wanaofanya ujangili kama huo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ni kuhusu sisi kuwa na *National Carrier*. Utalii wa Tanzania unaonekana ni wa ghali sana. Zamani *Air Tanzania* ilikuwa inaenda mpaka Ulaya inaleta watalii *direct* mpaka Tanzania, kwa hiyo wageni kuja Tanzania inakuwa ni rahisi kuliko wanavyopitia Kenya.

Mheshimiwa Spika, mgeni akipitia Kenya lazima aje tena Tanzania alipe zaidi, lakini kule Kenya huwa wanawapa *special package* ambayo ina-include *air fare*. Unakuta anaambiwa ukija Kenya pamoja na *flight* inaweza kuwa labda mara nyingine inafika hata dola 2000 lakini akija Tanzania utalii unaonekana *very expensive*, maana mtalii kuja Tanzania lazima awe na zaidi ya dola 3000 au 4000 na wengi wanalipa huko Ulaya.

Mheshimiwa Spika, hii *system* ya wageni kulipia nje bado ni tatizo, Watanzania hatufaidiki na fedha zile moja kwa moja, unakuta wageni wanalipia nje, akija Tanzania analipa zile *park fees* tu labda analipia na mishahara kidogo ya *ma-porter*, ya *ma-guide*, mfano kwenye Mlima Kilimanjaro, lakini mara nyingi sisi hatufaidiki na hiyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kuna tetesi kwamba TALA License sasa hivi mnataka kurudisha wageni wapandishe watalii Mlima Kilimanjaro, kazi hii ilikuwa ni kwa ajili ya ku-promote wazawa, lakini sasa hivi naomba Serikali isije ikarudia hilo kosa.

Mheshimiwa Spika, mkiangalia sasa hivi mnapata fedha nyingi sana kwa sababu wazawa ndiyo wanapandisha wageni Mlima Kilimanjaro, mkirudisha makampuni ya kigeni yakianza kuleta wageni *direct*, ina maana fedha zile zitabaki kule kule na Watanzania hatutaweza kufaidika na fedha hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru. Naomba Mheshimiwa Waziri ajibu maswali yangu niliyomuuliza. Ahsante sana. (Makofi)

MHE. MOSHI SULEIMAN KAKOSO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi hii na mimi nipate kuchangia kwenye Wizara hii muhimu. Kwanza niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa na Naibu Waziri wanayoifanya ili kuweza kunusuru Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Mpanda kuna Mbuga ya Katavi, mbuga hii haitajatangazwa kiasi cha kutosha. Mbuga hii ya katavi ni mbuga kubwa ambayo ina wanyama wengi na wazuri na ina vuvitio vingi vya watalii. Bahati mbaya sana Wizara haijaweke mipango mikakati ya kuitangaza ili iweze kufanya kazi na itoe tija kwa wananchi wa Mpanda na Taifa.

Mheshimiwa Spika, niombe sana Wizara hii iweze kufanya jitihada za makusudi ili iweze kuitangaza ipasavyo na iwanufaishe wananchi husika.

Mheshimiwa Spika, Mbuga ya Katavi haina miundombinu, mbuga hii ina wanyama, viboko, mamba ambao wanategemea sana mto Katuma. Mto huu kiangazi huwa unakauka na unafanya wanyama wale wakose maji ya kutosha kipindi cha kiangazi kuanzia mwezi wa tisa mpaka wa kumi, wanyama hawa hufa kwa wingi kwa kukosa huduma ya maji. Niombe Wizara iweke jitihada za makusudi kuchimba mabwawa ambayo yatasaidia kulinda na kuhifadhi wanyama wale ambao wanapoteza maisha mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, tukiimarisha Mbuga ya Katavi itaenda sambamba na Mbuga ya Mahale ambayo ina wanyama wazuri, sokwe na ni maeneo jirani ambayo yanaweza kukuza utalii katika Ukanda wa Magharibi. Naiomba sana Wizara ifanye jitihada za makusudi kuhakikisha inapanga mipango mikakati ya kuimarisha Mbuga hizi zilizoko ukingoni mwa nchi.

Mheshimiwa Spika, Migogoro ya WMA: Kuna WMA ya Ubende iliyoko Wilaya ya Mpanda. WMA hii ina matatizo makubwa sana ambayo haijawasaidia kabisa Wananchi wanaozunguka maeneo haya. Muda mwingi kumekuwa na migogoro na kusababisha baadhi ya Wananchi kupata mateso makubwa bila kupata kile ambacho wengine wananufaika na WMA. Kuna vijiji vya Kabage, Mkungwi, Sibwesa, Kasekese na Kaparamsenga, ni vijiji ambavyo vimezungukwa na WMA. Maeneo haya yana migogoro mikubwa sana, mipaka waliyoweka hawakuwashirikisha Wananchi. Kwa hiyo, walifika tu wakatengeneza mazingira ambayo hayawanufaishi Wananchi. Naiomba Serikali kupitia Wizara, iende mapema kuhakikisha wanapima upya mipaka ambayo itawasaidia na kutatua migogoro ambayo ipo kwa Wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni mgogoro wa Hifadhi ya Msitu wa Tongwe ulioko katika Kijiji cha Vikonge, Kitongoji cha Igarukilo. Eneo hili Serikali imewachomea Wananchi ambao wamekaa kwa miaka 20 kama Serikali ilivyokuwa imewapa hadhi ya Kitongoji kile. Baadaye Serikali imewachomea Wananchi na kuwafanya waishi katika mazingira ambayo hayafai. Naomba Serikali iangalie vizuri eneo hili na iweze kuwafidia Wananchi ambao walitendewa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

matendo ambayo si ya kibinadamu. Eneo hili Serikali ilikisajili kitongoji hicho kupitia Kijiji cha Majalila, bahati mbaya sana sasa hivi Serikali inakuja na maamuzi mengine mapya kwamba eneo hili halifai kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana, Wilaya ya Mpanda ni Wilaya ambayo ni kubwa na asilimia kubwa imezungukwa na mapori. Maeneo haya ambayo Wananchi wanafanyia shughuli, wanakosa maeneo ya kufanyia kazi kwa sababu maeneo yote yamekuwa kwenye Hifadhi ya Misitu au Hifadhi ya Mbunga ya Katavi au Hifadhi tu za WMA. Naomba Serikali iangalie upya, kuhakikisha inaangalia mazingira ambayo yatawasaidia Wananchi waweze kufanya shughuli zao bila kuwa na bugudha na Serikali.

Mheshimiwa Spika, hili si tu kwa Wilaya Mpanda hata kwa Wilaya ya Mlele ambayo ni mpya, ukifika eneo la Tarafa la Inyonga ambako ndiko Makao Makuu ya Wilaya ya Mlele, maeneo ya kufanyia shughuli za kilimo kwa Wananchi ni kidogo sana. Kila wanapotoka, hatua 20 kutoka katika maeneo ya vijiji, wanagusa maeneo ambayo yamezungukwa na Hifadhi.

Serikali kupitia Wizara na Waziri unanisikia, utakapokuwa unafanya majumuisho ni vyema ukatupa kauli ambayo itawasaidia Wananchi ili kutoa migogoro ambayo haina ulazima kuwepo kwa sababu tuna maeneo makubwa, yakipangwa katika mpango mzuri tutaepusha migogoro kati ya Wananchi na Hifadhi zinazomilikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Serikali ijenge mazingira ya kuimarisha miundombinu hasa katika Hifadhi ya Katavi. Iwaangalie watumishi na iwapatie zana za kisasa ambazo wanaweza wakazifanyia kazi, pamoja na magari na huduma ambazo zinaweza zikawasaidia kama jamii katika maeneo haya ili kuweza kuimarisha ile hifadhi na kuweka mazingira ambayo yatakuwa ni vivutio vizuri kwa watalii ambao wanaweza kukuza Mji wa Mpanda na Wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, atafuatiwa na Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii. Niungane na wenzangu kuwapongeza, Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara husika na Watendaji wake.

Mheshimiwa Spika, mimi nitajikita au nitatumia muda mwingi kuzungumzia suala la migogoro kati ya Wananchi na Wizara ya Maliasili. Mara nyingi nimekuwa nazungumzia sana suala la mgogoro wa Wananchi wanaozunguka Msitu wa Kazimzumbwi lakini kwa kutokea katika Kata ya Chanika, eneo la Nzasa. Hili ni jambo la muda mrefu mno, ni mgogoro ambao umeanza miaka ya sabini. Mimi niliukuta mgogoro na umenichukulia muda mrefu sana kuuzungumzia hapa Bungeni, lakini pia kuwa na vikao mbalimbali na Ofisi ya Waziri Mkuu hasa kwa kumtumia Mheshimiwa Nagu, ambaye yuko katika Wizara ya Uwekezaji na Uwezeshaji.

Mheshimiwa Spika, miaka ya 2011/2012, Wananchi wa Nzasa walichomewa nyumba zao zikiwa na mazao ndani, lakini hata mifugo yao ilichukuliwa na hata wengine walichukuliwa hatua wakawekwa ndani. Nasikitika kusema, tulipoteza maisha ya Wazee wawili ambao walipata mshituko na kupoteza maisha yao.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Nakumbuka kwamba, kikao chetu cha mwisho na Ofisi ya Waziri Mkuu, tulikubaliana kwamba Waziri Mkuu atatoa tamko la mipaka miwili ambayo imekuwa ni mgogoro mkubwa. Kuna mpaka ambao ni wa mwaka 1954, lakini kuna mpaka mwingine mpya wa 1998. Mipaka hii ilipelekea mpaka Wizara mbili; Wizara ya Ardhi na Wizara ya Maliasili, kutoa kauli tofauti mbele ya Bunge lako. Inavyojulikana, ni kwamba mpaka wa zamani ndiyo halali (Mpaka wa mwaka 1954).

Inasemekana kwamba, Watendaji wa Wizara ya Maliasili walikuja ku-*create* tena huu mpaka wa 1998 na kuwauzia Wananchi ile sehemu ya pale katikati. Hiyo ndiyo inayoleta mgogoro, kwa sababu ukifuata mpaka huu wa zamani, maana yake ni kwamba, Shule ya Msingi ya Nzasa itakuwa iko ndani ya Hifadhi na hata Ofisi ya Serikali ya Mtaa wa Nzasa nayo itakuwa ndani ya Hifadhi. Mimi namwomba sana Mheshimiwa Waziri, jambo hili limechukua muda mrefu sana, naomba atakapokuja kutoa hitimisho, hebu atoe hitimisho la mgogoro huu.

Mheshimiwa Spika, mimi sitaunga mkono bajeti yake mpaka nipate ufumbuzi wa jambo hili kwa sababu limechukua muda mrefu sana na linawafanya Wananchi washindwe kuishi kwa amani na kuendelea kufanya shughuli za maendeleo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie eneo lingine ambalo lina matatizo sana na wanyamapori. Upo msitu ambao upo katika Kata ya Msongora, Msitu wa Magereza. Msitu huu una nyani wengi na nyani hawa wamekuwa kero kubwa sana kwa Wananchi wanaoishi katika Mitaa ya Kiboga A, Kiboga B na Kiboga C.

Mheshimiwa Spika, nikwambie tu akina mama wenye watoto, hawawezi kuwaacha watoto majumbani kwao na kwenda kujishughulisha na shughuli za kiuchumi, kwa sababu nyani wanatoka katika Pori hilo la Magereza na kutishia watoto wanaoachwa nyumbani. Isitoshe siyo hilo tu, pia Wananchi wa pale wameshindwa kuendelea na kilimo kwa sababu nyani hao wanaingia sana katika mashamba ya Wananchi na kuharibu mazao mengi, lakini pia hata ufugaji, nyani ni wakubwa wanakula mpaka kuku wa Wananchi. Kwa hiyo, hata ufugaji wa kuku umekuwa ni tatizo katika maeneo hayo. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, alifanyie kazi hili ili ule msitu uweze kuwa na ulinzi kwa ajili ya kuzuia hao wanyama wasiingie katika maeneo ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongelea hayo mambo mawili ambayo yanatusumbua sana katika Jimbo la Ukonga Dar es Salaam, naomba sasa niongelee suala la utalii wa ndani. Kitabu cha Mheshimiwa Waziri kinaonesha ni namna gani utalii umepanda, lakini nataka niishauri Serikali, itumie nguvu zake nyingi kutangaza utalii wa ndani.

Mheshimiwa Spika, Utalii wa Ndani unaweza ukatuletea fedha nyingi sana, kwa sababu tukikaa tukategemea utalii wa nje kuna siku ambayo tunaweza tukajikuta hatuna mapato ya kutosha. Mimi niseme tu kwamba, kuna tatizo kubwa la mawasiliano kati ya Wananchi na sehemu za utalii. Unakuta maeneo mengi ya utalii yanatumia zile simu za mezani za *TTCL*, ambazo unapiga kuanzia asubuhi mpaka jioni hata siku mbili hazipatikani wala saa nyingine hazipokelewi. Kwa hiyo, kama mtalii wa ndani unajikuta unakosa ile fursa ya kwenda mahali kwa sababu hujapata taarifa za kukuwezesha kwenda mahali pale. Kwa hiyo, wajaribu kuweka mawasiliano ya kisasa ambayo yatawawezesha watalii wa ndani kupata taarifa za maeneo husika ili waweze kupata fursa za kutembelea, lakini zaidi sana kuendelea kuongeza pato la Wananchi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuzungumzia hayo mambo matatu. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri aje na jibu la Wakazi wa Kazimzumbwi na tatizo la mgogoro wake kwamba utakuwa umeshia wapi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi. (Makofi)

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse.

MHE. FAITH M. MITAMBO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Hotuba hii ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Mimi nitazungumzia tatizo la mgogoro wa mipaka uliopo kati ya Selous Game Reserve na Halmashauri ya Kijiji cha Kikuryungu Wilayani Liwale.

Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka wa nne ninazungumzia tatizo hili la mpaka kati ya Kijiji cha Kikuryungu na *Selous Game Reserve*. Nimeuliza maswali ndani ya miaka hii minne, nimezungumzia mgogoro huu kwa kuongea na nimekwenda Ofisini kwa Waziri wa Maliasili kwa mazungumzo bila mafanikio. Mgogoro wa mpaka kati ya Kijiji cha Kikuryungu na *Selous Game Reserve* umedumu kwa muda wa miaka kumi. Wizara ya Maliasili kwa maana ya *Selous Game Reserve* wanadai eneo la Kihurumila kwamba lipo ndani ya *Selous Game Reserve* na Wananchi wa Kijiji cha Kikuryungu wanadai kwamba, eneo la Kihurumila liko ndani ya Halmashauri ya Kijiji cha Kikuryungu.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Kijiji cha Kikuryungu wana Tangazo la Serikali la Mwaka 1974 na wana ramani ambayo inaonesha mpaka kati ya *Selous Game Reserve* na Kijiji cha Kikuryungu ni Mto Matandu. Tangazo hili lipo na wanalo, ni la mwaka 1974. Si hilo tu, wakati wa kutengeneza mpaka ule kuna Wazee ambao walishiriki katika zoezi lile na ambao wapo. Sasa Wizara imeshindwa kutatua mgogoro huu zaidi ya miaka kumi. Wananchi wanasema eneo la Kihurumila ni la kwao, Wizara inasema eneo lile liko ndani ya *Selous Game Reserve*.

Mimi naomba Wizara, hebu tusuluhishe, tuchukue tu busara, tufanye busara za kawaida, tusuluhishe mgogoro huu. Eneo lile la Kihurumila ni dogo sana, hebu tumalize mgogoro huu. Tumie busara za kawaida tuwarudishie Wananchi. Turudishe lile eneo, halii-cost Wizara ya Maliasili au Serikali kitu chochote kurudisha eneo lile katika Halmashauri ya Kijiji cha Kihurumila. Ninaomba tuwarudishie Wananchi eneo lao.

Kwa kuwa Wizara inasema eneo lile ni la Selous na Halmashauri ya Kijiji inasema eneo lile ni la Kijiji cha Kikuryungu, mimi naomba sasa Wizara ichukue hatua za haraka na za makusudi kabisa, Waziri wa Maliasili akifuatana na mimi, twende Wilaya ya Liwale, kule tuungane na Uongozi wa Wilaya na ikiwezekana Kamati ya Ulinzi na Usalama, twende katika Kijiji cha Kikuryungu, tuungane na Uongozi wa Halmashauri ya Kijiji cha Kikuryungu, tukakae pamoja tuzungumze tumalize tatizo hili. Ikiwezekana basi tuwashirikishe wazee na tuushirikishe Uongozi wa Kijiji cha Halmashauri ya Kikuryungu, tupime mpaka ule upya; tatizo liko wapi?

Kwa nini tunashindwa kumaliza matatizo ya mipaka? Kila mtu anayesimama hapa anazungumzia tatizo la mipaka, majibu tunayoyapata miaka zaidi ya minne ni hayo hayo. Mimi ninakuomba Mheshimiwa Waziri wa Maliasili, uchukue hatua za makusudi kabisa, tatizo la mipaka mwaka huu ulimalize.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie suala la mgawanyo wa mapato wa ile asilimia 25 inayotokana na uwindaji wa kitalii. Wilaya ya Liwale ni wadau wakubwa sana wa Sekta hii ya Utalii, kwa sababu eneo kubwa la *Selous Game Reserve* liko ndani ya Wilaya hii. Nimeangalia katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili, ambayo inaonesha mgawanyo wa mapato yale ya asilimia 25, Wilaya ya Liwale ukiangalia kilometa zilizowekwa pale ni nyingi,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

ni zaidi ya *Square kilometer* 1400 na mapato ambayo Wilaya hii imepatiwa kufuatana na Hotuba yake, mwaka 2012/2013 ni shilingi milioni 9.9. Ukiangalia miaka ya nyuma, mwaka 2008/2009 mapato yalikuwa milioni 44. Nataka kufahamu tatizo la chanzo cha upungufu huu ni nini?

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyoitoa wakati anawasilisha Hotuba yake ya Bajeti, ukurasa wa 44, alizungumzia masuala ya mapato yanayotokana na uwindaji wa kitalii. Amesema kwamba, Halmashauri 38 ziligawiwa jumla shilingi bilioni 8.7. Mimi ninataka kufahamu, je, katika zile Halmashauri 38 Wilaya ya Liwale imo; na katika mgawo huu wa asilimia 25 hizi milioni 8.7 Wilaya ya Liwale imepatiwa shilingi ngapi?

Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, anipe orodha yote ya Wilaya ambazo hizo pesa zimekwenda na aniambie ni *criteria* gani ameitumia katika kugawa hizo pesa. Orodha hiyo atakayonipa iwe ime-*indicate* Halmashauri ya Wilaya ya Liwale imepewa kiasi gani katika mgao huo wa asilimia 25.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, ninashukuru. Siungi mkono hoja mpaka nitakapoambiwa na Mheshimiwa Waziri ni lini atakuwa tayari kufuatana na mimi, twende katika Kijiji cha Kikuryungu tukamalize mgogoro ule wa mpaka. Siungi mkono hoja kwa mara ya kwanza. (Makofi)

SPIKA: Ahsante na kengele imegonga. Mheshimiwa Mchungaji Natse, atafuatiwa na Mheshimiwa Betty Machangu.

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Naomba kuanza kwa kusema, katika uumbaji, Bwana Mungu aliumba viumbe vyote na kiumbe cha mwisho kuumbwa ni mwanadamu na huyu mwanadamu akaambiwa avitiishe viumbe vingine vyote. Kwa hiyo, nataka kuzungumzia juu ya athari ya wanyama wakali katika Wilaya yangu ya Karatu na hawa ni kutoka katika Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro.

Katika Kitabu cha Hotuba ya Waziri, ukurasa wa sita, ameeleza juu ya ulinzi dhidi ya wanyama wakali na waharibifu na akataja Wilaya zilizoathirika na fidia zilizolipwa na Serikali. Cha kushangaza na cha ajabu ni kwamba, Wilaya ya Karatu haipo. Katika swali nililouliza jana, ambalo majibu yake yalikuwa ya kutatanisha kwa sababu jiografia pia ni ngumu kwa wahusika, kuna vijiji ambavyo vimeelezwa vimepata fidia. Wananchi wangu wa Kata za Mbulumbulu, Rhotia, Oldean, Endamaghang na Ganako, kila mwaka hupata usumbufu wa kuharibiwa mazao yao na wanyama wakali na hata kuuawa.

Tukio la mwisho, kama Serikali imesahau, mwezi Februari, 2014, ndani ya siku kumi, Wananchi wawili walipoteza maisha yao katika Kata ya Rhotia, kwa mauaji ya tembo wakilinda mashamba yao. Hatua zimechukuliwa ili kuhakikisha Wananchi hao wanapata fidia, hakuna matokeo hadi sasa. Jana nilipouliza swali, hoja ikawa ni Sheria ya Wanyamapori Namba Tano juu ya Hifadhi ya Wanyamaopri na Kanuni zake za Mwaka 2011.

Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza; kutokulipwa fidia na tathmini zinafanyika kila uharibifu unapotokea ni kwenda kinyume na sheria ya haki za kibinadamu. Sasa kwa kuwa labda haya maneno mawili yanachanganya, fidia na kifuta machozi, ni aibu, kama kweli Serikali itakataa kulipa fidia kwa watu wanaoharibiwa mazao yao na hata watu wanaouawa! (Makofi)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, ni wakati mwafaka sasa kama tatizo ni Sheria hii Namba Tano ya Uhifadhi wa Wanyama, Serikali ilete marekebisho ya Sheria hiyo. Anagongwa mtu na gari hapa, ni lazima alipwe fidia. Sasa tembo anamuua mwanadamu, hakuna fidia, kifuta machozizi! Mahindi, ngano, maharage, mwanadamu huyu anategemea ale, asomeshe, ajikimu katika mahitaji yake, ndani ya usiku mmoja, wanyama wanaharibu shamba lake lote, halafu Serikali inasema tutakupa fidia shilingi laki tano kwa eka kumi za mahindi, eka kumi za ngano!

Jamani, tunawatendea Wananchi wetu isivyo sawasawa na ndiyo maana Wananchi wamefika mahali na kusema, kama Serikali haituthamini, badala yake inathamini wanyama, ambao kimsingi katika uumbaji, tumepewa mamlaka ya kuwatiisha.

Ninaomba Serikali, Waziri uje na majibu, ndani ya *buffer zone*, *fire line* ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, ninashauri, aidha, ile *fire line* tui-fence moja kwa moja tuache shoruba za wanyama. Kwa njia hii tunaweza kuwatiisha wale wanyama, tuwachie shuruba zao, lakini ile *fire line* tui-fence.

Kila mwaka tunahangaika, Wananchi wanategemea kuvuna mazao, *overnight* tembo wamemaliza, nyati wamemaliza, wanaua watu. Sasa kama Serikali haiwezi kulinda watu wake, basi tupeni kauli kwamba Wananchi wajilinde na hawa wanyama, kitu ambacho hakitakuwa kizuri.

Ninafikiri, Mheshimiwa Waziri, uje na *solution*, hatuwezi kuendelea kila mwaka Karatu tunalia njaa, tunalia kuuawa na wanyama. (Makofi)

Jambo la pili, ni kwa jinsi gani vijiji vyote vinavyopakana na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro pamoja na TANAPA, Manyara, ni kweli tunakiri kwamba, kuna kitu tunaita ujirani mwema. Kwamba, kwa ujirani mwema tuweze kukaa vizuri na watusaidie. Nafikiri ujirani mwema *is just technical know who and know how*. Kwa nini tusihalalishe kwamba, vijiji hivyo vinufaike na 25% ya mapato hayo, kuliko kufikiri tu ujirani mwema, nikifurahi leo nakupa, nakujengea choo, nakujengea shule. Aaah, turasimishe, tuwe na kitu ambacho kinafahamika moja kwa moja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atambue, neema ya Wilaya ya Karatu inayopakana na mamlaka ya Ngorongoro na TANAPA, Manyara, athari ya wanyama ni kubwa na tuje na majibu ya kuwasaidia wale Wananchi wafanye kazi yao kwa amani na wale wanyama watunzike.

Mwisho, niseme hivi, mahusiano ni muhimu sana katika kulinda wanyama wetu, kati ya Wananchi na Serikali na Watumishi wa Mamlaka husika. Mahusiano mazuri zaidi ya sheria na amri na vitisho.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nilisema nitamwita Mheshimiwa Betty Machangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Asilimia 38 ya mapato ya TANAPA yanatokana na Utalii wa Mlima Kilimanjaro. Mwaka jana Wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro, bila kujali itikadi zetu, tulikaa na Waziri aliyekuwepo wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Kagasheki, tukakaa na Naibu Waziri wa wakati huo, Mheshimiwa Nyalandu ambaye sasa hivi ni Waziri na Mkurugenzi wa TANAPA. Kwamba, ule mlima unapotoa 80 billion kwa mwaka, kuna watu wanautunza. Ndiyo inawezekana TANAPA inafanya sana, lakini kuna watu wanautunza, moto ukitokea jamani Wakazi wa Rombo ndiyo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wanakimbia kwenda kuuzima. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atuambie ule mpango uliishia wapi?

Mheshimiwa Spika, naomba niendeleo na hii Wizara. Wizara hii ni muhimu sana, kwa sababu inasaidia sana kuinua pato la uchumi wa nchi yetu. Kwa mfano, Idara ya Wanyamapori peke yake, inatoa asilimia mbili ya Pato la Taifa na uwindaji wa kitalii kwa mfano, mwaka 2009 mpaka 2012, ulitupatia Pato la Taifa la shilingi bilioni 91.

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto nyingi na changamoto hizi ni mauaji na uuzaji wa wanyama wetu katika hizo Hifadhi. Naomba nijikite kwenye Taarifa ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu ambayo alitupa juzi.

Mheshimiwa Spika, katika Taarifa hii, CAG anasema, kwa mwaka 2010, wanyama 120 walio hai na ndege 16, waliuzwa bila kibali cha Serikali. Anasema, mwaka 2008 mpaka 2013, matukio 268 ya wanyama waliouawa yalifanyika. Hii inamaanisha kwamba, ni wanyama, siyo lazima tembo tu, hata na wanyama wengine. Mkaguzi Mkuu wa Serikali anasema kwamba, Wizara inaonesha udhaifu mkubwa katika kuweka takwimu sahihi. Anasema hawafanyi *analysis* au uchambuzi na hawapigi picha kujua ni maeneo gani ambayo yako kwenye *risk* kubwa ya uharamia wa kuua wanyama. Anasema, *patrol* zao zilitakiwa ziwe asilimia 60, lakini anasema *patrol* zao zilikuwa asilimia 37, sasa hivi zimepanda mpaka asilimia 47. Maana yake ni kwamba, hasa wakati wa mvua, wale wanaofanya *patrol* hawafanyi vya kutosha.

Kwa hiyo, wale wanaoua wanyama wanachukua *advantage* hiyo wanaendelea kuua wanyama. Anasema *indicator* inayowaonesha kwamba hapa ni *risk*, ni pale tu wanapokwenda wanakuta tembo ameuliwa, ndiyo hapo sasa Wizara inajua kwamba hapa kuna hatari.

Mheshimiwa Spika, nadhani wana haja ya kwenda na *recommendations* za CAG kwa ajili ya kulinda wanyama tulio nao.

Mkaguzi Mkuu anasema tembo 721 waliuawa katika maeneo matano mwaka 2009 mpaka 2012. Anasema inawezekana hao tembo ni wengi zaidi, kwa sababu ya Wizara kutokuwa na utaratibu wa kuwa na takwimu za uhakika. Anasema pia wapo wanyama wanaowindwa bila *quota*; kwa mfano, anasema, mwaka 2009 mpaka 2011, wanyama 366 waliwindwa bila *quota*, yaani watu wanakwenda tu msituni wanawinda. Inawezekana basi, kama wanafanya hivyo, hata ule mchango wa dola 5000 ambao kampuni za utalii zinatakiwa zitoe kwa Wizara, nazo hizi hazitolewi kwa sababu Wizara haina takwimu za uhakika.

Anasema yako makampuni 36 ambayo hayakulipa ankara za upigaji picha wa kitalii na kulikoshesha Taifa hili dola milioni 1.7. Hizo ni fedha nyingi na Wizara ingeweza kuchukua hatua kama ingefuatilia haya mambo. Ninaomba na ninaendelea kuomba kwamba, wafuatilie, waangalie Ripoti ya Mkaguzi Mkuu na watekeleze yale ambayo ame-*recommend*.

Mheshimiwa Spika, pembe za nduvu zinaendelea kukamatwa na *Ivory Room* ya Wizara ina tani 129. Ninaomba hizi tani za pembe za ndovu zichomwe. Ifanyike kabisa siku ambayo kweli hizi pembe zitachomwa, hii itatuletea heshima sana kama Nchi ya Tanzania kwamba tunataka kweli kumlinda huyu mnyama wetu anayelitwa tembo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Ripoti hii ya Mkaguzi Mkuu, hata mapato ya Wizara yamepungua. Mwaka 2009 mpaka 2010 yalikuwa 34 bilioni, lakini 2011/2012 yamefika 28 bilioni, kwa sababu ya hizo *loopholes* tunazosisikia.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ambayo yanasikitisha kama alivyosema mwenzangu kwamba, faru wanaoletwa kutoka kwa wahisani wanatozwa kodi. Nami niseme, sisi tuna Hifadhi ya Mkomazi kule Kilimanjaro katika Wilaya ya Same, bado tunaendelea kuhitaji faru na wanyama wengine. Kwa hiyo, *donors* wakisikia hili itakuwani tatizo kweli na inawezekana tusipate tena.

Mheshimiwa Spika, zipo taarifa ambazo zipo kwenye magazeti, taarifa za kukodisha Hifadhi za Taifa. Naomba niseme, kama hizi habari ni kweli, *TANAPA* inatosha, ipewe *facilities* za kutosha, *TANAPA* ina Uongozi bora, *TANAPA* inaweza. Tulishuhudia *Netgroup* ilivyofanya, kwa hiyo, hatutaki kurudi huko.

Mheshimiwa Spika, zipo taarifa nyingine za kuongeza vipindi vya kukodisha vitalu vya uwindaji kutoka miaka mitano mpaka miaka 15. Zipo taarifa nyingine za kusema muda wa uwindaji unatoka *six months* mpaka miezi tisa. Zipo taarifa za Mpaka wa Bulongola ambao umeshaongelewa, ambazo ziko kwenye magazeti.

Mheshimiwa Spika, naomba nisirudie kwa sababu wenzangu wameongea na mimi nashauri, Mpaka wa Bulogola ukifunguliwa, kama waasisi wetu waliona ni hasara, kwamba, mtalii atoke Kenya halafu aangalie wanyama arudi, ni hasara kweli, kwa sababu atakuwa hatuachii kitu. Naomba hili nalo liangaliwe, litaleta hasara kubwa kwa Serikali ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja, lakini Mheshimiwa Waziri atujibu Wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa nini Wilaya zetu hazipati gawio la *service levy* kutoka *TANAPA*? *(Makofi)*

SPIKA: Haya tunashukuru. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Grace Sindano Kiwelu na Mheshimiwa Josephine Genzabuke, yupo!

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, ninaitwa Grace Sindato Kiwelu, siyo Sindano.

SPIKA: *I beg your pardon. (Kicheko)*

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara hii. Nianze kwa kusema na mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Kama alivyosema Mwenyekiti wetu, tumeweza kufanya ziara katika maeneo ya Hifadhi zetu na katika Mapori ya Hifadhi za Taifa. Tumejionea upungufu ulioko kule, ikiwemo ukosefu wa vifaa, ukosefu wa magari kwa Askari wetu na hata uchache wa Askari wa Wanyamapori. Hii nayo imesababisha kuongezeka kwa wimbi la ujangili, ambapo Askari wetu wanakosa magari ya kufukuzana na majambazi na majambazi hawa wanatumia silaha kali za kivita ambazo Askari wetu hawana. Kwa hiyo, niungane na Kamati kwamba, tunaomba Wizara ifanikishe hayo, ili tuweze kupambana na janga hili la ujangili.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, niongelee, amesema Mjumbe mwenzangu, ule Mradi wa Faru Wekundu. Tulitembelea hiyo Hifadhi ya Mkomazi, lakini tulichokikuta pale, wale waliotuletea walisikitika sana.

Mheshimiwa Spika, haiingii akilini, Serikali ni moja, hata kama tunataka kukusanya kodi, lakini siyo kwa staili hiyo. Faru tumewaua sisi wenyewe, *either* kwa kushirikiana na majangili au kwa kuwahifadhi, lakini sisi tena tunataka kwenda ku-charge wale faru tuliopewa msaada, waje watuongezee pato la nchi, tunakwenda kuwatoza tena kodi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, hii haifai na wala haikubaliki. Tunaiomba Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, muwe mnakaa pamoja, mshauriane na mkubaliane. Vinginevyo, tutaonekana ni wendawazimu, tunatumia mali zetu vibaya halafu mwisho tunaletewa msaada, tunaendelea kwenda kuwatoza kodi na hii ni pamoja na zile silaha ambazo zilikaa bandarini kwa muda wa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la migogoro ya mipaka. Hili ni tatizo kubwa sana, tuliona katika Kamati yetu, Wananchi wanaopakana na Hifadhi zetu wanalalamika na kama hatutachukua hatua za haraka tunaweza kusababisha mauaji au matukio makubwa ambayo hatutaki yatokee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hatutalitilia maanani hili, hata ule ujirani mwema ambao tungetegemea Wananchi, yakitokea majanga au wakiona jambo baya linaendelea katika Hifadhi zetu, hawatatoa ushirikiano. *(Makofi)*

Niiombe Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi ione umhimu wa kutatua kero hii kubwa kwa Wananchi, ili tuwanusuru Wananchi na Wananchi waweze kutoa ushirikiano katika Hifadhi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, niongelee suala ambalo amesema Mbunge mwenzangu kutoka Kilimanjaro na tunamwomba Waziri, alipokuwa Waziri Kagasheki, jukumu hili alikuwa amekabidhiwa aliyekuwa Naibu Waziri na sasa hivi ni Waziri kamili. Tunamwomba sana, atupatie majibu wamefikia wapi, kwa sababu ule Mlima kama alivyosema mchangiaji mwingine, umekuwa ukiingiza pato kubwa sana kwa Taifa letu na imekuwa ni moja ya kivutio kikubwa Duniani; Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri, atupe majibu ya kutosheleza atakapokuwa anajibu hoja yake hapa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niipongeze TANAPA na nimpongeze Mkurugenzi Mkuu wa TANAPA, tulifanya ziara, wamekuwa wakishirikiana sana na jamii. Tumetembelea Miradi waliyoijengea jamii na niendeleo kuwaomba waendeleze ushirikiano wao na jamii. Leo yuko Mkurugenzi anayejali, lakini ningependa iletwe sheria kabisa ambayo itakuwa inasimamia. Leo yuko Kijazi, lakini anaweza akaja mtu mwingine asifanye kama anavyofanya yeye. Vizuri tukawa na Sheria ya hiyo 25% ambayo itakuwa inasimamiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, ninashukuru kwa kupata nafasi, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Genzabuke nimentaja, ataingia mchana. Mchana tukirudi hapa atakuwa Mheshimiwa Genzabuke, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi pia awepo.

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo, kuna wale Wakristo Wakatoliki huwa wanakuwa na lbada yao Jumatano, leo nimeelezwa niwatangazie kwamba, hakutakuwa na lbada hiyo; kwa sababu yule Padri anayewashughulikia ana dharura ya kitume mahali pengine. Kwa hiyo, hakuna lbada leo saa saba na muwaambie na wegine.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha Shughili za Bunge mpaka saa kumi.

(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Kama kuna mahali Duniani ambapo watu hawachelewi ni Bungeni. Hamuwezi kuwa mnakuja wakati sisi tumekaa ninyi mnaingia!

Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye na Mheshimiwa Genzabuke atafuatia. Anaanza Hilda Ngoye atafuata Mheshimiwa Genzabuke, si yupo?

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia machache katika Hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii.

Awali ya yote, naunga mkono Hotuba yake, ni nzuri lakini ina *challenges* nyingi ambazo nafikiri tutaendelea kuzijadili na hatimaye azifanyie kazi.

Mimi nitazungumza nje ya mazungumzo mengi yaliyopita asubuhi. Wengi walijielekeza kuhusu Wanyamapori na kwa hakika wa haki ya kujielekeza huko, kwa sababu wote tunaelewa kwamba uchumi wa nchi yetu unategemea sana ustawi wa wanyamapori na maliasili zetu kwa ajili ya utalii wa nchi kwa uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, mimi nilipenda kuzungumzia kuhusu uhifadhi wa milima yetu. Katika miaka ya nyuma tulikuwa na milima ambayo ilikuwa inahifadhiwa na ambayo ilikuwa na misitu mingi sana. Milima hii ilikuwa ndiyo asili kubwa sana ya vyanzo vya maji. Ukiangalia Milima ya Uluguru, kwa mfano, ukiangalia Milima ya Udzungwa, ukiangalia *ranges* za Milima ya Livingstone, utagundua kwamba, milima hii ilikuwa ndiyo chanzo kikuu cha maji katika miaka ya nyuma na kuleta mvuto kwa watalii.

Milima hii ingeweza kuhifadhiwa kama ilivyokuwa huko nyuma, kwa kweli ingechangia sana katika masuala ya utalii hasa katika masuala ya *eco-tourism*. *Eco-tourism* bado iko nyuma, tumejielekeza sana katika utalii wa wanyama, katika mbuga za wanyama, lakini *eco-tourism* tumeisahau. Kwa hiyo, naomba, kwa kuwa tunayo hii milima na sasa hivi imebaki vipara, ukipita Milima ya Uluguru utaona vipara ambavyo havichuruziki tena maji. Ukienda kule Safu za Milima ya Livingstone inayoanzia Wilaya ya Makete mpaka Wilaya ya Njombe mpaka Wilaya ya Lujewa na mpaka Wilaya ya Nyasa, milima hii ni kivotio kikubwa sana, hasa ile inayoteremka mpaka kupitia lake Nyasa, ni milima mikubwa, maumbile yake ni ya kuvutia. Ninaomba siku moja Mheshimiwa Waziri, ajitahidi afunge safari aipitie milima hiyo na kuona thamani ya milima hiyo.

Mheshimiwa Spika, milima imekwisha, hakuna mtu anayeijali, inachomwa moto, miti imekatwa yote. Kwa kweli uzuri ule wote umepotea. Sasa naomba, kwa kuwa tuna dhana ya ushirikishwaji wa jamii katika utunzaji wa wanyamapori, basi tuwe na dhana hiyo vilevile ya ushirikishaji Wananchi katika kuilinda milima hii ambayo imekuwa ni historia kwa muda mrefu sana. Ninaomba Wizara au Serikali izihusishe kwa asilimia mia, Halmashauri za Wilaya, kuzipangia mikakati ya namna ambavyo Wananchi wanaweza wakashirikishwa katika kulinda na kudumisha milima hii.

Kama inawezekana zile Sheria za Uhifadhi wa Milima zifanyiwe marekebisho ili kuwezesha Wananchi kuwa na hatamu katika kuilinda na kuisimamia. Mapato yanayotokana na uharibifu katika mazingira ya milima ile, basi asilimia fulani wapewe Wananchi ili na wao wapate hamasa ya kulinda ile milima isichomwe moto kabisa, wala miti isikatwe kabisa. Misitu ambayo ilikuwepo tangu awali iweze kuwepo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Tulikuwa tunatamani sana maji yaliyokuwa yanatiririka milima ambayo sasa hivi tunaiona ni upara. Ukienda kule Nyasa ninapozungumzia *eco-tourism*, ukipita kwa meli au kwa boti, ukazunguka ile milima ni ya kuvutia kweli kweli. Kwa hiyo, naomba sana, pamoja na mkazo tunaotoa kwa hifadhi za wanyamapori, hifadhi za ndege na kadhalika, basi sasa tujielekeze kwenye *eco-tourism* katika kuilinda milima hii ambayo imesahauliwa kwa kiasi kikubwa sana.

Ninaomba sana Serikali iamue na kuhakikisha kwamba, Halmashauri za Wilaya ambazo zipo kandokando ya milima hii inashiriki kikamilifu. Najua Serikali Kuu haiwezi kufanya kazi zote, lakini hao watakiwe kusimamia milima hii kwa uangalifu sana, badala ya hali ilivyo sasa kana kwamba milima hii haina mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, nakushukuru sana kwa kuniona na kuchangia hayo machache; ahsante sana. Namtakia kila la heri Mheshimiwa Waziri katika utekelezaji wa Bajeti yake. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Josephine Genzabuke, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Paresso.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu, kwa kunipa afya ya kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu. Nampongeza Waziri na Naibu wake, kwa taarifa yao nzuri waliyowasilisha tangu jana.

Mheshimiwa Spika, kupita Bunge lako Tukufu, napenda niishukuru Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, kwa kuweza kuendelea kuufungua Mkoa wa Kigoma. Tayari barabara zinajengwa, Daraja la Mto Malagarasi limekamilika na kiwanja cha ndege kinaendelea kujengwa. Kwa jitihada hizo zinazofanyika, nina imani kabisa Sekta ya Utalii itakwenda vizuri katika mkoa wetu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kigoma kuna utalii mwingi; ipo sehemu maarufu kule Ujiji, mahali ambapo Livingstone alikutana na Stanley chini ya mwembe, kwa hiyo, naamini watalii wanaweza kwenda pale wakafurahi. Ipo pia Gombe, kule kuna Sokwe Mtu, nako vilevile ninaamini kwa miundombinu hii ambayo sasa Serikali imeendelea kujenga Mkoani Kigoma, Watalii wataweza kuja Kigoma na tutaweza kupata kipato kwa kupitia vyanzo vyetu tulivyojaliwa na Mwenyezi Mungu. Naipongeza sana Serikali ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la ardhi katika Mkoa wa Kigoma na nchi nzima kwa ujumla. Misititu ya Hifadhi imeendelea kuwa tatizo kubwa sana, Wananchi wameendelea kupata shida, hasa wale wanaopakana na Hifadhi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali ilete sheria Bungeni, ifanye marekebisho, kusudi Wananchi waweze kupata maeneo ya kulima. Natambua faida ya misitu ni pamoja na mvua na kuhifadhi mito, lakini Wananchi nao wanahitaji kula, wanahitaji kuvaa, wanahitaji kusomesha watoto na wanahitaji kujiinua kiuchumi. Si hivyo tu, Wananchi wameongezeka mara dufu, ardhi imebaki ile ile. Kutokana na tatizo hilo, ndiyo maana kuna mgogoro mkubwa baina ya Hifadhi za Taifa na Wakulima.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri wa Maliasili na Utalii, Waziri wa Nyumba na Maendeleo ya Makazi, wakae pamoja waangalie ni jinsi gani wanaweza kukaa pamoja

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wakasaidia kupima mipaka ile ya Hifadhi ya Taifa kusudi Wananchi waweze kupata maeneo ya kulima.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wanateseka sana, kwa sababu wanapokwenda kuingia kwenye eneo ambalo siyo lao, kutokana na shida walizo nazo, Serikali nayo kwa kupitia sheria zilizotungwa humu Bungeni, wanakataa Wananchi wasiende kule, ni kweli. Sasa kutokana na ongezeko kubwa la watu, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, afikirie ni jinsi gani ya kuleta sheria hiyo haraka Bungeni ifanyiwe marekebisho Wananchi waweze kupata maeneo ya kulima.

Watu wa *Game Reserve*, yapo maeneo ambayo hayatumiki, wayapime kusudi maeneo yale Wananchi waweze kupewa walime. Maeneo yamekaa hayana kazi, waangalie sehemu ambayo haina kazi wapime Wananchi wapewe walime.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Serikali kuangalia sasa ni jinsi gani Wananchi wanateseka kutokana na kukosa eneo la kilimo. Hii si Kigoma peke yake, ni pamoja na maeneo mengine nchini. Kule Kasulu eneo la Kagerankanda, Wananchi wanateseka sana. Namwomba Waziri aje ajionee, Mawaziri waliotangulia walikuja, lakini walibadilishwa. Sasa na yeye ninaomba aje alione eneo hilo, ashirikiane na watu wa *Game Reserve*, waweze kuangalia maeneo hayo kusudi wapime upya Wananchi wapate maeneo ya kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, kwa mara nyingine tena niseme, naomba Sheria iletwe Bungeni ifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Spika, si mara yangu ya kwanza kusimama humu ndani kuomba sheria iletwe Bungeni; mimi ni Mbunge wa tangu mwaka 2005 - 2010. Mwaka 2007 niliwahi kusimama nikaomba sheria iletwe Bungeni ifanyiwe marekebisho na siyo mimi peke yangu, ni kilio cha Wabunge wengi. Sasa ni muda mwafaka, Serikali ilete sheria hiyo ifanyiwe marekebisho, Wananchi wapate maeneo ya kulima.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Nashukuru. Mheshimiwa Cecilia Paresso, atafuatiwa na Mheshimiwa Yusuf Salum Hussein.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, ni mwaka wa tatu sasa ninasimama katika Bunge hili na kuchangia Wizara hii, kuzungumzia suala la uharibifu wa mazao ya Wananchi, unaofanywa na wanyamapori katika Wilaya ya Karatu. Tumeeleza sana na swali niliuliza hapa Bungeni, Wizara ikanijibu kwamba, watakuja wakae na Wananchi wale, kuangalia namna gani wanaangalia ile mipaka kati ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na vijiji vilivyo jirani na Hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Waziri ulikuwa Naibu Waziri kipindi kile, uliahidi ungekuja hukuja. Wananchi wanaendelea kuumia, mazao ya Wananchi yanaendelea kuharibiwa, lakini hakuna kinachofanyika. Hicho kinachoitwa kifuta jasho hakifiki kwa wakati. Kuonesha ni jinsi gani Wizara hamjaona pia umuhimu wa matatizo ya Wananchi wa Karatu, katika ukurasa wa sita wa Hotuba ya Waziri, haikuonesha kuwa Wilaya ya Karatu ni miongoni mwa Wilaya ambazo Wananchi wanapata usumbufu mkubwa kutokana na wanyamapori kuharibu mazao yao.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Tunaomba baadaye wakati wa majumuisho, utuambie ni lini sasa matatizo haya yataisha katika kata mbalimbali na vijiji mbalimbali Wilayani Karatu ili Wananchi hao waweze kufaidika na kile ambacho wanakipanda na waweze kukipata.

Mheshimiwa Spika, ukisikiliza hawa Askari wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, wanajitoa kwenye wajibu huo, wanaona wao si wajibu wao kuwaondoa wanyama wakiingia. Wanaona ni wajibu wa Halmashauri, Halmashauri nayo inaona siyo wajibu wake. Hebu tuambieni ni nani anawajibika; ni Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro au ni Halmashauri ya Wilaya ya Karatu? Hilo utupatie jibu, lakini ni vyema mkatukutanisha wadau wa pande zote mbili ili matatizo haya yaweze kuisha na Wananchi waweze kuishi kwa amani.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Karatu ndiyo njia ya kwenda Ngorongoro, ndiko watalii wote wanakopita kwenda Ngorongoro. Wilaya hiyo ndiyo ambayo watalii wanapata mahitaji mbalimbali, hata wahusika wenyewe wa Ngorongoro wanapata mahitaji Karatu na wakati mwingine hata Wazungu wanapenda kulala kwenye hoteli za Karatu. Wilaya ya Karatu ina hoteli karibu 50 za kitalii. Wanapenda kulala Karatu na asubuhi kwenda Ngorongoro na kurudi kulala Karatu.

Mheshimiwa Spika, mapato yanayopatikana Ngorongoro. Je, Halmashauri ya Karatu itafaidika nini? Kwa sababu Karatu inategemewa na Ngorongoro, vivyo hivyo Ngorongoro inaitegemea Karatu, kwa hiyo, wote wanategemeana. Tunataka kujua, ni kiasi gani sasa kutokana na pato linalopatikana kwa mwaka katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kutokana na watalii kuingia Halmashauri ya Wilaya ya Karatu itafaidika na nini. Isionekane kama ni hisani tu; ndiyo kuna vitu wanavifanya hatuvipuuzi tunavikubali na tunavipokea, lakini sasa tuweke kabisa kiutaratibu kwamba, angalau katika mwaka wa fedha fulani Halmashauri ya Wilaya ya Karatu itafaidika kwa *percent* fulani kutokana na mapato yatakayopatikana katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, ningependa baadaye Mheshimiwa Waziri na Serikali watujibu ni kwa namna gani tunaweza kufaidika na mapato yanayotoka Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni mgogoro uliopo kati ya Wananchi wa Kata ya Bugel wanaopakana na Ziwa Manyara, wanaopakana na Msitu ambao uko chini ya Ziwa Manyara na unalindwa na TANAPA. Kumekuwa kuna mgogoro na malalamiko ya Wananchi; Wananchi wanalalamika mifugo yao inauawa, wananyang'anywa ardhi, wanakamatwa wanapigwa na wananyanyaswa na askari wa TANAPA. Malalamiko haya yamekuwepo kwa muda mrefu. Tunaambiwa ujirani mwema upo, kwenye Kikao cha RCC Arusha tulihudhuria wabunge na watu wa TANAPA walikuwepo, walituambia wangeimarisha suala la ujirani mwema.

Tunataka tupate majibu, ni lini wadau wote wa pande zote mbili, kwa maana ya Wananchi na hao TANAPA na askari, tutakaa kwa pamoja na kuona tatizo lipo upande gani ili tuweze kulimaliza na Wananchi waweze kuishi kwa amani?

Mheshimiwa Spika, nielezee suala la makampuni ya uwindaji. Kwa mujibu wa Taarifa ya CAG, anaonesha kabisa makampuni ya uwindaji, Wizara imeyaachia tu. Mmekuwa mkitoa vibali vya uwindaji halafu basi. CAG anaeleza kwamba, hakuna tathmini ya kina ya kufuatilia utendaji wa makampuni haya. Mkiwapa vibali ndiyo mnaona kama mmemaliza kazi. CAG anaeleza katika ripoti uyake kwamba, hamjafanya tathmini ya kina na kuna mfumo dhaifu wa kufuatilia makampuni haya ya uwindaji. Hii ni kwa mujibu wa Taarifa ya CAG.

Hamjui kuwa katika haya mapori ya uwindaji wanayopewa, kuna wanyama wangapi katika mapori hayo. Kwa hiyo, kuna mfumo dhaifu sana. Tunaomba kujua, Wizara imejipanga

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

vipi kuondoa udhaifu katika mfumo huu wa makampuni ya uwindaji wanaopewa kazi za uwindaji?

Mheshimiwa Spika, nimalizie la mwisho, udhibiti wa ukusanyaji wa mapato unaotokana na utalii wa picha. Kwa mujibu wa Taarifa ya CAG. Wizara mnapoteza karibia shilingi 2,700,000,000 kwa mwaka kwa sababu ya mapato yatokanayo na utalii wa picha. Hamkusanyi haya mapato na CAG anaeleza kwamba, hamna mpango, kutokuwa na utaratibu sahihi katika kusimamia suala hili la utalii wa picha.

Sasa tungelipata majibu ni kwa nini mnapoteza fedha hizi na ni kwa nini hakuna mfumo thabiti wa kusimamia utalii huu wa picha? Makampuni karibia 36 hayajalipa tozo hizi kwa ajili ya Utalii wa Picha. Tunataka kujua ni nini mikakati ya Wizara kuhakikisha fedha hizi zinazopotea zinapatikana na zinakuwa ni sehemu ya Pato la Taifa?

Mheshikmiwa Spika, mwaka 2013 niliuliza katika Bunge la Bajeti humu humu; ni lini mtaunda Bodi ya Ngorongoro? Baadhi ya Wajumbe wamesema hapa, mlituahidi kwamba mtaunda mpaka leo; kuna nini? Kwa nini hamuundi Bodi ya Ngorongoro kazi ziende kama inavyotakiwa?

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein!

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi jioni hii ya leo na mimi nichangie katika Wizara muhimu ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, Wachungaji watanisamehe, ninataka nianze kwa aya iliyomo ndani ya Biblia kwamba, kabla ya kutoa gogo katika jicho la mwenzako, kwanza toa kibanzi katika jicho lako.

MJUMBE FULANI: Boriti!

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Ndiyo maana nikasema mtanirekebisha, kumbe ni boriti, ninashukuru.

SPIKA: Hata Gogo ni hivyo hivyo tu. *(Kicheko)*

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, nimeanza hivyo kwa sababu wachangiaji wengi wanaelekeza tuhuma kwa wageni kwamba, ndiyo wanaotuharibia wanyamapori wetu au maliasili zetu; lakini tujjulize na sisi wenyewe hatuhusiki katika hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la wanyamapori kuharibiwa au maliasili zetu, haya mambo yalianza zamani, ni suala la muda mrefu sana, tokea wakati wa ukoloni. Tangu wakati wa biashara ya utumwa, watumwa walikuwa wanafanya kazi hii ya kuchukua maliasili kutoka Bara na kupeleka Bagamoyo na sehemu nyingine kama Zanzibar kwa ajili ya kusafirishwa. Kwa hiyo, ni suala la kihistoria. Sasa suala la kujiuliza hapa; hawa wageni wanapokuja kufanya ujangili huu na ukatili huu wanafanya na nani? *(Makofi)*

Ni dhahiri kwamba, sisi wenyewe tunashiriki katika hilo. Tunawakaribisha, tunashirikiana nao, tunawaonesha kwa sababu wao ni wageni na hawajui. Kwa hiyo, hapa ndipo ambapo mimi ninaiomba Wizara ianzie kwamba, sisi wenyewe tunahusika katika hili. Ninazungumza kuna

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

methali inayosema shoka haliwezi kukata bila ya mti. Kwa hiyo, mgeni hawezi kufanya ujangili ndani ya nchi yetu, kama sisi wenyewe hatushiriki. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Waziri akiwa Naibu Waziri, nilimkaribisha Pemba na sasa ni Waziri, ninamkaribisha Pemba aje tubadilishane uzoefu katika masuala kama haya. Sisi tulikuwa na tatizo kama hili kule, tulikuwa tunakula Popo kweli kweli.

MBUNGE FULANI: Popo!

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Popo ndiyo, hawa *Flying Fox*, mpaka wakawa katika hatari kabisa ya kumalizika, *endangered* kabisa. Hivi sasa kuna Popo kwa mamilioni. Mheshimiwa Waziri akija, tutabadilishana uzoefu katika haya na mambo mengine.

Suala la ushirikishwaji wa Wananchi katika uhifadhi wa maliasili zetu, *approach* yenu mnaoitumia huku, nadhani tukibadilishana uzoefu, utaona na sisi *approach* yetu. Utaona ni jinsi gani Wananchi wenyewe ndiyo wanaolinda hizi maliasili zao na hakuna tatizo lolote. Kwa hiyo, ninamkaribisha Mheshimiwa Waziri, nimefanya kazi katika sekta hii kwa miaka mingi, nina uzoefu, nitamwonesha mifano ya wazi wazi. Ninamkaribisha Pemba tubadilishane uzoefu ili tatizo hili limalizike.

Sasa ni nini kifanyike hapa? Kwanza, Watendaji waliopo katika Mbuga zetu ni wachache; kwa hiyo, ni lazima tuongeze Watendaji. Kama Watendaji ni wachache, maeneo ni makubwa tutalaumu nini! Majangili nao ni binadamu kama sisi, wanazo akili vilevile, kwa hiyo, wewe ukienda kufanya *patrol* upande wa Kaskazini, wao wataingia Kusini wafanye. Kwa hiyo, lazima tuongeze. Kwa hiyo, hapa Bajeti iangalie vizuri tuongeze wafanyakazi wa kutosha katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, la pili, hawa watu wanafanya kazi katika mazingira magumu; zile barabara kwenye Mbuga kule ni ngumu kusafiri na kufanya haya mambo; kwa hiyo ni lazima ziboreshe.

Cha tatu ni vitendea kazi. Wawe na vitendea kazi vya kisasa. Jamani sasa hivi Dunia inaenda katika sayansi na teknolojia, kwa hiyo, kama mtu anaingia na AK 47 ndani ya pori wewe una *Rifle* utafanya nini! Lazima sasa tubadilike na twende kisasa.

Mheshimiwa Spika, tutakapobadilisha haya mazingira, hali nayo itabadilika. Tusipofanya hivyo, hawa hawa wafanyakazi, kama mazingira yao ya kazi hayajabadilishwa; wao ndiyo watakaokuwa majangili au wao wenyewe watashirikiana na majangili katika kuendesha hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mfano; tuna Msitu wa Ngezi pale ambao ni *square kilometer* kama 14.5.8 hivi; walikuwa wanakuja majangili kutoka Kenya wakipasua mbao. Tulipokaa chini na kujiuliza, kwa sababu sisi ni Kisiwa, athari ndogo tu ni rahisi kuiona kwa haraka. Tukajua hili ni tatizo, tukarekebisha masuala yale kwa wale *Forest Guard*. Tukakaa na wanavijiji wanaozunguka pale, sasa hivi hili tatizo limeisha. Mheshimiwa Waziri, karibu upate uzoefu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niende kwenye Sekta ya Utalii, kwa sababu tayari nimepigwiwa kengele. Tuna vivutio vya kipekee ndani ya nchi hii vya utalii, Dunia nzima hakuna. Ukitaka kujua kama sisi utalii haujatusaidia, tuangalie pato linalotokana na utalii, rasillimali na maliasili zetu tulizonazo zinamnufaisha vipi Mtanzania wa kawaida, lakini pato linalopatikana ni kubwa mpaka wanatusaidia sisi huku. Sisi vyanzo vyote tulivyonavyo hivi, ambavyo Mwenyezi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mungu ametujalia peke yake Duniani, nikikupa mfano wa Pemba, tuna ndege watano ambao hawapo popote Duniani wako Pemba tu.

Watalii wanatoka huko kwao wanakuja kufanya *Bird Watching* pale Pemba tu. Tuna ufukwe wa bahari kwa Afrika ya Mashariki na Kati hii, suala hili la utalii wa baharini mambo ya *diving* haya, bahari yetu bado ni safi kabisa na ni *number one* kabisa. Kwa kuendeleza hilo, tumefungua *under water room* pale Kaskazini Pemba kwenye Hoteli ya *Manta Resort*. Nilikwambia Mheshimiwa karibu, uje uone inazidisha haya.

Ukilinganisha sasa rasilimali hizi tulizonazo na Mwananchi wa kawaida ananufaika vipi au pato lake linakuwa vipi haoani; ni kwamba, hatujajipanga kutumia rasilimali adhimu hizi kwa faida ya Wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuiangalie bahari. Wanatoka Kenya, mimi nilikuwa nafanya kazi karibu na Rasi pale Kigomasha; Wakenya wanakuja na maboti wanafanya *diving* na *fishing* pale. Yote haya ni mambo ambayo kama tutakuwa tumejipanga vizuri, tutainua Pato la Taifa hili kwa kiasi kikubwa sana. Sisi hatujajipanga vizuri na tunalalamika na tunawasingizia wageni, lakini na sisi wenyewe bado hatujajipanga vizuri katika masuala haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la utalii ni nyenzo kubwa sana ambayo Wizara hii kwa kupitia maliasili zake za misitu na mbuga na utalii, inaweza ikachangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa. Kwa mali tulizonazo na vivutio tulivyonyavyo, inatosha kabisa kuwezesha Pato la Taifa likatosha kwenye utalii tu.

(*Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, hiyo ni kengele ya pili kweli?

SPIKA: Ya pili.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: *Ooh, my God!*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante kwa mchango mzuri.

Mheshimiwa Magdalena Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi.

MHE. MAGDALENA HAMIS SAKAYA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, ninadiriki kusema kwamba, mambo makubwa ya kutisha aliyoyafanya Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Lazoro Nyalandu, ndani ya Wizara hii, kwa muda mfupi aliokaa pale ambao hauzidi miezi sita, vinatupa mashaka kama Watanzania, kama kweli anaweza kusimamia Wizara hii ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waziri kazi yake ya kwanza ni kusimamia sheria. Waziri amevunja sheria, kwanza, kwa kuwasimamisha Watendaji Wakuu, bila kufuata taratibu, sheria za kazi na utumishi wa umma. Pamoja na Katibu Mkuu kukiri kwamba hakufuata sheria na Ofisi ya Ikulu kukiri, Katibu Mkuu Kiongozi amekiri, lakini bado Waziri amekuwa na jeuri ya kuendelea kushinikiza kwamba lazima nitasimama kwenye maamuzi yangu. Ninajuliza maswali; Waziri Nyalandu jeuri hii anaipata wapi?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kingine hata kama kuna upungufu, sikatai kama watendaji, huwezi kudhalilisha watu wenye taaluma zao, tena waliobobea, wale ni Maprofesa kwenye Taaluma ya Wanyamapori, unawatoa ndani ya Kikao cha Kamati kama mbwa tokeni nje. Magazeti yanaandika. Wenzetu wa nchi za nje wanathamini taaluma za watu wao, sisi tunachezea taaluma za watu wetu. Leo ndiyo maana watu wetu wenye taaluma nzuri, wanakwenda kufundisha nje, wanakwenda kufanya kazi nje, kwa sababu ndani ya nchi tunashindwa kuwathamini. Alishindwa nini kutumia utaratibu mzuri wa kuhakikisha jambo hili linakwenda vizuri bila kuwadhalilisha kwenye vyombo vya magazeti?

Ninaomba Serikali ilifanyie kazi hili, vinginevyo, Maprofesa wengine watakata tamaa kufanya kazi hapa nchini kwa sababu wanadhaliishwa na watu wadogo kabisa kama hawa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, Waheshimiwa Wabunge wamezungumza hapa kuanzia asubuhi, Mheshimiwa Meghji amezunguza; ndani ya muda mfupi alioingia, anataka kufungua Mpaka wa Kenya na Tanzania kwa upande wa *National Park* ya Serengeti na Masai Mara. Maana yake ni nini? Maana yake wataingia Kenya, watalala Kenya, watakula Kenya, watafanya *shopping* Kenya, baadaye waje Tanzania kuangalia wanyama na kurudi Kenya. Hii ni hatari kubwa kwa uchumi wetu na uhifadhi wetu.

Mheshimiwa Spika, ndani ya muda mfupi huo, Mheshimiwa Waziri, anataka kurefusha muda wa uwindaji kutoka miezi sita mpaka miezi tisa. Vitu hivi vinawekwa kwa taaluma, kwa ushauri wa kitaalam, haviwekwi hivi hivi watu waote tu kwamba iwe miezi sita. Hata kama anayo hiyo taaluma, ilibidi atafute kwanza ushauri kwa wataalam.

Mheshimiwa Spika, anajua kabisa vitu vingine havihitaji hata kushauriwa; kwa mfano, suala la kwamba wanyama wanatakiwa wapumzike, miezi sita wakati wa mvua wanazaliana.

Haya yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, hayahitaji hata mtu kuomba ushauri; ni wewe mwenyewe kukaa na kujuliza kwa nini miezi sita iliwekwa haikuwekwa miezi tisa; ni nini *impact* yake?

Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utali ameshindwa kuliona hilo. Pamoja na kushauriwa, lakini bado anaendelea na msimamo wake, ameagiza aandaliwe GN mpya, aweze kuipitisha haraka, ili msimu ujao wa muda wa uwindaji uende mpaka miezi tisa badala ya miezi sita. Tunaomba Serikali ilisimamie hili, uhifadhi wetu tunalenga *objective* ya kwanza ya Uhifadhi wa Tanzania ni kulinda mali zetu, ni uhifadhi kwanza na biashara baadaye.

Mheshimiwa Spika, ndani ya muda mfupi, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ana mpango wa kurefusha muda wa umiliki wa vitalu kutoka miaka mitano mpaka miaka kumi na tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunashauri hapa Bungeni, wakati nchi za wenzetu Kenya, Uganda, Zambia, Zimbabwe, wanafunga wanakataa uwindaji wa kitalii, kulinda wanyama wao wazaliane vizuri; sisi tunaongeza muda *(Grace Period)* kwa Makampuni ya Kitalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na amefanya mkutano nao, akawatangazia hilo. Wataalam wameshauri, wala hasikii; hili linaumiza sana. Lingine pia, amefika pale amerefusha muda wa kulipa ada za vitalu vya uwindaji. Mimi nimekuwa ninajuliza; katika Wizara hiyo walikuwepo Mawaziri wengine na walikuwa wanasimamia; huwezi ndani ya miezi sita ukajifunza kila kitu, lazima vitu vingine u-buy time u-learn taratibu. Hili linatisha sana. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano suala la vitalu, wamesema *deadline* ni tarehe 31 Machi. Maana yake ni kuwa, wanaoomba vitalu siyo wote wanaolipia. Kwa hiyo, wameweka *deadline* ili wale ambao hawalipii vitalu vile vitangazwe tena, waweze kufanyiwa usaili na wapewe muda wa kujadiliwa waweze kupewa vitalu. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ameingia haraka na kufanya mabadiliko ya ajabu sana; hili linasikitisha.

Mheshimiwa Spika, suala lingine la kutaka uwekezaji kwenye Hifadhi zetu; hili linatisha. Bila hata ya kufanya utafiti, bila hata kufanya utafiti na wenzetu wan je; nani asiyejua jinsi ambavyo Mataifa mengine yanatamani sana Hifadhi zetu? Leo tunataka kupeleka Hifadhi ya Katavi kwenda kwenye Uwekezaji, eti tunatumia PPP; haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, hata baada ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, kushauriwa na Wataalam, tarehe 24 Machi, 2014, cha kusikitisha tarehe 26 ameondoka yeye na Watumishi wengine wa Idara ya Wanyamapori na baadhi ya Wajumbe kutoka TANAPA, wamekwenda kuwafuata hawa APN kule South Africa! Alikuwa anafuata nini huko? Anatumia fedha za Serikalikwenda kuwabembeleza nini? Hifadhi zetu zinajiuza, kwanza, ni rasilimali kwa ajili ya Taifa letu na ni urithi kwa ajili ya watoto wetu. Hili linatisha, ndiyo maana ninasema, nina wasiwasi na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, liko suala lingine, ninaomba nimwulize Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ni kwa nini Serikali inaruhusu Makampuni haya mawili ya Uwindaji; Kampuni ya Mwiba na Wilbard Wildworth yanaendelea kuleta vurugu kwenye Sekta ya wanyamapori kiasi cha kuathiri mapato ya Serikali na yeye amenyamaza?

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limegusiwa na Waheshimiwa Wabunge, wapo waliosema kwamba, vile vitalu ambavyo Watanzania wameshindwa kuviendeza virudishwe wapewe wageni. Suala hili ninalipinga kwa nguvu zote. Sababu ya sisi kuleta Sheria hapa Bungeni mwaka 2009 ilikuwa ni kuwashirikisha wazawa kwenye Sekta ya Uwindaji.

Tukaishauri Serikali iwawezeshe wazawa waweze kushiriki kikamilifu kwenye Sekta ya Uwindaji. Leo tuangalie, Serikali imewasaidiaje hawa wazawa na imewawezeshaje hawa Wazawa.

Hatuwezi kufanya biashara za utalii ni biashara za watu wa nje, watu weupe, hapana; lazima wenzetu washiriki. Kwa hiyo, ninakataa kabisa, Vitalu vya Watanzania viendelee kuwa vya Wantanzania na Sheria ya Wanyamapori iheshimiwe. Serikali iwasaidie wazawa waweze kushiriki vizuri sana kwenye Sekta ya Uwindaji wa Kitalii kwa sababu na wao pia wana uwezo na dhamira, tatizo ni uwezo mdogo.

Mheshimiwa Spika, lipo suala lingine la wale ambao walishiriki kwenye Operesheni Tokomeza, siku 56 hawajawahi kulipwa. Tunaomba Serikali iweze kuwalipa, walifanya kazi ngumu kama walivyosema wenzangu, tunaomba sana wasiachwe.

Wanasikitika na wanaumia lakini pia wanatakiwa waendelee kufanya kazi. Kwa hiyo, Serikali iangalie katika Bajeti ya mwaka huu, watengewe pesa yao wapewe, ni Watanzania waweze kushiriki vizuri kwenye suala la uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante, kwa mchango wako. Sasa nimwite Mheshimiwa Joseph Mbilinyi. Zile Kamati za Kisekta ndiyo kazi zao hizo, hawawezi kukwepa lawama. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiswa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, leo hii tunaongea hapa, kama nikirejea mchango wa Mheshimiwa James Mbatia, hatuzungumzi tena Operesheni Tokomeza, zaidi ya watu kupongezana, wakati kuna Wafugaji bado wamebaki maskini hawajui hatima zao na wengine wamebaki na ulemavu hawajui hatima zao. (*Makofi*)

Leo tunaambiwa Mheshimiwa Rais ameunda Tume. Sasa mimi ninajuliza kama Mheshimiwa Rais ameunda Tume, Ndugu yangu Mheshimiwa Balozi Kagasheki kwa nini alipigwa chini? Ina maana yeye alifanywa *scape-goat*, kwa sababu kama lilikuwa ni suala la kuwajibika kwenye ile Wizara, mimi kila ninapomwona Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, amekaa pale, ninaiona bado Operesheni Tokomeza inatokomea na inazidi kutokomeza mali za Wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nami ninasema kabisa ninaunga mkono suala la Wabunge kutokuwa Mawaziri, kwa sababu wanachokifanya Mawaziri wetu ni kupiga siasa. Sote ni mashahidi kwenye *Media*, kuelekea uteuzi mpya wa Mawaziri; Mheshimiwa Nyalandu alikuwa *all over the Media*, mpaka nikawa ninashangaa hii imekuwaje kila siku yuko kwenye Gazeti na Vyombo vingine vya Habari, kumbe anapiga siasa ili apate *post*. Amepata *post* anazingua! Wanyama bado wanaangamia na wanyamapori bado wanakufa. Sasa huyu mtu, Wazungu wana msemu unasema: "*Be careful what you wish for, you might receive it.*" Kuwa makini na unachoomba, kwa sababu unaweza ukakipata kumbe hauko tayari kukifanyia kazi, matokeo yake utakuja kuumbuka tu.

Mheshimiwa Spika, hii haiwezekani kabisa. Nami nikiangalia kwa juu juu ninaona Wizara hii imeshindikana; kwa sababu katika Bunge hili tumebadilisha Mawaziri watatu, lakini *debate* na majadiliano ni yale yale.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu; japokuwa mnaogopa kuwapa nchi Wanajeshi, mimi ninashauri hii Wizara apewe Mwanajeshi. Kwa sababu huko si tunasema kuna watu wanatumia silaha kali, sijui kuna watu wanakuja na zana za moto kutoka nje; chukueni Jenerali mmoja au *Brigadier* mmoja, tufuate taratibu, Rais ampe Ubunge, ninatumaini ana nafasi bado, mkabidhini hii Wizara, tuone kazi itakayokwenda kufanyika kule kukabiliana na haya yote. Vinginevyo, tutaendelea kupiga siasa na hii Wizara wakati kimsingi Wizara hii ilitakiwa ituondolee kabisa umaskini. Tunaambiwa Wizara hii ina mchango mkubwa kuliko hata madini. Sasa inakuwaje kwa sababu ya mtu tu kushindwa kutoa *leadership* tunabaki tunapiga *mark time!* (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa mfano wa Malaysia. Tulikuwa Malaysia, kwa nini huwa ninapenda kutoa mfano wa Malaysia? Kwa sababu Malaysia mwaka 1981ukienda kwenye historia ya uchumi tulikuwa *almost* tunafanana. Mwaka 2013 tumekwenda Malaysia, wanasema mwaka huu wana-expect kupata Watalii milioni 28, yaani zaidi ya *population* yao.

Unamwuliza yule mtu *any-present* kwamba, vivutio vyenu ni nini? Ni maghofa tu, wamejenga maghorofa marefu yale mawili, *Petronas Twin Towers*, wamejenga na daraja.

Zaidi ya hapo wana *beach*. Ukimwuliza hakuna zaidi; wanasema zaidi ni chakula. Sisi Tanzania tunaambiwa ni wa pili kwa vivutio, halafu Watalii tunaowapata ni 800,000 au 1,000,000; sasa hii inakuwaje, unashindwa kuelewa!

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, tatizo ni nini, hatujitangazi *properly*. Tumeweka matangano pale *Airport* mfano, wameweka *screens* za kutangaza utalii kwamba mtalii anaposhuka anapata *preview* ya nini anachokwenda kukiona, lakini zile mashine hazifanya kazi na nasikia zimetumika zaidi ya dola 500,000 na Mheshimiwa Rais alikwenda kuzindua ile mitambo, lakini haifanyi kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, angalia watu wakitoka hapa wanakwenda kutangaza matangazo Marekani wanakwenda kulipia *CNN International*. *CNN International* ni kwa ajili ya Afrika zaidi, nchi za *third world*, *Europe* kidogo ndiyo watu wanaangalia. Kule ndani kama unataka kupata Wamarekani, Mheshimiwa Nyalandu nenda *ABC*, *MSNBC* hizo ndizo *channels* ambazo Wamarekani ndani ya Marekani wanaangalia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mara kumi hata uangalie namna ya kwenda kutangaza *C-SPAN*, najua unaifahamu ingawa haina matangazo, mara mia ufanikiwe kupenyeza matangazo kwenye *C-SPAN channel* ya bure unaweza ukapata Wamarekani wengi zaidi wanaoangalia kuliko hawa.

Mheshimiwa Spika, zaidi leo inabidi Mheshimiwa Waziri aniambie, nafahamu kulikuwa na programu ya kutumia kampuni za nje kutangaza utalii wetu Marekani, London kwa mfano kwenye London *tubes* zile tulikuwa tunasikia, sasa leo ningeomba nijue kwamba ni kampuni gani zilipewa hizo kazi, je, ni za Watanzania au wageni? Zilifanya kazi kwa mafanikio ya kiasi gani, vinginevyo tutaendelea kupiga *mark time* tu.

Mheshimiwa Spika, sijasikia mkakati wa dhati kuhusiana na utalii Kanda ya Nyanda za Juu, *International Airport* iko tayari, lakini hakuna mkakati thabiti. Sasa Mheshimiwa Waziri na msaidizi wake waje sasa watueleze kwa dhati wana mkakati gani wa kuimarisha utalii upande wa Kusini, Nyanda za Juu, na hii programu iwe ya wazi kwamba, hatua ya kwanza tumejenga *Airport*; hatua ya pili tutajenga barabara na hatua ya tatu, tuwashirikishe na wananchi wa Mbeya, Iringa, kuna wafanyabiashara kule wana fedha, pengine kuna mtu ana fedha ana mtaji wa kununua *trucks* 100 au 200, lakini ukimpa program kwenye masuala ya utalii anaweza akaji-tune akabadilisha uwekezaji wake akaangalia namna gani anaweza kujenga hoteli za kisasa.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu wote tunajua moja ya changamoto kubwa za utalii katika nchi hii ni *hotel rooms*, hiyo iko kwenye *records*. Hata huko Arusha hakuna vyumba vya kutosha vya watu kulala. Kwa hiyo, kuna watu wanataka kuja kuangalia wanyama, lakini wakiangalia hoteli wanaona kuna upungufu wana-*cancel*, wanakwenda Barbados na Malaysia huko kuangalia madaraja badala ya kuja kuangalia wanyama na vivutio vya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niambiwe mkakati wa Mheshimiwa Waziri ni upi katika kukuza utalii katika Nyanda za Juu Kusini ikiwemo Mbeya. Ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Haya ahsante kwa mazungumzo!

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, nianze na kuwapongeza Mawaziri wote na watendaji wa Wizara kwa kuleta hotuba ya kuwasilisha bajeti yao ili tuweze kujadili hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, yapo baadhi mambo yahusuyo Wizara hii ambayo ningependa kupatiwa ufafanuzi na Wizara hii.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhaulishaji wa misitu iliyopo mijini, naomba kujua sera ya uhaulishaji wa misitu iliyopo katikati ya mji mfano, msitu wa Kihesa, Kilolo katika Jimbo la Iringa Mjini.

Mheshimiwa Spika, msitu huu upo katikati ya makazi ya watu kikiwepo Chuo Kikuu cha Tumaini – Iringa, msitu huu hauna kitu chochote, ni pori ambalo limekuwa hatarishi kwa maisha ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, miaka yote mitatu iliyopita nimekuwa nikiuliza kwa kuchangia hapa Bungeni na nilishawahi kuleta swali linalohusu uhaulishaji wa msitu huo katika Wizara yako na mkatoa majawabu na baadaye nikatofautiana na aliyekuwa Waziri Mheshimiwa Balozi Hamis Kagasheki wakati mpo katika Wizara moja, *Hansard* inayo majibu. Ningeomba kupitia Bunge hili la Bajeti sasa nipatiwe jibu sahihi la msitu huu kwa kuwa upo sawa kabisa uliokuwa msitu wa Mbeya yaani *Mbeya Forest*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara ya Maliasili na Utalii ina kitengo ambacho kinasimamia uhifadhi wa mazingira lakini kitengo hiki kipo chini ya Halmashauri (TAMISEMI) inapotokea mfanyakazi huyo akifanya tatizo Wizara ipi inamuwajibisha kati ya Wizara ya Maliasili au TAMISEMI?

Mheshimiwa Spika, naomba nipatiwe ufafanuzi mfano, mtu akitaka kupata kibali cha kuchoma mkaa analipia fedha kupata kibali, fedha hizo zinalipiwa Halmashauri, je, mgao wake unakuwaje?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la wanyamapori, kwa kuwa wanyama wetu wa Tanzania wamekuwa wakiteketea kwa kuuawa na umetuambia kuna baadhi ya nchi nyingine zimeonyesha kuguswa sana na jambo hili mpaka kutoa misaada ya helikopta, magari na kadhalika kwa ajili ya kulinda tembo wetu, je, wananchi wa Tanzania wameshiriki na wameguswa vipi katika jambo hili la kuuawa kwa wanyama wetu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu miundombinu katika mbuga zetu, inasikitisha kuona Serikali yetu bado haijaweka kipaumbele katika kuhakikisha kuwa mbuga za wanyama nchini zinakuwa na barabara za lami ili kuvutia watalii kwenda kwa wingi. Mbuga ya Ruaha (*Ruaha Nation Park*) ni mbuga ya pili kwa ukubwa Afrika lakini tatizo kubwa lililopo ni miundombinu ya barabara ya kwenda mbugani ni mibovu, pia kiwanja cha ndege kilichopo katika Mkoa wa Iringa (*Nduli Airport*) ni tatizo. Nashauri Serikali katika vipaumbele vya kukuza uchumi wa nchi hii vingeanzalia zile barabara zinazobeba uchumi kama hiyo inayokwenda *Ruaha National Park* na viwanja vya ndege vyenye tija.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sera ya upandaji miti, Serikali imeweka siku maalum ya upandaji miti kwa nchi nzima ambayo ni tarehe 01 Aprili na kwa kuwa nchi yetu imetofautisha hali ya majira ya mwaka, Mikoa mingine huwa masika na mingine ni kiangazi, kwa nini Serikali isipange kila Mkoa uwe na siku yake ili kuwa na uhakika wa miji hiyo tunayoipanda kukua vizuri kwa sababu Serikali huwa haifuatili miti iliyopandwa maendeleo yake.

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kupatiwa ufafanuzi ya kwamba nchi yetu ina misitu ambayo ina miti ya asili na misitu ya miti ya kupandwa na binadamu na faida za misitu zinafahamika ni pamoja na kuleta mvua na kuhifadhi mazingira, je, Serikali ina *data bank* ya misitu yetu yote nchini kujua kama kiasi gani cha miti kinapandwa kwa mwaka? Kwa kuwa miti ni kitu kinachohesabika, Serikali ituambie ni miti mingapi iliyopandwa na itavunwa mingapi hata kwa msitu wa Mufindi tu?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huu naomba kuunga mkono hoja.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa bajeti ya Wizara hii ni ndogo sana ukilinganisha na mahitaji mbalimbali ambayo Wizara hii inahitaji.

Mheshimiwa Spika, uwindaji haramu Tanzania umekithiri, takwimu zinaonyesha kwa mwaka 2010 wanyama 120 na ndege 16 walisafilishwa kinyume na sheria. Sasa hali hii itaenda mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na udhaifu katika kufanya doria hususani kipindi cha mvua na hivyo kufanya eneo la doria linakuwa dogo na hivyo sehemu nyingi kutokufikia.

Pia uchache wa wafanyakazi na vifaa unaendelea kuwa tatizo katika *game reserve* nyingi hivyo kutoleta tija katika shughuli za Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa *report* ya CAG makampuni 36 hayakulipa tozo za Serikali kwa gharama za utalii wa picha *on time* hivyo hali hii inapelekea Wizara kukosa au kupoteza Dola za Kimarekani milioni 1.7 ambayo inathamani za Kitanzania shilingi bilioni 2.7 je, Serikali inachukua hatua gani dhidi ya hili?

Mheshimiwa Spika, hata hiyo Wizara imeendelea kulaumiwa kwa kutofuatilia utekelezaji wa sheria ya wanyamapori. Shughuli za wanyamapori hazisimamiwi vizuri, mapato hayakusanywi ipasavyo, hivyo Wizara ina mikakati gani dhidi ya changamoto hizi?

Mheshimiwa Spika, shukrani.

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu ili niweze kupatiwa majibu wakati wa hitimisho za hoja hii.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mpaka kati ya kijiji cha Makao - Wilaya ya Meatu na Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro ni takribani kiasi cha kilometa za mraba 135 za Wilaya ya Meatu katika kijiji cha Makao kimeingia katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Mipaka inayotambulika ulimwenguni kote ni mipaka ya kiutawala na si mipaka ya Hifadhi. Tunawataka wenzetu wa Mamlaka walione hili na waweze kutulipa fidia kila mwaka kwa ajili ya hilo eneo letu la Wilaya katika Kijiji cha Makao lililoingia kwenye Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa eneo ninaloliongelea lipo katika mgogoro kati ya Wilaya ya Meatu katika Kijiji cha Makao na Hifadhi ya Ngorongoro katika Kijiji cha Kakesio na kwa kuwa wenzetu wa Mamlaka wameamua kuanzisha ranchi ya ng'ombe, naomba kuishauri Wizara kuwa ujenzi wa ranchi ile usimame mpaka tutakapoweza kutatua mgogoro uliopo baina ya wananchi wa Kijiji cha Makao (Meatu) na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, mgogoro huu endapo hautashughulikiwa mapema na haraka unaweza kusababisha vita baina ya wananchi wa Makao na wale waishio katika Kijiji cha Kakesio ambapo ni takribani kilomita za mraba 135 za eneo la Kijiji cha Makao limeingia ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulisisitiza ni ulimbikizaji wa malipo 25% kwa ajili ya uwindaji kwenye Pori la Akiba la Maswa (*Maswa Game Reserve*). Ninaomba malimbikizo haya ya fedha hizi yaweze kurudishwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Meatu katika vijiji vinavyozunguka pori hili ili viweze kufaidi mapato yatoakanayo na hilo Pori la Akiba la Maswa.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri wananchi wanaolizunguka pori hili (vijiji husika) wakaona faida ya wao kuishi karibu na pori hilo.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa endapo hiyo 25% itarudishwa kwenye Halmashauri ya Meatu kwa ajili ya vijiji husika, basi itakuwa rahisi kwa wananchi kuzidi kulilinda na kuliendeleza Pori hili la Akiba la Maswa.

Mheshimiwa Spika, namuomba Waziri atoe ufafanuzi wa kina juu ya haya mambo mawili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaomba kuunga mkono hoja hii.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Waziri kwa kuteuliwa kwake katika nafasi yake, lakini nakubaliana na utendaji wake kwa kiasi kikubwa ifuatayo ni mchango wangu kwa Wizara.

Mheshimiwa Spika, pamekuwepo migogoro baina ya vijiji kadhaa na maeneo ya mapori ya wanyamapori yanayomilikiwa na Wizara nchini kuingiliana, nashauri tatizo hili litafutiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Lwanfi Game Reserve* Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ilitoa pori hili kwa Wizara lakini mipaka ya pori hili imekuwa haieleweki hasa baada ya pori kukabidhiwa kiasi cha kuleta shida katika vijiji vya asili ambavyo vilikuwepo muda kabla ya kutambuliwa kwa pori lenyewe vijiji hivi ni Mlambo, King'ombe, Kasapa, Mtapenda, Ng'undwe na Namansi, vijiji hivi vinasumbuliwa na wasimamizi wa pori kuwa vipo ndani ya pori.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara kulitafutia ufumbuzi suala hili kwani ni kero kwa wananchi, kama Mbunge wa Jimbo nimekuwa nikichangia mara kwa mara kuhusu kurekebisha mipaka na kuwaachia maeneo wananchi wa vijiji hivi ili wasiendeleo kubughudhiwa na wapate ardhi ya kulima. Mara kadhaa wananchi kutoka vijiji hivi wanahoji viongozi wa Serikali akiwemo Mkuu wetu wa Wilaya kwamba sisi tumezaliwa katika vijiji hivi kwa nini leo tunaambiwa tupo ndani ya *reserve* na hakuna majibu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mahusiano, pamekuwa na mahusiano yasiyo rafiki sana kati ya wananchi, wafugaji na wahifadhi wa wanyamapori hasa katika mapori makubwa ya Kaskazini, naomba kujenga mazingira rafiki ili kujenga uhifadhi endelevu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Operation Tokomeza* ukiacha madhara yaliyojitokeza zoezi hili lisiachwe kuendelezwa, naomba liandalawe na lidhibitiwe kwa kutofanya madhara kwa wananchi lakini likomeshe uhalifu wa wanyamapori na miti (maliasili yetu) na wale wote waliohusika kufanya ndivyo sivyo wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Wildlife Management Association (WMA)* ni muhimu kwa ulinzi wa wanyamapori na mapori yenyewe, ulinzi wa kutegemea wahifadhi hauwezi kufaulu kuleta uhifadhi endelevu. Naomba ushirikishwaji huu wa wananchi ufanyike pia katika pori la Lwanfi lililopo Nkasi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na nitashukuru kama suala la mipaka na vijiji husika litafafanuliwa kwani sio geni, kwa nini vijiji vionekane vipo ndani ya hifadhi wakati vina hati za usajili?

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wa Wizara bila kumsahau Katibu Mkuu wa Wizara kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri ninazo changamoto zifuatazo ambazo zitasaidia katika kujenga.

Kwanza ni uboreshaji wa utalii wa mambo ya kale, naomba tuboreshe katika eneo hili. Nikiwa kama mdau nimeona jinsi India inavyokusanya fedha nyingi kwa watu wanaotembelea mambo ya kale, kwa mfano, Mikindani, *Bagamoyo Ruins*, Pangani na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu tuboreshe moja baada ya nyingine kwa mfano, Bagamoyo (*Kaole ruins*) wanafunzi wengi sana kutoka Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani wanaenda kwa wingi. Bagamoyo ingeboreshwa kwa haraka na ubora unaostahili na kuifanyia *promotion*, hapa tutapata fedha ambazo zitasaidia Serikali baada ya hapo tunaweza kuangalia eneo lingine ambalo lina idadi kubwa ya watalii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu makumbusho ya Taifa, bajeti ni ndogo sana Shirika liongezewe bajeti ili waweze kufanya maonesho/events mbalimbali, kwa kuwa Serikali tayari wamejenga jengo zuri sana napongeza sana. Sasa kazi ifanyike, ni lazima kuwa na fedha.

Mheshimiwa Spika, pia naomba waongeze fedha, lakini pia ni vizuri zaidi kwa wafanyakazi wa Makumbusho ya Taifa na wale wahifadhi wameshaenda kuona nchi nyingine wanavyofanya. Nashauri fedha zitolewe wapelekwe kwa haraka China na India wakaone na wakapate mafunzo ambayo yatawasaidia sana katika utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mji wa kihistoria Dar es Salaam ilielekezwa kuwa mji wa kihistoria, je, jambo hili limeishia wapi? Nyumba za kihistoria makao makuu ya *TANU* (Lumumba), Magomeni nyumba ya Mwalimu Nyerere, Pugu Sekondari sijaona bajeti ya uhifadhi wa maeneo haya ya kihistoria au kuna utaratibu gani wa kuyatangaza na kuyahifadhi maeneo hayo?

Mheshimiwa Spika, mwisho napongeza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Kitengo cha Historia chini ya Profesa Mapunda kwa kuwezesha kupata wataalam wengi ambao leo tunatetea na kuona umuhimu wa yale aliyotufundisha katika kazi yake ya *Cultural Heritage and Tours Management*.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana Profesa Mapunda na pale ninapoenda nchi nyingine ndiyo nilizidi kuona umuhimu wa kazi hiyo. Nashauri Serikali na Wizara hii iongeze nguvu na bajeti yao iongezwe tuweze kupata wataalam wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja 100%, nisipopata majibu nachukua mshahara wa Waziri na sitoachia mpaka.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Spika, kuhusu ujangili unaoendelea kuwaangamiza tembo wetu unajenga taswira mbaya katika vita hivi kama kuna mtandao ambao kudhibitiwa ni lazima tuombe msaada wa Mataifa mengine.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kati ya askari wetu wa wanyamapori wapewe zana na silaha za kisasa kuweza kukabiliana na majangili.

Mheshimiwa Spika, tunashauri Wizara itoe motisha ya fedha kila mara baada ya askari wa wanyamapori wanapofanikiwa kupambana na majangili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utalii wetu bado haujakidhi haja ya kuongeza Pato la Taifa kulingana na wingi wa vivutio vya utalii, mapango yenye kuvutia, fukwe za bahari zilizo nzuri, misitu na Hifadhi za Taifa, kwa pamoja hazijaandaliwa kuweza kuendana na ushindani wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, nchi ya Vietnam wanategemea zaidi ya 30% ya uchumi wake kwa mapango (caves) na visiwa vidogo vidogo katika bahari na maziwa na sisi Tanzania tunayo aina ya vivutio hivyo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nielezwe kuwa ni majangili wangapi wamekamatwa na kupatiwa hukumu kati ya Machi, 2013 hadi Aprili, 2014.

Mheshimiwa Spika, mnyama anapomjeruhi na kumuua binadamu hutolewa fidia ndogo, lakini binadamu atakapomuua mnyama kama tembo analipa fidia kiasi cha shilingi milioni mbili, wanyama wanajeruhi binadamu na kupoteza maisha wakati mwingine unasababishwa na mamlaka husika kuwa wazembe namna ya kuwaua wanyama, ninaishauri Serikali kuangalia upya fidia ambapo binadamu anajeruhiwa na kupoteza maisha kutokana na wanyama.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, kuhusu ulinzi wa wanyamapori ni suala ambalo Wizara imelitolea maelezo yasiyojitoshela katika ukurasa ya nne na wa tano kipengele (iii) aya ya 9, 10, 11 na 12. Hivyo naomba Waziri katika majumuisho atoe maelezo ya ziada juu ya masuala yafuatayo:-

Kwanza, kiwango cha faini kilicholipwa kilinganishe na idadi ya watuhumiwa wanaokamatwa ni kidogo sana yaani shilingi 75,686,000/= . Aidha, katika kesi 154 zenye watuhumiwa 227 zinazoendelea katika mahakama mbalimbali, zipi ni kesi kubwa na je, ni hatua gani kati ya utoroshaji wa wanyama hai wakiwemo twiga imefikia na je, habari zinazosambaa kwamba mtuhumiwa Ahmed Kamran ametoroka zina ukweli?

Katika kuelezea *Operation Tokomeza* ya doria kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, Wizara imekwepa kueleza matatizo makubwa yaliyojitokeza katika *operation* hiyo. Aidha Wizara haijaeleza miaka saba toka maazimio ya Bunge yapitishwe imechukua hatua gani dhidi ya waliosababisha hali hiyo, imewezaje kwa kushirikiana na Wizara nyingine kuwasaidia walioathirika na operesheni hiyo, pamoja na kueleza hatua zilizochukuliwa kurekebisha kasoro zilizojitokeza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu misitu na nyuki imezungumzwa katika hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii kuanzia ukurasa wa 13 mpaka 22 aya za 32 mpaka 52, maelezo hayajatolewa kuhusu namna ufiisadi na upotevu wa mapato wanayoshughulikia. Doria dhidi ya uvushaji haramu wa biashara haramu ya mazao ya misitu pekee zinazoelezwa katika aya ya 36 haziwezi kutosha kuziba mianya ya ufiisadi, unyonyaji, upotevu na uharibifu. Sekta ndogo hii ilipaswa kutazamwa kwa upana ikiwemo juu ya misitu inayopandwa na ruzuku kutolewa au fedha kurejeshwa kama sehemu ya mikakati ya kitaifa na kimataifa inayohusu kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, mbinu zinazotumika kwenye sekta ya madini na ufuatiliaji unaofanywa na wananchi juu ya kudai kunufaika na maliasili za nchi na kumiliki rasilimali hizo zinapaswa pia kutazamwa katika muktadha wa udhibiti wa biashara ya mazao ya misitu. Jamii zenye madini zinalenga kunufaika na rasilimali zilizo katika eneo hilo. Hivyo hivyo jamii zenye misitu zinapaswa kunufaika na misitu.

Aidha kwa namna operesheni za udhibiti wa biashara haramu ya misitu na ujangili wa wanyamapori zilivyotekelezwa kwa udhaifu mkubwa sikubaliani na pongezi kwa Serikali na Rais zilizoingizwa katika taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, badala yake naunga mkono Kamati katika kutaka Serikali itekeleze Maazimio ya Bunge na kuwasilisha taarifa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii, ina uwezo wa kuchangia kiwango kikubwa zaidi katika uchumi wa nchi na kudumisha urithi wa Taifa letu. Wizara inaweza kufanya hivyo kwa kuhakikisha mipango inayopitishwa na fedha zinazotengwa, zinatolewa kwa wakati na kutumika kwa ufanisi kutekeleza kazi zilizopangwa kwenye Sekta Ndogo za Wanyamapori, Misitu na Nyuki, Utalii na Mambo ya Kale. Naomba kuhusu mapitio ya utekelezaji kwa mwaka 2013/2014 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2014/2015, yafuatayo yazingatiwe na Wizara, Mifuko, Watendaji na Taasisi zinazohusika:-

Mheshimiwa Spika, Sekta Ndogo ya Wanyamapori, iendelezwe kwa pamoja na mambo mengine, Serikali iwasilishe Taarifa Bungeni ya utekelezaji wa maamuzi ya Bunge kufuatia Ripoti ya Kamati kuhusu Opereshini Tokomezwa. Tume iliyoundwa na Rais ishauriwe kujielekeza katika masuala yenye kuhitaji uchunguzi zaidi. Hata hivyo, Maazimio yote ambayo hayahitaji uchunguzi, taarifa ya utekelezaji iwasilishwe katika Mkutano huu wa Bunge

Mheshimiwa Spika, aidha, Mfuko wa Hifadhi ya Wanyamapori (*TWPF*), uongeze mchango katika kuligawa Pori la Akiba la Pande kuwa Hifadhi ya Wanyamapori na Kivutio cha Utalii Jijini (*city, reserve or park*).

Mheshimiwa Spika, pili, Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki, inapaswa kuendelezwa na Wakala wa Huduma za Misitu, Wakala wa Mbegu za Miti, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania, Mfuko wa Misitu na Wizara, kulinusuru Taifa dhidi ya uharibifu mkubwa wa misitu unaoendelea na athari za mabadiliko ya tabianchi. Wizara na Vyombo tajwa vishiriki pia katika uboreshaji wa Pori la Akiba la Pande. Kwa upande mwingine, juu ya mazao ya misitu na viwanda vya mazao hayo, Wizara iliniahidi miaka iliyopita kufuatilia na kuchukua hatua kuhusu kasoro zilizojitokeza katika ubinafsishaji wa kiwanda cha *Tembo Chip Board*, Mkumbara Tanga, kilichokuwa chini ya Wizara. Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, tatu, Sekta Ndogo ya Utalii ambayo ina mchango mkubwa katika uchumi na ustawi inapaswa kuendelezwa kwa kuongeza kutangaza vivutio, lakini pia kuongeza vivutio. Kwa upande wa utalii katika Jiji la Dar es Salaam, Bodi ya Utalii (*TTB*), inapaswa kuliwezesha Pori la Akiba la Pande kuanza kutumika kama eneo la kambi mjini (*Camp Site*) na eneo la kujivinjari (*tracking/trailing*) wakati hatua nyingine za kuongeza au kuleta wanyamapori zikisubiriwa.

Mheshimiwa Spika, nne, Sekta Ndogo ya Mambo Kale ni muhimu kuendelezwa ikiwa pia ni kielelezo cha urithi wa kiutamaduni na historia ya nchi. Hivyo, Bodi mpya ya Shirika la Makumbusho iteuliwe. Makumbusho ya Dar es Salaam yaboreshwe yawe kituo muhimu ambacho watalii wengi wapitao jijini watatembelea kama zilivyo *museums* za majiji mengine Duniani. Aidha, Tamasha la Utamaduni wa Tanzania lipanuliwe kuhusisha jamii toka mikoa mingine mfano Mwanza.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kama Mjumbe taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge la Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2013/2014 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya Wizara tajwa kwa mwaka 2014/2015 isipokuwa pongezi Kamati ilizotoa kwa Serikali na Rais kuhusu Operesheni Tokomeza na vita dhidi ya ujangili kutokana na udhaifu uliojitokeza katika mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza na kuzingatia maoni na mapendekezo ya Kamati, naomba Wizara ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa kuzingatia yafuatayo katika majumuisho na utekelezaji. Katika kushughulikia changamoto zilizotajwa kwenye 3.1.2, ukurasa wa tatu juu ya kubomolewa kwa majengo ya kale yanayostahili kuhifadhiwa mijini kipaumbele kiwe Jiji la Dar es Salaam ambapo hivi sasa majengo mengi ya kale yanabomolewa. Hivyo, katika kutekeleza mikakati iliyotajwa kwenye 3.2.2, ukurasa wa nne, Wizara itushirikishe Wabunge wa Dar es Salaam kama sehemu ya wadau.

Mheshimiwa Spika, katika kufanya majumuisho na katika kuzingatia maoni na ushauri wa Kamati sehemu ya 5.0, kipengele cha 5.1, aya ya 2.2, ukurasa wa saba, kuhusu utalii wa ndani, katika mwaka wa fedha 2013/2014 niliwaunga mkono Bodi ya Utalii (TTB) katika tukio ambalo liliandaliwa katika "bar" mojawapo ya Jimbo la Ubungo kuhamasisha utalii wa ndani. Katika hotuba yangu nieleza kwamba shughuli zaidi zinapaswa kufanyika ukiondoa matangazo kwenye vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, ili kurahisisha kukua, TTB iweke mstari wa mbele viongozi wa wananchi, watu mashuhuri au maarufu wa kutoka rika na fani mbalimbali pamoja na baadhi ya wananchi wa kawaida kama mabalozi wa vivutio hivyo. Binafsi niko tayari kushiriki katika uhamasishaji kwa Mkoa wa Dar es Salaam ambapo kwa msingi wa idadi ya watu, aina ya kazi wanazofanya kwa wenye ajira na mchanganyiko wa kutoka maeneo mbalimbali nchini ni soko kubwa zaidi la utalii wa ndani. TTB inapaswa kueleza mkakati uliopo wa kufanikisha azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, kipengele cha 3.4 kuhusu ya uchimbaji wa madini katika mapori ya akiba, bado kuna kasoro juu ya ruhusa iliyotolewa kwa Kampuni ya *Mantra Tanzania Limited* kwa masuala ya msingi niliyoyahoji au kupendekeza kwa Serikali kwa nyakati mbalimbali kati ya 2011, 2012 na 2013 wakati wa mijadala ya mapitio ya utekelezaji wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara mbalimbali. Wizara irejee kumbukumbu hizo na kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, katika masuala mengine kipengele cha 7.8, ukurasa wa 14, nakubaliana na pendekezo la kuboreshwa kwa Pori la Akiba la Pande (*Pande Forest/Reserve*), kuwa kivutio kingine cha utalii. Kwa kuwa toka 2012, Waziri Nyalandu wakati huo akiwa Naibu Waziri aliahidi utekelezaji, atoe mrejesho/majibu leo.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kukamilisha mchakato wa kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Wanyamapori hapa nchini (TAWA). Hii ni hatua nzuri sana katika usimamizi wa sekta hii muhimu sana kwa uhifadhi wa maliasili hii lakini pia kwa uchumi wa Taifa na watu wake.

Mheshimiwa Spika, hifadhi ya jamii ya wanyamapori ya Wami-Mbili iliyopo Morogoro na Pwani iliyoanzishwa mwaka 1997 chini ya ufadhili wa shirika la *Danish Hunters Association* na kushirikisha wanavijiji 24 vinavyozunguka eneo hilo lina hali mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, eneo hili lina rasilimali nyingi sana ya misitu, wanyamapori wa aina zote, mito yenye samaki wa rangi mbalimbali, vilima vizuri, mabwawa ya viboko na vingine

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

vizuri. Eneo hili ni *corridor, migration route* ya wanyama katika *Selous Game Reserve* kwenda Mkomanzi.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka zaidi ya kumi na sita (16) sasa wananchi wamelinda hifadhi hii kwa nguvu zao zote kwa kutumia silaha duni kwa lengo la kuja kunufaika nalo baada ya kuanza biashara ya utalii. Eneo hili limeachwa bila uangalizi wowote na Wizara, mfadhili amemaliza muda wake tangu mwaka 2012, tembo wanapigwa kona zote mchana kweupe, wanyama wanawindwa kwa magari na wanajeshi wamefanya eneo lao la uwindaji, mbao zinakatwa kwa makontena kwenda Dar es Salaam, mkaa unachomwa kwa *tones with* na mchana limekuwa ni shamba la bibi, hifadhi hii ipo kilometa 170 tu kutoka Dar es Salaam. Ni kilio kikubwa kwa watalii.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kuiweka hifadhi hii chini ya TANAPA ili kunusuru maliasili iliyopo pale, Serikali imekuwa na kigugumizi kwa zaidi ya miaka minne sasa kuhusu kupandisha tozo za vitanda kwa mahoteli ya kitalii yaliyopo ndani ya hifadhi zetu. Tozo zilizotozwa miaka 10 iliyopita kwa *ku-charge* dola 10 mpaka 15 kwa kitanda wakati kitanda kililipiwa dola za Kimarekani 50 mpaka 100 ndizo zinazoendelea leo wakati kitanda ni dola za Kimarekani 300 mpaka 1000 kuna nini hapa. Ni maslahi ya nani yanalindwa hapa? Waziri aeleze Bunge kwa nini kuna kigugumizi na kila TANAPA wakitaka kupandisha tozo wanazuiwa?

Mheshimiwa Spika, kuna wizi mkubwa unafanywa kwenye meno ya tembo yanayokamatwa maeneo mbalimbali hapa nchini, meno ya tembo yanakamatwa, yanawekwa kwenye vituo vya polisi bila *register* yoyote.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi Lindi meno ya tembo 108 na kilo 20 za ndovu yamepotea katika Kituo cha Polisi bila maelezo yoyote. Meno ya tembo 103 yamegunduliwa Kituo cha Polisi Liwale bila Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori kupewa taarifa. Waziri alieleze Bunge ni utaratibu gani umewekwa na Wizara kufuatilia meno ya tembo yanayokamatwa maeneo mbalimbali? Ni kwa nini hakuna *registration* ya meno ya tembo kwenye Vituo vya Polisi?

Mheshimiwa Spika, utalii wa ndani umeshindwa kupata kasi hapa nchini kwa sababu wageni wengi wazawa wameshindwa kulipia gharama za malazi zilizopo ndani ya hifadhi zetu, gharama za hoteli ni kubwa sana. Watanzania wamekuwa wanafanya *day trip* kwa uwezo walionao na hivyo kushindwa kutembelea vivutio kwa mapana.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kutoa vibali/upendeleo wa pekee kwa wazawa wajenge hoteli za bei nafuu ndani ya hifadhi zetu ili watoe malazi kwa bei nafuu kwa Watanzania?

MHE. SELEMANI S. JAFU: Mheshimiwa Spika, naomba kupata ufafanuzi katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kwa nini makampuni yanayolalamikiwa ya TGTS na WWS yanaendelea kukalia vitalu ambavyo Wizara yako ilishatoa maamuzi? Kuna nini kinaendelea mpaka makampuni hayo yanakuwa na kauli nzito? Wizara itoe tamko leo ya kuyataka makampuni hayo kuondoka katika vitalu hivyo ili makampuni ya Kitanzania yaweze kupata fursa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa mbalimbali zinaonyesha kwamba WWS walitakiwa kuondoka kitalu cha *Lake Natron GCA* tangu tarehe 23/05/2013. Je, kuna nini mpaka leo kitalu hicho kinaendelea kukaliwa kinyume na taratibu? Je, ujasiri huo wa kukiuka taratibu unatoka wapi? Naomba leo itoke kauli juu ya jambo hili.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Msitu wa Kazi Mzumbwi na Msitu wa Ruvu Chini unaathirika sana je, Serikali hailioni hili? Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka kwa kugeuza msitu wa Ruvu Chini kuwa mbuga mpya ya utalii kwa kupanda wanyama ili kuleta faida kwa Taifa na Wilaya ya Kisarawe ikilinganishwa na hali ya sasa ambapo Msitu wa Ruvu Chini umekwisha kabisa licha ya fedha nyingi zinazotumika kwa doria.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali isifungue mpaka wa kuwezesha watalii kutoka Kenya kuingia moja kwa moja katika hifadhi zetu. Je, kwa nini mpaka huo ufunguliwe? Tunaitaka Serikali iachane na mpango huo kwa maslahi ya Taifa.

MHE. FAITH M. MITAMBO: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hotuba hii ya Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuzungumzia tatizo la mpaka lililoko kati ya Pori la Akiba la Selous (*Selous Game Reserve*) na Halmashauri ya Kijiji cha Kikulyungu, Wilayani Liwale.

Mheshimiwa Spika, mgogoro huu uko zaidi ya miaka 10, na kwa upande wangu tangu nimekuwa Mbunge, huu ni mwaka wa 4 nazungumzia swala hili ama kwa kuongea ama kwa kuuliza maswali ama kwa kwenda na kuonana na Waziri anayehusika kwa mazungumzo ya moja kwa moja bila mafanikio.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kijiji cha Kikulyungu, Wilaya ya Liwale wana ramani na Tangazo la Serikali la mwaka 1974 na vitu hivyo vyote kwa pamoja vilielekeza kwamba mpaka kati ya *Selous Game Reserve* na Halmashauri ya Kijiji cha Kikulyungu, ni Mto Matandu.

Mheshimiwa Spika, ghafla huko miaka ya katikati, mpaka ule umekuwa *diverted* na kuingia eneo ambalo wananchi wa Kijiji cha Kikulyungu, wanaamini kwamba ni eneo la Halmashauri ya Kijiji cha Kikulyungu.

Mheshimiwa Spika, eneo linalogombaniwa ni dogo sana, eneo la bwawa la Kihurumila na wananchi wa Kikulyungu wamenituma, wanailalamikia Serikali na wanahitaji kupata sasa jibu la madai yao ya muda mrefu na wameendelea kuonesha kutoridhika na jinsi ambavyo Wizara hii ya Maliasili inavyoshindwa kutatua tatizo hili la mgogoro wa mpaka huo.

Mheshimiwa Spika, naiomba na kuishauri Wizara ya Maliasili ichukue hatua za makusudi na za haraka za kumaliza mgogoro huu na niombe pia Wizara hii, hebu mkubali mkapime ule mpaka tena upya na tumieni tu busara za kawaida, warudishieni lile eneo na bwawa la Kihurumila wananchi wa Kikulyungu ili mgogoro huo uishe. Hivi mnasubiri mpaka yatokee maafa na uvunjifu wa amani katika eneo hili ndipo Serikali ichukue hatua?.

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu ni lini Mheshimiwa Waziri wa Maliasili yuko tayari kufuatana na mimi kule Liwale tukaungane na Kamati ya Ulinzi na Usalama na Viongozi wengine ngazi ya Wilaya tuungane na uongozi wa Serikali ya Kijiji cha Kikulyungu, wataalam wa Wizara ya Maliasili, sote kwa pamoja twende Kikulyungu ili tukamalize mgogoro huu.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikipata majibu yasiyoridhisha na yasiyowaridhisha wananchi wa Kijiji cha Kikulyungu, leo katika majumuisho yako, naomba kupata jibu la ushauri wangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapato yanayotokana na vitalu na uwindaji wa Kitalii.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Liwale ni wadau wakubwa sana wa Hifadhi ya Selous na ukiangalia ukurasa wa 52 wa hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri imeonesha kwamba mapato yaliyotokana na uwindaji wa kitalii na mgao ulivyofanywa kwa Vijiji 72, Wilaya ya Liwale ikiwa na Vijiji 10, mwaka

- 2008/2009 – vijiji vile 10, vilipatiwa Shilingi milioni 20.5
- 2009/2010 – vijiji vile 10, vilipatiwa Shilingi milioni.
- 2010/2011 – vijiji vile 10, vilipatiwa Shilingi milioni 14.1.
- 2011/2012 – vijiji vile 10, vilipatiwa Shilingi milioni 7.6.
- 2012/2013 – vijiji vile 10, vilipatiwa Shilingi milioni 9.9.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mtiririko huu, ni kwamba mgawanyo huo wa mapato umeendelea kupungua, ni kwa nini?

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa 44, Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema kwamba, Halmashauri za Wilaya 38, zenye vitalu vya uwindaji zilipatiwa jumla ya shilingi bilioni 8.7 kwa mwaka wa fedha 2013/2014, ikiwa ni mgawo wa asilimia 25 ya mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Spika, bado namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hotuba yake, nitataka anipe takwimu, Wilaya hizo ni zipi na kila Wilaya ilipelekewa shilingi ngapi na kwa vyovyote vile Wilaya ya Liwale imo ndani ya Wilaya hizi 38 na je, Wilaya hii imepewa shilingi ngapi na *criteria* wanayoitumia katika kuzigawa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Spika, mimi ni mdau wa Utalii wa zaidi ya miaka 20, nina uzoefu na nimesomea uendeshaji wa kuongoza shughuli za utalii. Kwa misingi hiyo nashauri Serikali yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, uuzaji wa bidhaa ya Utalii (*Marketing of Tourism Destination/Products*) ili kuweza kuuza bidhaa hizi lazima uwe na:-

(a) Mkakati *Tourism marketing strategy* isiyo ya kubabaisha kama hii ya Tanzania ya kubandika matangazo kwenye viwanja au vituo vya treni Ulaya na huko America.

(b) Lazima kuwe na *National Airline* kwenda na kuondoka kwenye hiyo *destination*, ndege ambayo wafanyabiashara wake watakuwa na *access to concessional prices*.

(c) Bodi imara ya Utalii yenye fedha za kutosha kufanya *destination and marketing* huwezi kufanya *marketing* kwa fedha ndogo kama ya Tanzania *Tourism Board* US\$ 2.27 million ukilinganisha na Afrika Kusini US\$ 70 million yaani (TShs. 114bn) mara mbili ya bajeti ya Wizara ya Utalii ya Tanzania TShs. 83.1bn na jirani yetu Kenya US\$ 30 TShs. 49bn nusu ya bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, wataalam na watumishi katika sekta (*Tourism Administrators and services providers*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kufungua lango la Bologonja. Kwa ufupi lango hili utafiti wa wanasayansi umependekeza kwamba, hii ni *interface* ya *two equal systems* yaani Masai Mara National Park na Sengereti. Kwa hiyo, ikifunguliwa kutumiwa kama barabara ya kupitisha magari ya watalii na magari mengine itaharibu uhifadhi wa eneo hilo. Pili kwa sababu ya kiuchumi likifunguliwa lango hili biashara ya utalii kwa *Tour Operators* wa Tanzania umekwisha hasa wale wa Arusha, Moshi na Karatu.

Mheshimiwa Spika, *meeting incentives conference and exhibition (MICE)* ili kutumia Kituo cha Mikutano cha Arusha *International Conference, Julius Nyerere International Conference Centre* nashauri juhudi ifanywe kupata wataalam watakaouza bidhaa hiyo kwa ustadi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mipaka ya Vijiji na Hifadhi za Taifa/Mapori ya Akiba Tengefu, kwa kuwa maisha ya watu wengi na mali yao yamepotea, nashauri Taasisi hizi ziweke zuio kwenye maeneo kuzuia wanyamapori wasitoke (*fenced*). Hii inafanyika *Kepruga, National Park Afrika* ya Kusini na *Tsavo National Park, Kenya*.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi kwa hotuba nzuri ya bajeti ya 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo napenda kutoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na migogoro mingi kati ya wakulima, wafugaji, wachimba madini na Hifadhi za Taifa. Migogoro hii imeleta madhara makubwa kwa wahusika ikiwa ni pamoja na baadhi ya wananchi kupoteza maisha. Aidha, mifugo mingi imeuawa na hata kushikiliwa kwenye mabomba ya hifadhi bila huduma muhimu na hivyo kusababisha vifo vingi vya mifugo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kero hii kubwa kwa wahusika, nashauri Wizara ifanye tathmini ya kina ili kuona iwapo mipaka hiyo ya hifadhi bado inakidhi sifa ya kuwa hifadhi hasa baada ya kuzingatia mwingiliano mkubwa uliopo kati ya watumiaji mbalimbali na uhitaji mkubwa wa ardhi. Ikumbukwe kwamba idadi ya watu na mifugo inazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko kubwa la ujangili na hasa wa tembo, nashauri Serikali yetu ikishirikiana na rafiki wa maendeleo waongoze kampeni ya kupiga vita biashara ya meno ya tembo duniani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi hoja hii iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze Mawaziri wote wawili kwa kazi kubwa wanayoifanya na naendelea kuwatia moyo waendeleo kupambana katika kuhifadhi mbuga zetu na wanyama waliopo ili kuendeleza na kukuza utalii nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa, Jimbo la Chalinze limebaki kuwa na deni kubwa sana ambalo limetokana na ahadi ya Wizara kuwalipa fidia.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe baada ya zoezi la Operesheni Tokomeza kumeibuka matatizo makubwa ambayo ningeiomba Wizara husika itupe majibu.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mpaka wa Hifadhi kati ya Vijiji vya Mkange, Uvinje, Matipwili, Gama, Makurunge, Manda-Mazingala, Kwekonje, Kwang'andu, Changalikwa, Kwamsanja na Kibindu na Hifadhi ya Saadani na Hifadhi ya Kwaruhombo, ni lini tatizo hili litakwisha na Serikali ina mpango gani kutekeleza hilo?

Mheshimiwa Spika, pili, baada ya mvutano wa muda mrefu kati ya Mamlaka ya Hifadhi (TANAPA), wananchi wa Kijiji cha Tengwe zote mbili walikubali kuondoka katika eneo lao kupisha hifadhi. Serikali kupitia Wizara ya Utalii ilikubali kuwalipa fidia wananchi wa Kijiji hicho. Je, ni lini fidia hizo zitaanza kulipwa?

Mheshimiwa Spika, *note*: Tengwe 71 Matipwili na Tengwe 57 Saadani. Tathmini imekwishafanyika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. STEPHEN M. WASIRA: Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono, naomba kauli ya Wizara kuhusu ulipaji wa fidia. Ukurasa wa sita wa Hotuba ya Waziri, ametenga maeneo ambayo yameathirika kwa uharibifu wa mazao. Wilaya ya Bunda ambayo imewasilisha madai yaliyotokana na uharibifu wa mazao haikutajwa, wala hakuna fedha/kifuta machozi ambacho kimekipwa. Hili sio jambo jema hata kidogo. Naiomba Wizara ishughulikie madai ya wananchi wa Bunda.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana 2013 askari wa VIP huko Grumet, waliswaga ng'ombe zaidi ya 100 na kuwatumbukiza katika Mto Rubama. Tatizo hili lilifikishwa Wizarani na Wizara iliahidi kulishughulikia suala hili. Hadi sasa, hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, uhusiano wa wahifadhi na wananchi wanaopakana na *Grumet Game Reserve* ni mbaya sana. Uhusiano huu mbaya, unawafanya wananchi kuichukia Serikali. Utozaji faini zisizo na risiti na unyanyasaji unaofanywa na wahifadhi kwa wananchi unahitaji kukomeshwa, namkaribisha Waziri kuja Bunda, kuwasikiliza wananchi kama sehemu ya kujenga mahusiano baina ya wananchi na hifadhi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuanzisha Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania. Uamuzi huu muhimu ulichelewa sana kiasi cha kuzitorotesha uhudumiaji makini wa Hifadhi ya Mapori ya Akiba kama Rungwa, Kizigo, Mhezi na Chaya. Mapato mengi yaliishia Idara ya Wanyamapori ya Wizara hii kwa kutumika kwa mambo mengine ya utawala na si kwa faida ya maendeleo ya hifadhi ya mbuga hizi. Bila shaka matatizo yaliyopo yatatatuliwa na mamlaka mpya itakayoanza.

Mheshimiwa Spika, aidha naishauri Serikali iangalie upya uamuzi wa kuteua Morogoro kuwa Makao Makuu ya Mamlaka haya. Napenda kujua ni vigezo gani vilitumika kuteua Morogoro badala ya Manyoni ambako ni katikati ya nchi na kuna mapori pia kama Rungwa, Kizigo, Muhesi na Chaya. Manyoni ni *centre* ya KDU kanda ya kati ingefaa kabisa, Mamlaka ya Wanyamapori yangukuwa Manyoni.

Mheshimiwa Spika, *TWP Fund* haiko wazi katika matumizi ya Mfuko huu. Hauwelekezwi kuwasaidia zaidi wananchi wa maeneo yanayozunguka Mapori na Mbunga za Wanyamapori

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

28 na Mapori Tengefu 43. Badala yake zinapelekwa kuhudumia maeneo yasiyokuwa na mahusiano yoyote na wanyamapori. Naishauri Serikali kusimamia kwa karibu zaidi Mfuko huu uelekezwe kuwaletea wananchi na maeneo husika kwa kuwapatia maji, zahanati, vituo vya afya na shule ili yapige hatua katika maendeleo. Maeneo haya yako nyuma sana hata ujenzi wa maabara katika shule zao za sekondari umekwama.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua fedha zilizotengwa na TWPF Sh. 250,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la Rungwa miaka saba iliyopita ziliishia wapi? Bwawa hilo hadi leo halijajengwa bila maelezo kutoka Wizara hii, naomba maelezo Bwawa hili litaanza kujengwa lini.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya mipaka inaendelea kufukuta. Tatizo la umbali kutoka ukanda wa hifadhi hadi makazi ya watu linaendelea kuleta usumbufu kwa wananchi. Miti 500 michache sana kuwa *buffer zone* kati ya makazi na hifadhi, suala hili liangaliwe upya ili kutoa nafasi zaidi kwa wanadamu kufanya shughuli zao za maendeleo kwenye kilimo na ufugaji. Naomba kupata maelekezo juu ya suala hili. Hifadhi ya Mapori ya Mhesi, Rungwa na Kizigo imebana sana wananchi hawa mahali pa kufugia hata nyuki.

Mheshimiwa Spika, faini inayotozwa kwa wananchi wanaochunga mifugo kwenye mapori ya hifadhi ni kubwa mno, ni sawa na kuwafilisi wananchi na kuwafanya maskini hata kama uharibifu ni mdogo. Serikali ilianganalie suala hili la faini ilizoweka na usimamizi wake, zaidi faini hizi zinanufaisha wafanyakazi binafsi na si Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, ajira kwenye maeneo haya ya hifadhi hakuna, vijana hawana kazi na mara nyingine wameletwa vijana wasiohusika katika maeneo hayo. Hii huchochea uharibifu wa misitu na kuhamasisha ujangili na kadhalika. Serikali itafute ufumbuzi wa suala hili, ili wananchi na hasa vijana washirikishwe katika uendeshaji wa mapori hayo kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, fidia za uharibifu wa mazao na vifo vya wanadamu wanaouawa na wanyamapori wakali, bado ni kitendawili na pia ni ndogo. Serikali ihuishe malipo ya fidia hizo na ilipe kwa wakati.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii inachelewesha ujenzi wa barabara katika Mkoa wa Rukwa kwa kukataa kutoa kibali kwa Wakandarasi wa Kichina kuendelea na ujenzi wa barabara kwa kukataa barabara kupita maeneo ya Kisumba. Barabara ya Kasanga *port to* Sumbawanga tafadhali tunaomba kibali kwa ajili ya maslahi ya wananchi wa Rukwa na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pili, barabara ya Kanazi – Kibaoni wamezuia Wachina wasichukue changarawe maeneo ya Kanazi na kuchelewesha barabara hiyo na *TANROAD* eti mpaka walipe mamilioni ya pesa na *TANROAD* haina pesa kwa kuwa haja ya Wizara ya Maliasili kutoa kibali ili kazi ifanyike na wananchi wafaidike na barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni kero kubwa kuchelewesha maendeleo ya wana Rukwa. Naomba jibu haraka.

Mheshimiwa Spika, hao wananchi ndio walenzi na hiyo misitu ya maliasili. Mwisho watapata hasira na kuleta madhara katika hiyo misitu.

Mheshimiwa Spika, tafadhali sana kwa Mheshimiwa Waziri, barabara pia ni muhimu sana pia kwa ulinzi wa misitu yetu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, zote hizo ni barabara za lami.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa kupata fursa hii ili nami nichangie Hotuba hii ingalau kwa njia ya maandishi. Naomba nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Japokuwa kuna misukosuko na changamoto nyingi, lakini wameendelea kuwa wamoja na kufanya kazi bila kusita. Nawashauri wakaze kamba, wasiyumbishwe, hii ni vita na bila kuwa wamoja ni vigumu kushinda vita hasa ya ujangili.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa mikakati na juhudi zake katika kuutangaza utalii nchini na duniani kote kupitia maonesho mbalimbali na vyombo vya habari, hata Balozi zetu, lakini naomba kutoa ushauri ufuatao:-

Kwanza, naomba ni-*declare interest* kwamba mimi ni msanii wa muziki wa Injili na nimekuwa mtetezi na msimamizi wa shughuli za sanaa ndani ya Bunge na nje ya Bunge. Hivyo, naifahamu Sekta ya Utamaduni/Sanaa. Naiomba Wizara ijitahidi sana kutumia wasanii wetu wa ndani, kwani wana nafasi kubwa sana katika kuutangaza Utalii wa Tanzania ndani ya nchi na nje ya nchi. Suala kubwa ni kupewa mwongozo na nafasi tu, pia kuwezesha.

Mheshimiwa Spika, mfano, nchi ya Kenya, inatumia msanii mkubwa wa muziki hapa nchini anayejulikana kama *Diamond*. Pia Miriam Odemba anavaa nguo za wabunifu huko Ulaya na kuzitangaza. Pia Milen Magesa yuko Afrika Kusini na Amerika, kote huko wanatumia kutangaza biashara za watu. Je, Wizara haioni kuwa kuna kila sababu ya kufanya hivyo? Mfano, hata kutoa fursa ya wanamuziki maarufu bila kujali anaimba *Gospel* au *Bongo Flava*. Wote waende maeneo husika watengeneze wimbo wa mwaka na utakaoambatana na video inayoonesha uzuri na vivutio vya nchi ili kurusha hewani na majukwaani ndani ya nchi na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, utalii wa kitamaduni (*Cultural Tourism*), sina hakika na kipengele hiki kama kinafanyiwa kazi kweli kwani hata Waziri wakati anawasilisha aliruka kipengele hiki hakukisoma, hivyo kinaonesha ni jinsi gani kisivyo na umuhimu kwa Wizara. Naomba kufahamu kitengo hiki kinafanyaje kazi. Pia nashauri, kama kweli Wizara iko makini katika kudumisha utalii wa kitamaduni, ni vema wakaimarisha vitengo vyao kwenye kila Mkoa kwani kule ndio kwenye tamaduni nyingi na za kila aina na ni za kuvutia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya mwaka 2014/2015. Vile vile nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalam wake kwa kuandaa bajeti nzuri, kwani imeandaliwa kwa umakini mkubwa ili kukidhi mahitaji ya nchi katika sekta ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia katika Sekta ya Utalii, katika Tanzania historia ya uhifadhi wanyamapori inarudi nyuma hadi mwaka 1891 wakati sheria za kudhibiti uwindaji zilipoanzishwa na utawala wa Wajerumani. Sheria hizi zilidhibiti uvunaji wa wanyama; mbinu za uwindaji; biashara ya wanyamapori ambapo baadhi ya aina ya wanyama waliokuwa hatarini kutoweka wakiwa wamelindwa kabisa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Hifadhi za kwanza za wanyamapori, zilianzishwa na Wajerumani mnamo mwaka 1905 katika eneo ambalo sasa linajulikana kama Pori la Akiba la Selous. Maeneo ya hifadhi wanyamapori yalichaguliwa kutokana na kuwepo kwa wanyama wakubwa na wala si kutokana na sababu za makundi yao anuwai ya kibiolojia.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 1921 Serikali ya Uingereza ikaanzisha Idara ya Wanyamapori, ambao ilifuatiwa kutangazwa na Serikali kwa Pori la Akiba la kwanza ambalo lilijulikana kama Pori la Akiba la Selous, mwaka 1922. Shughuli za idara ya Wanyamapori zilikuwa ni pamoja na kusimamia mapori ya Akiba na kutekeleza kanuni za uwindaji na kuhakikisha kwamba watu na mazao yao hawaingiliwi au kuvamiwa na wanyama.

Mheshimiwa Spika, baadaye hifadhi nyingine mbili zilianzishwa. Hifadhi iliyokuwa Bonde Kuu Funge la Ngorongoro, iliyoanzishwa mwaka 1928; Pori la Akiba la Serengeti, lililoanzishwa mwaka 1928. Wanyamapori wa Tanzania ni urithi wa asili wa pekee na rasilimali yenye umuhimu mkubwa Kitaifa na Kimataifa. Umuhimu wake umejikita katika thamani ya kibiolojia ya spishi zenyewe na mazingira ya asili yaliyopo Tanzania, thamani yake ya kiuchumi na uweza wake katika kuchangia kwenye maendeleo endelevu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, uhifadhi wa wanyamapori na maeneo yote yenye mapori huhitaji maarifa ya kitaalam, wafanyakazi waliopata mafunzo maalum na fedha na hivyo tunaomba mataifa mengine yashirikiane nasi katika kazi hii muhimu ambayo kufanikiwa au kutofanikiwa kwake hakuathiri tu Bara la Afrika bali ulimwengu mzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina *spektra* anuwai za wanyama na mimea, ikiwa ni pamoja na spishi ndogo na spishi kuu ambazo hupatikana kwa nadra sana. Uanuwai na kiwango cha upatikanaji wa spishi adimu sana katika Tanzania unajitokeza wazi kwa upande wa *primata* (spishi 20 na nne (4) ambazo ni adimu sana), jamii ya paa (spishi 34 na mbili (2) ambazo ni adimu sana), samaki (kukiwa na spishi nyingi adimu katika Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa na katika maziwa mengine madogo na mito), *reptilia* (wanyama wataga mayai, spishi 290 na spishi 75 kati yake zikiwa adimu sana), amfibia (wanyama waishio majini na nchi kavu), spishi 40 adimu sana; wanyama wasio na uti wa mgongo na mimea (kwenye spishi 11,000 kukiwemo spishi zilizo adimu sana).

Mheshimiwa Spika, kuna uwezekano kwamba kuna spishi nyingine katika Tanzania ambazo bado hazijulikani katika sayansi na zinazongoja kugunduliwa. Mbali na uanuwai huo na kuwepo kwa kiwango kikubwa cha spishi adimu, Tanzania ina idadi muhimu ya spishi ambazo zimo hatarini kutoweka, lakini ambazo zimeenea sana Afrika kote. Spishi hizo ni pamoja na mbwamwitu, faru weusi, mamba wembamba wenye kunguruma, ngedere, ambao maisha yao siku zote yamo hatarini; duma na tembo wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, aidha, Tanzania pia ina idadi kubwa ya nyumbu, pundamilia, twiga, nyati wa Cape na spishi za jamii ya paa, ambao nao halikadhalika ni muhimu katika muktadha wa Kimataifa. Kulingana na aina tofauti tulizobarikiwa na Mungu kuwa nazo kama Taifa, hatuna budi kuandaa mikakati mizuri ili hazina hii iweze kuwa sehemu kubwa ya kuliingizia Taifa letu pato la kila mwaka, kwa kuandaa mipango mizuri ya kuitangaza sekta hii ya utalii duniani kote.

Mheshimiwa Spika, kuna mifano mingi sana ambayo baadhi ya nchi wamekuwa wakitumia rasilimali hii kujiinua kiuchumi na kupata faida kubwa kama nchi. Tena ukizingatia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

baadhi ya hizo nchi wana vivutio vichache sana tofauti na hapa kwetu Tanzania. Hivyo basi, naiomba Serikali kutilia mkazo katika jambo hilo kwa kufanya mabadiliko makubwa katika utalii.

Mheshimiwa Spika, janga zima la wanyamapori ambao ni adimu wako katika hatari ya kupotea bado inaendelea, wanyama wetu wamekuwa wakiuliwa kila siku na hivyo kutishia kabisa uwepo wao kwa vizazi vijavyo. *Operation Tokomeza* ilianzishwa makusudi kama zilivyoanzishwa operesheni nyingine ili kukabiliana na majangili hao, lakini kutokana na kasoro zilizojitokeza operesheni hiyo ikasitishwa. Hivyo basi, kusitishwa kwake kumewapa mwanya mkubwa majangili hao kuendelea kuwaua wanyama wetu bila woga wowote.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kufikiri kwa mapana juu ya kuwatunza na kuwahifadhi wanyama hawa kwa kuweka mikakati ya kukabiliana na majangili hawa na iondokane kabisa na dhana iliyozoeleka kuwa mpaka itokee janga ndio kuundwe chombo maalum cha kukabiliana na janga hilo kama ilivyokuwa kwa operesheni tokomeza. Serikali ijiwekee utaratibu wa kawaida wa kuwalinda wanyama hawa na kuwasaka wahusika ili wafikishwe katika vyombo vya sheria na kuchukuliwa hatua kali ili iwe fundisho kwa maharamia wengine.

Mheshimiwa Spika, kuna maswali wananchi wanajuliza, hivi majangili hawa wamekuwa na nguvu kiasi gani kuizidi Serikali kiasi kwamba wanashindwa hata kukamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria? Haya yanazungumzwa kwa kuwa bado tembo wanauawa kila kukicha na majangili.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo yanayoikabili sekta nzima ya wanyamapori. Sekta ya wanyamapori haijaweza kuendelezwa kufikia uweza wake kikamilifu kutokana na matatizo yafuatayo:-

Kutokuwepo na Sera ya Wanyamapori iliyo wazi, kushindwa kwa uhifadhi wanyamapori kushindana kikamilifu na namna nyingine za matumizi ya ardhi, hasa katika jamii za vijijini, kutokuwepo na mwamko juu ya uhifadhi wa wanyamapori miongoni mwa wapangaji mipango na maafisa wenye mamlaka na hivyo basi, suala la ardhi na wanyamapori kupewa uzito kidogo sana wakati wa upangaji mipango, kupotea au kutoweka kwa makazi ya wanyamapori kutokana na makazi ya watu, kilimo, malisho ya mifugo, uchimbaji migodi na ukataji miti; mambo ambayo husababishwa na kuongezeka kwa idadi ya watu, kuongezeka kwa ujangili kwa kasi kubwa na biashara isiyo halali.

Mheshimiwa Spika, pia kutotosheleza kwa mahitaji ya kifedha na kuiwezesha Serikali kutoa madaraka ya usimamizi wa wanyamapori kwa watu wa vijijini nchini kote, mfumo uliopo wa umiliki wa Serikali juu ya wanyamapori huzuia uwekaji na uendelezaji wa tasnia ya wanyamapori wa sekta binafsi, kutokuwepo kwa haki toshelevu juu ya matumizi ya wanyamapori, hasa kwa jamii za vijijini, kutokuwepo na uwezo wa kutosha wa kuwadhhibiti wanyama wakali na waharibifu, utengewaji kidogo wa fungu la bajeti kwa ajili ya hifadhi na uendelezaji wa Sekta ya Wanyamapori, malipo kidogo ya wafanyakazi ambayo husababisha kushuka kwa *raghba* katika kazi na mmomonyoko wa maadili ya kikazi, upungufu wa watendaji wa kuendesha shughuli za kuhifadhi wanyamapori. Katika kutambua umuhimu wa kuhifadhi, naiomba Serikali ichukue hatua madhubuti ili kuweza kukabiliana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie suala zima la uharibifu wa mazingira nikiwa na maana ukataji wa miti katika misitu yetu. Misitu na mapori ni miongoni mwa maliasili muhimu sana ambazo nchi imejaliwa kuwa nazo. Nchi ina maeneo makubwa sana ya kufuga nyuki, yenye uwezo wa kuzalisha kiasi cha tani 138,000 zinazokadiriwa kuwa katika eneo la hekta milioni 33.5 au kiasi cha asilimia 38 ya jumla ya eneo la ardhi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya eneo hilo, hekta milioni 13.5 zimetangazwa katika gazeti la Serikali kuwa ni Misitu ya Hifadhi ya Taifa, ambapo hekta milioni 1.6 zinasimamiwa kama misitu ya vyanzo vya maji na hekta 90,000; hekta 150,000 na hekta 120,000 zinasimamiwa na Serikali, viwanda binafsi na maeneo ya mapori ya viwango vidogo na mashamba ya misitu ya ukubwa wa kati yanayomilikiwa na wamiliki wadogo wadogo kwa mfuatano huo.

Mheshimiwa Spika, nyingine zinasimamiwa kama misitu ya hifadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, hivyo basi, utapata kuona ni kiasi gani nchi yetu ilivyojaliwa kuwa na utajiri wa misitu, lakini takwimu zinaonesha asilimia 90 ya matumizi ya nishati nchini inapatikana kutoka kwenye kuni na mkaa ambako mkaa hutumika mijini kwa mfano kama Miji ya Dar es Salaam na kuni hutumika vijijini.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo ikiachwa na kuendelea, Taifa litaingia katika janga kubwa la janga kama tuonavyo katika baadhi ya nchi nyingine ambazo hivi sasa wana matatizo makubwa katika upatikanaji wa mvua na hivyo kusababisha mabadiliko makubwa sana ya tabia nchi. Uvunaji huu holela wa misitu unaofanywa na wananchi ni hatari kama nilivyokwishasema hapo awali, hivyo naishauri Serikali pale inapokamata magogo ama mbao ambazo zimevunwa bila kibali basi kila Halmashauri au Mkoa waweze kutengeneza madawati na kuyagawa katika shule zetu ambazo zimekuwa na uhaba mkubwa sana wa madawati na kupelekea watoto wetu kukaa chini.

Mheshimiwa Spika, suala zima la ufugaji wa nyuki na kupata asali. Hapa nataka kuzungumzia ni jinsi gani Serikali inaweza kuwahamasisha wananchi wajajiri katika sekta hii. Ufugaji wa nyuki hauhitaji mtu wa kuwachunga kwa ajili ya malisho au maji, hawana shida ya kumwona daktari kwa ajili ya matibabu, hata mlinzi hawana haja naye, wenyewe ni hatari tupu kwa adui yeyote atakayesogea. Gharama ya kuwafuga haifikii ya ng'ombe, mbuzi, kondoo au kuku.

Mheshimiwa Spika, wanyama kama hao niliowataja hapo juu wanahitaji fedha za kununua chakula, maji na dawa ili kuhakikisha wanakuwa na afya bora, mbali na kutokuwa na gharama hizo, lakini nyuki wamekuwa wakiwapatia watu mbalimbali wanaofuga nyuki na kuvuna asali kitita cha zaidi ya shilingi milioni sita kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, tofauti na makundi ya ng'ombe, kondoo na mbuzi ambao kwa wale wafugaji wa kienyeji, mchungaji hana budi kuambatana nao kwa umbali mrefu kwa ajili ya kutafuta malisho. Nyuki wamekuwa wakizunguka umbali wa zaidi ya kilomita 1,000 kwa ajili ya kutafuta chavua wanayotumia kutengeneza asali. Asali inatajwa kama chakula kitamu zaidi kuliko mazao mengine yatokanayo na mifugo kama nyama, maziwa, mayai na kadhalika. Mbali na utamu kwa upande wa kula, lakini pia asali inatumika kutibu magonjwa mbalimbali baada ya kuchanganywa na vitu vingine.

Mheshimiwa Spika, utamu huo na matumizi hayo ndivyo vinavyowapa baadhi ya watu wachache kujikita katika biashara hiyo katika maeneo mbalimbali hapa nchini na kuwafanya wakusanye fedha za kutosha kutokana na mizinga kadhaa wanayoitumia kuzalishia asali.

Mheshimiwa Spika, taarifa za Baraza la Asali Tanzania linasema kiasi cha asali kinachozalishwa bado ni kidogo licha ya mahitaji yake kuwa makubwa. Jumla ya tani 9,380 zimekuwa zikizalishwa kila mwaka, kiasi hiki ni sawa na asilimia saba (7) tu ya uzalishaji wa asali nchini. Kwa kweli naweza kusema tunazalisha kidogo sana. Kwa upande wa nta tunazalisha tani 625.3 ambazo ziliingiza Shilingi 2.8 bilioni kwa mwaka wakati asali iliingiza Shilingi 14 bilioni, bado ni kiwango kidogo. Tunaomba Serikali kuhamasisha ili watu wajitokeze zaidi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, soko la asali ya Tanzania lipo Falme za Kiarabu (UAE) Oman na Iran, lakini kwa hapa Afrika asali yetu inauzwa zaidi Kenya, Uganda na Rwanda. Kwa kuonesha jinsi sekta hiyo inavyopiga vita umaskini nchini, hivi sasa sekta hiyo imeajiri watu milioni mbili nchini kote. Idadi hii inahusisha warinaji, wauzaji, watengeneza vifungashio, watengeneza mizinga na vifaa vingine vya urinaji wa asali. Asali nyingi nchini inazalishwa katika Mikoa ya Tabora, Dodoma, Kigoma na Singida. Mikoa mingine iliyopo katika uzalishaji ni Iringa, Kilimanjaro, Arusha na Tanga.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa wafugaji kufuata kanuni na taratibu za ufugaji nyuki zilizowekwa na Serikali, lakini pia wajiunge na Baraza la Asali kwa ajili ya kupata maelekezo zaidi. Tukiangalia faida za asali katika tiba, asali ina manufaa kwa watu wenye kikohozi, lakini pia ni nzuri kwa mtu aliyepungua na moto kwa kupaka kwenye majeraha yake. Mfano, mchanganyiko wa asali na mdalasini, unatibu ukungu wa miguu (*fungus*) kwa kupaka sehemu iliyoathirika.

Mheshimiwa Spika, asali haiharibiki na kwamba inapokaa muda mrefu inaendelea kuwa bora zaidi. Hii ina maana unaweza kukaa nayo kwa zaidi ya miaka 30 bila kuharibika endapo itahifadhiwa sehemu nzuri. Ikikaa kwa muda wote huo, inabadilika rangi tu na kuwa nyeusi, ndiyo kwa sasa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFD), hawakulazimishi kuweka tarehe ya mwisho ya matumizi ya asali.

Mheshimiwa Spika, hivyo, naomba Serikali kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi kuhusu ufugaji nyuki kwani pia ni ajira ambayo itamsaidia mwananchi kujikimu na maisha na kunyanyua uchumi wake na Taifa kwa kuuza asali ndani na nje ya nchi. Nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa mdau wa kwanza kuwahamasisha wananchi kufuga nyuki kwani yeye mwenyewe amekuwa akifanya hivyo na kupata faida.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kuzungumzia suala zima la ugawaji wa vitalu vya uwindaji, naomba Serikali kupitia Wizara kusimamia vizuri vibali hivyo ili kuepusha ubadhifu wowote unaoweza kutokea kwa watumishi wasiokuwa waaminifu, kwani kuna mifano mingi ya matukio kama hayo yameshatokea. Hivyo, ni vizuri kujifunzia kupitia makosa yaliyokwishawahi kutokea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BENEDICT N. OLE NANGORO: Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wa Wizara kwa hotuba ya Bajeti nzuri.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maliasili ndiyo msingi muhimu kwa uzalishaji nchini sasa na kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, misitu, wanyamapori, malikale na Utalii zisimamiwe kwa namna endelevu.

Mheshimiwa Spika, uhifadhi uwe shirikishi na utazamwe kwa mapana yake, na *ecosystems* zitunzwe kwa umuhimu wake. *Wildlife corridors* - (shoroba) ya Mashariki na Magharibi zifunguliwe kama maeneo maalum ya uwekezaji. Wanyama kutoka Serengeti waweze kupitia Shinyanga, Tabora/Singida – Katavi a Ruaha – Seleous. Aidha, wanyama kutoka Serengeti kupitia Engaruka Manyara, Tarangire, Makami (Kiteto) kupitia Mwitangos, Suledo, Mikumi hadi Seleous ni *corridors* hizo wafidiwe. Huu mkakati wa muda mrefu na *programme* yake iandaliwe na kupatiwa fedha ya kutosha ili kuwa na maliasili na utalii endelevu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba karibu asilimia 30 ya ardhi ya Tanzania imewekwa chini ya uhifadhi wa aina moja ama nyingine, mkazo uwe siyo kiasi tu (*nor only quantity*), bali pia ubora (*quality*).

Mheshimiwa Spika, uwindaji wa kujikimu kwa makabila ya Hadzabe na Akiye (Ndorobo) uruhusiwe, kwani *livelihoods* zao daima imetegemea uwindaji, ulimaji asili na ukusanyaji matunda. Uwindaji wao wa kujikimu siyo fishio kwa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, *program* ya ujirani mwema uliobuniwa na TANAPA uboreshwe na kupatiwa fedha za kutosha na itumike kujenga mahusiano kati ya hifadhi na vijiji/jamii jirani.

Mheshimiwa Spika, jamii zenye tamaduni na desturi ya ki-uhifadhi zitambuliwe, ziungwe mkono na jitihada zao ziungwe mkono. Jitihada za jamii za Wilaya ya Kiteto katika kuhifadhi msitu wa Suledo (vijiji 11), (Endema – Makami WMA), (vijiji 5) na hifadhi ya jamii Mwitangos (vijiji 7) ziungwe mkono kwa hali na mali.

Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba Mkungunero ni mpango uliobuniwa Kondo na haupaswi kuwa bugudha kwa wenyeji wa Simanjiro na Kiteto. Wizara imalize mgogoro huu.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Utalii Tanzania iwezeshe kuajiri timu yenye taaluma, uzoefu na weledi katika biashara ya Utalii.

Mheshimiwa Spika, dhana nzima ya Uhifadhi itazamwe upya ili kuona jinsi ya kuhuisha *concept* hii. Ni wakati muafaka sasa kutathmini uhifadhi wa kutotumia rasilimali zilizo ndani ya *park* na kuona kama iendelee hivyo hivyo, ama *elements* za RAMSAR *Concept* ya matumizi ya busara (*wise use*) ziingizwe katika dhana nzima ya uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, maadam wanyama wengi wanakaa, kulisha na kunywa maji katika ardhi ya vijiji hasa Simanjiro na Ngorongoro, wakati umefika sasa kupitia sheria ili maji yanapoisha na majani katika ardhi ya vijiji na wanyamapori kurudi kwenye hifadhi, basi kuwepo na uwezekano wa mifugo ya maeneo hayo pia kuruhusiwe kuwa na *limited access and use* ya mifugo ya maji na majani Tarangire na Serengeti.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ninachangia Bajeti ya Wizara hii ambayo ni moja kati ya Wizara nyeti na mtambuka hasa ukizingatia mchango mkubwa unaopatikana katika pato la Taifa kupitia Utalii, Uwindaji, mambo ya kale na Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa mwongozo unaoeleweka kuhusu michango inayotolewa na TANAPA; taarifa zinaonyesha kwamba kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2010/2013 TANAPA imeweza kulipa Shilingi bilioni 10.4 kwa Serikali, Mashirika ya Umma na Taasisi mbalimbali ambapo zinazolipwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Utaratibu wa sasa ni makubaliano tu na Msajili wa Hazina juu ya kiasi cha kulipa. Kutokana na kutokuwepo kwa mwongozo unaoeleweka katika kuchangia maeneo hayo, ni dhahiri juhudi zinazofanywa na TANAPA kujiendeleza zinazorota.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili ni hatua gani za makusudi zitachukuliwa kulinda rasilimali fedha za TANAPA.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa TANAPA ambayo shughuli zake kuu ni kulinda Maliasili, vifaa vya hifadhi na watalii pamoja na kulinda mazingira, hata hivyo katika kikao cha Bodi ya wadhamini cha 177 Bodi ilitaarifiwa kuundwa kwa shirika jipya la ndege na Bodi iliridhia mapendekezo hayo ambayo yaliletwa na Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi ambapo tarehe

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

20/11/2012 kupitia barua CGA 376/517/01/C/16 kutoka Wizara ya Utalii na Maliasili ilimtaka Mkurugenzi Mkuu wa TANAPA kupeleka maamuzi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maagizo ambayo yanatolewa na Serikali, namwomba Waziri atupe maelezo juu ya mpango huo wa Serikali ambao kwa kweli unaweza kuzorotesha kutekelezwa kwa majukumu ya TANAPA.

Mheshimiwa Spika, hifadhi hii ya Tarangire ni moja kati ya hifadhi ambazo zinafanya vizuri. Taarifa tulizonazo ni kwamba hifadhi hii inakusanya zaidi ya Shilingi bilioni nane kwa mwaka. Namwomba Waziri atueleze ni kwa nini Halmashauri ya Babati ambayo hifadhi hiyo ipo hainufaiki na mapato hayo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu katika usimamizi wa Nyara za Taifa kwa mujibu wa taarifa ya CAG ulibaini kutokuwepo kwa Rejista inayoonyesha orodha ya mali zote zilizoko katika chumba cha kuhifadhi pembe za ndovu (*Ivory room*) iliyoko Dar es Salaam. Hii inaonyesha ni udhaifu mkubwa. Ni vyema Waziri atoe maelezo ni kwa nini hakuna kumbukumbu ya nyara ambazo zinahifadhiwa katika *Ivory room* na hata zile ambazo zinakamatwa na kuhifadhiwa mikononi. (Katika kituo cha Polisi Kilwa meno makubwa ya tembo 108 yalitoweka katika kituo hicho). Je hatua gani iliyochukuliwa na Wizara kwa uzembe huo?

MHE. CECILIA D. PARESO: Mheshimiwa Spika, kuhusu malalamiko ya Ngorongoro Wilaya ya Karatu inapakana na hifadhi ya Ngorongoro, hata mahitaji yote ya Ngorongoro ikiwemo watalii wenyewe wanapata mahitaji Karatu Mjini. Pamoja na Karatu kupakana na kutegemea na Utalii huo, hakuna mapato ya uhakika yanayotolewa kwa Wilaya ya Karatu. Misaada inayotolewa inakuwa kama hisani tu. Je, ni mkakati gani wa kuweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha Wilaya ya Karatu inapata mapato angalau ya uhakika kila mwaka wa fedha wa Serikali?

Mheshimiwa Spika, ni lini Wizara itateua Bodi ya Mamlaka ya Ngorongoro ili majukumu ya kibodi yaweze kutekelezwa?.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuna udhaifu katika kukusanya mapato yatokanayo na Utalii wa picha, takribani Shilingi bilioni 2.7 hupotea kutokana na udhaifu wa kutokuwa na utaratibu sahihi katika kusimamia utalii wa picha. Makampuni takribani 36 yalibainika kutolipa bili kwa ajili ya utalii wa picha. Hata hivyo, malipo hayo yalifanyika wakati wateja walipomaliza ziara zao (kwa waliolipa). Je, nini mkakati wa Wizara kuhakikisha mapato hayo ya utalii wa picha hayapotei?.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Buger Wilayani Karatu kuna malalamiko ya wananchi kunyanyaswa, kuuawa, kupigwa, mifugo ya wananchi kukamatwa na mengineyo. Kata hii imepakana na hifadhi ya Ziwa Manyara. Manyanyaso hayo hufanywa na Askari Wanyamapori wanaofanya doria katika msitu wa Marang. Suala la kuwa na mahusiano mazuri kati ya wananchi na Askari ni muhimu ili nao pia wahusike katika kulinda wanyama na misitu husika. Je, nini mpango/mkakati wa Wizara chini ya TANAPA kukutana na wananchi hao ili kujenga na kurejesha mahusiano mazuri kati ya pande hizo mbili?.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalakimo mengi katika maeneo mengi ya nchi yetu juu ya mipaka ya hifadhi na makazi ya wananchi. Kila mara mara inapotekea migogoro hii, anayeathirika ni mwananchi kwa kiwango kikubwa. Naomba Wizara ieleze ni kwa namna gani itaondoa sintofahamu hii ya kutumia nguvu nyingi na mara nyingine za kudhalilisha wananchi kama sio binadamu. Mfano, ni mgogoro mkubwa ulitokea katika eneo la Mgori - Singida

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(Jimbo la Singida Kaskazini) ambapo wananchi walidaiwa kuvamia pori la hifadhi kwa shughuli zao za kilimo.

Mheshimiwa Spika, wananchi hawa waliteswa, walichomewa nyumba zao, waliharibiwa mazao yao, na kufanyiwa udhalilishaji mkubwa. Cha kushangaza, kulitokea majibizano yasiyo na tija kati ya DC na Mbunge wa Jimbo. Wananchi wale walinyanyasika kwa kukaa nje huku wakinyeshwewa na mvua kwa siku kadhaa. Je Serikali haioni kwamba hii ilitokea kwa kuchelewa kwake kuainisha mipaka halali kati ya hifadhi na makazi? Mfano mwingine, ni mgogoro ulitokea katika Kijiji kilichoko Manyoni ambapo wananchi walichomewa nyumba zao na mazao yao, na mpaka kupelekea kifo cha mtoto mmoja. Serikali iko wapi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu utoroshaji wa Nyara za Taifa ni aibu kwa Serikali kukaa kimya ilhali nyara za Taifa zikitoroshwa na wanyama kama tembo kuuawa na yenyewe kukaa kimya. Hakuna tija kwa Serikali kusema kwamba haiwafahamu majangili wanaojihusisha na biashara hii haramu hasa ya meno ya tembo, lakini inawapa muda wa kuacha kufanya hivyo. Huu ni utendaji wa aina gani? Ni kwanini watu hawa hawatajwi ili wananchi wawajue na wawatangaze kwamba ni maadui wa Taifa letu? Kama kweli Serikali haiwalindi watu hawa na siyo miongoni mwao, basi iwataje na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu lango la Bologonja, siyo siri, habari za Serikali kufungua lango hilo la Bologonja zimezagaa na kwa kweli hazileti afya kwa Taifa letu. Naunga mkono hoja ya Kamati kwa Serikali kutoruhusu jambo hilo kutokea maana kwa kuruhusu huu mpango, siyo tu utadhoofisha biashara ya utalii nchini, bali itaiua kabisa ukizingatia kwamba sekta yenyewe haifanyi vizuri kama ilivyokusudiwa. Naomba kuwasilisha.

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Igalula Kata ya Miyenze na Kizengi ziliomba kumegewa maeneo ya hifadhi za Miyenze/Kizengi na Nyahua/Sikonge/Kizengi kwa ajili ya ufugaji. Mkuu wa Mkoa Fatma Mwasa aliwaahidi mwaka 2013 wananchi kupata kilometa tano za hifadhi ya Miyenze/Kizengi na Nyahua/Sikonge/Kizengi. Naomba maelezo ya kina, ni lini watapata maeneo hayo?

Mheshimiwa Spika, ufugaji nyuki wa kisasa wa wananchi wa Igalula itaongeza kipato cha Kata na Halmashauri ya Wilaya ya Uyui, tupate wataalam na mitaji ili ufugaji nyuki uwe na tija.

Mheshimiwa Spika, Miyenze, hifadhi ina tembo 277; makundi 15 ya Tembo. Tatizo ni maji. Tembo wanazurura kutafuta maji na hivyo kuharibu mazao. Muhimu ni kuchimba mabwawa. Tunaomba Wizara itusaidie kuchimba malambo na mabwawa, pia tufuge samaki, pia upande mmoja kilimo cha umwagiliaji na mifugo/binadamu wapate maji.

Mheshimiwa Spika, mpango wa matumizi bora ya ardhi uandaliwe ili tembo na wanyamapori wengine; mifugo kama ufugaji samaki mpango wawepo. Ni rasilmali muhimu kwetu Igalula, na wanafanya ufyekaji wa matawi (*Pruning*) asilia. Tunahitaji hawa tembo ili zianzishwe WMA katika vijiji vya Miyenze, Kizengi, Tura, Goweko, Nsololo na Igalula ili tuwatunze na kuwalinda tembo hawa na kutuletea mapato katika Jimbo la Igalula.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa na vitalu kila Kijiji, Kata zote 10, Igalula, ili miti asilia inayotoweka kama *mining*, mikola, mitundu, mivule ioteshwe na kuvunwa baadaye itakapokomaa kwa faida ya Jimbo, Wilaya, Mkoa na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mifumo ya hali ya hewa sasa ina mabadiliko ya tabianchi, hewa ukaa ni tatizo na linaongeza joto na mafuriko na ukame nchini. Tupande miti kwa wingi ili ifyonze hewa ukaa (CO_2) na tulipwe pesa na nchi zinazozalisha hewa ukaa kwa wingi na kufyonzwa na miti, mapori na mbuga zetu.

Ahsanteni Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri. *Big Up* sana.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, kwa miaka kadhaa nimekuwa nikidai maliasili zilizopo nje ya nchi hasa *Dinosaur* iliyopo Ujerumani miaka kadhaa. *UNESCO* wapo tayari kusaidia kifedha kurudisha mali zilizopo nje ya nchi. Azimio la *Pan African Parliament* ilisema hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Utalii wa *Culture Tourism* sasa hivi watalii wamechoka kuona mlima Kilimanjaro tu, sasa wanataka *Cultural Tourism*. Lindi kuna Utalii wa aina zote.

- Bahari ya Hindi – *white sand*;
- Milima, mabonde na mito;
- Wanyama pori la *Seleous* ;
- Uwindaji wa kitalii pori la *Seleous* Kilwa;
- Magofu ya Utalii Kilwa;
- Makaburi 40 ya Masharifu;
- Kuna *book* wanaosema na watu mto Nyange;
- Diving;
- Magofu makubwa makubwa; na
- Mpango mkubwa katika Afrika na mengi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Utalii mwingi upo Mkoa wa Lindi/njoo mwone.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Utalii ni Wizara muhimu ambapo Serikali inaitegemea katika kunuia uchumi wa nchi ya Tanzania. Idara ya Wanyamapori pekee inachangia asilimia 20 katika pato la Taifa (*CDP*). Uwindaji wa Kitalii uliilingizia Taifa Shilingi bilioni 91 katika mwaka 2009 - 2012.

Mheshimiwa Spika, ingawa Taifa linapata fedha hizo katika Idara hiyo, iko changamoto kubwa ya wizi wa wanyama na mauaji ya wanyama wengine mfano tembo ili kupata pembe. Mfano, Novemba, 2010, wanyama kiasi cha 120 walio hai na ndege hai 16 waliouzwa bila kibali cha Serikali.

Mheshimiwa Spika, 2008 - 2013 matukio 268 ya upatikanaji pembe yalifanyika, hii ikimaanisha wanyama hao waliuawa. Katika ukaguzi wa Mhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, waligundua udhaifu mwingi uliopo katika Wizara ya Maliasili, mojawapo ikiwa Wizara kutokuwahi kufanya uchambuzi na kutambua maeneo katika hifadhi zetu za Taifa ambayo yana uwezekano mkubwa wa wanyama kufanyiwa uharamia (*risk of poaching*). Tembo waliouawa kwa ajili ya pembe ndiyo tahadhari peke yake inayoonyesha utata wa eneo husika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, tembo 721 waliouawa katika maeneo matano mwaka 2009 - 2012, lakini inawezekana waliuawa zaidi ya idadi hiyo kwa sababu Wizara imekuwa na upungufu wa kutokuwa na takwimu sahihi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekuwa haifanyi *patrols* za kutosha hasa kipindi cha mvua. Ufuatiliaji umekuwa mdogo, asilimia 37 katika mwaka 2010/2011 na asilimia 47 katika mwaka 2011/2012 badala ya lengo lilowekwa la asilimia 60.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009 - 2011 wanyama 366 waliwindwa bila kufuata gawio la *quarter* Kampuni nyingi za uwindaji hazilipi mchango wa mwaka USD 5,000 kwa wakati, na Wizara haiweki takwimu za uhakiki kuhusu hili. Kampuni 36 hazikulipa Ankara za upigaji picha wa kitalii, na hivyo Serikali kukosa fedha USD 1.7 milioni (Shilingi bilioni 2.7) Novemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inasema, Wizara haifuatilia Sheria za Uwindaji kwa umakini na hata uwindaji wenyewe haifuatiliwi.

Mheshimiwa Spika, pembe zinazokamatwa zinazidi kuongezeka kutoka mwaka 2008 (kg 264) mpaka kg 8,254.8 kwa mwaka 2013. Idadi ya tembo waliouawa imezidi kuongezeka mwaka 2009 (tembo 53), mwaka 2012 (tembo 187). Nashauri Operesheni Tokemeza ianze upya.

Mheshimiwa Spika, mapato ya Wizara ya Utalii yameendelea kupungua tangu mwaka 2009/2010 Shilingi bilioni 30.5 mwaka 2010/2011, Shilingi bilioni 34.2 na 2011/2012 Shilingi bilioni 28.1.

Mheshimiwa Spika, zipo habari nyingi zinaandikwa katika magazeti kuhusu kukodisha mbuga za Taifa (mfano Katavi). Tulishuhudia *Netgroup* iliyofanya TANESCO. Watanzania wana imani na TANAPA, Taasisi hii ipewe vifaa, itafanya vizuri. Wizara iweke mipango mizuri ya kufuatilia uwindaji, *patrols*, ukusanyaji mapato, na kuweka wataalam wa kuweka takwimu za uhakika.

Mheshimiwa Spika, wako wataalam wa wanyamapori walio na uaminifu ambao wanaweza kusimamia Idara ya Wanyamapori. Serikali itoe ajira kwa Watanzania wenye weledi na uadilifu ambao wanaweza kusimamia Idara tofauti za maliasili.

Mheshimiwa Spika, ziko taarifa za Viongozi wa Wizara kuongeza kipindi cha uwindaji badala ya miaka mitano iwe miaka 15 (tofauti na Kamati ya Bunge ilivyoshauri), Wizara kuongeza kipindi cha uwindaji badala ya miezi sita iwe miezi tisa. Ziko taarifa za kufungua mpaka wa Bolongoja ambapo watalii kutoka Kenya wataingia nchini waone wanyama Serengeti na kuondoka.

Mheshimiwa Spika, yapo mengi yaliyoandikwa kuhusu Wizara hii ambayo kama yalifanyika, yatakuwa hayana tija kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iangalie mapendekezo ya Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali waondoe udhaifu na mapungufu yaliyopo ili kuweza kupata pato zuri zaidi katika utalii. Taratibu za kuachisha wafanyakazi kazi zifuatwe na haki itendeke ili kutokuleta migomo baridi kwa wafanyakazi ambayo itakoshesha utendaji mzuri wa kazi zao katika idara zote.

Mheshimiwa Spika, mapato yatokanayo na utalii na Mlima Kilimanjaro ni Shilingi bilioni 80 kwa mwaka ambayo ni asilimia 38 ya mapato.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa nne umeongelea kuhusu TANAPA, mapato haya yanapatikana kwa sababu kuna Wilaya zimezunguka huo mlima Siha, Hai, Moshi Vijijini, Moshi Mjini na Rombo. Wilaya hizo hazipati hata senti mojakwa ajili ya utunzaji wa mazingira ya mlima huo. Tunasikia Mtwara/Lindi wanajengewa kiwanda cha cement, watoto wao wanasomeshwa bure sekondari ya Mahongo. Hii ni kwa sababu ya *investment* ya *gas* katika maeneo yao. Je, mlima unatoa shilingi bilioni 80 kila mwaka kama pato la Taifa kulikoni Wilaya zetu zisipatiwe walau asilimia kidogo au kujengewa viwanda kukuza ajira za Mkoa wa Kilimanjaro?

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja kama hoja yangu hii itapatiwa majibu.

MHE. LEDIANA M. MNGO'NGO: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Nawapongeza Watendaji wote wa Wizara hii pamoja na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua kwamba Mkoa wa Iringa una vivutio vingi ikiwemo Mbuga ya Ruaha, Udzungwa, Makumbusho ya Kalenga na *Ismila Old Stone Age*.

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu mikakati mahususi iliyowekwa kuhakikisha kwamba Mkoa huu unanufaika na fursa hizi zilizoko ili kusaidia wananchi kuondokana na umasikini. Wananchi wameandaliwaje ili kufanya shughuli za utalii ikiwemo kuhifadhi na kuwinda wanyamapori hasa katika *Ruaha National Park*?

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu vijiji vya Wenda ambapo *Ismila Old Stone Age* ilipo na Kijiji cha Kalenga na Lugalo vimeandaliwaje ili kutumia fursa zilizopo vijijini mwao kwa utalii ikiwemo Utalii wa kiutamaduni?

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kuweka mikakati itakayoweza vijiji hivi kunufaika na fursa za Utalii zilizopo vijijini mwao.

Mheshimiwa Spika, ili watalii waweze kutembelea *National Park* ya Ruaha, ni lazima miundombinu iwe bora. Naomba Wizara ishirikiane na Wizara nyingine zinazohusika kuhakikisha kwamba barabara ya Iringa - Ruaha inajengwa kwa kiwango cha lami, pia kuimarisha kiwanja cha Ndege cha Nduli.

Mheshimiwa Spika, Utalii wa Fukwe unatakiwa kuangaliwa, na hizi ni pamoja na fukwe Ziwa Victoria. Je, ni lini Serikali itaanza kutangaza fukwe zetu na kuhamasisha utalii kama ilivyo Shelisheli, Mauritius, Syprus na kadhalika? Fukwe hizi ni pamoja na Busekela, Bufundi, Murangi, Kome Wilaya ya Butiama. Utalii pia unaweza kufanyika Iringa Mjini katika mto Ruaha.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kuhamasisha utumiaji wa majiko yanayotumia kuni na mkaa kidogo. Majiko haya ni pamoja na Vyuu/Taasisi, misitu inateketea kwa kukatwa ili kupata kuni na mkaa. Kwa kuhamasisha utumiaji wa majiko haya, tutasaidia kuhifadhi mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, utalii wa ndani ni muhimu, hivyo elimu na uhamasishaji uendelee kufanyika ili Watanzania waweze kutembelea mbuga zao. Tatizo kubwa ni gharama za malazi katika mbuga zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba ziazishwe klabu mashuleni na rafiki wa mazingira na utalii ili kujenga tabia ya watoto wetu kuhifadhi mazingira na kupenda utalii.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ichukue jukumu la kusomesha watoto wa familia ambazo wazazi wao wanauawa na wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri. Wizara imejitahidi sana kusimamia masuala ya uhifadhi katika maliasili zetu nyingi hasa misitu, wanyamapori na kadhalika hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara sasa ijielekeze katika kuifadhi milima yetu na misitu yake kwa umuhimu wake kama vyanzo vya maji iliyotokana na misitu minene iliyotanda katika milima hiyo. Mfano halisi ni safu za Milima Livingstone, Milima ya Udzungwa, Milima ya Uluguru Mkoani Morogoro. Kama tunavyofahamu, milima au safu za milima ya *Livingstone* kama ingehifadhiwa ingekuwa ni eneo muhimu sana katika *Eco-Tourism*.

Pamoja na umuhimu wa wanyamapori katika utalii, umefika wakati sasa *Eco-Tourism* nayo inaendelezwa. Milima *Livingstone* na Uluguru imeharibiwa sana kiasi cha kubadilisha kabisa sura yake na mvuto wake wa asili. Watu wameachiwa kukata misitu yote ya asili, watu wanachoma moto, wanalima ndani ya misitu kwenye miteremko mikali na hakuna hatua zozote zinazochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri Serikali ianze utaratibu wa kuwashirikisha wananchi wanaoishi katika maeneo hayo ili washiriki kikamilifu katika uhifadhi wa safu za milima hiyo na kusimamia utekelezaji wa sheria zinazohusu uhifadhi kama ilivyo katika ushirikishwaji Jamii (*Participatory Forest Management*) kwa wanyamapori. Serikali sasa ijitahidi kujielekeza katika kusimamia uhifadhi wa milima hii muhimu. Wizara hii izielekeze Halmashauri za Wilaya kuona hakuna wananchi wanaojenga karibu na mpaka wa misitu. Huko nyuma sheria ilikataza kabisa kujenga ndani ya kilometa saba kutoka kingo za milima lakini hivi sasa watu wamejenga ndani ya misitu na wahalifu wanaoiba mbao wanajificha huko bila kuhojiwa na mtu. Inapendekezwa kuwa sehemu ya maduhuli yanayopatikana kutokana na misitu hiyo, irudishwe kwa wananchi ambao ndio walenzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo machache, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aangalie ukurasa wa 177 kuhusu taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa hakuna Rejista katika chumba cha *Ivory room* na hata mikononi, na kwa taarifa yako ukienda kuangalia hivi sasa utaona kuna pembe feki na *orginal* nyingi zimeibiwa.

Mheshimiwa Spika, kuna *Reserve Forest* ya Ikomwa iliyotangazwa na Tangazo la Serikali No. (G.N) 32 mwaka 1958, naona tangazo hili limepitwa na wakati kwani wananchi wengi wako wanaishi ndani ya *reserve* hii tangu wakati wa kikoloni, iko haja ya kuangalia tena.

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mbuga ya Kitulo ni muhimu ikiwemo na mbuga ya Ruaha *National Park*, pamoja na umuhimu huo, bado wakazi wanaozunguka mbuga hizi hawana uelewa wa kutosha juu ya uhifadhi wa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, nashauri uhifadhi wa wanyamapori kwa shule za pembezoni mwa maeneo ya uhifadhi uwe unaelimishwa kwa wanafunzi wa shule zinazozunguka maeneo hayo na *Local Government Authorities*. Hivyo, naomba *Capacity Building* kwa wakazi wa maeneo ya Tarafa ya Idodi Pawaga jirani na Ruaha *National Parks* na support ya shule zinazozunguka

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Ruaha Nationa Parks. Naomba ujenzi imara katika Shule ya Sekondari Idodi ili wasiathiriwe na wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, kufuatia utendaji kazi mzuri waTANAPA na ushirikiano kati ya TANAPAna jamii, naomba kuleta maombi kwa niaba ya wakazi wa Makete Kitulo kupewa *support* ya mchango katika sekta ya elimu katika sekondari ya Kitulo. Mchango huo ni kwa ajili ya masuala ya upandaji miti na madawati ili kupata jamii yenye elimu inayozunguka *Kitulo National Park* na Idodi Sekondari iliyopo *Ruaha National Park* Iringa. Maombi haya yamezingatia uwepo wa *Corporate Department* na *Social Welfare*TANAPA.

Mheshimiwa Spika,masuala ya ufugaji nyuki ni masuala muhimu sana hususani kwa Wilaya ya Ludewa/Njombe/Makete na Wanging'ombe. Kwa niaba ya wananchi, naomba Wizara inipe mtaalam atoe elimu (*capacity building*) kuhusu ufugaji nyuki, upatikanaji wamizinga, nahitaji mizinga ya kutosha na mbegu za miti. Hivyo ningeeomba mtaalam wa kutoa semina kwa wadau wapatao 200 Mkoani Njombe juu ya masuala ya nyuki na asali. Masuala haya yatasaidia MKUKUTA kwa wakazi wa Njombe na MDG's.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Ludewa inao wataalam waliosomea masuala ya nyuki, je, Wilaya inaweza ikapata Mkuu wa Idara wa masuala ya nyuki (Bwana Nyuki)?

Mheshimiwa Spika, naomba semina ya *capacity building* kutoka Tanzania *Forest Fund* au Wizarani kwa wadau 100 wa Njombe kutoka Wilaya nne za Mkoa wa Njombe. Lengo ikiwa ni kuongeza elimu na kupunguza umaskini kwa shughuli za urinaji wa asali kwa wananchi.

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, naomba kufahamu kuhusu upotevu wa pembe za ndovu katika ghala la kuhifadhia pembe hizo. Zipo taarifa kuwa pembe nyingi zinazokamatwa zinatoka katika ghala la kuhifadhia pembe hizo. Ni hivi karibuni kuna pembe zilizokamatwa Mtwara, inasemekana zimetoka mahali zilipokuwa zimehifadhiwa na Serikali. Nataka kufahamu ukweli wa mambo haya na hatua zilizochukuliwa na Serikali. Pia Waziri atuambie ni kiasi gani cha pembe za ndovu zilizopotea ndani ya ghala la kuhifadhia?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri pamoja Watendaji wote,kwa kazi nzuri na hasa kwa kuonesha nia ya kulinda wanyama hasa tembo wanaoendelea kuuwawa kwa kasi katika siku za karibuni.

Mheshimiwa Spika, ushauri, elimu itolewe zaidi kwa watu waishio pembezoni mwa mbuga zetu ili washiriki kulinda wanyama wetu hasa kwa kujenga utamaduni wa kutoa taarifa.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Ileje, kuna nyani weupe, mbega, ambao hawapatikani maeneo mengine hapa nchini isipokuwa Ileje katika Milima ya Gwajondo na Msima kule Tarafa ya Bundali.

Mheshimiwa Spika, ninashauri Wizara ifanye juhudi za makusudi ili kuona haja ya kuendeleza hifadhi hii ili wanyama hawa wasipotee.

Mheshimiwa Spika, kuhusu misitu, katika Wilaya ya Ileje kuna mvua na pia ipo misitu ya asili ambayo ipo kwa muda mrefu sana. Ipo haja ya kuendeleza misitu hii kwa kutoa kipaumbele kwenye eneo hili la nchi ambalo lina hali ya hewa nzuri yenye mvua ya kutosha na milima ya wazi yenye rutuba nyingi kwa kutoa fedha ili kupanda miti mipya.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushuru wa TRA kwa faru wanaotolewa na wafadhili kama msaaada: Kwa kuwa Wananchi wamemsikia Msemaji wa Kamati ya Maliasili na Utalii akisema juu ya jambo hili ambalo haliingii akilini kuwa ni vipi mtu anayekusaidia anatozwa kodi kwakitu ambacho kitakuwa faida kwako.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri alitolee ufafanuzi wa kina jambo hili ili Taifa la Watanzania waelewe jambo hili.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii ni miongoni mwa Wizara inayoingiza mapato kwa Taifa. Hata hivyo, Wizara hii imekumbwa na kashfa za ujangili wa mara kwa mara unaopelekea Mawaziri kujuzulu mara kwa mara na hivyo kupelekea utendaji wa Wizara hii kudorora na kutofikia malengo.

Mheshimiwa Spika, mauaji ya Tembo na Faru yanayofanyika kila leo nchini yamepelekea kupunguza wanyama hao ambao nikivutio kikubwa cha watalii.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kwa nchi ya Tanzania ambayo imebarikiwa kuwa na mito, maziwa na bahari zenye fukwe ambazo ni kivutio kikubwa cha watalii ukiacha mbuga za wanyama pamoja na Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, nchi kama Malaysia, Dubai, Shelisheli, Singapore ni nchi ambazo zinajiendesha kwa kutumia utalii wa bahari, pamoja na bandari na fukwe walizonazo na mapato yao ni ya hali ya juu kuliko sisi ambao tumebarikiwa kuwa na mambo mengine ya utalii ya ziada.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa matatizo makubwa katika Wizara ya Maliasili na Utalii ni idadi ndogo ya wafanyakazi na mishahara midogo ambayo haikidhi mahitaji ya wafanyakazi hao. Lngine ni mazingira magumu ya kazi, barabara mbovu na uchache au uhaba wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kasoro ambazo nimezitaja, lakini kwa kiasi kikubwa inaelekea baadhi ya wakubwa wanachangia katika uporaji wa nyara za Serikali na kuendesha biashara hii haramu kinyume cha sheria. Tujiulize pembe za ndovu na meno ya ndovu yatafikaje Zanzibar kama wakubwa hawashiriki? Kuna hatua gani za kiuchunguzi zilizochukuliwana wangapi wamekamatwa na hatua gani zimechukuliwa dhidi yao?

Mheshimiwa Spika, kama Serikali haijakuwa tayari katika kuisimamia Wizara hii kimkakati na kuwashughulikia wafanyakazi ipasavyo kwa kuwapatia uwezo stahiki, basi uendelezaji wake utabaki pale pale na siku zote tutaomba Mawaziri waendeleo kujuzulu, jambo ambalo halileti tija.

Mheshimiwa Spika, Tanzania pamoja na Mlima Kilimanjaro, mapori yenye wanyamapori wenye kuvutia, mbuga za wanyama, miti, maziwa na bahari zilizojaliwa kuwa na fukwe zenye kuvutia, bado tumebakia kuwa ombaomba ambao tumeshindwa kuendesha bajeti ya nchi. Tunategemea nchi zile zile ambazo wao wako chini kiutalii kuliko nchi yetu. Bado tunaendesha bajeti kwa kutegemea wafadhili wakati miundombinu ya kiuchumi tunayo lakini tumeshindwa kuiendeleza. Tanzania siyo maskini lakini Watanzania wataendelea kuwa maskini kutokana na Serikali kutokuwa makini katika utendaji wake.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nitoe mawazo yangu katika mjadala huu muhimu wa Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba, ujangili wa wanyamapori katika nchi yetu umekuwa kubwa na umekuwa ukiongezeka kila siku. Pamoja na jitihada zinazoonekana kuchukuliwa kudhibiti hali ya ujangili hapa nchini, lakini juhudi hizo zinaonekana kutozaa matunda tarajiwa kwani hali ya kutoweka kwa wanyama wetu inazidi. Ninashauri Serikalikuongeza wafanyakazi na vifaa vya kisasa zaidi kukabiliana na hali ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, kama tujavyo, majangili wanafanya ukatili huu wakiwa na nyenzo na silaha nzito na za kisasa. Hivyo, ni jambo la lazima sasa kuelekeza bajeti toshelezi kwa Wizara hii hasa katika Idara ya Wanyamapori. Jambo hili likifanyika, kwa kiasi fulani tunaweza kupunguza uhalifu huo.

Mheshimiwa Spika, kwa muda sasa kumekuwa na tetesi kwamba, majangili wanaoendesha biashara hii haramu, wana udhamini mkubwa kutoka kwa wafanyabiashara wakubwa hapa nchini, pamoja na baadhi ya vigogo wenye nyadhifa Serikalini. Tamko lililowahi kutolewa na Waziri wa Maliasili mwenyewe limezidi kutiliwa mashaka na Wananchi wengi hasa pale Mheshimiwa Waziri aliposema anawafahamu vigogo wanaofadhili majangili hapa nchini. Je, ni kwa nini mpaka sasa Mheshimiwa Waziri ameshindwa kuwataja vigogo na wafanyabiashara hao huku akiwa tayari amekwishabainisha kwamba anawafahamu vigogo hao? Je, anaogopa au ametishiwa na nani kuwataja na kuwachukulia hatua za kisheria wahalifu hao wanaoitia madoa nchi yetu Duniani?

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aweke uzalendo na utaiifa mbele na kuondoa hofu huku akijua kwamba Tanzania ni muhimu kuliko vigogo hao anaowaogopa kuwataja au kuwachukulia hatua. Tunatambua uzalendo wa Mheshimiwa Waziri kwa jinsi anavyojali kazi zake na Taifa lake; hivyo, ni vizuri afunguke na kuweka wazi kila kitu.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, ujangili unaoendelea katika Hifadhi zetu na hasa tembo kuuawa unatisha. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ukurasa wa nne, kuna taarifa kwamba, jumla ya watuhumiwa 391 wamekamatwa kwa kuhusishwa na makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009. Kesi 123 zenye washtakiwa 164 zimeisha kwa watuhumiwa kulipa faini ya Shilingi 75,686,000.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba, majangili wanapokamatwa pamoja na kushtakiwa mahakamani, lakini pia wawekwe au picha zao ziwekwe kwenye vyombo vya habari ili wajulikane na hivyo iwe kama njia ya kuwazuia wasiendelee na ujangili baada ya kulipa faini.

Mheshimiwa Spika, fedha ya kutosha itengwe na itolewe kwa wakati ili kuimarisha doria katika maliasili zetu.

Mheshimiwa Spika, mambo ya kale au mali kale ni sehemu muhimu sna katika kutuletea mapato na hasa fedha za kigeni kwa upande wa utalii. Kwa bahati mbaya, malikale yetu haitangazwi ipasavyo katika vyombo vya habari vya ndani na hata vya nje.

Napendekeza majengo ya zamani yaliyojengwa maeneo ya pwani, Lindi, Bagamoyo, pia michoro ya kale, Mapango ya Amboni, ambayo ni vivutio vikubwa vya utalii, vitangazwe kwa bidii. Idara ya Habari na Mawasiliano ya Wizara hii ifanye kazi yake kwa uzalendo na kwa ubunifu ili kutangaza mali kale yetu katika Soko la Utalii Duniani.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naomba kuwasilisha.

MHE. BERNADETA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kukamilisha majukumu yao vizuri na kwa uandishi na uwasilishaji mzuri wa Hotuba.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Wizara inasimamia Sekta ambayo inaweza kuiondoa Tanzania katika umaskini.

Mheshimiwa Spika, leo hii Sekta hii inachangia ukuaji wa Pato la Taifa kwa asilimia 17. Hongera kwa hatua hiyo, lakini nina hakika mchango huu unaweza kuongezeka ukizingatia rasilimali na utajiri mkubwa wa fursa mbalimbali zilizo.

Mheshimiwa Spika, nasikitishwa na mahakama wanapochelewesha kutoa maamuzi au hukumu kwenye kesi nyingi zilizo mahakamani kuhusu ujangili, utoroshaji wa wanyamapori na uvunaji haramu wa Misitu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anieleze, ile kesi ya kutoroshwa wanyamapori wengi kwa ndege ya kijeshi iliyotua nchini mwaka 2010 inayowahusu akina kijana hatari Kamran imefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Wazirina Naibu Waziri, kwa juhudi kubwa wanazofanya. Wameanza vizuri.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawashauri Wabunge wenzangu tuwape nafasi hawa Viongozi wapya kwenye Wizara, waweze kutekeleza mikakati yao ya kutokomeza ujangili tusiwakatishe tamaa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono.

MHE. JUMA SURURU JUMA: Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa siku nyingi kuwa, Mlima Kilimanjaro unatangazwa sana na jirani zetu wa Kenya kwa kukuza utalii wao. Sasa nilitaka kujua ni kweli suala hili? Kama ni kweli hatuoni kama tunaibiwa mali yetu mchana na nini mikakati ya Serikali katika kupata suluhu ya jambo hilo?

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa jitihada zake kuboresha vyuo vya wanyamapori. Kwa kuwa nchi yetu ni kubwa sana na Wananchi wetu wanahitaji elimu hii muhimu ya wanyamapori, naiomba Serikali ianzishe vyuo hivyo kikanda ili kukidhi haja ya elimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua kamahali ya ujangili nchini imepungua na kama haijapungua Serikali ina mpango gani endelevu wa kudhibiti hali hiyo? Tokea kusimamishwa Operesheni Tokomeza, Serikali inachukua hatua gani mbadala ya kudhibiti ujangili nchini?

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kupata fursa ya kuchangia hoja hii ya Maliasili na Utalii. Hakika katika Hotuba hii pamoja na kueleza mikakati ya kibajeti, nilitegemea kupata majibu ya hoja zilizotolewa ndani ya Bunge hili Tukufu katika Kikao cha Kumi na Nne, Mkutano wa Kumi na Nne.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, katika mkutano huo na kikao hicho, Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Utalii juu ya Operesheni Tokomeza iliyowasilishwa Bungeni, nilichangia suala la Wakala wa Misititu (TFS), kuwawekea mabango Wananchi wa Kata ya Kaniha, Kijiji Kaniha na Mpago, vijiji ambavyo vimesajiliwa rasmi na mamlaka zinazohusika. Pia kuna shule ambazo zimesajiliwa na kujengwa na Wananchi chini ya usimamizi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, swali la kujiuliza; je, wakati mambo haya yote yanaendelea Serikali au wakala hawa wa misitu hawakulijua hili; na kama walilijua walitoa ushauri gani kabla ya kusajili eneo la hifadhi kama eneo la kijiji?

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali kuwa, sasa si muda mwafaka wa kuwabughudhi Wananchi ambao wamekuwa wakiendesha shughuli zao za maisha kwa maana ya kilimo na ufugaji wa nyuki, waendeleo na shughuli hizo kwani wamekuwa wakifuata sheria na taratibu za ufugaji wa nyuki na kilimo pia. Napenda kukemea suala la Watumishi wa Serikali wanaowapatia Wananchi taarifa potofu, lakini Serikali muda wote imekuwa ikishughulikia suala hili kwa kasi ndogo sana au isiyotoa matumaini. Naomba Serikali ilishughulikie kwa haraka sana ili Wananchi hawa waweze kuishi kwa amani na kuendeleza shughuli zao za kujikimu kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kuhusu Pori la Akiba la Burigi – Kimisi. Pori hili limekuwa likitumiwa sana na askari wa wanyamapori kama sehemu ya kuendeleza ukatili juu ya mifugo na wafugaji wamekuwa wakikamata mifugo na kuipeleka hifadhini kwa kudai kupewa rushwa. Rushwa inapokosekana, basi mifugo hiyo hupigwa risasi au kuuwawa kwa namna yoyote ile. Naomba Mamlaka zinazohusika zilifanyie kazi suala hili na hasa kwa watumishi wasiokuwa waadirifu wala hawana uzalendo.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuishauri Serikali kuhusu hali halisi ya Pori la Burigi. Hakika Pori hili sasa limeishiwa wanyama hasa kutokana na kuvunwa kwa kasi kubwa kipindi cha wakimbizi katika Kambi ya Benaco, Rumasi na Rukola. Kwa sasa wanyama ni wachache hivyo napendekeza kuwa, Serikali ione jinsi ya kuligawa Pori hili la Akiba ili sehemu yake itumike kwa wafugaji na sehemu nyingine ibaki kama sehemu ya Pori la Akiba.

Mheshimiwa Spika, mwisho, huduma za jamii kwa hawa Wananchi wanaolinda na kuishi karibu na maeneo ya hifadhi hii ya Pori la Akiba. Hakika, wanafanya kazi kubwa lakini pale wanapovamiwa na wanyama wakali au kuharibiwa mazao, utaratibu wa kuwalipa fidia siyo mzuri hata kidogo. Wananchi hawapati haki yao ya kupewa fidia. Nyaraka zimetolewa lakini zimebaki kuishia makabatini hakuna elimu inayotolewa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ifafanue jambo hilo kwa Wananchi ili wajue haki yao ya kupewa fidia. Utaratibu wa zamani wa kuwapatia kitoweo wakati wa sikukuu urudiwe kwani ulikuwa unatoa motisha kwa Wananchi.

MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID: Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa hivi sasa la shughuli katika hifadhi ni ulinzi. Hivi sasa tunakabiliwa na uchache wa walinzi. Pia uadilifu katika hao walinzi.

Mheshimiwa Spika, walinzi hawatoshelizi hata kidogo, inatakiwa kuongeza walinzi zaidi ya waliopo.

Mheshimiwa Spika, walinzi wanahitaji kupata zana za kisasa, lakini pia wanahitaji kuongezewa mafao zaidi ili kuweza kuzidisha uadilifu ndani ya mbuga husika na kuweza kuwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

tayari wakati wowote wa kazi. Wanyama pori lazima wawe na maadili mazuri na kuweza kuleta mashirikiano mazuri na majirani walio karibu na hifadhi.

Mheshimiwa Spika, tuna wajibu wa kusambaza vipeperushi katika Balozi zetu za nje ili kuweza kuutangaza Utalii. Sisi tulio ndanipisa tunawajibu maeneo ya magofu kuhifadhiwa na kuendelezwa ili historia isipotee.

Mheshimiwa Spika, watendaji wapatiwe vifaa vya mawasiliano ili kuweza kuwasiliana kwa lolote ambalo litajitokeza katika harakati za ulinzi.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kuchangia kama ifuatavyo:-

Mwaka jana niliuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri juu ya Serikali kuchukua hatua ya kupunguza uwingi wa mamba katika Ziwa Rukwa, Mto Momba na maeneo mengine nchini, kutokana na wanyama hao kuuwa wavuvi, akina mama na watoto, wanapokwenda kuchota maji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Waziri alitoa ahadi ya kutoa kibali cha kuwapunguza wanyama hao, hadi hivi leo hakuna utekelezaji wowote. Naomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo; vinginevyo, sitaunga mkono hoja na nitaondoa shilingi.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya pili, naomba Hifadhi ya Pori la *UwandaGame* Reserven Hifadhi ya Akiba na Hifadhi hii imekuwepo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, cha ajabu Serikali haijachukua hatua yoyote ya kuendeleza, kwa kukosa watumishi wa kutosha kulinda hifadhi hiyo, kukosa vifaa vya kutendea kazi kama pikipiki, magari hata majengo ya makambi ya watumishi hakuna, kutokuimarisha mipaka na hakuna motisha yoyote iliyowahi kutolewa kwa kusaidia Wananchi ambao wamepakana na Hifadhi hiyo, kama vile kuwasaidia ujenzi wa zahanati au shule, kiasi kwamba, Wananchi wanakata tamaa na kuona Mbuga hiyo haina faida yoyote kwao na kuona kwamba, ni bora watumie kwa matumizi ya kilimo na kulisha mifugo yao.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atoe maelezo, vinginevyo, siungi mkono hoja na nitaondoa shilingi.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri Lazaro Nyalandu, ameanza vizuri na namshauri asiteteleke na makandokando ya magazeti hasa Gazeti la Jamhuri. Gazeti hili hili lilituhumiwa na uongozi uliopita kuandika taarifa za uzushi kwangu ambazo walishindwa kuzithibitisha. Leo wamekugeukia wewe na Wizara yako. Chapa kazi mdogo wangu. Fuata sheria na kanuni zilizopo na Mungu atakuepusha na ushetani wa wabaya wako.

Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, ile Tume iliyoundwa na Mheshimiwa Rais, ifike Tunduru kukutana na walioathiriwa na *operation* zilizopita; ni vyema sana Tume hiyo ikafika Tunduru ili wapate fursa ya kuupata ukweli wa yale yote niliyoyaeleza hapa Bungeni. Ombi langu kwako ni kuwajulisha kuiweka Tunduru kwenye orodha ya maeneo watakayopita, kama Tunduru imeasahuliwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, uhifadhi wa wanyama ni muhimu sana kuzingatia ushirikishwaji wa jamii inayozunguka hifadhi husika. Aidha, kuwajali pale wanaposhambuliwa na kuharibiwa mazao yao ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua kiasi cha pesa kilichopelekwa Tunduru (i) Kama kifuta machozi. (ii) Kifuta jasho.

Mheshimiwa Spika, namtakia kila la heri Mheshimiwa Waziri na Mungu ambariki sana.

MHE. KAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya, kusimamia maliasili zetu na kuendeleza Utalii Nchini. Pamoja na pongezi hizi, ninayo maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 1995 Mpaka wa Hifadhi ya Misitu ya Kizigo na *Mhasi Forest Reserves* ulisogezwa kuingia maeneo ya vijiji katika Kata za Sasilo na Iseke. Baada ya takribani miaka 20 kupita, idadi ya wanavijiji imeongezeka mara dufu na pia shughuli za kilimo na ufugaji nazo zimeongezeka. Kwa hiyo, kumejitokeza uhaba mkubwa wa ardhi na ndilo chimbuko la ombi la Wananchi kuomba Mpaka huo urudi kama ilivyokuwa 1995. Ombi hili tayari limemfikia Mheshimiwa Waziri, ambaye ameahidi kutembelea maeneo hayo ili ayaone na pia ili awasilize Wananchi kabla ya kutoa jibu. Ahadi hii ya Mheshimiwa Waziri imeleta faraja, hivyo kinachosubiriwa ni utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, mara kwa mara katika vijiji vinavyopakana na Hifadhi za Kizigo na Mhesi huvamiwa na wanyamapori ambao huharibu mazao yao na hata kuua watu. Malalamiko ya Wananchi hao ni kwamba, yanajitokeza madhara hayo, hatua za Serikali kuwalipa fidia ya mazao yao au kulipwa kifuta machozi kwa urasimu mkubwa uliopo kuchelewa na wakati mwingine malipo hayatolewi kabisa. Nashauri Wizara itazame upya utaratibu huo ili kuondoa urasimu na pia malipo ya fidia yatolewe kwa uhakika na bila ucheleweshaji.

Mheshimiwa Spika, hatua ya kufungua Mpaka wa Gologonja haina masilahi kwa uchumi wa nchi yetu. Mpaka huo ukifunguliwa, Watalii wataingia asubuhi Serengeti, wataona wanyama na jioni wataenda kulala Masai Mara (Kenya); hivyo, Tanzania tutakusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Operesheni Tokomeza Ujangili kuna silaha zinazomilikiwa kinyume cha sheria zilikamatwa, lakini pia kuna silaha zilizokuwa zinamilikiwa kiholela na hazijawahi kutumiwa kwa njia haramu nazo zilikamatwa kwa uchunguzi zaidi. Baada ya miezi sita kupita, bila shaka uchunguzi na uhakiki umekamilika na zile silaha ambazo zimeonekana hazina matatizo basi zinarudishwa kwa wenyewe kwani kwa Serikali kuendelea kuziua bila ya sababu za msingi siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, baada ya kuipongeza Wizara kwa kutayarisha Hotuba nzuri. Napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kama inavyotambulika kuwa Wizara hii ni muhimu sana katika maendeleo na uimarishaji wa uchumi katika nchi yetu na kuwa kama tukizingatia kanuni majukumu yake ni mazito na mengi sana, ingetakiwa itapangiwe bajeti kubwa iweze kukamilisha kazi zake vizuri.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kinachosikitisha ni kule kupatiwa fungu dogo la bajeti kila mwaka, kitendo ambacho kimefanya malengo ya Wizara hii kutokukamilika vizuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali iwe inapanga bajeti ya kutosha (kubwa) kila mwaka katika Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Wanyamapori Mweka ni muhimu sana Tanzania na Afrika yote, kuelimisha wanafunzi na kupatikana wataalamu wengi wa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, Chuo hiki nimuhimu na wanafunzi wake na wafanyakazi wake (walimu) wanachangia katika uimarishaji wa ulinzi wa mapori yetu yenye wanyama wenye kutuletea thamani katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Chuo hiki cha Mweka katika utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi kinahitaji kupatiwa bajeti ambayo itaweza kukidhi mahitaji yake. Mfano wa mahitaji hayo ni vifaa kama magari, vifaa vya ulinzi, *uniform* nakadhalika.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iwapatie fungu kubwa la bajeti Chuo hiki cha MWEKA ili kiweze kukamilisha kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja hii, pamoja nakuitakia heri Wizara hii kwani Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri ni Watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, Wizara hii licha ya kuomba fedha za matumizi kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali pia zimo Taasisi nyingi ambazo zinakusanya mapato. Pia imo mifuko kwenye Wizara hii ambayoinakusanya fedha kwa ajili ya mifuko hiyo. Mfano ukiangalia ukurasa wa saba wa hotuba ya Waziri, Mfuko wa Uhifadhi Wanyamapori Tanzania ulikadiriwa kukusanya Tshs.16,410,524,584 kwa mwaka 2013/2014. Hadi Machi 2014, makusanyo yamefikia Tshs. 9,999,829,839. Imebakia miezi mitatukwa kuanzia Machi bado asilimia 39% fedha kufikia lengo. Je, uwezekano wa kufikia lengo hilo upo? Je, kwa makisio yenu kama hamtafikia lengo itakuwa ni sababu gani?

Mheshimiwa Spika, pia ukiangalia ukurasa wa 21 wa Hotuba ya Waziri, Mfuko wa Misitua Tanzania ulikadiriwa kukusanya Tsh.4,561,000,000 kutoka vyanzo vyake lakini hadi Machi, 2014 mfuko ulikusanya Tsh. 2,281,231,061. Je, upo uwezekano wa kukamilisha lengo la makusanyo?

Mheshimiwa Spika, mapori yetu ya akiba yanakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo uhaba wa Askari Wanyamapori na uchache wa fedha za kuhudumia mapori hayo. Hayo yanatokana na fedha zinazopatikana kwenye mapori hayo kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili kukabili utendaji usioridhisha wa mapori ya akiba imeshauriwa kwa muda mrefu kuundwe Mamlaka ya Wanyamapori. Je, mchakato wa uundaji wa Mamlaka ambao hivi sasa uko mbioni, kuwepo kwake kutatosheleza kwa kutegemea Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009?

MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, kupitia maandishi nichangie bajeti ya Wizara ya Maliasili. Sekta hii ni muhimu sana kwa uchumi wanchi ukizingatia fursa inayotoa kwa kuajiri vijana wetu wengi ambao hawana kazi. Kwa maslahi mapana ya Serikali na wananchi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

nashauri utaratibu uandaliwe ili mapato yatokanayo na shughuli za maliasili na utalii moja kwa moja yatumike kuajiri wawezeshaji wa sekta hii.

Mheshimiwa Spika, mkipitia taarifa za sekta hii na kwa wale tunaoishi karibu na rasilimali za sekta hii utaona kuwa ufanisi wa shughuli hii unakwamishwa na kutokuwa na watumishi wakutosha. Tunahitaji kuwa na walinzi wa *National Parks* na *Game Reserve* wakutosha ili moja, kulinda misitu na wanyama isiharibiwe na pili kuzuia wanyama wasivamie maeneo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja naupungufu wa rasilimali watu unaoikabili sekta hii, naishauri Serikali ielekeze nguvu katika kusimamia hifadhi za Burigi na hifadhi zote Mkoani Kagera. Tofauti na hifadhi nyingine nchini, hifadhi za Mkoa wa Kagera zinahusisha suala la usalama wa nchi kutokana pale zilipo.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli uliowazi wahamiaji haramu wakiwemo wapiganaji toka nchi jirani wamekuwa wakitumia sehemu hizi kama maficho. Watu hawa ambao huandamana na makundi ya ng'ombe wamekuwa wakiendesha shughuli za ufugaji hali ambayo inawatisha wanyama na kupelekea kuvamia mashamba ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, uvamizi wa binadamu (wa nje na ndani) umepelekea Kata za Wilaya ya Muleba hasa Rutoro kuvumiwa na tembo. Kwa sasa Kata ya Rutoro vijiji vyake mazao yao yameharibiwa na tembo kiasi kwamba sasa wananchi wanakabiliwa na tishio la njaa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara hii kulichukulia kwa upekee suala la tembo kuvamia Kata ya Rutoro. Wananchi wamekuwa waungwana wakishuhudia mazao yao yakiharibiwa. Kumekuwepo na ongezeko la tembo hali ambayo ni nzuri kwa Taifa lakini haipaswi kuwa kero kwa wananchi maskini na tabia hii ya wanyama hawa imetokana na uwepo na shughuli za kibinadamu katika hifadhi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. WILLIAM V. LUKUVI: Mheshimiwa Spika, pongezi kwa viongozi wa Wizara na watendaji wa TANAPA, Mfuko na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba yafuatayo:-

(1) Maagizo ya kujenga *airstrip* nje ya Ruaha *National Park* litatekelezwa lini pale? Naomba ratiba ya utekelezaji.

(2) Ahadi za kujenga Kituo cha Polisi na nyumba za Polisi Idodi na Pawaga zimeanza kutekelezwa kwa kujenga nyumba. Ni lini sasa Kituo cha Polisi kitajengwa Idodi na Kimande ili kesi za ujangili na msaada wa ulinzi wa Polisi kwa kushirikiana na Mbonipa iwe rahisi na imara.

(3) Naomba msaada wa ujenzi wa shule ya sekondari ya Mahuninga.

- Bweni la wasichana Mlwe Sekondari.
- Ukarabati wa zahanati ya Mahuninga.
- Gari la wagonjwa kituo cha afya Mlwe.
- Uunganishaji wa umeme katika shule ya Sekondari ya Idodi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

- Kukamilisha bweni la shule ya sekondari ya W.V. Lukuvi na kuongeza bwalo la chakula na bweni lingine.

(4) Naomba Wizara iingilie kati kukomesha migogoro ya Mbonipana kwa kipindi hiki chenye migogoro naomba wapewe ruzuku ili waimarishe ulinzi.

(5) Wizara itume wataalam ili wafanye tathmini ya mazao yaliyoliwa na wanyama kwa miaka kadhaa katika vijiji vya Mlowa, Idodi, Mapogoro, Tingamalenga, Mahuningana Makifu na naomba sana fidia stahiki walipwe wananchi haraka iwezekanavyo.

(6) Kasi ya miradi na misaada ya umeme imepungua sana kwa vijiji vinavyozunguka *Ruaha National Parks* ukilinganisha ni vijiji vya Mbuga za Kaskazini? Naomba tuongeze misaada ili ulinzi shirikishi usitetereke.

(7) Lunda Mkwembi *North* ipewe Mbonipa.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kidogo katika Wizara hii. Mimi ni Mjumbe wa Kamati hii ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Kamati yetu imetembelea baadhi ya hifadhi zetu na tumejionea wenyewe upungufu uliopo katika hifadhi zetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kusema sekta hii ya maliasili kama itatumika vizuri na kuweka malengo yatakayotekelezwa kwa wakati inaweza kuongeza pato letu la Taifa. Kwa kiasi kikubwa katika ziara yetu tulikutana na tatizo kubwa la mipaka kati ya vijiji na Hifadhi za Taifa na mapori ya Akiba na Tengefu. Tatizo hili kama hatua za dharura hazitachukuliwa tunaweza kusababisha hali mbaya au ya hatari katika maeneo hayo. Niombe Wizara ya Ardhi pamoja na Wizara hii ifuaatilie suala hili. Kama hatutafanya hivyo tujue hatutaweza kupata ushirikiano toka kwa jamii zinazozunguka maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Wanyamapori. Tatizo la ujangili bado ni kubwa katika nchi yetu. Kila kukicha tunaona kwenye vyombo vya habari tembo wanavyouawa katika hifadhi zetu pamoja na mapori yetu lakini yako matatizo yanayosababisha hayo kutokea moja ni uhaba wa Askari wa Wanyamapori. Maeneo ni makubwa sana na idadi ya Askari ni ndogo. Kibaya zaidi miundombinu ya barabara ni mbaya na magari waliyonayo si mazima sana, mengi ni mabovu na hii inasababishwa na ubovu wa barabara. Tunaiomba Wizara ifanyie kazi masuala haya haraka ilituweze kuondoa tatizo la kuuwawa hovyoy kwa wanyama wetu hasa tembo.

Mheshimiwa Spika, mradi wafaru. Tulitembelea hifadhi ya Mkomazi na tuliona faru hao lakini cha kushangaza na kutia aibu ni kutoza ushuru faru hao. Naomba Serikali kwa kuwa ni moja itazame mambo haya. Faru tumepewa msaada baada ya kuwawinda sisi wenyewe wa kwetu, hata kama tunataka kukusanya kodi si kwenye mambo haya ambayo yanasaidia kuongeza hiyo kodi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la uteuzi wa Bodi za Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii. Napenda kujua kuna tatizo gani linalosababisha uteuzi huo kutofanyika mpaka sasa, huku tukijua kutokuwepo kwa Bodi hizo kunasababisha mambo kwenda ndivyo sivyo katika mashirika hayo? Naiomba Serikali ione umuhimu wa Bodi hizi na iweze kufanya uteuzi huo kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza TANAPA kwa kazi nzuri ambazo wamekuwa wakifanya katika jamii zetu. Kamati yetu iliweza kuona miradi hiyo na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

mingine tuliweza kuizindua. Nawapongeza sana naniwaombe waendeleo kushirikiana na jamii zinazowazunguka, hii inasaidia kujenga mahusiano mazuri katika kuhifadhi na kutunza hifadhi zetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuandika hayo machache, naomba kuishia hapo, niwatakie Wizara kila la kheri katika kutekeleza bajeti hii ya mwaka 2014/2015.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Wizara kwa kazi nzuri hadi kuongeza idadi ya watalii nchini na pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, natoa ushauri, Wizara itoe matangazo ya kutosha kwa mbuga/hifadhi nzuri ya Sadani. Vilevile watumishi katika ile Mbuga wana hali mbaya sana kifedha. Naomba sana Serikali iliangalie suala hili ili kuwawezesha watumishi kutimiza wajibu wao wa uhifadhi kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, pia uchomaji mkaa hifadhi ya Sadani unatishia usalama wa misitu. Serikali ifanye ufuatiliaji na udhibiti dhidi ya uharibifu huu mkubwa wa mazingira katika hifadhi ya Sadani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri Nyalandu na Naibu wake Mheshimiwa Mgimwa kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, pili, naiomba Wizara ya Maliasili na Utalii kuchukua hatua za haraka kumaliza mgogoro uliopo kati ya Hifadhi ya Pori la Swagaswaga Wilayani Chemba katika kijiji cha Handa na wale wa Nduamhanga Wilayani Singida ambako ni Jimboni kwako Mheshimiwa Nyalandu ili wananchi hawa waishi kwa amani. Ahsante.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, kutokana na hali ya ukiukwaji mkubwa katika Operesheni Tokomeza, Serikali ifikirie namna ambavyo itafidia wananchi walioathirika na zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu Serikali imefanya kazi kubwa katika kutangaza utalii, jitihada hizi ziongezwe ili kutangaza utalii. Iharakishe utumiaji wa *Electronic Visa* ili kurahisisha uingiaji wa wageni wa kitalii. Kwa kuboresha na kurahisisha, wananchi na wageni wataweza kushiriki katika utalii. Aidha, mpango wa kurejesha huduma za Shirika la Ndege Tanzania (ATC) uharakishwe.

Mheshimiwa Spika, malalamiko ya wananchi kuhusu fidia ya mazao yao pale wanyama wanapoyaharibu yazingatiwe.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, kuhusu meno ya tembo yote yaliyokamatwa, nashauri yauzwe na pesa zitakazopatikana zisaidie kununua zana kwa ajili ya ulinzi wa Hifadhi zetu kama vile magari na kuongeza Askari. Nchi yetu nimaskini hakuna sababu ya kuchoma pembe, hiyo ni kufuru kwani pembe za tembo siyo sawa na dawa za kulevya, hiyo siyo kweli kabisa. Hatuwezi kupata hasara mara mbili, napinga baadhi ya Wabunge wanaosema tuchome wakati Wizara haina pesa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa rehema na neema zake nyingi kwangu, familia yangu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inaumuhimu mkubwa na jukumu zito la kulinda, kuhifadhi na kuimarisha maliasili na uhifadhi wake kwa faida ya vizazi vya sasa, vijavyo na mpaka siku ya mwisho (kiama).

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, Wizara hii inachangia kwa kiasi kikubwa (17%) katika pato la Taifa. Msisitizo hapa ni kuongeza juhudi na uwazi katika ukusanyaji wa mapato ili kuongeza pato na kuziba mianya iliyopo ya kuvuja mapato. Pia iongeze juhudi na uwazi katika uhifadhi wa maliasili kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Makumbusho ya Taifa lina wajibu na jukumu muhimu sana katika kutoa elimu shuleni, kwenye hoteli za kitalii na taasisi mbalimbali katika kuhamasisha wananchi na wageni kutembelea makumbusho. Makumbusho ya Taifa yana umuhimu wake kwa kuhifadhi kumbukumbu za kale na historia mbalimbali za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu huo lina jukumu pia la kuhakikisha kuwa historia iliyohifadhiwa kwenye makumbusho ni historia halisi (ya kweli) na sio historia ya kupikwa, ya uwongo wenye chuki na ambayo inaendeleza chuki katika Taifa na kusababisha ubaguzi badala ya umoja na mshikamano. Kuna ukweli kiasi gani katika biashara ya utumwa kama inavyoonyeshwa kwenye makumbusho? Huhitaji elimu ya Chuo Kikuu kuona uwongo, uzushi, fitina na chuki dhidi ya jamii fulani.

Mheshimiwa Spika, hivi ni kweli mtu anauza watumwa awafunge minyororo shingoni na miguuni watumwa hao na kisha awabebeshe magogo mazito vichwani mwao? Kwa kufanya hivyo atapata faida katika biashara hiyo? Jibu ni hapana, bila shaka atapata hasara, kwani watumwa hao watakosa soko kwa kudhoofika kwa matesohayo. Ni mfanyabiashara gani anayefanya biashara ili apate hasara? Bila ya shaka mfanyabiashara huyo atakuwa ni "Halikuniki" anayevaa fulana kiunoni badala ya kifuni. Ni huyu tu ndiye akinunua mayai kwa senti 25 kwa yai moja na kuuza kwa senti 20, eti kwa sababu yananunuliwa haraka kwa bei hiyo?

Mheshimiwa Spika, sipingani na hoja ya biashara ya utumwa laa hasha! Napingana na namna *illustration* ya biashara hiyo iliyofanywa nchini. Ni kwanini anayetajwa kununua watumwa Tip Tip kuwe na kumbukumbu ya picha yake halisi, lakini kusiwe na kumbukumbu ya picha halisi za watumwa? Picha zote za watumwa ni za kuchora kwa mikono (yaani picha za kubuni). Ni kwanini iwe hivyo kama si kwa nia ya kujenga chuki, fitina na ubaguzi katika Taifa? Hivi ni kweli baada ya miaka 53 ya uhuru wasomi wetu wameshindwa kuliona hili? Wameshindwa kutafiti juu ya hili au na wao wamekariri kama kasuku?

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni Wizara muhimu sana kwa ustawi wanchi yetu. Nilikuwa naomba Wizara iweke umuhimu mkubwa kwa kuongeza bajeti ambayo itakidhi mahitaji ya uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, suala la migogoro ya wananchi na misitu inayopakana na vijiji. Kumekuwa natatizo kubwa sana kati ya wananchi na maeneo ya uhifadhi. Ni vyema sasa Serikali iangalie upya suala la mipakahasa maeneo ya Wilaya ya Mpanda ambayo asilimia kubwa ya maeneo ya Wilaya hiyo ni mapori. Niombe sana Wizara iangalie mgogoro wa vijiji vya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kabage, Kapalamsenga, Sibwesa, Bugwe na kitongoji cha Igalukilo – Luhafwe litatuliwe mapema sana ili wananchi watengewe maeneo ya kufanyia shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, Operesheni Tokomeza. Suala hili lilitokelezwa kwa kukiuka haki za binadamu na udhalishwaji mkubwa ulifanywa, ambao kimsingi haukuzingatiwa misingi ya ubinadamu. Niombe sana isirudie makosa yaliyojitokeza. Niiombe Wizara wale watu ambao waliathirika ifikirie kuwalipa fidia kwani wapo ambao sasa ni vilema ambao hawawezi tena kufanya shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, mbuga ya Katavi. Mbuga hii haijaendelezwa wala kutangazwa vyakutosha. Ni kwanini mbuga hii haitangazwi ili ilete maslahi kwa wananchi wa Mpanda na Taifa kwa ujumla? Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri afikirie juu ya kuboresha mfumo wa barabara na kuongeza watumishi na vitendea kazi ambayo vingeweza kusaidia shughuli za uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja nikipata ufafanuzi.

MHE. DKT. FENELLA E. MUKANGARA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hojana pongezi kwa kazi nzuri ndani ya mazingira magumu. Naishauri Wizara ijipange kimkakati katika kutoa elimu kwa umma iliyo endelevu. Wananchi wanatakiwa kuwa na uelewa sahihi na wajibu wao katika sekta hii ya utalii. Hatujachelewa, vijana wanatakiwa kuibeba kwa mtazamo chanya, tulinde na kuhakikisha vijana wanaibeba na kuachana na *statements* za ulalamishiulalamishi.

Mheshimiwa Spika, suala la “Borogonja” nisensitive sana na muhimu kwa maendeleo ya utalii nchini. Hili mimi nilikutana nalo miaka mitatu iliyopita na nililipinga katika mkutano. Sababu za kiuchumi na kiusalama. Mpaka wa “Borogonja” ukifunguliwa magendoitakuwa vigumu kuya-manage. Kenya watafaidika zaidi na viwanja vyetu vya ndege, hoteli zetu zitafungwa, hili halina mjadala kwa kweli. Hili kwangu sikubaliani nalo ili kulinda kazi za vijana na usalama wa Taifa letu. Baba wa Taifa alizuia na mimi katika mkutano nilioenda kumwakilisha Waziri Maige niliwaambia Baba wa Taifa alifunga na ufunguo alitupa katika Ziwa Victoria. Bado *pressure* ipo ya kutaka ufunguliwe, tusikubali, elimu hii vijana waipate hasa wenye kuishi sehemu hizo.

Mheshimiwa Spika, pongezi, kazi nzuri sana, ni ngumu lakini ni muhimu lifanyike hasa hilo la Operesheni Tokomeza iliyo sahihi. Wale watovu na waharibifu katika utekelezaji wabainishwe tu. Nia ninjema na wananchi washirikishwewafichue wanaohujumu sekta ya utalii. Utalii ni soko kubwa na vijana wetu watapata kazi huko za aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tuhakikishe tuna ndege zetu wenyewe, hili ni muhimu sana. Hivyo Wizara ifanye kazi kwa karibu sana na uchukuzi; *Hoteli Tour Operators* na mafunzo ya *hospitality*. Amani na utulivu ni muhimu sana na vijana kuwa na ufahamu sahihi wa umuhimu wa utalii na wajibu wao. Kutumia Wizara ya Habari na Michezo kwa karibu kutangaza utalii kwa usahihi na kukuza ushirikiano wa karibu na sekta ya Utamaduni, Michezo na Habari ni muhimu. Nashauri kuwe na *Steering Committee* ya kuangalia maeneo ya wazi ya ushirikiano wa karibu yafanyiwe kazi kwa usahihi na matokeo yaonekane nayawe na tija endelevu.

MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya, kazi ya uhifadhi siyo rahisi. Wakati Wizara inahangaika na uhifadhi wapo watu wachache wenye uchu wa fedha wanaohujumu uhifadhi na kuendeleza ujangili, kuvamia maeneo ya hifadhi pia katika misitu. Nashauri Wizara ianzishe *operation* maalum ya kupambana na majangili lakini pia kuwaondoa watu waliovamia katika misitu ya hifadhi. Napongeza kazi nzuri ya uhifadhi, bila jitihada za

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

namna hii leo Serengeti wala Ngorongoro zisingeweza kuingia kwenye maajabu ya dunia. Ni kwa jitihada hizo ndio maana tumefanikiwa, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ifanye jitihada za makusudi kutangaza utalii wetu wa ndani kwenye Balozi zetu. Najua kila mwaka Mabalazi wetu wanakuja nchini, Wizara iwatembeze kwenye mbuga zetu na hata Mlima Kilimanjaro maana watakuwa kielelezo kizuri cha kutusaidia kutangaza utalii wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anapohitimisha hotuba yakeatuambie je, haoni kwa kufungua mpaka wa Bologonjaatadidimiza utalii wa Tanzania? Kwani ni rahisi sana Mkenya kutoka Maasai Mara kuingia Serengeti na kurudi kuliko mtalii anayetoka Ngorongoro?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kupongeza kwa kazi nzuri.

SPIKA: Sasa nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri, nitampa dakika 15 maana mmedai vitu vingi. Mheshimiwa Naibu Waziri ndiyo wakati umefika!

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyenijalia kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwa namna ya kipekee naomba nimshukuru sana Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyeniteua kuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Mufindi Kaskazini kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya Kibunge.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kusema na kwa kuandika. Sisi kama Wizara tunathamini sana michango ya Waheshimiwa Wabunge na tunaamini wamechangia kwa nia njema kabisa ya kuisaidia Serikali yetu. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tunaikubali na tutakuwa tayari kuifanyia kazi kwa kadri ya maelekezo yao waliyotupatia.

Mheshimiwa Spika, nitajielekeza katika maeneo makubwa mawili. Eneo la kwanza ni lile linalohusu migogoro. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia suala la migogoro. Hapa kuna migogoro ya aina mbili, kuna migogoro ambayo iko kati ya wananchi na misitu na kuna migogoro ambayo iko baina ya wananchi na hifadhi.

Mheshimiwa Spika, nikianza na migogoro ambayo ipo baina ya misitu na hifadhi, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo na akaunda Tume kushughulikia migogoro hiyo. Nataka niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba, migogoro hiyo tunaifanyia kazi na tumeiweka katika programu mpaka ifikapo Desemba, nina uhakika tutakuwa tumepita katika maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba, pamoja na migogoro hiyo iliyopo tusitumie fursa hii kujijenga sana kisiasa, tuangalie hali halisi na sheria ambazo zinatuguide katika migogoro hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ninalotaka kuzungumzia katika eneo la misitu ni kuhusiana na vibali. Katika suala la vibali tuna maeneo mengi hapa nchini na tumeweka utaratibu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

maalum wa watu kupata hivyo vibali. Mwaka huu tumeweka utaratibu kwamba kila atakayeomba alipie sh. 50,000/=. Nimemwona ndugu yangu Mheshimiwa Kigola amelizungumzia sana suala hili, lakini nataka nimweleze nini essence ya kulipia sh. 50,000/=. kwa sababu maombi yote yanapitia kwenye taratibu na vikao mbalimbali, kwa hiyo, zile sh. 50,000 zinazolipiwa zinachangia kuendesha ule mchakato katika vikao mbalimbali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, siku za nyuma hakukuwa na huo utaratibu kwa hiyo, sisi kama Wizara tulikuwa tunapata fedha kutoka maeneo mengine na imeendelea kutu-cost sana. Safari hii tumesema kwamba, hawa wananchi ambao wanaomba vibali wana haki na wenyewe ya kuchangia gharama hizi. Hata hivyo hiyo peke yake haim-guarantee mtu kwamba kama ametoa sh. 50,000 *automatically* apewe kibali. Huo utaratibu haupo, haya ni kama maombi au tenda zingine ambapo mtu anaomba na asipopata hana sababu ya kulalamika.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili ni kwamba, tumetaka kuweka utaratibu tu wa kuwazua watu ambao walikuwa na choyo na roho mbaya. Unakuta mtu mmoja alikuwa anaomba vibali mpaka 100, lakini sasa hivi akiambiwa alipie sh. 50,000/= tu aliyekuwa anaomba vibali 100 hawezi kuomba tena, ataogopa kwani ataona kwamba hizi fedha ambazo anatakiwa kulipa ni zaidi ya shilingi milioni tano. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba walikubali na tunajiangalia upya, mwakani inawezekana tukaweka zaidi ya sh. 50,000/=. Mwaka huu kwa utaratibu huu tumekusanya jumla ya shilingi milioni 400, hizi zitatusaidia katika kuendeleza mashamba yetu katika maeneo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kigola wakati anachangia alizungumza kwamba, kuna watu wanakusanya fedha. Nataka niseme hilo ni kosa la jinai na kama kuna watu wa aina hiyo wanaonekana katika maeneo hayo wachukuliwe hatua za kisheria. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kusisitiza ni kwamba, ule msitu ni wa Serikali siyo wa watu wa Mufindi, hivyo watu wote wana haki ya kupata. Kwa hiyo, watu wote watakoomba *either* wanatoka ndani au nje ya Mufindi tutawapa kwa kutokana na sheria na taratibu ambazo ziko wazi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ninalotaka kuzungumzia ni suala la mipaka na hifadhi. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia suala la migogoro kati ya hifadhi na mipaka yetu. Ni kweli, hili tatizo tumeliona na limekuwa lina changamoto nyingi sana. Kama nilivyoeleza sisi kama Serikali tumejipanga na tutashughulikia migogoro yote na kuna baadhi ya maeneo tumeshaanza kushughulikia na kuna baadhi tumeshaanza kulipa fidia. Kwa mfano, eneo la Saadani, eneo la Uvinje tunategemea kulipa fidia siyo muda mrefu na tumekubaliana na Mbunge aliyeko katika eneo hilo, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, baada ya hotuba hii tutakwenda pamoja kushughulikia jambo hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi yamejitokeza katika mjadala hapa. Wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mbunge wa Biharamulo alizungumzia suala la ng'ombe walioingia kwenye hifadhi zetu. Nataka nilizungumzie kidogo jambo hili kwa sababu najua na Mbunge wa Ngara linamgusa kidogo.

Mheshimiwa Spika, ng'ombe kuingia ndani ya hifadhi zetu ni kosa. Walikuja wachungaji kutoka maeneo husika (Kanda ya Ziwa) kwenye Wizara yetu wakatueleza kwamba, zaidi ya ng'ombe 8,300,000 wako kwenye hifadhi zetu. Kwa hiyo, niliambatana nao tukaenda kwenye *site* tukaangalia na kweli tulijiridhisha tukakuta ng'ombe wapo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, tulirudi tukaongea na Mheshimiwa Waziri Mkuu, tukatengeneza utaratibu suala hili lilikuwa mtambuka ambalo linahusisha Wizara zaidi ya 10. Kwa hiyo, tumekubaliana tumejipanga, Wizara zote 10 tutaitisha mkutano wa pamoja, tutalizungumzia na tutapanga matumizi bora ya ardhi ili tuone utaratibu utakaotumika kuhakikisha jambo hili tunalimaliza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tumeongea na Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, tumekubaliana kwamba atahakikisha ranchi zote ambazo hazifanyi kazi sasa zinaanza kufanya kazi na wale ng'ombe wahamishiwe katika maeneo yale. Sisi kama Wizara tutajiangalia na kujitathmini tuone maeneo yote ya *Game Reserves* na Mapori Tengefu ambayo hatuwezi kuyatumia *properly* tuangalie namna ya kuyashughulikia na ku-release maeneo ambayo hatuwezi kuyatumia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, najielekeza kwenye maeneo hayo machache tu. Baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (Makofi)

SPIKA: Kwa hiyo, dakika zangu zote umenirudishia. Aah, zilikuwa 15 hazikuwa saba7. Mheshimiwa mtoa hoja!

WABUNGE: Hajaunga mkono hoja.

SPIKA: Kwani si inajulikana, sasa nyie mnataka mpaka aseme.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (Makofi/Kicheko)

SPIKA: Mheshimiwa mtoa hoja, *it goes without say*, kwamba naunga mkono hoja, nyie vipi! Mheshimiwa mtoa hoja una saa yako moja. (Makofi)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kwanza kukushukuru wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu na kujadili kwa kina hotuba hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa kadri muda utakavyoniruhusu hapo baadaye nitafurahi sana kuwatambua Waheshimiwa Wabunge wote ambao waliweza kuchangia.

SPIKA: Hutambui, naomba uanze moja kwa moja, mambo waliyosema hapa ni mengi sana. Kwa hiyo, wanajulikana.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii tena kutoa ufafanuzi na maelezo kuhusu hoja mbalimbali ambazo zimeibuliwa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kipekee, kwanza nijielekeze kwenye mambo machache ambayo Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, aliyasema na yeye kama Waziri Kivuli wa Maliasili na Utalii nimpe tu heshima na uzito wa kuyajibu baadhi ya mambo moja kwa moja, halafu nitaendelea na hoja zote zilizotolewa na Kamati na Waheshimiwa Wabunge.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kadhaa alizoieleza Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, ambazo ningependa kuchukua nafasi hii kuzijibu. Hoja ya kwanza ilikuwa ni ahadi ya Serikali ya kuunda Tume ya Kimahakama na kwamba, Tume hiyo ilichukua muda mrefu.

Mheshimia Spika, naomba niseme kwa heshima tu kabisa kwamba, Mheshimiwa Rais alichukua muda aliouhitaji kuuchukua kuteua aina ya Majaji aliokuwa anahitaji kuwateua na kama ambavyo sisi sote tunafahamu Tume hii ya Kimahakama imeundwa na tayari imepewa hadidu za rejea na imeanza kazi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mchungaji Msigwa kwamba, kazi ya Tume hii itafanyika kwa uwazi na itakapokamilika italetwa na tutapata matokeo ya taarifa hii ambayo kwa kweli wananchi wote nchini wanaisubiri kwa hamu. Hii tume ilikuwa ni matokeo ya Maazimio ya Bunge baada ya kukamilika kwa zoezi la Operesheni Tokomeza.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya pili kwamba Waziri wa Maliasili na Utalii, mimi hapa nilipokuwa Naibu Waziri nilikejeli Operesheni Tokomeza. Hapa naomba niseme ukweli ni kama huu ufuatao:-

Taarifa ambazo zilitoka katika vyombo vya habari zilikuwa zinapotosha kabisa ukweli wa kile kilichotokea. Kunako mwezi wa Pili tulipata tatizo kubwa sana pale katika Pori la Mkungunero. Katika Pori la Mkungunero kulikuwa na hatihati kati ya askari wa Wanyamapori na wenyeji kuingia katika vita wakigombania suala la mipaka na suala la lile pori. Uamuzi nilioutoa kama kiongozi wa Wizara wakati ule ulikuwa ni muhimu tukizingatia yale yaliyotokea katika Operesheni Tokomeza na hiyo ndiyo ilikuwa *spirit* tu ya kuweza kufanya kile kikao.

Nikaitisha kikao cha haraka, nikawaomba Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Manyara ikiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Manyara, nikaiomba Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Dodoma ikiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma na nikaomba Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya zote zilizopo katika yale maeneo yanayozunguka, tukawakaribisha Mkurugenzi Mkuu wa TANAPA, viongozi Waandamizi wa Idara ya Wanyamapori na viongozi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha pale Babati ambapo tulijadiliana kwa kina jinsi gani tutaokoa uwezekano wa kutokuwa na amani, tukizungumzia ni jinsi gani tutaokoa uwezekano wa kutokuwa na amani tukizungumzia kwamba, yaliyotokea kwenye Operesheni Tokomeza yangeweza kutokea katika eneo hili kwa sababu askari wangu walikuwa wamebeba silaha na wananchi pia walikuwa na silaha nyingi za jadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa busara uliotoka ni kwamba, mgogoro ule wa Mkungunero utatuliwe kwa njia ya amani. Baada ya ripoti ambayo iliandikwa kwanza na moja ya magazeti, Tanzania Daima katika ukurasa wa tatu ilisema Nyalandu akajeli Bunge na ilikuwa ni sehemu ndogo tu, lakini watu wengine wakaichukulia *out of context* na ikafikia pale ilipofikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nili-clarify hilo jambo kwa kukuandikia barua na kumwandikia Mheshimiwa Waziri Mkuu barua kumpa tu yale yaliyojiri na kuhakikisha kwamba, Mheshimiwa Lembeli na wengine wote walipata nakala. Nilitaka tu nili-clarify hili kwa sababu lilikuwa ni suala la ripoti ambayo haikuwa sahihi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni hoja ambayo pia imejirudia sehemu nyingine, lakini nichukue nafasi hii kuielezea, hoja ya wafanyakazi waliofukuzwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, naomba nilithibitishie Bunge lako kwa mara nyingine tena. Upotoshaji mkubwa sana ambao unatokana na ripoti za baadhi ya vyombo vya habari unakuwa haututendei haki katika utendaji wa Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba hakuna mfanyakazi Mwandamizi aliyefukuzwa kazi, siyo Mkurugenzi Mkuu, bwana Songoro au siyo Mkurugenzi wa *Utilization*. Hatua ambazo Wizara ilichukua na mimi kama Waziri mwenye dhamana, nilichukua hatua za kuwahamisha vituo vya kazi. Profesa Songorwa anakwenda Chuo cha Mweka na ni chuo chenye heshima, na dada yangu Mheshimiwa Magdallena aliongea kwa uchungu kabisa kwamba, watu wamedhalilishwa. Siyo kweli, ni chuo chenye heshima na anakwenda kufundisha.

Mheshimiwa Spika, Profesa Jafari Kidiagesho anakwenda *Selous Game Reserve* kwenda kuwa Namba Mbili. Niseme tu kwamba, Sheria ya Utumishi wa Umma haikuvunjwa, wala Kanuni zake. Ningependa tu nilithibitishie tena Bunge lako kwamba habari hizi nyingi ambazo zimejitokeza kwenye magazeti hazikuwa na usahihi wowote.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ya rafiki yangu Mheshimiwa Mchungaji Msigwa ilikuwa ni hoja kuhusu kuteuliwa kwa Bwana Paul Sarakikya kukaimu nafasi ya Mkurugenzi wa Wanyamapori na nafikiri nilisikia kwa Waheshimiwa wengine wawili. Ukweli ni kwamba yaliyotokea katika Operesheni Tokomeza hatutaweza kuyafahamu yote kabisa mpaka Tume ya Kimahakama itakapokamilisha kazi.

Mheshimiwa Spika, katika utumishi bora wa Serikali watumishi wote wa Serikali ikiwa ni pamoja na wale ambao *administratively* tu katika uendeshaji wa Wizara tuliweza kuwahamisha vituo au tumewahamisha maeneo yao ya kazi. Watumishi wote hawa wa Wizara ya Maliasili na Utalii wanaendelea na kazi zao mpaka tutakapopata Tume ya Kimahakama. Kwa vyoyote vile Ndugu Sarakikya ni mmoja kati ya watumishi Waandamizi na ni kati ya wahifadhi ambao wamebobeza katika kazi walizofanya. Katika hali yoyote ile Serikali haitamwonea mtu yeyote haya endapo atagundulika na akabainishwa na Tume hii kwamba alivunja maadili yake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hapa hapa nijibu, kuna *comment* Mheshimiwa Mbunge mwingine alisema kwamba Wizara hii inaonekana haikuwa na *code of conduct*, siyo kweli. Katika taarifa ambazo watakuwa walizipokea kwenye vyombo vya habari, kutokana na yale yaliyojitokeza kwenye operesheni tokomeza na habari hizi tulizipata, ziliwagusa watu, habari za baadhi ya watu walivyotendewa ziligusa moyo wangu.

Mheshimiwa Spika, tulichokifanya ni uamuzi wa mimi kama Waziri mwenye dhamana kuamua kwamba, ni lazima *code of conduct* (mwenendo wa utendaji kazi) wa Maaskari wa Wanyamapori upitiwe upya. Tukakubaliana kwamba katika siku zijazo kila askari lazima atie saini mwenendo huo na kila mtu lazima awajibike katika kufanyiwa tathmini ya uwajibikaji na uaminifu wake katika kazi anayofanya. Hili jambo linafanyika kwa uaminifu mkubwa. Ni matumaini yangu kwamba matokeo yataendelea kuonekana katika muda siyo mrefu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nigusie hoja iliyotolewa kuhusu baadhi ya vyombo vya habari tuliowaalika hapa nchini. Baada ya ripoti ya *Mail on Sunday* ambayo ilikuwa ni ripoti mbaya, iliidhalilisha sana nchi na kwa vyovyote vile walioiandika aidha walisikia maneno ya upande mmoja au hawakuweza ku-*balance* kama vile mwandishi wa habari ambavyo anatakiwa kufanya.

Mheshimiwa Spika, nilichokifanya nikiwa London Uingereza, nilikutana na *Mail on Sunday*, niliwatembelea katika ofisi yao nikazungumza nao. Lakini pamoja na wao nilitembelea

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

vyombo karibu vyote vikuu vilivyopo Uingereza ikiwa ni pamoja na BBC na vyombo vingine vilivyopo Uingereza. Nilichokifanya ni kuwakaribisha waandishi wa habari kuwapa fursa nyingine tena na tukasema kwamba Serikali yetu haina jambo lolote la kuficha.

Mheshimiwa Spika, uwazi huu umeendelea, bwana Fletcher alituandika vibaya, lakini bado alikuja na akatembelea ofisini kwangu na nilimwona na nilimshika mkono na tukamruhusu kwa kadri anavyoona inafaa atembelee Selous. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, moja; haikufanyika kwa nia mbaya, mbili; hakualikwa yeye peke yake, wamekuja waandishi wa habari wengine wengi, tatu; *BBC Hardtalk* ambayo mimi mwenyewe nili-appear pale London, wanakuja Juni 2, anakuja Steven Saka na atafanya mahojiano na pamoja na kufanya mambo mengine na kutembelea yale maeneo.

Mheshimiwa Spika, tunaamini hii ni moja ya jitihada za Serikali za kupanua wigo wa watu wengi wa kufahamu. Ripoti nyingi sana zimetokea kutoka Nairobi na sasa waandishi wa habari pamoja na vyombo vikuu wanakuja moja kwa moja Dar es Salaam na sehemu zingine na ni matumaini yangu pamoja na nia nzuri hii tuliyonayo, watajionea wenyewe na tutaona *reporting* itaendelea kubadilika.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tunawapokea *The CNN on the Road Show* na maandalizi yanaendelea kuwaruhusu waweze kufanya kazi yao hapa. Tunaingia kwenye majadiliano na CNN kwa mara ya kwanza sisi kuweza ku-host *The CNN African Journalist of the Year* katika nchi yetu. Tumeanza mazungumzo ya MBC ya Riyadh na Dubai na vyombo vingine vingi. Nirudie tu kumhakikishia Mheshimiwa Msigwa kwamba ni jambo ambalo linafanyika kwa nia na kwa dhamira thabiti ya kuhakikisha kwamba uwazi huu unaendelea.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kile alichokisema Mheshimiwa Mchungaji Msigwa juu ya hoja kwamba Jumuiya ya Kimataifa imeshangazwa na kitendo cha Tanzania kuomba kuuza meno CITES. Moja, Mchungaji Msigwa amesema kweli kwamba Tanzania tumekuwa tukiomba kuuza meno CITES, tuliomba Doha tukashindwa, tuliomba tena iliyopita Bangkok tukashindwa na kura hizo zilipigwa dunia nzima iliona.

Mheshimiwa Spika, lakini kitu ambacho ningefurahi sana kama Mchungaji Msigwa angekiweka wazi, ni kwamba mwezi Februari mwaka huu, Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete yeye mwenyewe akiwa amesimama London Uingereza katika mkutano wa dunia ulioalikwa na Mwana wa Mfalme, alitangazia dunia na kusema Tanzania kuanzia sasa haina mpango wowote wa kuyauza meno yake ya tembo. Naomba nimhakikishie Mchungaji Msigwa na nihakikishie dunia, neno lililotumika la Kiingereza lilisema Tanzania *is putting it's ivory stock piles beyond economic use*.

Mheshimiwa Spika, sasa nikienda mbele kwa hoja za Waheshimiwa Wabunge wengine, kuna hoja zinazungumzwa kwa nini tusifanye sherehe ya kuchoma hayo meno. Naomba nichukue nafasi kusema tuna meno ya tembo ya aina mbili:- Moja, tuna meno ya tembo ambayo ni ya kawaida, tembo wataendelea kuzeeka, wataendelea kufa, tutaendelea kuwa na meno ya tembo. Tuna meno ya tembo ambayo yana urefu ambao unaingia kwenye *Guinness Book of Record*. Kuna meno ya tembo ambayo hayapatikani tena duniani na haya ni meno ya tembo halali, tembo wamejifia, tunayo mengi.

Mheshimiwa Spika, pia tuna baadhi ya meno ya tembo yaliyotokana na jitihada za Serikali hii kuwakamata majangili na wezi wa mali za umma. Tumewakamata na yale meno ya tembo pia tunayo. Sasa yale tunayaita *illegal ivory stock piles*. Tulipokuwa tunaiomba dunia waturuhusu kuuza, tulikuwa tunaomba waturuhusu kuuza yale ambayo ni *legal ivory stock piles*, yale ambayo ni meno ya tembo sahihi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi meno ya tembo haya ni mali ya Watanzania wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uamuzi tu wa Waziri wa Maliasili kuchukua kiberiti na kusema tuyachome utakuwa siyo uamuzi sahihi, ni jambo ambalo ningependa kumhakikishia siyo tu Mchungaji Msigwa, lakini Watanzania wote na Wabunge wenzangu, ni jambo ambalo Serikali inaruhusu *debate*, njooni tusemezane, tujadiliane, tuone jitihada ipi, ni kitu gani tufanye juu ya haya meno ambayo kwa kweli ni mali yetu sisi wote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba hili niliweke wazi, aliniuliza hili swali Steven Saka nilipotokea mwenyewe katika *BBC Hardtalk*, London Uingereza aliniambia umesemekana katika vyombo vya habari na alikuwa ananukuu, umesema majangili unawajua. Naomba nichukue nafasi hii kusema, sisi na mimi kama sehemu ya Serikali tunajua vitu vingi, tunawajua watu wengi, hata baadhi ya waovu ambao tunawajua, utaratibu wa kumkamata mtu ni mpaka umkamate na kidhibiti na ndiyo maana tunachokifanya, tumeandaa *Task Force*, tuna utaratibu wa watu ambao wanaonekana wamevaa *uniform*, kuna watu ambao hawajavaa *uniform*, kuna watu ambao wanatembea kwa miguu, kuna watu ambao wanatembea kwa mabasi. Lakini hawa watu wote wanatusaidia shughuli za intelijensia na ndiyo maana tunaendelea kuwakamata na ndiyo maana Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maana ya ukamataji wa haya meno ya tembo ambayo dunia ndiyo imekuja kufahamu, yamekamatwa kwa sababu Serikali ilifanya juhudi ambazo zilikuwa siyo za kawaida. Kuna watu wengi wamejitolea. (Makofi)

Kwa hiyo, tuliposema katika hotuba ya msingi kwamba kuna watu zaidi ya 2,000 ambao tuliwakamata, hao wote ni majangili, hawa wote wana majina, majina yao yako Mahakamani. Tuliposema tuna watu zaidi ya 70 ambao wameingia jela wamehukumiwa kutokana na hivi vitendo, hawa mabwana wote ni majangili, wote wamekamatwa, wote wako jela. Tuliposema kuna kesi nyingi ambazo sitaweza kuzitaja hapa, ni kwa sababu tunao watu, tunao maaskari.

Mheshimiwa Spika, tuna maaskari ambao hawalali. Kila siku namfikiria askari Doricas, ni binti aliyeanza kazi pale Maswa, lakini katika siku zake za kwanzakwanza alipenda kuwa ni mhifadhi, walivamiwa na majangili usiku, alikuwa wa kwanza kupigwa risasi na alifariki. Hawa watu wanajitolea na unaweza ukaongea, lakini tunapokuwa tunaongea hili jambo tutazame upande wa pili, kuna watu ambao wametoa maisha yao kwa ajili ya uhifadhi na kwa sababu yao tumefanikiwa, tunafanikiwa kuwakamata majangiri wengi.

Mheshimiwa Spika, mwezi wa tatu mwaka huu Serikali ilitoa ripoti iliyosema kwamba ukilinganisha mizoga yote ambayo tulikuwa tumeipata nchini kwa kuhesabu kuanzia mwezi wa Kwanza, wa Pili na wa Tatu, mwaka 2014 na mwaka 2013 kulikuwa na tofauti ya asilimia 54. Kwa maneno mengine hatua zipo zinazochukuliwa na kuna dalili kwamba ujangili tunazidi kuushinda.

Mheshimiwa Spika, vita hii bado ni kubwa na ndiyo maana lile neno ambalo Mchungaji alirudia la kusema *international syndicate*. *International syndicate* ipo, ipo kila mahali na ipo hapa na ndiyo maana tunasema tunavishinda hivi vita kwa sababu wananchi wamesimama, wananchi wa kawaida mmoja mmoja wanatupigia simu. Nakaa, Mheshimiwa Naibu Waziri ananiambia nimeletewa habari hii. Sisi wenyewe tunawapigia wale tunawaambia pelekeni maaskari. Tembo anauawa mahali, maaskari wetu hawajafika, hawatoshi, lakini wananchi wa Tanzania wamesimama.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii mbele ya Bunge lako Tukufu kumshukuru kila askari wa wanyamapori, kumshukuru kila askari ambaye wakati sisi tumelala usiku wa manane amekuwa katika lindo, wale ambao wameumia tukaweza kuwapelekea aidha ndege au magari kuokoa maisha yao, kwa niaba ya Serikali nzima na kwa niaba ya Wabunge wote tulioko hapa, naomba wafahamu kwamba tuko pamoja nao na ndiyo maana tumeamua

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kuchukua uamuzi wa makusudi, uamuzi ambao Serikali imeuchukua, umechukua miaka sita tangu 2009 tumeweza kuanzisha TAWA. Mamlaka hii ya Wanyamapori Tanzania ndiyo inakwenda kuwa suluhisho la mambo mengi ambayo yametokea. Nilisikia Waheshimiwa walizungumzia na Mheshimiwa Msigwa na Mheshimiwa Lembeli katika hotuba yake alizungumzia juu ya kuwa na mfumo wezeshi, mfumo thabiti ambao utaweza kutusaidia kulinda wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka hii tunapokwenda kuanza sasa hivi rasmi baada ya kusainiwa, itakuwa ni suluhisho kubwa sana la muda mrefu la kuweza kuhakikisha kwamba tunawalinda wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo, dada yangu Magdalena Sakaya aliongea, tunaita kwa *emotions*, kwa hiyo nafikiri ni heshima kidogo nimjibu na nimitake radhi, unajua wakati mwingine mwanadamu unaghafilika kwa sababu ya kile ulichokisikia. Wanasema katika maisha yetu, maneno, ulimi ni kiungo kidogo, lakini matatizo yake ni makubwa. Unaweza ukautumia ulimi ukampelekea Mheshimiwa Mbunge habari, lakini ile habari akaghafilika kwa sababu sisi Waheshimiwa wote Wabunge tunaishi kwa habari ambazo tunazitumia. Kwa kweli sina neno lolote la kuweza kumlaumu, lakini ningependa nitumie nafasi fupi tu kumjibu yale ambayo sijayajibu.

Mheshimiwa Spika, moja Mheshimiwa Magdalena nataka tu niseme, nirudie tu kwamba, hakuna wafanyakazi au watumishi ambao Serikali imewafukuza wala kuwafedhehesha na hilo limeripotwa vibaya na wale walioripoti wanajua wenyewe, hawakuwa na nia njema.

Mheshimiwa Spika, la pili, amezungumzia suala ambalo limejitokeza sana, Kamati ya Bunge ya Mheshimiwa Lembeli ambayo tulikutana nayo Dar es Salaam ililileta hili jambo la mpaka wa Bologonja na baadaye likaendelea kupita katika vyombo vingi vya habari kama ni tatizo kubwa kweli kweli, lakini tukaipa majibu na Kamati ikaridhika.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii Mheshimiwa Meghji alilielezea sana hili suala, Waheshimiwa Wabunge wengi kwa sababu ya muda sitaweza kulirudia tena, lakini kupitia kwako Mheshimiwa Magdalena Sakaya nilijibu kama ifuatavyo:-

Katika vikao vya kawaida vya majadiliano vya Mawaziri wa Afrika Mashariki, kikao ambacho kiliitishwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki chini ya usimamizi wa Wizara yetu inayosimamia masuala ya Afrika Mashariki, tulikutana mimi, Waziri wa Maliasili wa Tanzania, mwenzangu kutoka Kenya, mwenzangu kutoka Rwanda na mwenzangu kutoka Uganda kuzungumzia mambo yanayotusibu.

Mheshimiwa Spika, katika kuzungumzia, moja ya jambo ambalo lilikuja ni suala la mpaka wa Bologonja. Wenzetu Wakenya wakaja na hoja inayosema sisi tunaomba kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki ifanyike *independent study* tuone kama huu mpaka wa Bologonja una manufaa kwa Taifa zima kwa maana ya Afrika Mashariki au hauna na ambacho walikuwa wanasema wenzetu Wakenya ilikuwa ni kwamba turuhusu watu waweze kuingia Bologonja waende Kenya na waweze kuingia Bologonja waende Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika mazungumzo ya kwanza na hili nilisema, sisi tulisema moja, hatutafanya jambo lolote bila kuwa na *study*. Lakini pili naomba watu wafahamu kwamba haiwezekani Waziri wa Maliasili na Utalii akaamka asubuhi saa nne wakati anakunywa kahawa akasema mpaka wa Bologonja nimeufungua. Ni *system* ambayo lazima ifanyike Kiserikali, ni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

system ambayo lazima iende katika Kamati yetu ya Bunge, ni system ambayo lazima Bunge litaarifiwe kwamba linatokea.

Sasa kwa sababu vyombo vya habari vile ambavyo vilikuwa vinapotosha habari kila siku viliuandika, baadaye ikaonekana kwamba Nyalandu amekaa anataka kufungua Bologonja. Tulichokisema na ambacho tumekisimamia katika vikao vya Kamati ya Bunge, hatutafungua Bologonja kwa sababu kinachoitwa *status quo* inabadilika. Labda tupate jambo lingine ambalo litakuwa na ushawishi mkubwa ambao utakubalika ndani ya Bunge hili, ndiyo hatua hiyo inaweza ikatokea. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba hilo niliweke kama lilivyo na niwahakikishie siyo tu Waheshimiwa Wabunge walioko hapa, lakini wananchi wote kwamba Serikali ya Tanzania haijabadilisha kabisa msimamo wake juu ya mpaka wa Bologonja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja aliizungumzia Mheshimiwa ya kurefusha muda wa uwindaji. Hili suala ni la sayansi. Tunapambana na ujangili kupita kipindi chochote kile katika historia, kinachotokea Hifadhi za Taifa (TANAPA) zinasimamia ukubwa wa eneo wa kilomita za mraba 57,000; Mamlaka ya Ngorongoro inasimamia kilomita za mraba 8,500 tu. Eneo lote nchi nzima takriban kilomita za mraba 200,000 ambayo ni sawasawa na Mataifa ya Rwanda, Uganda na Burundi ukiyachanganya, bado ni eneo kubwa sana kwa sababu tunao askari wa wanyamapori wasiozidi 1000 hadi sasa hivi, wale wanaosimamia eneo hili peke yake nikiwatoa wa Ngorongoro na TANAPA, tunayo mahitaji makubwa ya rasilimali watu, rasilimali magari.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo yaligawiwa kwa uwindaji katika utaratibu ambao umebadilika mara nyingi, maana wameenda miezi tisa, wakarudi miezi sita, ni kwamba kila baada ya miezi sita mambo mawili yanatokea. Moja, katika kipindi cha miezi sita wanaingia wawindaji wakiwa wamebeba bunduki zao, katika kipindi kifupi sana wanaua wanyama wengi na wanyama wengi wameanza kubadilisha tabia. Tabia tu za wanyama zinaanza kubadilika kwa sababu wanajua hii miezi sita ni ya mauaji, wanakwenda wanauawa wengi kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, baada ya ile miezi sita, Makampuni haya yote ya Uwindaji yanafunga virago yanaondoka, anayeingia ni mtu anayeitwa *poacher*, na hawa majangiri hawana cha *quotas* wala hawana cha nini, wamekwenda kufyeka wanyama katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, azimio ambalo nililitoa, nimeagiza wawindaji wote; moja, hakuna mwindaji aliyepewa kitalu anayeruhusiwa kuvunja kambi yake na tutampima kwa kiwango gani maaskari wake wa kuzuia ujangili wanaendelea kuwepo mwaka mzima. Mbili, hakuna mwindaji ambaye anaruhusiwa kuwinda zaidi ya *quota* ile aliyopewa, ndiyo *concern* kubwa sana ambayo dada yangu hapa alikuwa nayo. Kama alipewa *quota* ya wanyama 15 haibadiliki hiyo *quota* ya wanyama 15 na ili tuondoe tishio la wanyama kuuawa kwa muda mfupi, hii miezi tisa anaruhusiwa kwa *quota* ile ile ambayo amepewa na hili jambo litatuhakikishia mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na uwepo wa ulinzi wa wanyamapori kama ambavyo Idara, TANAPA na Ngorongoro wanavyofanya nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, hoja kwamba Waziri Nyalandu anarefusha vitalu miaka mitano hadi miaka 15. Habari hizi zinatokana na kitu tunachokiita umbeya, yaani majadiliano mnayojadili pale, kwa sababu urefu wa vitalu umetokana na Sheria ya Bunge, haiwezekani kabisa mtu mmoja akatunga sheria nyingine kule halafu ikatangazwa katika vyombo vya habari. Naomba hawa watu wanaoandika hizi habari ambazo zinasononesha mioyo ya watu, halafu zinachukuliwa zinakuwa kama habari za ukweli. Moja naomba mikono yao ione aibu kushika

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kalamu iliyojaa wino na kuandika uongo. Mbili, wengi wa wale watu, habari hizi nilizokuwa ninazisoma zilikuwa ni za pale pale ndani tu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa amesema Nyalandu akaenda Afrika Kusini. Afrika Kusini nilikwenda nilitumwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenda Afrika Kusini. Kulikuwa na ukweli aliosema Mheshimiwa kama ule wa Adam na Hawa, akaambiwa ukila tunda hili katika ule mti utajua mema na mabaya, hilo lilikuwa ni kweli, lakini shetani akamalizia akamwambia utafanana na Mungu, huo ulikuwa ni uongo.

Sasa hili la Nyalandu kwenda Afrika Kusini lilikuwa ni la kweli kwa sababu nilitumwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenda kuwasikiliza Bodi ya Kimataifa ya *African Park Networks*. Bodi hii iko duniani kote, wanafanya kazi katika nchi jirani ya Rwanda, wanafanya kazi katika nchi ya Afrika ya Kati, wamefanya kazi katika nchi ya Malawi. Walikwenda kunijulisha juu ya mfumo wao. Halafu hapakuwa na mazungumzo kabisa juu ya *National Park system*. Waongo wote sehemu yao ni katika ziwa liwakalo kwa kiberiti. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mazungumzo haya yalikuwa ni mazungumzo ya uwezekano wa kushirikiana na *African Parks* na wala siyo uamuzi, tuangalie *system* walizozifanya na hata hapa nilipo nimewakaribisha baadhi ya Wabunge wa Kamati yangu waende Rwanda namtuma Naibu Waziri aende Malawi, tunatuma baadhi ya wataalam waende Ethiopia, waangalie mfumo huo ulifankiwa kiasi gani, kwa sababu tumezungumza ya Ulaya wanatoa fedha kwenye *African Parks*, tumezungumza na Benki ya Dunia wanatoa fedha katika *African Parks*, lakini wale wanasaidia mapori yote ambayo yameshindikana kuendeshwa, wanasaidia mapori yote ambayo yamemalizwa na majangili.

Mheshimiwa Spika, kilichotokea ambacho kinaendelea na ambacho nitakifanya, moja tutahakikisha tunaujua ukweli juu ya hili suala *African Parks*. Ukweli ule utatuweka huru tutaamua nchi hii tutaamua Ushirikiano na *African Parks* kuendesha baadhi ya Mapori Tengefu na baadhi ya misitu ambayo tumeshindwa kuiendesha au lah! Lakini ambayo walikuwa wanasema watu tuko kwenye vikao, safari bado sijafika, nilipofika mimi Johannesburg nilipotua tu, kulikuwa na gazeti naomba nisilitaje limeandikwa Nyalandu na Lembeli wanakwenda kuuza Katavi, waongo wote ninaomba nisimalizie.

Mheshimiwa Spika, hoja ya dada yangu pale na yenyewe imetoka kule ndani, lakini naomba nichukue nafasi kujibu kwamba, Nyalandu huyu sasa anaongeza muda wa watu kulipia vitalu, watu hawa walikuwa wanamaliza kulipia vitalu mwezi wa tatu na vile vitalu tunavirudisha.

Mheshimiwa Spika, nimrudishe Mheshimiwa Magdalena nyuma kidogo, amesema kwamba Nyalandu huyu pia ana mpango wa kuwapa vitalu wageni, naomba niseme kilichotokea, kilichotokea ni kwamba vitalu vingi vimerudishwa, vitalu vingi ambavyo tuliwapa wazawa kwa nia njema vimerudishwa, wameshindwa kuviendesha.

Mheshimiwa Spika, vitalu vile vilikuwa vinaendelea kurudishwa na ule mwezi wa Tatu ningekuwa ngangari nikasema sikubali kuwaongezea muda ambao tungewanyang'anya walikuwa ni Watanzania watupu. Uamuzi ule ulizingatia Sera ya Chama cha Mapinduzi ya kuhakikisha tunawawezesha Watanzania kiuchumi. Uamuzi ule ulikuwa siyo wa kuwasamehe wao kutokulipa kodi ya Serikali, uamuzi ule ulikuwa ni wa kuwaongeza muda. Watu wameshika kalamu, Nyalandu leo amevaa tai ya rangi gani, haya hii leo ni ya zambarau.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, uamuzi ule ulikuwa sahihi na umesaidia makampuni mengi ya wazawa wakamudu kulipa tozo zao na kuanzia mwezi wa Saba wataendelea na hili ambalo Mheshimiwa alilielezea sana kuwa labda nani anawatuma, hili suala la *Green Miles* na *Wengert Windrose*, Mheshimiwa Msigwa amelielezea tofauti na dada yangu Magdalena.

Mheshimiwa Msigwa amelizungumzia kwamba *Green Miles* wanafanya uwindaji bila ya kufuata Sheria na amewasilisha hoja yake na amewasilisha vielelezo. Nikuhakikishie kwamba kuanzia kesho asubuhi vile vielelezo nitavichukua na kuwataka wataalam wangu waviangalie, tubainishe ukweli wa hilo jambo na kwa sababu Mheshimiwa Msigwa umetoka CHADEMA haina maana kila unachotuambia sisi tuone kwamba hakifai, lakini tutavifanyia kazi vile vielelezo na kuhakikisha kuwa Bunge hili tutalijulisha juu ya ukweli wa kilichosemwa.

Mheshimiwa Spika, alichokisema Mheshimiwa Magdalena ni kwamba kuna hawa watu wengine wanaitwa Mwiba na *Wengert Windrose*. Nichukue nafasi hii kusema utaratibu wetu wa kawaida, jambo linapokuwa katika Mahakama hatulijadili katika Bunge letu na ile kesi itatajwa tarehe 9/6 na natumaini kuwa busara itatumika ki- *adiministratively* mimi na watu wangu kuhakikisha huu mgogoro kwa maslahi ya nchi wawe wameumaliza kabla ya kufika mwisho wa mwezi wa Sita ili mwezi wa Saba unapoanza basi waweze kuendelea na kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee na mengine yaliyojiri. Katika haya tumezungumzia kuhusu suala la ujangili na limezungumzwa na watu wengi, lakini niseme kuanzisha Mamlaka litakuwa ni suluhisho litakaloitoa nchi hii katika tatizo la mfumo ambapo Mamlaka yale yote yaliyokuwa Wizarani, sasa yanahama yanakwenda kwenye Bodi ya Wananchi itakayosimamia mamlaka hii kama vile *TANAPA* ilivyofanikiwa na mamlaka zingine.

Mheshimiwa Spika, ninapozungumzia hapo tutaunda Bodi mpya na nimekumbuka suala la Bodi litajirudia. Naomba nikuhakikishie tena, tulisema hapo nyuma, nakumbuka nilijibu swali la nyongeza kuhusu ni lini tungekamilisha kuteua Bodi. Naomba nikuhakikishie taratibu zote za Wizara tumezikamilisha, Bodi zile zimeteuliwa na Bodi zile zinakwenda katika utaratibu wa kawaida wa kupekuliwa na wakati wowote Mamlaka zinazohusika zikituletea jina la Mwenyekiti, sisi tutakuwa tayari kuzitangaza na naamini kwamba katika mwaka huu wa fedha, nitakuwa na Bodi zote ambazo tunategemea ziendeshe haya mashirika.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya mipaka ameleezea vizuri Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa vyovyote vile kwa sababu ya muda tulionao hatutaweza kuelezea kila mpaka, lakini kuna aina mbili; kuna ile Tume ambayo imeundwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Kikosi Kazi kinaendelea na kazi tutapata taarifa yake. Tutahakikisha kama tulivyoanza na kama nilivyomtuma Mheshimiwa Naibu Waziri wangu juzi katika baadhi ya maeneo, tutahakikisha kuwa hatutaonea haya migogoro, tutafanya maamuzi ambayo yanahitaji kufanyika na naomba Bunge lako lituamini na naomba msaada wa Waheshimiwa Wabunge kwa kadri itakavyowezekana ili tuweze kujinasua na migogoro ambayo siyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, moja ya jambo ambalo nimeliagiza lifanyike; nimeagiza katika Wizara yangu tuangalie mifumo yote ya Mapori Tengefu, tuangalie ni Mapori Tengefu yapi bado yana hadhi ya kuendelea kuwa Mapori Tengefu na Mapori Tengefu mengine tunaweza tukafikiria kuya-release ili yatumike katika sehemu za ufugaji.

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji wa wananchi. Hili tumelizungumzia WMAs ambazo zinaendelea kuanzishwa, tutahakikisha kwamba tuna *fast track*, uanzishwaji wa hizi WMAs na nitahakikisha kwamba tunaondoa *bureaucracy* ambazo siyo za lazima na ni matumaini yangu kuwa, Idara hii ya Wanyamapori ambayo sasa na naomba nirudie, shughuli zote za Idara ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Wanyamapori sasa zinakwenda kuchukuliwa na Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania na Idara itaendelea kubaki kushughulikia Sera na vitu vinavyofanana na hivyo.

Mheshimiwa Spika, wanyamapori wakali na waharibifu limekuwa ni tatizo kubwa, lakini hapa naomba niseme na Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamelizungumzia hili suala, tunaipitia hii Kanuni, Kanuni ambayo ilikuwa inazingatia juu ya kifuta jasho na fidia; moja, imepitwa na wakati, lakini tuangalie uhalisia wa wakati huu na changamoto tulizo nazo.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie Wabunge wote na wananchi wote ambao wamewakilishwa hapa, Serikali itakuwa sikivu katika hili suala na tutalifanyia kazi kwa muda mfupi ujao. Kulikuwa na hili la ucheleweshaji wa mgao wa mapato wa WMAs nimefanya mazungumzo na viongozi wa WMAs kadhaa. Moja ya mazungumzo niliyoyafanya ilikuwa ni kukutana na Halmashauri nzima ya Wilaya ya Ngorongoro, walikuja kuanzia Mwenyekiti wakiongozwa na Mheshimiwa DC na Waheshimiwa Madiwani. Tumezungumzia hili suala la mapato na asilimia ya mgao ambao umechelewa sana, natumaini hili katika mwaka wa fedha unaokuja halitakuwa tatizo. Tutahakikisha kwamba tunalitatuwa kwa sababu liko chini ya uwezo wetu na liko chini ya uwezo wa watendaji wangu.

Mheshimiwa Spika, hili la Bologonja limejitokeza mara nyingi nitaliacha.

Mheshimiwa Spika, utangazaji na uboreshaji wa vituo vya utalii, makumbusho ya Taifa na vituo vya Mikutano ya Kimataifa. Kama tulivyosema, tunayo kazi kubwa ya kuutangaza Utalii wa nchi na hatua ambazo tunazichukua sasa hivi, moja ni kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa *rebranded* kama nchi, Tanzania inakuwa *rebranded* na Watanzania wenyewe watajiona katika kioo na hii *rebranding* ni lazima ifanyike kwa kuzingatia *standards* za juu sana za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hatua hii inaendelea, bajeti ya *TTB* tuliyonayo ni ndogo, lakini tunahakikisha kuwa bajeti zote zilizoko *TANAPA* na Ngorongoro zinazohusiana na utangazaji wa Utalii zote zinashirikiana na zile namba zinasomeka kwa sababu nchi zingine kama Kenya, wana *Kenya Tourist Board* lakini hawana *TANAPA* na wala hawana Ngorongoro na wala hawana mamlaka nyingine ya wanyamapori wana kitu kingine kinachosimamia wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni kwamba, tutahuisha hii mifumo ili Watanzania waweze kupata namba halisi ya fedha ambazo tutazitumia na tunaendelea kuzitumia kwa ajili ya Utangazaji. Hili suala limekuwa palepale ni sawa na ambavyo watu wengi wanafikiria kuwa Tanzania ina askari wa wanyamapori mia tisa tu, lakini kumbe tunazungumzia wa Idara moja ya Wanyamapori na hatujazungumzia wale wa *TANAPA*, wa Ngorongoro na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie kwamba, tutajitahidi na tutaendelea kwa kadri inavyowezekana kutangaza Taifa letu na kama nilivyosema kwenye *speech* yangu tunategemea *video* ambayo inaandaliwa ya *kui-rebrand* Tanzania itakapokuwa tayari na zenyewe zinashindanishwa, Mheshimiwa Rais ataizindua na Mheshimiwa Rais atakapoizindua rasmi itaingia katika vyombo mbalimbali vya habari.

Mheshimiwa Spika, kuna Mheshimiwa alitaja akasema kuwa *CNN International* inawafaikia tu Waafrika na nchi zingine. Niombe kumhakikishia kwamba sisi tunatangaza katika *CNN America* ambayo inawafikia Wamarekani, lakini pia tunatangaza kwenye *BBC World* ambayo inawafikia watu wengi kwa ujumla wake duniani.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua umuhimu wa kuweka Maafisa Utalii katika Balozi zetu na hasa katika masoko makuu kama Uingereza, Marekani, Italia, Ujerumani, Canada na kwingineko. Wizara imechukua ushauri huu, lakini tunaendelea kuangalia na katika mfumo mzima wa kuhuisha Tanzania *Tourist Board*, muda siyo mrefu tutaleta Muswada wa Sheria wa kuifanya Tanzania *Tourist Board* iwe ni Tanzania *Tourist Authority* kama ambavyo Mamlaka hizi ziko nchi zote duniani ili tuweze kujengea nguvu na uwezo wa kisheria, uwezo wa kimapato, lakini pia uwezo wa kuweza kutekeleza mzigo huu mkubwa ambao tunawatwisha. Ni matumaini yangu kwamba, Bodi ya Utalii kwa sasa kwa kadri ya uwezo na kwa kuzingatia hali tuliyo nayo, itafanya kazi kwa uadilifu na tutahakikisha kwamba, nchi yetu haitaendelea kuwa nyuma katika suala zima la utangazaji wa utalii.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja ya gawio la fedha za Mlima Kilimanjaro. Moja ningependa niseme Shirika letu la TANAPA limekuwa likichangia maendeleo ya vijiji kupitia huu mpango wa ujirani mwema. Kutokana na kupanda Mlima Kilimanjaro zaidi ya bilioni 8.8 ambazo tunaziita *indirect* zimekuwa zikiingia katika ajira, katika mauzo, katika vyakula, vinywaji, malazi na usafiri wa watalii katika eneo linalozunguka mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia niseme kwamba, Wizara inaendelea kufanyia kazi suala la uanzishwaji wa Mfuko wa Mlima Kilimanjaro. Niseme tu hapa, nilikutana na Waheshimiwa Wabunge wote wa Kilimanjaro na Serikali ilifanya hatua kadhaa, moja tuliandaa hadidu za rejea (*Terms of Reference*) kwa ajili ya huu Mfuko zimekamilika. Pili, Serikali iliandaa mkutano wa kwanza ambao ulikuwa ni lazima uwe ni mkutano wa mashauriano ili tukubaliane juu ya zile hadidu za rejea katika mfumo wa ule Mfuko.

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa kwanza ulishindikana kwa sababu Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro na Ma-RAS na viongozi wengine hawakupatikana na mimi nilitaka kwa kweli wapatikane wote. Mkutano wa pili pia ulishindikana kwa sababu Waheshimiwa Wabunge walikuwa katika Bunge la Katiba.

Kwa hiyo, tukasema badala ya kulazimisha mkutano bila ya kuwa na wadau ningependa huu mkutano bado ufanyike, lakini kwa kweli tuwe na wadau wote ili hili jambo tunapoliamua kwenda mbele, tuwe tumeliamua kwa uwazi mpana zaidi na niliwasiliana na Mheshimiwa Mwanri kwa upande wa Wabunge wa Kilimanjaro na Mheshimiwa Mbowe ili waweze kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge wengine.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya masuala ambayo ni masuala mtambuka kwa ridhaa ya muda ulio mbele yetu. Kulikuwa na hoja juu ya ajira kwa vijana wanaozunguka Hifadhi lakini vile vile kwa vijana wanaozunguka Mlima Kilimanjaro. Naomba niseme ni jambo ambalo ni la kistaarabu, lakini ni la kawaida kwa makampuni yote ambayo yanafanya kazi katika haya maeneo kuhakikisha kuwa wanakuwa sehemu ya ujirani mwema ikiwa ni pamoja na kutoa ajira kwa vijana wanaozunguka katika hayo maeneo.

Vile vile jitihada mbalimbali zitafanyika ili kuzingatia katika ajira ambazo ni rasmi na watu wanaozunguka yale maeneo wanakumbukwa kwa sababu tunawategemea sana kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wengi kwamba, moto unapowaka Kilimanjaro tunawategemea majirani wasimame na tunaamini kwamba tutaendelea kwa kadri inavyowezekana bila ya kuvunja Sheria yoyote ya nchi, kuhakikisha kuwa ujirani mwema unaendelea kudumishwa.

Mheshimiwa Spika, kuna suala liliibuliwa juu ya motisha kwa Watumishi. Wizara imekuwa ikitoa motisha kwa Watumishi wake labda suala la kujiuliza ni kwamba, je, motisha hii ni kubwa? Jibu hapana! Tunaendelea kuboresha. Tulichokifanya katika Wizara yetu tumeagiza kwamba,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

stahili zote ambazo Watumishi wanastahili ikiwa ni pamoja na maaskari wetu wa wanyamapori walio mbali ziwafikie haraka.

Mheshimiwa Spika, moja ya kitu ambacho niliagiza mapema sana ilikuwa, siyo tu tuligawa Selous Game Reserve katika Kanda nane, lakini tulihakikisha kwamba, fedha zinazotoka za mgawo kwenda Selous na Selous tunauita ni mradi, ziende moja kwa moja kwa Wakuu wa Kanda ili ziweze kuwafikia maaskari na kuweza kufanya kazi muhimu tunazozifanya za doria.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la uhaba wa Watumishi katika Hifadhi. Ni jambo ambalo tumelielezea vizuri sana na mchakato huu tunaendelea nao na Wizara ina mchakato wa kuajiri Wahifadhi 2,000 kwa kipindi cha miaka minne kuanzia 2013, 2015 hadi 2016 na kama nilivyosema kufikia mwisho wa mwezi ujao, tutakuwa tumefanikisha kuajiri askari wa wanyamapori 430 na tunategemea kuajiri wengine 500 hadi kufikia Desemba 2014, lakini kubwa zaidi ajira ya maaskari wa wanyamapori kuanzia sasa hivi na baada ya mwezi wa Saba itakuwa chini ya mamlaka tatu chini ya mamlaka ya Ngorongoro moja kwa moja, chini ya mamlaka ya TANAPA moja kwa moja na chini ya Mamlaka mpya ya Wanyamapori moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, hili la uteuzi wa Bodi ya Mashirika ya Umma nimelisemea.

Mheshimiwa Spika, naomba baada ya kuyasema hayo na naomba baada ya mambo yote ambayo yamezungumzwa hapa ambayo mengine kwa kweli unaona kabisa yana *emotions*, ningepomba Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili, Wabunge wa Vyama vyote vya Siasa, kwa suala la Uhifadhi ningepomba tuwe pamoja.

Mheshimiwa Spika, naomba wakati tunao maaskari wetu ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu na ningepomba wakati Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete katika jitihada zake ameifanya dunia kwa mara nyingine tena kutazama Uhifadhi kwamba ni jambo la muhimu na waanze kusaidia wakati ambao Umoja wa Mataifa kwa kumsikiliza Mheshimiwa Rais Dkt. Kikwete na baada ya mkutano wetu wa Kimataifa wa Dar es Salaam kwa mara ya kwanza wameanzisha Mfuko, Mfuko ambao ni wa *Basket Fund* kwa ajili ya uhifadhi wa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, jambo hili limetuletea heshima, lakini naomba sana katika yale tunayoyafanya na katika yale tunayoyasema, tuhakikishe kwamba kuna watu ambao wametoa maisha yao kwa ajili ya wanyamapori na tuhakikishe kuwa, kuna watu ambao tutahitaji kwa kauli zetu na kwa mienendo yetu tuwasaidie na nategea kuwa Bunge hili litakuwa ni eneo ambalo tutaendelea kujadiliana na sisi katika Wizara tuko wazi kujadiliana juu ya hoja hizi ambazo zinapingana.

Mheshimiwa Spika, hizi hoja zinajenga, hizi hoja zinawafanya siyo tu Watumishi wangu katika Wizara ya Maliasili na Utalii wajitahidi zaidi, lakini zinatufanya kama Taifa tuwe imara zaidi. Ningepomba tuendeleo na haya majadiliano, nihakikishe kwamba, hoja za Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamezisema hapa tumezisikia, tumezirekodi na kwa kadri itakavyowezekana nitaagiza kila Mheshimiwa Mbunge tumwandike kwa maandishi, tukimjulisha juu ya jibu sahihi la hoja yake.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kuchukua nafasi hii kwa sababu ya umuhimu wa haya mambo ambayo yametokea niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa maandishi na naomba kuchukua nafasi hii kuwatambua kama ifuatavyo:-

SPIKA: Nataka ueleze kuhusu wafadhili wanaotaka kuleta faru, halafu sijui wanalipiwa kodi, suala hili mmelifanyaje? (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa hoja hiyo. Moja, ni kweli tumekuwa na changamoto, lakini ni changamoto ya kimfumo, ni changamoto ya Kisheria na Sheria ambazo tumezipitisha sisi wenyewe hapa Bungeni ambazo zinasimamiwa na Mamlaka tofauti tofauti. Kabla sijasema hili la faru, niseme tu kwamba, katika wakati fulani sisi tulikuwa na silaha, Kamati ya Mheshimiwa Lembeli imelielezea vizuri sana hapa, silaha za AK47 ambazo tulikaa nazo takribani mwaka mmoja na nusu zikiwa zinadaiwa kodi.

Mheshimiwa Spika, lakini na hawa faru ambao walikuja changamoto ya kodi ilitokea na kwakweli sisi katika Serikali tumeliona hilo na tumeanza mazungumzo na wenzetu katika Wizara ya Fedha kuangalia ni jinsi gani, na jinsi gani bora tutakuwa na mfumo utakaotoa kipaumbele katika Sekta hii ya Uhifadhi ili mgongano huu ambao ulitokea usitokee tena.

Mheshimiwa Spika, nakiri kwamba mgongano huo ulitokea lakini Serikali imechukua hatua madhubuti za kuhakikisha kwamba jambo hili kwa namna moja au nyingine litakuwa na mwongozo ambao ni endelevu na halitajitokeza tena.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba sasa nichukue nafasi hii kwakweli kuwashukuru wote ambao mlischangia kwa maandishi na kwa maneno.

Nimshukuru sana Mheshimiwa Peter Msolla, Mbunge wa Kilolo, Mheshimiwa Lukuvi, Mheshimiwa Charles Mwajjage, Mheshimiwa Ali Hamis Seif na Mheshimiwa Suleiman. Hawa ni Waheshimiwa Wabunge ambao walichangia kwa maandishi.

Wale ambao nimewashukuru, basi nimeshawashukuru, niwashukuru na wengine wote ambao kwa kweli sitapata nafasi ya kuwasema na kuwataja lakini naomba mtambue kwamba mchango wenu tunautambua.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba sasa kutoa hoja.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja hiyo imeungwa mkono, tuendeleo.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 69 - WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukubaliane, msiniletee barua hapa, mimi na-*concentrate* na mambo ya hapa. Hiki ndiyo kipindi kikubwa sana cha maamuzi. Mkiniletea barua, nafanya nazo nini sasa? Kwa hiyo, ukileta naweka kwenye *dustbin*. Kwa hiyo, msiniletee. Wale ambao wanaotakiwa kuzungumza kwenye mishahara ya Waziri huwa wanazungumza na Vyama vyao, huwa wananisaidia kabla, msiniletee hapa, mnanichanganya. Kwa hiyo, tumekubaliane, msiniletee barua. (*Kicheko*)

Kifungu 1001 Admin. and HR Mgt. Shs. 5,494,610,000/=

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mrema!

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Spika, nasikitika sana Mheshimiwa Waziri nilikupa hoja yangu na ukaniandikia hapa, Mheshimiwa Mrema tutakujibu vizuri wakati wa hitimisho. Hukunijibu! Lakini unaweza ukanijibu sasa. Kata zangu zilizoko Vunjo; Kata ya Kirua magharibi, Kata ya Kirua Mashariki anakotoka Mheshimiwa Mbatia, Kilema Kaskazini, Marangu Magharibi, Marangu Mashariki, Mwika Kaskazini, Mamba Kaskazini, zote zinapakana na Msitu wa Kilimanjaro.

Tangu utawala wa kichifu wa Mangi Mkuu wa Wachaga na hata wakati wa Wakoloni, tulipewa wananchi walio karibu na msitu ule, walipewa kipande cha nusu maili. Lengo lilikuwa wanachi wale watumike kulinda msitu. Kweli tulifanya kazi hiyo vizuri, wanawake waliruhusiwa kwenda kukata majani ya ngombe, kuokota kuni zilizokauka na mambo madogo madogo na kweli walitunza msitu ule wa ukanda wa nusu maili.

Baadaye tukaporwa, tukanyanganywa tukaambiwa kuna chombo chenye uwezo wa kulinda eneo lile. Naomba tuambatane na Mheshimiwa nikuonyeshe eneo lile, halina miti. Lenye miti ni yale maeneo tuliyokubaliana na Askofu wetu mmoja mashuhuri yupo pale, ambaye tunaotsha miti katika eneo lile. Wananchi wanajitolea wapenda msitu wao, wanataka maji, wanataka mifereji iwe na maji wakati wote.

Sasa naomba kujua sera ya Wizara yako, lile eneo la nusu maili kwanini mnatupora? Kwanini mnatunyang'anya? Kwanini hamtaki wananchi walinde eneo lile, wapande miti, watunze mazingira? Nye mnaamini kabisa askari wenu wanaweza kutunza eneo lile kuliko wale wapigakura wangu wa Vunjo? Naomba unijibu, tufanyeje, Mheshimiwa Waziri?

SPIKA: Sasa mkifuatana nao itabidi tuiache hiyo hoja, au vipi? Bado unaendelea kuhitaji mfuatane leo? Mheshimiwa Waziri! (Kicheko)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la nusu maili katika Kilimanjaro lina historia fupi tu kama ifuatavyo:-

Moja, kama alivyosema Mheshimiwa Mrema, hili eneo lilikuwa chini ya wananchi. Katika wakati tofauti tofauti, Halmashauri zote za Wilaya zinazozunguka mlima Kilimanjaro, ziliomba Serikali kutokana na uharibifu mkubwa uliokuwa unatokea katika hilo eneo, hilo eneo likabidhiwe TANAPA. Taratibu zikafanyika, hilo eneo likakabidhiwa na TANAPA na GN ikaandikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye kukawa na mazungumzo mengine kwamba kwa kweli hilo eneo la nusu maili limekuwa la kihistoria na lilikuwa linawafaidisha wananchi; Serikali iangalie uwezekano wa matumizi endelevu ya nusu maili ya akina mama kuingia kuokota kuni na shughuli ambazo kwa kweli haziathiri eneo hasa la uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, naomba nilijulishe Bunge lako Tukufu kwamba hatua hizo zinaendelea. Niwataarifu wananchi wa Kilimanjaro kupitia Mheshimiwa Mrema kwamba hapa tulipo utaratibu ambao tumeufanya ni kuhakikisha kwamba mpango wa jinsi ambavyo tutawaruhusu hao wananchi waingie katika nusu maili, siku na saa ambayo tutawaruhusu waingie ili sisi na Maaskari wetu katika TANAPA tuweze kuwa na *control* na tuweze kupambana na majangili ambao wangeweza kujifanya na wao wanaingia kwenye nusu maili kumbe wanaenda kuua wanyama wetu, utaratibu ule unafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mrema kwamba RCC chini ya Mkuu wa Mkoa wanajiandaa kukaa wakati wowote ili waupitie ule utaratibu uje, Serikali na mimi nitawakubalia.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Nyalandu. Uendeleee!

SPIKA: Mzee, tunafuata kanuni. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Msigwa!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika hotuba yangu ya mchango wangu wa asubuhi, nilizungumza kuhusu uendelezaji wa *Southern Circuit*. Kwa mfano, nilizungumzia Mbuga ya Ruaha kwamba ni kubwa kuliko mbuga zote, lakini utangazaji wake umekuwa chini. Siyo Ruaha tu, tunaangalia nyanda za juu kusini pamoja na Katavi yaani Iringa, Njombe na Mbeya; Maua kule Kitulo na maeneo kadha wa kadha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaona majibu ya Waziri katika majibu yake, ameeleza ni mikakati gani ya msingi ambayo utalii ukitangazwa kwa nguvu na maeneo yale yakaboreshwa wananchi wa maeneo hayo kwa mfano Iringa Mjini ajira zitaongezeka kwenye Mahoteli, wataua vitu vyao? Kwa hiyo, wale akina mama pale Mitaani ambao hawana kazi na vijana ambao hawana ajira tukitangaza kama ambavyo *Northern Circuit* imetangazwa, hayo maeneo yatakata fursa hizo, yaani Mikoa ya kwa mfano ya Mbeya na Iringa na katika mchango wa Mheshimiwa Sugu amezungumza vizuri. Ningeomba nipate ufafanuzi mzuri.

Vinginevyo kama sitapata ufafanuzi, kwa sababu kwa muda mrefu watu wa Kusini hatujatangazwa vizuri katika eneo hilo, nitakusudia kuondoa Shilingi. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mchungaji Msigwa kwamba moja ya hatua za makusudi zinafanywa na Serikali.

Tumefungua sasa uwanja wa Mbeya ambao ni uwanja wa Kimataifa na Serikali inasisitiza kwamba uwanja ule utaboreshwa zaidi, watu waweze kuanza kutoka Mbeya na kwenda kwenye Mataifa mengine duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la Mbeya linakuwa ni kitovu ama *epic centre* maana yake Ruaha inaanzia siyo mbali sana na Jiji la Mbeya na ni matumaini yangu kwamba sasa watu wanakwenda kwa *Fast Jet* au kwa *Precision Air*, watalii wengi inakuwa rahisi kwenda Ruaha kupitia moja kwa moja Mbeya. Vilevile kupitia ongezeko la ndege ambazo zinakuja katika uwanja wa Iringa na Iringa na Mbeya ndiyo maeneo mawili ambayo ndiyo langu kuu la kuingilia katika hifadhi kubwa kuliko zote Afrika, ya Ruaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba Serikali inatazama Hifadhi za Kusini zote, Hifadhi ya Ruaha ina idadi ya Tembo zaidi ya 20,000 ambayo ni sawa na idadi ya Tembo wote waliopo katika nchi ya Kenya. Ina umuhimu sana na Serikali itajitahidi kwa njia nyingi tofauti kuhakikisha kwamba tunai-promote. Ahsante.

MWENYEKITI: Si umeridhika jamani? Au!

MHE. MCH. PETER MSIGWA: Ndiyo Mheshimiwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Sasa unataka kufanyaje? Haya, toa Shilingi. Maana vinginevyo huruhusiwi kusema.

MHE. MCH. PETER MSIGWA: Mheshimiwa Spika, natoa Shilingi.

MWENYEKITI: Mh! Endelea!

MHE. MCH. PETER MSIGWA: Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, kwa muda mrefu sana hili tatizo limekuwa kubwa na vile vile katika maelezo yangu nilizungumza jinsi ambavyo wale wanaozungukwa na ile Mbuga ya *Ruaha National Park*, hawapati hata yale mahusiano mema.

Kwa hiyo, hata ile fursa ya kuwalinda wale wanyama inakuwa haipo. Kwa hiyo, kwa kitendo hicho Mheshimiwa Waziri ni kwamba tumekosa fursa za msingi kama mwenyewe ulivyokiri kwamba hii ni Mbuga kubwa kuliko zote katika nchi yetu na maeneo mengi katika bara la Afrika.

Kwa hiyo, mikakati tunayosema ni mikakati ambayo hairidhishi kiasi kwamba wananchi wa maeneo ya Iringa na Mbeya wamekuwa hawapati hizo fursa ambazo maeneo mengine wanayapata na huu ndiyo urithi pekee ambao Mungu ametupa. Umekiri mwenyewe kwamba katika maeneo hayo kuna tembo zaidi 20 ambao kwa namna moja au nyingine wananchi wa maeneo yale wamejitahidi sana kuwalinda hao tembo ambao mpaka sasa wamekuwepo.

Kwa hiyo, hujanipa mkakati ambao unajionyesha; labda ungesema umeshirikiana na Wizara ya Ujenzi kwamba tunapanua Uwanja wa Iringa ili ndege zishuke pale badala ya kwenda *Iringa National Park*, hujanipa mikakati hiyo kwamba unashirikiana vipi na ujenzi kupanua uwanja ule. Hujanipa mikakati ni namna gani unashirikiana na Mheshimwa Magufuli kutengeneza ile barabara ambayo hata watalii wakitua pale Iringa wanaweza kwenda kwenye Mbuga ya Ruaha? Sioni hiki kitu ambacho ni *tangible* ambacho naweza nikaridhika.

Kwa hiyo, kwa hoja hiyo nawaomba Wabunge wengine hasa wa nyanda za juu kusini, akina Lukuvi pamoja na kwamba ni Waziri, tusaidiane kuhakikisha tunaibana Wizara hii ili iweke mikakati muhimu kwa ajili ya kuinua utalii, nyanda za juu kusini hususan Ruaha ambayo ni Mbuga kubwa kwa muda mrefu imezalilishwa. Kwa hiyo, wananchi wangu wa Manispaa ya Iringa hawapati kipato kizuri. Walimu hawana mishahara, Madaktari, akina mama ntilie kwa sababu hatujatilia mkazo katika maeneo ya Manispaa ya Iringa na kwa ujumla muda wote.

Mheshimiwa Spika, naomba nipate majibu, na naomba pia uniunge mkono kwa sababu na wewe unatoka huko. *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwanza wale tembo ni 20 ama 20,000?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ni 20,000.

MWENYEKITI: Maana yake nilitaka kuogopa kabisa! Mimi nitakuunga mkono tu ilimradi ukikubali kurudisha Shilingi. *(Kicheko)*

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, nami pia namshawishi Mheshimiwa Msigwa kama siyo lazima sana hiyo Shilingi tutaomba uirudishie.

Nimhakikishie tu Mheshimiwa Msigwa kwamba kuna mambo ambayo yanafanyika, tumeweka bajeti kupitia *TANAPA*, hiyo ni kwaajili ya ku-improve barabara, *networks* ya barabara zetu zote.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Hiyo ni moja kwa moja, na itakuwa na *impact* kubwa pale Iringa kwa sababu Watalii wengi wanaruka kwa hizi ndege za *Coastal* na nyingine, wanakuja Iringa, halafu kutokea Iringa wanakwenda katika sehemu mbalimbali ya hiyo Mbuga ya Ruaha.

La pili kwa maana ya mahusiano na wananchi, Serikali inaendelea kuhakikisha kwamba hizi WMA's zilizo pale *MNABOMIPA* na hizi nyingine zinawezeshwa. Kilichotokea kwenye WMA's ni kwamba wananchi na *associations* za vijiji zimekuwa na *capacity* ndogo sana za kuweza kujua haki zao, mifumo ya Sheria na kadhalika.

Tunapenda kuwahakikishia kwamba tutaweka nguvu mpya kuhakikisha kwamba WMA's za eneo hili la Ruaha na za nchi nzima zinaangaliwa upya, zinawezeshwa ili ziweze kumudu hili suala la mahusiano, lakini la kuwawezesha wananchi kiuchumi kutokana na uwezo wa wao kuweza kujenga kambi za Kitalii, kuweza kuingia Mikataba ambayo ni endelevu ambayo ningependa sana Waheshimiwa Wabunge muione. Kwa sababu mikataba mingine ya WMA's kwakweli imeingwa, inawanyonya wananchi na ni mibaya.

Inafanyika huko huko katika maeneo ya Vijiji katika hiyo mifumo ya WMA. Kwa hiyo, nikuhakikishie tu kwamba tutangaza. Moja ya kitu ambacho tunakifikia, kama vile Serengeti ambayo imekuwa ni *brand* inayojitegemea, tunatazama ambayo Ruaha kwa sababu ni *giant* inaweza ikawa ni *brand* ambayo itaanza kusika katika masikio ya watu kwa hali ya kipekee kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hili jambo linaangaliwa tuna mkakati wa miaka mitano ya Utalii ambao umekuwa *developed*, unaonyesha pia ni namna gani *individual parks* kutokana na umarufu wake na umuhimu wake vinaweza kuwa *promoted alongside*, hii *idea* ya ku-rebrand nchi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa rudisha Shilingi. Sasa akijibu usiwe unarudi kwa mwenye hoja bwana! Tunakubaliana na wewe mia kwa mia, afadhali ungeanza zamani tungekuwa tumefika mbali! (*Makofi*)

MHE. PETER MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshimiwa yako narudisha Shilingi lakini mwakani nitakufuatilia kwelikweli kwa sababu ni king'ang'anizi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Anachokisema Mheshimiwa Msigwa, unajua Mheshimiwa Msigwa kipindi hiki amekuwa *very constructive*. Kwa maana hiyo, kwanini tumpinge? *He is very constructive* kwa kweli toka ameanza hili Bunge. Kwa hiyo, nasi tunaangana naye alivyosema.

Mheshimiwa Malocha.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Katika mchango wangu wa maandishi nilielezea namna ambavyo kumekuwa na ongezeko kubwa sana la mamba katika baadhi ya maziwa yetu na mito na nikatoa mfano wa Ziwa Rukwa na Mto Momba. Kwa bahati nzuri mwaka jana, 2013 niliulizwa swali kwa Waziri huyu huyu akiwa Naibu Waziri juu ya tatizo hili na akaahidi kutoa vibali vya kuwapunguza mamba.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji hajaeleza na katika maelezo yake hajatoa ufafanuzi wowote. labda nimpe taarifa, toka mwaka 2008 mpaka 2014 wananchi wapatao 21 wamekamatwa na Mamba na kuliwa na wananchi wanne wamejeruhiwa na ni vilema mpaka sasa hivi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Juzi tu kuna mzee mmoja anaitwa Mzee Edward Seme, mtoto wake amekamatwa na mamba na kwa hasira amechukua zana za kisasa na kumuua huyo mamba ambaye sasa hivi ana ngozi kule nyumbani kwake. Sasa kutokana na maelezo ya Waziri, sikubaliani naye na ninakusudia kushika Shilingi kama hatatoa ufafanuzi wa utatuzi juu ya jambo hili. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya Wizara kuwapa pole waliopata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie tu ndugu yangu Mheshimiwa Malocha kwamba ni kweli kuna sehemu tumezembea, lakini sisi kama Wizara nataka nimhakikishie tu kwamba safari hii tulifanyia kazi na ndani ya Bunge hili nitawapa Wataalamu wangu wataenda kulishughulikia jambo hili.

MWENYEKITI: Tumelewa? Kwa sababu ulisema unatoa Shilingi, Mheshimiwa Malocha!

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzembea katika kutoa maisha ya watu siyo jambo jema. Labda Mheshimiwa Waziri angenithibitishia baada ya Bunge hili, ni hatua zipi anazichukua au anaagiza nini kuhusu taratibu za kuwapunguza hao mamba? Vinginevyo, nashika Shilingi.

MWENYEKITI: Ndiyo maana nimekupa nafasi ya pili, kwa sababu umeshika Shilingi. Huruhusiwi kusema kwa mara ya pili *unless* umeshika Shilingi. Kwa hiyo, umeshatoa Shilingi, sasa unataka wakuhakikishie ni lini? Kwamba watafanya nini sijui.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Malocha kwamba jambo hili tutalishughulikia haraka iwezekanavyo. Naomba aturudishie Shilingi ili tuweze kufanya kazi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Malocha!

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali. (Makofi)

MWENYEKITI: Haya, tunaendelea na Mheshimiwa Zakia Meghji.

MHE. ZAKIA HAMDANI MEGHJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, langu lilikuwa la Bologonja. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyosema kwamba hatutafungua Bologonja na *status quo* haijabadilika. Lakini ningependa kusema kwamba, alivyosema juu ya suala la *independent study*, huu ni ujanja. Hii *Independent Study* imekuwa inazungumzwa miaka yote hiyo, huu ni ujanja wa upande wa Kenya. Kwa hiyo, tunasema kwamba kwa kweli ni kama vile kusema kitu hiki ni cheupe au kitu hiki ni cheusi, halafu ukasema nataka kufanya *study* kujua kama ni cheupe au ni cheusi. Tulishasema suala la uchumi, kwa hiyo, tunaomba msimamo wa Serikali uwe hapo hapo wa kutofungua Bologonja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Hivi karibuni Mheshimiwa Rais ameteua Tume ya Kimahakama ili kufuatilia utekelezaji ambao umetiliwa mashaka sana wa Operesheni Tokomeza. Katika mchango wangu wa maandishi nilimwomba

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Waziri atusaidie kuhakikisha kwamba Tume ile inafika Tunduru ili kubaini matatizo makubwa ambayo yamefanyika kule Tunduru, watu kudhalilishwa na kudhulumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeamua kumwomba Waziri afanye hivyo kwa sababu katika ile ziara ambayo ilifanywa na Kamati ya Bunge ya Maliasili, kwa bahati mbaya haikuweza kufika Tunduru kwa sababu mbalimbali, tukalazimika kuwasafirisha wapigakura wetu ambao walidhalilishwa na kudhulumiwa kwenye kituo cha Masasi. Kwa bahati mbaya katika maelezo yake hakuweza kabisa kugusia jambo hili.

Mwenyekiti, naomba nipate maelezo kutoka kwake ili kuwatia imani wananchi wa Tunduru kwamba Tume ile itaweza kufika hasa ukizingatia kwamba Mbunge wao alikuwa ni mtu wa kwanza kabisa kuleta malalamiko haya katika Bunge hili Tukufu. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, maelezo.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue tu nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Abdallah Mtutura kwamba Tume hii ya Kimahakama ambayo imeteuliwa na Mheshimiwa Rais siyo tu kwamba inapaswa kufika maeneo yote, lakini kwa uhakika kabisa itafika Tunduru na tutahakikisha kwamba wale wananchi ambao wana mambo ya kueleza wanapata fursa hiyo, na tutahakikisha kwamba hili jambo linafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nakubaliana na maelezo aliyotoa Mheshimiwa Msigwa, nami pia hoja hizo nilizitoa kwa maandishi na wakati nachangia hotuba ya Waziri Mkuu niliyazungumza hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika mchango wangu pia...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwanjelwa, naomba urudi ulikotoka. Naomba urudi ulikotoka! Mheshimiwa Ledian, endelea.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia suala la Kalenga kwamba Kijiji cha Kalenga ni mahali pa historia, ndiyo kuna fuvu la Mkwawa, mpigania uhuru wa nchi hii na linatambulika Kimataifa.

Nimezungumzia suala la *Isimila Old Stone Age* ambayo iko katika Kijiji Awenda, Wilaya ya Iringa Vijijini, Kata ya Mlolo. Nimezungumzia pia suala la Lugalo ambako katika Tarafa ya Mazombe Kijiji cha Lugalo, nimezungumzia suala la Mlambalasi Kijiji cha Mlowa Tarafa ya Idodi. Vijiji hivi vyote ni mahali pa makumbusho yenye historia kubwa kwa nchi yetu, lakini vijiji vyenyewe na maeneo vyenyewe hayajafaidika na kulinda maeneo haya ya kihistoria. Nilitegemea Waziri atanijibu, Kijiji cha Awenda kinafaidikaje na kulinda makumbusho yaliyopo pale? Kijiji cha Kalenga, Mlowa, Lugalo; maeneo haya ni ya historia kubwa. Je, kuna utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba maeneo haya yanafaidika kama vile ambavyo maeneo mengine? Tumesikia Mlima Kilimanjaro watu wa maeneo yale wakidai haki kwamba na wao wafaidike. Je, kuna utaratibu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitajibiwa na mimi nitatoa Shilingi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Kwanza suala lako siyo la kisera sana. Maana una vitu *specific* hapa. Wenzako wote tumewaacha, tumewapa ninyi nafasi ili muulize maswali ya kisera. Utajibiwa lakini kutoa Shilingi, hutoi.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali lakini naomba nijibiwe kwa sababu ni maeneo ambayo ni ya kihistoria, wote tunayajua lakini ukienda pale Vijijini, hata wewe unapita pale barabarani, hakuna kitu chochote.

MWENYEKITI: Waziri naomba ujibu, dakika tano zilishapita.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inalitambua hilo na tayari ilishatenga pesa katika eneo la Kalenga na tumeanza kulishughulikia. Pia eneo la Isimila lilitengewa pesa na sasa hivi maeneo haya yameanza kushughulikiwa. Lengo kubwa ni kuvutia utalii katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nikiri kwamba eneo la Lugalo na Mlambalasi bado hatujalishughulikia, lakini haya maeneo mawili kwenye bajeti ya mwaka huu yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o atuachie nafasi tuyaangalie na haya maeneo mawili yaliyobaki.

MWENYEKITI: Tunaendelea, Mheshimiwa Machali.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina jambo moja ambalo ninaamini ni la kisera. Ninaamini kabisa kwamba siyo sera ya Serikali yoyote ile na ikiwemo Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwahudumia watu huku ikionekana kwamba baadhi ya maeneo fulani ni kama vile yanabaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo Wabunge tumekuwa tunali-*address* hasa ambao tunatoka Wilaya ya Kasulu kwa muda mrefu sana. Suala hili ni kuhusiana na hifadhi ya Msitu wa Makere Kusini ambalo Mheshimiwa Waziri ana taarifa. Tumepata kuomba, hebu waje wafanye ziara huko na waweze kuwasikiliza wananchi ambao wamekuwa wanalima katika eneo ambalo wanadai kwamba ni hifadhi, na kwa miaka zaidi ya 30 watu wamekuwa wanalima huko, Serikali haikuweza kuwazuia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi wanasema kwamba hifadhi ile ni ya tangu mwaka 1955, lakini *population* ya wakati ule Wilaya ya Kasulu ilikuwa na watu pengine laki moja na kidogo, leo *population* hii almost inaweza kuwa inaelekea kwenye watu milioni moja. Ukijaribu kuangalia na iliyokuwa sehemu ya Wilaya ya Kasulu kwa maana ya Wilaya ya Buhigwe, watu wote wanalima kule. Ongezeko la watu siku zote linakwenda sambamba na uhitaji wa ardhi kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kauli ya Serikali, ni lini itaweza kutii kilio cha wananchi wa Kasulu kama ambavyo imeweza kuitikia kwenye maeneo mengine? Kuweza kuona umuhimu wa ku-*extend* mipaka ili wananchi waache kuendelea kupigwa, kunyang'anywa raslimali zao kama baiskeli, pikipiki, mazao na wengine wamefungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Mheshimiwa Waziri wakati ukiwa Naibu Waziri tumepata kuzungumza, ni lini sasa utaona umuhimu wa kuja Kasulu ili tuandamane twende tukaangalie ni jinsi gani ambavyo tunaweza tukamaliza tatizo hili?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi tu wa *commitment* yako ni wakati gani?

MWENYEKITI: *Commitment* ya kwenda huko?

MHE. MOSES J. MACHALI: Ndiyo.

MWENYEKITI: Sema, ni rahisi tu! (*Kicheko*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba Mheshimiwa Moses Machali amezungumza na mimi hili suala mara kadhaa na pia tumekuwa na mazungumzo kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu juu ya hili suala na hili suala wananchi wake wafahamu kwamba alilifikisha. Kitu ambacho ningependa kusema ni mambo mawili; moja, tumeagiza watalaam wetu waliangalie hili suala, watupe uchambuzi tuone kina juu ya hili suala. Uhifadhi ni lazima tuende kwa kufuata taratibu nyingi sana. Nikuhakikishie mbele ya Bunge hili Mheshimiwa Machali kwamba mimi au Mheshimiwa Naibu Waziri, kati yetu wawili, mmoja atakuja, tutalitembelea hili eneo na tutapenda tupate suluhu ya hili eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika hoja zangu ambazo nimezitoa, nashukuru Waziri amejibu baadhi. Lakini ipo moja ya msingi niliyoanza nayo, suala la kuwaondoa Maprofesa wawili kwenye nafasi zao. Katika majibu yake amesema kwamba sheria hazikukiukwa na anasema kwamba alifanya utaratibu wa kuwahamisha kwenye vituo vingine vya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili ameeleza kabisa kwamba hakujulishwa na Waziri Nyalandu kuhusu uamuzi wake. Katibu Mkuu Kiongozi, amesema na Watanzania wote tumesikia kwamba sheria na taratibu hazikufuatwa. Kurugenzi ya Habari, Ikulu, imetoa kwenye Vyombo vya Habari, haijakanushwa mpaka leo kwamba taratibu na sheria hazikufuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Nyalandu aseme kwamba wote hawa ni waongo? Leo taarifa zikitoka kwenye Mawasiliano, Habari Ikulu zisiaminiwe kwa kuwa ni za Uongo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, ameshafanya hivyo na akakiuka taratibu, nataka nijue kwamba sasa yupo tayari kuwaomba radhi Maprofesa wale kwa kuheshimu taaluma zao kwa sababu tunataka taaluma za Tanzania ziheshimiwe, na yuko tayari kuwarudisha kwenye nafasi zao ili kama ni kuwahamisha awahamisha kwa taratibu zinazotakiwa?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ningependa kwanza kwa upendo tu nimwambie Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwamba Serikali ina taratibu zake za kazi na maamuzi ambayo yametokana na uamuzi wa Waziri mwenye dhamana hayakukiuka sheria yoyote. Hoja hapa iliyopo ni kama mtu alifukuzwa kazi. Jibu ni kwamba, hakuna mtu yeyote aliyefukuzwa kazi, ni taratibu za kawaida ambazo zimefanyika na utaratibu huo pia hautabadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kuwa Utumishi wa Umma ni Utumishi wa Umma na hili jambo ambalo amelielezea kwamba Ikulu ilikuwa imetoa taarifa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

tofauti, hilo pia siyo kweli kwa sababu taarifa ya maelezo Ikulu kabla hata hayajatoka niliiona. Ilihithibitisha tu kwamba kilichotokea Maliasili na Utalii watu hawakufukuzwa kazi. Kwa sababu hoja ilikuwa kama wamefukuzwa kazi, utaratibu wa Serikali upo wazi. Unapomfukuza mtu kazi, utam-charge, atajitetea. Hii imekuwa ni *internal arrangement* ambayo imefanyika na haihusiani na mtu yeyote kushushwa cheo wala kufukuzwa kazi na hili jambo linabaki kama lilivyo. Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sakaya hukutoa Shilingi, wala hukutupa taarifa kwamba unakusudia kufanya hivyo. Kwa hiyo, kesi yako imekwisha. Tunaendelea, Mheshimiwa Faith Mitambo, hayupo. Mheshimiwa Felista Bura.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni zinazoongoza utendaji katika Wizara za Serikali ni vizuri zikaheshimiwa na Watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri amesema kwamba yeye hakurefusha muda kwa Wamiliki wa Vitalu wala hakurefusha muda wa malipo ya ada ambayo ndiyo fedha ambazo zinasaidia kuwalipa Askari ambao wapo katika mapori ya akiba. Kwa hiyo, hakuvunja GN. Na. 209 ya mwaka 2012. Kama ni hivyo basi, nasisitiza kwamba kanuni ziheshimiwe zinazoongoza Wizara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Waziri kuona kwamba Wazawa ambao walimilikishwa vitalu wameshindwa kuendeleza vitalu hivyo na vitalu hivyo vimerudishwa Wizarani na mpaka sasa baadhi ya vitalu havijapata Wamiliki, namwomba sasa Waziri atuambie ni lini ataleta sheria ambayo tutaifanyia marekebisho na ambayo itaruhusu wageni ambao wana uwezo kwa asilimia 40 wamiliki vitalu na asilimia 60 ibaki kwa wazawa kuliko ilivyo sasa kwamba wazawa ni asilimia 85 na wengi wameshindwa kuendesha vitalu hivyo na wageni asilimia 15 na wageni wengi wana uwezo wa kumiliki vitalu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atuambie ni lini ataleta sheria hiyo ifanyiwe marekebisho? Ahsante.

MWENYEKITI: Sasa kuna mambo mawili; *extension* na mgawo wa vitalu. Ndiyo unachokisema wewe, vyote hivi? Tupe moja tu.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu lile la kwanza amelijibu, naomba ajibu sasa hili la sheria.

MWENYEKITI: Waziri!

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Felister Bura. Ni jambo ambalo linazungumzwa sana kule Wizarani na kwa vyovyote vile ili mamlaka ya Wanyamapori iweze kufanikiwa, iweze kufanyakazi kwa ufanisi, tutaleta katika Bunge hili Tukufu Sheria ya Mabadiliko ya Sheria kadhaa katika kuiwezesha mamlaka hii. Moja ya jambo ambalo tunataka tulilete litakuwa ni hili suala la ni asilimia ngapi ya vitalu vimilikiwe na wazawa na asilimia ngapi imilikiwe na wageni na utaratibu wa kufanya *consultation* utafanyika kabla hatujafika hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Haji Mponda.

MHE. DKT. HAJI H. MPONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango ambayo baadhi ya Wabunge tulitoa kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri tulizungumzia suala la mapori tengefu. Lakini jibu lililotolewa ni kwamba wanalifanyia kazi mpaka Desemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme wazi kwamba sijaridhika kabisa na jibu ambalo limetolewa na Waziri. Nina imani kubwa sana juu ya utendaji wa Mawaziri wote wawili, nawaamini sana kwamba wana uwezo mkubwa kwa nafasi ambayo wamepewa na Mheshimiwa Rais. Lakini inaelekea wametegemea sana watendaji wao ambao mimi naweza nikasema wamewa-*mislead* kwa suala la pori tengefu la Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitu vitatu ambavyo vipo wazi, kwanza kuna barua na maelekezo ambayo yametoka kwa Kiongozi wao, Waziri Mkuu. Dokezo aliwapa tarehe 17 Aprili, na kwamba mchakato ule kwa lile pori tengefu la Kilombero kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha huu wawe wamekamilisha.

Pili, hali halisi ya Bonde la Kilombero kwenye lile pori tengefu, nimeeleza wazi asubuhi jamani, kuna vijiji 15 na vitongoji 18 viko kule vimesajiliwa. Watu wale wanaishi kule kihalali, lakini toka mwaka 2011 wananchi wanaishi kwa wasiwasi baada ya maboresho au marekebisho ya Sheria ya Wanyamapori. Hawa watu wataendelea kuishi hivyo mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anasema hapa mwezi wa Kumi na Mbili mwaka huu ndiyo huenda wakamaliza. Kilimo wamelima kwa kubahatisha tu na kilimo kinaanza mwezi wa tisa.

Lingine la tatu, kitu kingine ambacho kipo wazi mezani kwake Mheshimiwa Waziri, anatakiwa afanye uamuzi; tafiti za TAWIRI, ripoti ya mwaka 2007, 2008, imeeleza wazi maeneo haya yarudishwe kwa wananchi kwa ajili ya matumizi ya binadamu.

MWENYEKITI: Kengele yako imegonga.

MHE. DKT. HAJI H. MPONDA: Sasa!

MWENYEKITI: Kengele imeshagonga!

MHE. DKT. HAJI H. MPONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, uniruhusu nieleze.

MWENYEKITI: Hapana! Wengine wote watataka hivyo hivyo.

MHE. DKT. HAJI H. MPONDA: Natoa Shilingi!

MWENYEKITI: Utatoaje Shilingi? Kwa sababu nimekukatalia, unanitolea mimi? Huwezi kutoa Shilingi kabla ya maelezo ya Waziri kwamba umeridhika au nini. Kama hujaridhika, utatoaje Shilingi sasa? Mheshimiwa Naibu Waziri. Hawa jamaa waliokuwa Mawaziri hawa, Kanuni zinawapa shida! (Kicheko)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mponda ameshakuja Ofisini kwetu mara nyingi. Mimi na yeye tumelizungumza pamoja, nikamwambia maagizo ya Waziri Mkuu tunayafanyia kazi. Nilimwahidi Mheshimiwa Mponda kwamba baada ya bajeti yetu mimi na yeye tutaongozana kwenda kwenye *site* kuliangalia hilo tatizo kwa kina tulitolee maamuzi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona ameliwahisha tu. Kusema Desemba siyo maana yake hili jambo tutalimaliza ndani ya Desemba. Desemba ni *period* ambayo tutashughulikia matatizo yote kwa wakati mmoja. Ninataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya bajeti hii tutakwenda pamoja, tujaribu kulishughulikia hili jambo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Rajab Mohamed Mbarouk!

MHE. RAJABU MBAROUK MOHAMED: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Mimi nitaomba tu nitakapotoa maelezo yangu kama busara ya Kiti chako zitakubali. Najua Kanuni hazikubali, nataka nikamate mshahara wa Naibu Waziri, sitaki wa Waziri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wa maelezo, nilizungumzia suala zima la maagizo ya Serikali yanavyoweza kusababisha hasa TANAPA kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi. Tunajua majukumu ya msingi ya TANAPA kwamba ni kulinda maliasili, vifaa vya hifadhi, kuendeleza hifadhi, kulinda mazingira, kufuatilia afya za wanyamapori. Agizo la Serikali, kwa kutumia Wizara ya Uchukuzi, iliwataka TANAPA, Shirika la Hifadhi la Ngorongoro na Bodi ya Utalii kuanzisha Shirika jipya la Ndege Tanzania.

Sasa nilikuwa naomba maelezo ya Waziri juu ya mpango huu ambao kwa kweli unaweza kuhatarisha maeneo yetu haya matatu ambayo yanaingizia Taifa pato kubwa huku Serikali ikijua kwamba Wizara ya Uchukuzi imeshindwa kuiendeleza ATC, sasa wanataka kuingia upande mwingine kuweza kuangamiza maeneo haya. Naomba maelezo ya Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, maelezo.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Rajabu kwamba kumekuwa na mazungumzo kati ya Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Maliasili na Utalii na Mashirika yetu ya TANAPA, Ngorongoro, vile vile na Shirika la Bandari na wengine. Lengo lilikuwa ni kuangalia ni jinsi gani Serikali inaweza ikafufua Shirika letu la Ndege la Tanzania.

Ukweli ni kwamba mtazamo ulikuwa siyo agizo kwamba mashirika haya yatoe pesa, isipokuwa ilikuwa ni fursa kwa mashirika haya kuangalia uwezekano wa kuwekeza katika Shirika la Ndege la nchi ambalo kwa maana sisi tupo kwenye utalii.

Shirika la Ndege ndiyo lina-*guarantee* uwezo wa sisi kuweza kuwatoa walii kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine na kwa sasa hivi kwa kweli hali ya usafiri wa anga Tanzania ni duni. Tunafanya kila linalowezekana kuhakikisha pamoja na matatizo yaliyopo ya ATL, Wizara ya Maliasili na Utalii itashirikiana na itaendelea kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi tuhakikishe kwamba Shirika la Ndege la Nchi linafufuka.

Nimalizie tu kwa kumhakikishia Mheshimiwa Rajabu kwamba *concept* ya uwekezaji ipo. Kwa mfano, Shirika letu la Ngorongoro sasa hivi linawekeza katika jengo la Kitegauchumi kubwa sana Arusha. Nia ilikuwa kama tukiwekeza fedha za ziada, basi itasaidia utalii na hizi fedha zitarudi. Lakini hakuna uamuzi wowote mpaka ambao umefikiwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shibuda.

MHE. JOHN M. SHIBUDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii. Naunga mkono juhudi za Serikali za kuhakikisha pana lindo la usalama kwa wanyamapori na vile vile juhudi za kukuza utalii.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna chochote chema kisicho na kasoro. Nasikitika sana kusema kwamba wakati Mheshimiwa Waziri anazungumza hapa, hajatoa pole kwa maafu yaliyowafika wafugaji pamoja na mifugo iliyopata athari mbalimbali za kutokana na utumishi mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri, sasa anaweza akatusaidiaje kutuambia hapa leo kwamba atachukua hatua za kuhakikisha watumishi ambao hawana uwoga, hawajali, wamekuwa ni mabingwa wa kutoza rushwa kwa wafugaji na kutotoa risiti kwamba atahakikisha wanaondolewa katika maeneo mbalimbali yaliyopo?

Vile vile napenda kusema ya kwamba tarehe 4 mwezi wa Tano mwaka huu, 2014, Naibu Waziri alikabidhiwa orodha ya watumishi 34 ambao walinyakua Shilingi milioni 77,380 kwa muda wa siku 26 kutoka kwa wafugaji. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kumtuma Katibu Mkuu ambaye ni Msimamizi wa Maadili aende akisikilize vilio vya wafugaji hivyo, pasije pakatokea mgogoro na mizozo kama walivyosimamishwa watumishi wengine? Nategemea kutoa Shilingi kama sitapata majibu yakinifu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nahitimiza nilitoa pole kwa wafugaji. Nafikiri Bunge lako Tukufu lilisikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitumwa kwenda Biharamulo na katika safari yetu tuliambana na Mheshimiwa Shibuda. Ni kweli nilipewa orodha ya watumishi 34 ambao sio waadilifu. Lakini haya mambo ni ya kisheria na nilihakikisha tu kwamba hatua za kisheria zitachukuliwa kwa wafanyakazi ambao watakuwa sio waadilifu. Kwa hiyo, tunaomba atupe subira, asije ikajitokeza kama ilivyojitokeza hapo katikati.

MHE. JOHN M. SHIBUDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo maneno ni matamu sana. Ni ya tabia ya kufuniko kwa udhalimu. Watu wanaendelea kuteseka kule. Ninachotaka mimi kwa sababu hawa ni watu wanaoenda kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya, watambulishie Mheshimiwa Katibu Mkuu wako tayari kumtuma aende akasikilize vilio vya kule. Kwa sababu yeye ndio msimamizi wa maadili, baada ya hapo hatua ziendele. Naomba majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli. Nitamtuma Katibu Mkuu.

MWENYEKITI: Eeh, usijibu kwa urahisi, kwa sababu unataka kumwondoa huyu. Haya ni mambo ya kisheria. Ndiyo utaratibu?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimesema tutamtuma Katibu Mkuu akawasilize wananchi, kwa sababu ile orodha tayari tunayo. Tutampatia na tumeshampatia pale Ofisini. Kwa hiyo, ataenda kuhakiki na kujua wale Watendaji wake ni waadilifu au sio waadilifu kwa kiasi gani. Ndiyo maana nasema hatua za kisheria zitachukuliwa, maana yake hatujazungumza hapa kuwaondoa madarakani. Yeye ataenda ataangalia kwa mujibu wa Sheria.

MWENYEKITI: Haya rudisha hela yetu, kwa sababu sisi hatuwezi kubishana na wewe na hilo sisi hatulijui.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. JOHN M. SHIBUDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekubali kurudisha hiyo Shilingi, lakini vile vile naomba kumpa nasaha Waziri. Nakuomba Mheshimiwa Waziri awe na kauli mahsusi akitambua kwamba anawajibika kwa maslahi ya jamii na ataondoa migogoro na awe tayari kupokea simu za watu wanaohitaji kuongea naye. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Haya, tunaendelea. Mheshimiwa Betty Machangu! Ah, mtandao unakuwa mbaya. *(Kicheko)*

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mheshimiwa Waziri amejibu swali letu kuhusu Halmashauri za Wilaya zinazozunguka Mlima Kilimanjaro. Napenda tu nimwambie Waziri kwamba ameongea amesema kunatolewa kama Shilingi milioni nane kusaidia kwa mambo madogo madogo, lakini naomba tu Mheshimiwa Waziri ajue kwamba Wilaya moja tu kwa mfano ya Moshi Vijijini ina vijiji 161.

Kwa hiyo, hizo Shilingi milioni nane ni kidogo kabisa. Kwa hiyo, tunaomba Mkutano ufanyike ili tujue hatima ya hizo Halmashauri zinazotunza Mlima Kilimanjaro. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Si imepata na kupata! Mheshimiwa Ritta Kabati.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kupata ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia kwa maandishi nilitaka kujua Sera ya Uhaulishaji wa misitu iliyopo katikati ya Miji. Kwa mfano, katika Jimbo la Iringa Mjini kuna msitu ule wa Kihesa Kilolo. Msitu huu umekuwa ni kero sana kwa wananchi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali, rudi ulikotoka.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, msitu huu umekuwa kero kubwa sana kwa wananchi ambao wameuzuka ule msitu. Msitu huu kipo Chuo cha Tumaini ambapo sasa hivi ni Chuo cha Iringa. Tumeshafanya Mkutano wa RC, nafikiri Wabunge wote wa Mkoa wa Iringa wanajua. Mkuu wa Mkoa ameshashughulika sana na tatizo hili la huu msitu, kwa sababu pale pana majoka tu, hakuna kitu chochote.

Sasa tulikuwa tunaomba Mheshimiwa Waziri, nafikiri hata kwako nimeshakuja mara nyingi sana na nilishaleta swali hapa Bungeni na wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri ulilijibu. Sasa tunaomba Mheshimiwa Waziri, leo hii wananchi wa Iringa wameshaniandikia message nyingi sana, na ninashukuru kwamba Mheshimiwa Mwenyekiti umenipa hii nafasi; wasikie unawaambia nini kwa sababu ule msitu ni kero kubwa sana kwa wananchi wa Iringa Mjini. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Kwa maana kwamba wakate ule msitu, au wafanyeje? Maana yake sijaelewa.

MHE. RITTA E. KABATI: Uhaulishwe. Mheshimiwa Waziri anajua kwa sababu alishajibu hata swali na *Hansard* ninayo.

MWENYEKITI: Haya, maana yake na sisi ukitushirikisha lazima tuelewe. Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishapewa tayari, ilishaisha hiyo!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri! Hapo umefanya fujo. *(Kicheko)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo swali liko Mezani na lilishashughulikiwa.

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Faith Mitambo!

MHE. FAITH M. MITAMBO: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati natoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Maliasili na Utalii asubuhi nilikuwa nimemwomba Waziri wa Maliasili mambo mawili. La kwanza, nataka kufahamu, ni lini yuko tayari kufuatana nami kwenda Wilayani Liwale na tukaungana na uongozi wa Wilaya ya Liwale kwenda katika Kijiji cha Kikulyungu kwa ajili ya kumaliza tatizo lile la mgogoro wa mpaka ambao limedumu kwa zaidi ya miaka 10? *(Makofi)*

Pia nataka kufahamu, zile Shilingi bilioni 8.7 ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu alizisema katika hotuba yake ya Bajeti na ambazo alisema kwamba zimekwenda katika Wilaya 38 zimegawiwa, nataka kufahamu, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili kwa sababu ni mdau mkuu wa Sekta hiyo, nitaomba anipe majibu, Wilaya hizo 38 ni zipi na kila Wilaya imepata mgao kiasi gani na labda ametumia criteria gani kugawa hizo fedha Shilingi bilioni 8.7?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Nalo ni la kisera hilo? Maana yake tukifika kwenye kifungu lazima hilo hela zitapatikana, ndiyo ungepata kuuliza. Hilo siyo la kisera. Mimi nilifikiria unazungumzia lile la mipaka ulilolisema karibu unalia kabisa, kumbe siyo! Mheshimiwa Waziri unaweza kujibu unavyotaka.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Faith kwamba tulishajadiliana na Mheshimiwa Naibu Waziri, mmoja kati yetu atafanya hiyo ziara.

MWENYEKITI: Haya. Kwa hiyo, lile la hela halijajibiwa hapa; ni lile la kumkaribisha ziara, atakuja.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi ya Bunge bila Mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Kwanza, naomba nitoe taarifa. Huu mshahara wa Waziri leo nime-extend kwa sababu tunao muda. Lakini kawaida Kanuni zetu, ni dakika 25 kwa wote. Kwa hiyo, msidhani huo ndiyo mchezo wa kawaida, hapana. Tunaendelea.

Kif. 1002 – Finance and Accounts... Sh. 2,121,505,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 – Policy and Planning.... Sh. 1,513,508,000/=

MWENYEKITI: Mheshimia Jafo.

MHE. SELEMAN S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu 1003 nilitaka kupata *clarification* vizuri hapa katika hiki kifungu 221600 inaonekana kuna sifuri. Sasa najua hiki ni kitengo cha Mipango. Je, hawa watu katika suala zima la *printing and advertising* watatumia fedha kutoka wapi?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Mheshimiwa umekipata kifungu hicho? Umeipata *item*? Umeipata *sub-item*? Maelezo!

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki cha 221600 katika *sub-vote 1003 - Policy and Planning* kinahusu *printing and advertising and information supplies* na kimewekewa sifuri. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba pesa hizo zimekasimiwa katika Idara nyingine.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 1004 – Govnt Comm. Unit Sh. 450,224,000/=

MWENYEKITI: Samahani sikukuona, nilikuwa naangalia huku. Mheshimiwa Suzan Lyimo.

MHE. SUZAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nirudie kile cha mwanzo?

MWENYEKITI: Hapana.

MHE. SUZAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimesimama lakini hukuniona.

MWENYEKITI: Ndiyo, kama *the Speaker's*

MHE. SUZAN A. J. LYIMO: Haya naendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Pamoja na kwamba nilikuwa na hoja ya msingi, lakini niko kifungu 221200 - *Communication and information*, ni wazi kwamba katika kifungu hiki nimesoma kwenye Randama ni Kitengo ambacho kinahusiana na masuala ya matangazo na TV; wananchi wengi sana hata kama ni hapa hapa ndani wangependa kujua masuala ya utalii ili waweze kwenda kutembelea kwenye mbuga zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kifungu hiki kimepungua kwa takriban Shilingi milioni 10. Nilikuwa naomba kujua ni kwa sababu gani hasa ukizingatia kwamba tunaona utalii ndiyo unaoingizia pato na kwa maana hiyo bila mawasiliano bila matangazo ya televisheni na radio, basi itakuwa vigumu sana wananchi kupata taarifa. Nilikuwa naomba ufafanuzi.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Suzan. Ni kweli alivyotoa angalizo hilo, lakini nimhakikishie tu kwamba kifungu hicho kimekasimiwa katika *TTB*.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 1005 – *Internal Audit Unit* Sh. 592,868,000/=

Kif. 1006 – *Procurement Mgt Unit*.... Sh. 714,576,000/=

Kif. 1007 – *Legal Unit* Sh. 333,204,000/=

(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kif. 1008 – *Mgt Inform. Systems* Sh. 615,169,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafo.

MHE. SELEMAN S. JAFU: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Katika kifungu hicho nilitaka nipate ufafanuzi vizuri, katika kifungu kidogo cha 271100 najua kwamba Wizara inataka ianzishe tower.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafo, hatujakuwa na wewe. Kifungu gani?

MHE. SELEMAN S. JAFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 271100. Kwa maelezo ya Waziri hapa na hotuba yake ni kwamba hivi sasa Tanzania kunaanzishwa tower kwa ajili ya wanyamapori. Sasa naona hiyo bajeti iliyowekwa hapo ni ndogo sana. Jinsi gani hiyo Taasisi mpya itakayoanzishwa itaweza kuwa-accommodate wakati tunajua kwamba hiyo pesa inazidi kupungua hapo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante.

MWENYEKITI: Tuko kwenye *sub-item 1008*. Hii mbona hatuioni sisi? Labda umekwenda mbele.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 - *Wildlife* Sh. 20,836,752,000/=

MWENYEKITI: Inawezekana hapo, Mheshimiwa Jafo.

MHE. SELEMAN S. JAFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Suala langu liko katika hiyo hiyo, yaani yale maelezo ya mwanzo. Nilitaka kujua kwamba uanzishwaji wa *tour* mpya ambao najua ni chombo muhimu sana...

MWENYEKITI: Rudia kile kifungu.

MHE. SELEMAN S. JAFU: Kifungu 271100.

MWENYEKITI: Eeeh endelea.

MHE. SELEMAN S. JAFU: *Current grants to other level of Government*. Naona hapo pesa yenyewe iliyotengwa ukilinganisha na mwaka 2013 imeshuka, lakini tuna Taasisi mpya inaanzishwa. Je, Taasisi hiyo itapata pesa kutoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ehee, Mheshimiwa Lugola! Mawaziri, mwandike!

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 410700 kuna suala la mradi pale, sasa nilitaka kujua huu mradi kama unahusu pia mradi wa uvunaji wa mamba wanaosumbua wananchi wa Mwibara kwenye Ziwa Victoria, kwa sababu hata mwaka jana, niliulizia kifungu kama hiki na Mheshimiwa Nyalandu akiwa ni Naibu Waziri akasema kwamba fedha za kuvuna mamba kwa wananchi wa Mwibara zimo. Lakini mpaka leo hazijavunwa. Sasa nataka kujua na hizi leo pia mradi huu unahusu mambo kama hayo? Naomba majibu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwijage, naomba m-note.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niko kifungu kidogo 411100 - *New Construction and other Civil Works*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Hifadhi ya Burigi wamekuwa wakishindwa kuitikia miitikio yetu wanapokuja Biengeregere Kata ya Rutoro kuweza kuwazuia hawa wanyama tembo wanaokuja kusumbua kwetu. Hii inatokana na kwamba hawana vibanda, *huts* za kuweza kukaa kuzuia wale wanyama. Nilitaka kujua kifungu hiki kinahusisha *construction* ya hivyo vibanda vya kusubiria hao wanyama wasiwashambulie wakulima wetu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, jibu yote matatu. Unajibu moja moja.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hili la Mheshimiwa Mwijage, Kifungu Namba 411100 – *New Construction And other Civil Works*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo zimetengwa kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa nyumba za watumishi kwenye mapori ya akiba na nina uhakika kabisa Burigi - Biharamulo ni eneo ambalo linaweza likanufaika nah ii bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu ambacho amekizungumzia Mheshimiwa Jafo juu ya fedha ambazo zinatengwa kwa ajili ya *Tanzania Wildlife Authority* ambayo ni Mamlaka Mpya tunayoanzisha; nimjibu tu kwamba, fedha zote ambazo zitatumika kwa sasa hivi zitatoka katika kasma mbili. Moja ni kasma ya Serikali ambayo ni Mfuko wa Wanyamapori unaojulikana kama *Tanzania Wildlife Trust Fund* ambao uko chini ya Wizara, lakini pili utatoka kwenye *Basket Fund* ambayo imeanzishwa na *Donor Community* na kusainiwa hivi karibuni Dar es Salaam. Tunaamini hizi *resource* ndiyo zitakuwa *seed money* kwa ajili ya hii Tower.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ilikuwa ni Mheshimiwa Kangi, Swali lake katika 4107200. Hizi fedha ambazo zimepangwa kuhusiana na suala la *feasibility study*, zimepangwa kwa sababu ya mradi ambao Serikali inategemea kuufanya wa kuendeleza shughuli za uhifadhi *around* Jiji la Dar es Salaam na zimetengwa kwa ajili ya kufanya hiyo kazi.

MWENYEKITI: Kifungu kinaafikiwa?

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 3001 - Forestry And Beekeeping.....18,487,316,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 4001 - Tourism.....11,997,830,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Aliko Kibona.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi. Katika mchango wangu wa maandishi nilimjulisha Mheshimiwa Waziri kwamba, kule maeneo ya Rungwe, kuna *Lake Ngozi*, kuna...

MWENYEKITI: Umesema ni *sub-item* gani?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Subvote...*

MWENYEKITI: *Sub-item!*

MHE. ALIKO N. KIBONA: *Sub-Item 229...*

MWENYEKITI: 4100...

MHE. ALIKO N. KIBONA: 229900.

MWENYEKITI: Umesema ngapi? *Item* ngapi?

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni 229900.

MWENYEKITI: Ok. Ahsante.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimemweleza katika mchango wangu wa maandishi nikimjulisha uwepo wa kivutio cha *Lake Ngozi*, Kijungu kule Kiwira, Mto Kiwira, Daraja la Mungu, *Kapologwe Falls* na kule Ileje, milima ya Mswima ambako kuna nyani weupe ambao hawapatikani sehemu nyingi duniani. Sasa nilitaka kujua kwa sababu, maeneo haya yanaonekana kusahaulika, katika pesa hii pia zitahusika kuendeleza maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: *Other Operating Expenses?*

MHE. ALIKO N. KIBONA: Yes!

MWENYEKITI: Haya. Mheshimiwa Machali pia, uliza? M-mark hiyo Mawaziri.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Najielekeza pale kwenye *Sub-Item 270300 – Current Grant to Non-Financial Public Units Academic Institutions*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nina swali moja tu ambalo ningependa nipate ufafanuzi kutoka kwa Serikali. Ukisoma hii fedha ambayo imetengwa hapa Sh. 3,194,271,000/= inatofautiana na ambayo iko kwenye Randama ambayo nimeitoa Mezani hapo na hali iko hivyo hivyo hata kwenye Kifungu kinachofuata 270500, kiasi ambacho naona, sasa ukija kujumlisha pale itatupa *figure* tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba ufafanuzi kutoka Serikalini.

MWENYEKITI: Kwamba, hii *figure* kwa nini inatofautiana na Randama?

MHE. MOSES J. MACHALI: Ndiyo Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwa sababu, huku inaonekana kwamba kwenye Randama inasomeka kama 3,799,626,000/= ambayo ni ukurasa wa 91. Lakini pia hata kifungu kinachofuata kingine...

MWENYEKITI: Hicho hicho kwanza tujibu, halafu tutaendelea.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sikupata ufafanuzi, nitatoa Shilingi.

MWENYEKITI: Aah, utatoaje Shilingi kwenye hela hizo? (*Kicheko*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwaiposa!

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kupata nafasi, lakini niko kwenye *Sub-Item 221200 – Communication and Informations*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri itakumbukwa wakati nilipokuwa nachangia mchana nilizungumzia sana suala la umuhimu wa mawasiliano na habari katika Sekta hii ya kuendeleza zaidi mambo ya utalii. Sasa nilikuwa nataka tu kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba, Kifungu hiki naona kimepunguziwa fedha kwa 25%. Sasa nilikuwa nataka kujua tu ni kwa nini, kutokana na umuhimu wa Habari na Mawasiliano katika Sekta hii ni kwa nini Kifungu hiki kimepunguziwa kiasi hicho cha fedha?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, jibu moja moja kati ya hayo yote.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 221200 – *Communications and Informations*, kama alivyouliza Mheshimiwa Mwaiposa, kiwango cha fedha kimepungua kutokana na baadhi ya shughuli nyingine zinazosimamiwa na Idara hii kuhamishiwa katika *TTB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kinachofuata alikiuliza Mheshimiwa Kibona, kifungu namba 229900 – *Other Operating Expenses*; naomba nimjibu tu kwamba, hizi *operating expenses* zinatumiwa kama OC kwa ajili ya shughuli mbalimbali zinazohusiana na Idara hii ikiwa ni pamoja na Watumishi wetu kufanya kazi zao katika majukumu yao nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ameuliza Mheshimiwa Machali, hili liko kwenye 270300 – *Current Grant to Non-Financial Public Units*. Swali lake hapa ilikuwa ni kwa nini hesabu zilizoko katika hiki kitabu ziko tofauti kwa kiasi kidogo na tulivyoandika katika Kitabu cha *Randama*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, inawezekana tumefanya *typing error*, naomba iingie katika *Hansard* kwamba, hesabu kamili ni Sh. 3,194,271,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 4002 Antiquities Unit.....5,763,486,000/=

MWENYEKITI: Mpaka isomwe hesabu ndiyo mnasimama. Mheshimiwa Mangungu?

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Katika Fungu hilo, *Sub-Item 270800*; Kwenye maandishi ya mchango wangu nilitaka kujua kwamba, ni lini Serikali itaanza kuwalipa wananchi gawio la watalii ambao wanafika kwenye visiwa vile vya Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitaka kujua hizi fedha...

MWENYEKITI: Ngoja kwanza, samahani. Umesema kifungu gani?

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, 270800.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Halafu unaulizaje swali?

MHE. MURATAZA A. MANGUNGU: Je, pesa hizi ni zile ambazo zitakuwa zinakwenda kama gawio kwa wananchi?

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwenye kasma 270800 kuna suala halikujitokeza kwenye Kamati, sasa kwa sababu limejitokeza kwenye Hotuba ya Waziri hapa...

MWENYEKITI: Ngoja basi ajibu kwanza hilo swali! Si ameuliza mwenzi katika hiyo *Sub-Vote*? Haiwezi kuwa na hesabu mbili. Si ndio ameisemea Mheshimiwa Mangungu hiyo?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Ila jambo tofauti.

MWENYEKITI: Aaah, haiwezi kuwa tofauti! Hesabu ni hizo hizo.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, maana ikishaamuliwa siwezi tena kuuliza.

MWENYEKITI: Naomba ukae chini, nikipata jibu nitakuuliza tena. Mheshimiwa Jafo?

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ilikuwa katika Kifungu hicho hicho. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni, naomba niitoe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri jibu, hela ni za kazi gani? *Full stop*.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni Kifungu 270800 – *Current Grant to Non-Financial Public Units* na hii ni *General Fund*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hizi fedha zinakwenda kama *grant* katika *Institutions* zetu mbalimbali ambazo ni *Non-Financial Public Units* ambazo zinafanya kazi zinazoendana na masuala ya *antiquities* nchi nzima.

MWENYEKITI: Enhee, unasemaje wewe?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya Waziri. Nafahamu hii kasma kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati; nilichokuwa nataka kusema tu ni kwamba, kwenye Hotuba ya Waziri ukurasa wa 45, sehemu ya hizi pesa zinakwenda Shirika la Makumbusho ya Taifa. Sasa kati ya kazi ambazo Waziri amezielezea hapa Bungeni ni kwamba, Shirika pia litaratibu Tamasha la Utamaduni wa Mtanzania utakaoshirikisha jamii kutoka Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilipendekeza kwenye mchango wangu wa maandishi kwamba, kwa kiwango cha Kasma ambacho Shirika la Makumbusho ya Taifa wanapata, kwa mwaka mmoja wa fedha, wanaweza kuendesha zaidi ya Tamasha moja la Utamaduni wa kutoka Mkoa wa Kagera peke yake na nikapendekeza pendekezo la Mkoa mwingine.

Sasa katika ufafanuzi Mheshimiwa Waziri hakutoa ufafanuzi. Kwa hiyo, ningepomba kupata ufafanuzi tu katika hili kwamba, kwa hii kasma ambayo imeongezeka ya Shirika la

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Makumbusho: Je, mko tayari katika matumizi ya hii, kuongeza Mkoa mwingine katika huu utamaduni wa Mtanzania badala ya Mkoa mmoja pekee?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio hilo ambalo nataka ufafanuzi.

MWENYEKITI: Unatakiwa kusema ni Mikoa ipi iliyotakiwa? Kama ni huo huo, basi. Hebu jibu hilo Mheshimiwa Waziri?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimjibu Mheshimiwa Mnyika kwamba, ni kweli Mkoa wa Kagera ndiyo ambao umeteuliwa kwa ajili ya huu Utamaduni wa Mtanzania na tunategemea kwamba watafanya vizuri sana. Lakini bajeti hii siyo kubwa kwa maana ya majukumu makubwa waliyonayo Makumbusho. Kwa hiyo, kwa mwaka huu tuta-*stick* na ile ambayo ilikuwa *budgeted* na pesa nyingine zitafanya shughuli nyingine za kuhakikisha kwamba, Makumbusho na shughuli zake nyingine zinaendelea. Ahsante.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kitabu cha IV Miradi ya Maendeleo

Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii

Kif. 1002 Finance and Accounting.....125,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 Wildlife.....4,506,803,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru; Kasma 4811 -*Sustainable Management of Natural Resources*. Kwenye maelezo ambayo yaliwasilishwa mbele ya Kamati inaonesha kwamba, pamoja na kusaidia kwenye masuala ya wanyamapori kwenye maeneo ya Serengeti na Ngorongoro, kwenye kasma hii vilevile kuna fedha kwa ajili masuala ya uanzishaji...

MWENYEKITI: Umesema kasma ipi? Samahani tunakurudisha nyuma.

MHE. JOHN J. MNYIKA: 4811.

MWENYEKITI: Aah, okay. Ahsante.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishaji wa Mamlaka ya Wanyamapori. Sasa kwenye Hotuba ya Waziri hapa mbele ya Bunge, ameeleza habari njema kwamba tayari muundo umeshapitishwa na amri ya kuanzisha mamlaka hiyo, tayari iko mstari wa mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri atakumbuka kwamba mwaka 2013 mbele ya Kamati na hata mbele ya Bunge aliahidi kwamba, katika Mwaka huu wa Fedha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Sheria itakuwa imekamiliwa ya kuanzisha hii Mamlaka. Sasa katika maelezo yake ya kuhitimisha Mheshimiwa Waziri katika suala la Sheria ameahidi kwamba mchakato wa Sheria utakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata ufafanuzi, kiwango cha fedha kilichoko katika huo mradi cha uanzishaji wa Mamlaka ya Wanyamapori: Je, kimepangwa kwa ajili ya kukamilisha Sheria hiyo katika mwaka huu wa fedha na kuhakikisha inakuja Bungeni kwenye huu mwaka wa fedha ambao tunapitisha Bajeti hivi sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata ufafanuzi.

MWENYEKITI: Kwamba, hizi hela zote ni za kutungia Sheria?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mnyika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Sheria ya Bunge Na. 5 ya mwaka 2009, Bunge liliipa Serikali Mamlaka ya kuweza kuanzisha hiyo Mamlaka ya Wanyamapori na mchakato wa kuanzisha Mamlaka ya Wanyamapori, pamoja na kwamba ulikuwa unaanzishwa kwa amri au kwa *Establishment Order*, ilikuwa ni lazima ufuata taratibu zote za mchakato ya kuanzisha Sheria kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mchakato wa kuanzisha, *Establishment Order*, umekamilika. *Establishment Order* ya kuanzisha Mamlaka ya Wanyamapori imesainiwa na sasa ni mamlaka kamili. Hatua inayofuata sasa, kuna baadhi ya Sheria; na nilichokisema leo, nimezungumzia juu ya marekebisha ya Sheria ndogo ndogo ambazo tunaita *Miscellaneous Amendments*. Ni lazima tutele *Miscellaneous Amendments* kwa ajili ya baadhi ya mambo ambayo tunadhani yana upungufu kuweza kuipa nguvu zaidi hii Mamlaka. Itafanyika kwa utaratibu wa kawaida kupitia kwa Mwanasheria Mkuu.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 3001 Forestry And Beekeeping.....8,366,413,000/=

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu Kidogo 4629, nilikuwa naomba waweze kutueleza ni *donor* gani au Wafadhili gani? Kwa sababu, kuna *amount* ya Shilingi bilioni moja, lakini ukiangalia zote zinatoka ni *forex*, lakini hapajaoneshwa ni *donor* gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nilitaka kujua, kama sehemu ambayo hamna hela yoyote kutoka nje, lakini wameandika *donor*, inamaanisha nini? Kwa sababu ukiangalia kifungu cha juu yake hakina hela, lakini wameandika *DANIDA*. Kwa hiyo, nilikuwa naomba maelezo?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimjibu tu Mheshimiwa Susan. Mahali ambako hatuja-*indicate* ni *donor* gani, ina maana ni fedha zetu za ndani zinatumika. Mahali ambako tume-*indicate donor* ni mahali ambako tunatumia fedha za Wafadhili.

Katika kifungu alichokitaja cha 4628 – *Participatory Management Forestry*, Mradi huo ulikuwa unaendelea chini ya *DANIDA* na Mradi huo umefikia mwisho ndiyo maana kile kifungu kimewekewa sifuri.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwangu siyo hilo. La kwangu ni 4629 na ni *Forex 1.2 billion*, lakini hakuna jina la *donor*. Hii ni *Forex, 4629?*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Nadhani rudia tena?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri nirudie tu kama nilivyosema kumjibu Mheshimiwa Susan. Tulichokisema katika huo utaratibu wetu, mahali popote ambako hatujaandika jina la *donor*, hata kama fedha zitakuwa zimekuwa *indicated* katika *forex* ni fedha za ndani.

Mara nyingi tunakuwa tunatenga fedha za ndani na *anticipation* ya ahadi nyingine ambazo tuna-*match* fedha kubwa zaidi za *Donor Community*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko kwenye Kasma 4629 – *Support to Forest, National Forest Program*.

MWENYEKITI: Ngoja kwanza, *Sub-Item* gani?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Kasma 4629 iliyotengewa Shilingi bilioni 1.198 *Forex* na milioni 41.6 fedha za ndani.

MWENYEKITI: Si ndio aliyosema Mheshimiwa Susan?

MHE. JOHN J. MNYIKA: 3001 – 4629.

MWENYEKITI: 4629?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Ndiyo!

MWENYEKITI: Ndiyo aliyosemea Mheshimiwa Susan?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, haijaamuliwa bado kwa hiyo, ningeomba kupata ufafanuzi?

MWENYEKITI: Enhee, eleza?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 14 wa Taarifa ya Kamati, Kamati imependekeza kuwa Pori la Akiba la Msitu wa Pande, (*Pande Forest Reserve*), ambayo inagusa Jimbo la Ubungo, Jimbo la Kawe, Manispaa ya Kinondoni, maarufu kama Msitu wa Mabwepande, linaweza kuboreshwa na kuwa kivutio kingine cha utalii. Serikali ione umuhimu wa kuboresha na kuliendeleza pori hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimejaribu kuangalia mchanganuo wa kiwango cha fedha cha kifungu hiki, nimeona pamoja na kusaidia Vyuho vya Masuala ya Misisi, inahusika vilevile kuratibu asasi za kiraia na sekta binafsi kwenye masuala ya misitu. Natambua kwamba, Wizara inakusudia, kupitia *TFS*, kuboresha lile pori la akiba la Pande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa ufafanuzi kuhusu matumizi ya hizi fedha za asasi za kiraia na sekta binafsi, kama zitatumika vilevile kuratibu asasi za kiraia na sekta binafsi kwenye maeneo ambayo Wizara inakusudia, kupitia *TFS*, kuendeleza misitu hii kama huu wa Akiba wa Pande. Ningeomba majibu kutioka kwa Waziri?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hoja ya Mheshimiwa Mnyika ya Pori la Pande, ningependa kusema kwamba, kupitia Mfuko wetu wa Maendeleo ya Misit, tuna kazi ambayo tumepanga kuifanya katika lile Pori la Pande. Kwa maana ya bajeti, kifungu hiki cha 4629 kitatumika kama kilivyokuwa kimepangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 4001 Tourism.....1,200,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

SPIKA: Dalili ya watu waliochoka, wanasema sema tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa mtoa hoja, taarifa!

TAARIFA

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya fedha za Wizara ya Maliasili na Utalii, Fungu 69, kwa mwaka 2014/2015, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo basi, naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii
kwa Mwaka 2014/2015 yalipitishwa na Bunge)*

SPIKA: Napenda kuwapongeza Wizara kwa kazi nzuri mliyofanya, lakini nadhani kitu kimoja ambacho ningependa kwa Wizara yako, mkajaribu kutengeneza umoja wa kufanya kazi. Kwa sababu, huo umoja wa kufanya kazi kama hamna, hakuna kazi itakayofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, hiyo ni *political responsibility* yako kutengeneza umoja wa kufanya kazi na palipokuwa na tatizo mnaongea. Sio kufanya zaidi ya hapo, kwa sababu, vinginevyo hiyo Wizara itawashinda kweli. Pengine habari zinazotoka, hizi ni dalili ya kwamba kuna tatizo mle ndani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hiyo mjitahidi na watumishi nao wafanye kazi kwa mujibu wa sheria na kila mtu afanye kazi kwa mujibu wa sheria. Sisi tunategemea utalii ni sehemu yetu ambayo nchi inaweza kuishi vizuri zaidi bila kuleta vinenoneno. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Ni kweli kwamba toka mimi nimeingia katika Bunge hili, Wizara hii ni tete kila mwaka. Mimi nilifikiri Nyalandu wewe utafanya mabadiliko! Nategemea utafanya hivyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawapongeza watumishi wote kwa kazi nzuri na ninyi wote mzidi kushirikiana, kwa sababu hapa ni suala la kitaifa na siyo suala la mtu binafsi. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Mnyika, unaweza kusoma? Soma basi *statement* yako. Kama huna tunaweza kukupa nafasi kesho?

Alikuwa ametoa maelezo binafsi, nikawa nimeletewa hapa Mezani, nikamwandikia kwamba mimi siwezi kusoma *document* kubwa nikiwa hapa Mezani, pelekeni Ofisini. Bahati nzuri Ofisini wameshanialelea, wakasema unaweza kutoa. Kwa hiyo, tunayo nafasi.

Mheshimiwa Mnyika, kama unaweza kusoma!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, ninasitasita kwa sababu, nimeshaelewana na Mheshimiwa Magufuli...

SPIKA: Mmeshaelewana?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Ndiyo. Ameniahidi kwamba atatoa maagizo ya kusitisha lile zoezi ambalo TANROAD walikuwa walifanye. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Okay, basi ahsante; basi nashukuru, ndio uungwana wenyewe.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, sina matangazo mengine. Naahirisha Shughuli za Bunge mpaka Kesho Saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.03 jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Alhamisi,
Tarehe 15 Mei, 2014, Saa Tatu Asubuhi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)